

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Ishirini na Tatu - Tarehe 3 Julai, 2010

(Mkutano ulanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Zubeir Ali Maulid) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Kituo cha Kimaifa cha Mikutano cha Arusha(AICC) kwa Mwaka 2008/2009[*The Annual Report and Audited Accounts of the Arusha International Conference Centre for the year 2008/2009*].

MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MHE. WILSON M. MASILINGI-MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa za Hotuba ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y.) MHE.KHALIFA SULEIMAN KHALIFA MSEMAJI MKUU WA UPINZANI WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Taarifa za Hotuba ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA A WATOTO:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011
Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, wote mtakuwa mashahidi kwamba leo tutakuwa na hoja mbili za Wizara mbili tofauti. Kwa hiyo, kwanza kabisa nitamwita Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili awasilishe hoja yake, baada ya hapo nitamwita Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Utangulizi; kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uteuzi huu ni heshima kubwa kwa Taifa letu, na kielelezo cha imani kubwa walijonayo wana Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza pia Rais kwa kufanikisha Mkutano wa Uchumi Duniani (*World Economic Forum*) uliofanyika Jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 5 hadi 7 Mei, 2010. Jukwaa hilo lilitoa nafasi ya kuitangaza Tanzania katika dunia, na kupambanua changamoto zinazoikabili Dunia hususan nchi

zinazoendelea na kubainisha hatua za ufumbuzi wa changamoto hizo. Jukwaa hilo pia lilitoa nafasi ya kujadili masuala muhimu ya kiuchumi na kijamii, ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa mtangamano na uimarishaji wa ushirikiano wa kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza pia Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samuel Sitta na Naibu Spika, kwa kuliendesha Bunge letu kwa viwango na ufanisi mkubwa. Aidha, napenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano walionipa wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukunu kwa dhati wapiga kura wa Jimbo langu la Nkenge kwa imani yao kwangu na kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa kama Mbunge wao katika kutekeleza majukumu yangu. Wananchi wa Nkenge wameendelea kunionyesha upendo mkubwa na hivyo kunipa nguvu katika kuwatumikia. Ninawaahidi kuititia Bunge lako Tukufu kuwa nitaendelea kutekeleza jukumu langu la kuwawakilisha na kuwatumikia kwa uwezo wangu wote. Ninawaomba, na ni matumaini yangu kuwa tutadumisha na tutaendeleza ushirikiano huu muhimu wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru sana mke wangu mpendwa Adelaida Kamala na familia yangu kwa ujumla kwa upendo wao, ushirikiano na mshikamano ambao umeniwezesha kufanya kazi yangu kwa furaha, kujiamini na ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa imani aliyonayo kwangu kunitua kuwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais na wananchi wote kwa ujumla kuwa nitaendelea kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa kadri ya uwezo wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wizara ya Ushirikianao wa Afrika ya Mashariki, na kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, napenda kuwashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha mwaka 2009/2010 katika kutimiza malengo yetu, ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma, Sekta Binafsi na Taasisi Zisizo za Kiserikali. Aidha, shukrani zetu ziwaendee pia washiriki wenzetu wa maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kutekeleza programu na mipango mbalimbali ya Jumuiya ya Afrika Mashiriki, hususan, Serikali za Uingereza, Ufaransa, Kanada, Norway, Sweden, Ubelgiji, Denmark, Finland, Marekani, Japan na Ujeruman; Mashirika na Taasisi za kimataifa za Jumuiya ya Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *DFID*, Benki ya Japani ya Maendeleo ya Kimataifa, Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Japani, na Benki ya Dunia, *GTZ*, *Rockefeller Foundation*, *Kilimo Trust*, *The Investment Climate Facility for Africa (ICF)*, *AWEPA*, *African Capacity Building Facility (ACBF)*, *British American Tobacco (BAT)*; na *International Planned Parenthood Federation Africa Region (IPPFAR)*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Mawaziri na Wadau mbalimbali kutoka Sekta na Taasisi za Kiserikali na Sekta Binafsi kwa michango mikubwa wanayoitoa, na ushiriki wao katika kuendeleza mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushiriki na ushirikiano wao ni nguzo

muhimu katika kuleta msukumo na kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushiriki, uwajibikaji na umahiri wa wadau umewezesha kuendeleza mtangamano hatua kwa hatua kwa kasi inayotarajiwa, na kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa na Jumuiya yanalindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa naomba niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ushirikiano mkubwa na michango yao mahiri katika majadiliano na shughuli mbalimbali za kuendeleza mtangamamo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nina imani kuwa ushiriki na mshikamano huu utaendelezwa na kufanya ushiriki wa nchi yetu katika mtangamano wa Afrika Mashariki kuwa wenyewe tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, Mbunge wa Muleba Kusini, kwa uchambuzi wao wa kina wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka 2009/2010 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2010/2011. Katika utendaji wetu, Wizara itazingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii. (*Makofit*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwashukuru viongozi wenzangu katika Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, nikianzia na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mbunge, Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki; Dr. Stergomena L. Tax, Katibu Mkuu; Bwana Uledi Mussa, Naibu Katibu Mkuu; Wakuu wa Idara na Vitengo; na Watumishi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuichapisha Hotuba hii kwa umakini na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mkutano wa Bunge la Bajeti la mwaka jana, tumeshuhudia matukio mbalimbali hapa Bungeni. Napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia kutoa hotuba hapa Bungeni kuwapongeza Wabunge wapya walioteuliwa na Mheshimiwa Rais amba ni Mhe. Ismail Jusa Ladhu Mbunge na Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majonzi makubwa, naungana na Mawaziri wenzangu katika kutoa salamu zangu za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais, na familia ya aliyekuwa mwasisi wa Taifa letu na Waziri Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Hayati Rashidi Mfaume Kawawa. Kifo chake ni pengo kubwa kwa Taifa letu. Tutamkumbuka Marehemu kwa mchangwa wake mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, nachukua nafasi hii kutoa pole kwako binafsi na Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Mheshimiwa Hayati Sigfrid Ng'itu aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ruangwa. Kifo chake kimeleta majonzi makubwa kwa familia, wananchi wa Jimbo la Ruangwa na Taifa kwa ujumla. Tutamkumbuka Marehemu kwa mchangwa wake mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu. Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya hotuba hii, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki imezingatia maudhui yaliyotolewa katika Bunge lako Tukufu kupitia Hotuba ya Mhe. Mizengo Kayanza Pinda Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, hotuba hii imezingatia Hotuba za Hali ya Uchumi na Bajeti ya Serikali zilizowasilishwa na Mhe. Mustafa Mkulo Mbunge, Waziri wa Fedha na Uchumi. Nawapongeza kwa hotuba zao nzuri zilizoweka mwelekeo wa shughuli za Serikali na dira ya Bajeti ya Taifa katika mwaka wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo na Mipango ya mwaka 2009/2010: Malengo na Mipango ya mwaka 2009/2010; katika mwaka wa fedha 2009/2010, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwa ni pamoja na: kubuni sera; kuratibu maandalizi ya mikakati na programu za kisekta; kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; kuratibu, kusimamia, na kushiriki katika majadiliano kuhusu shughuli za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kuhimiza ushiriki na kukuza uelewa wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na kuwezesha utumiaji wa fursa za kiuchumi na kibashara zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kuimarisha na kujenga uwezo wa Wizara kutoa huduma bora kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na shughuli zilizopangwa kufanywa na Wizara katika mwaka 2009/2010 ni kama ifuatavyo:

- (i) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano wa Kikanda wa Afrika Mashariki;
- (ii) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake;
- (iii) Kukamilisha majadiliano ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (iv) Kuandaa na kusimamia Mkakati wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (v) Kufanya tafiti na tathmini za utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake na kuishauri Serikali ipasavyo;
- (vi) Kuratibu na kushiriki katika kufanya tathmini ya utekelezaji na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Miradi na Programu za Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (vii) Kuratibu na kushiriki katika mikutano na vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuanzia ngazi ya Wataalam, hadi Mkutano wa Kilele wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

- (viii) Kufanya maandalizi ya majadiliano ya Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (ix) Kushirikisha Sekta binafsi katika masuala mbalimbali ya uendelezaji wa Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (x) Kutoa elimu kwa umma na kwa wakati kuhusu fursa na changamoto zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; na
- (xi) Kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji, kuwaendeleza watumishi na kutoa huduma bora kwa wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2009/2010 yalizingatia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2005; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA); Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; Mkakati wa Tatu wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2006-2010); na Maamuzi mbalimbali ya Wakuu wa Nchi Wanachama na Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Malengo na Mipango ya Mwaka 2009/2010; katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 13,919,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi 146,789,000 kwa ajili ya shughuli za mradi wa Maendeleo wa Maboresho ya Watumishi (PSRP II). Hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2010 Wizara ilipokea kutoka Hazina kiasi cha shilingi 13,919,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 146,788,991 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Maendeleo wa Maboresho ya Watumishi (PSRP II). Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010 Wizara iliweza kutumia fedha zote zilizopokelewa. Sera na Mikakati ya Wizara; Jumuiya ya Afrika Mashariki inakamilisha maandalizi ya Sera ya Mtangamano itakayotoa mwongozo wa shughuli za mtangamano wa Jumuiya kulingana na Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya. Ili kuhakikisha kuwa Tanzania inajipanga ipasavyo, na inanufaika na fursa mbali mbali zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara imeanza maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano. Sera hii itatoa mwongozo wa kitaifa kuhusu shughuli za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2007 – 2010 umekwisha muda wake, hivyo Wizara imefanya mapitio na kuandaa Mpango Mkakati unaofuata wa miaka mitatu, 2010 – 2013. Mkakati huu umehuishwa na Mpango wa Maendeleo wa Jumuiya, na unatoa mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha miaka mitatu ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa hatua za Mtangamano: Utekelezaji wa Umoja wa Forodha; pamoja na malengo mengine, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inalenga kukuza uchumi imara na wenyewe uwezo wa ushindani katika masoko ya nchi jirani na ya dunia kwa ujumla. Kifungu cha 40(a) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kinabainisha kuwa Serikali itaweka mikakati itakayowezesha

kuhimili ushindani wa kibiashara kimataifa na kuwa na uwezo wa kushiriki na kufaidika na mfumo wa biashara wa kimataifa kwa kuzingatia mazingira ya utandawazi. Aidha, kifungu cha 40(b) kinabainisha kuwa Serikali itachukua hatua ya kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kikanda na wa kimataifa kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo namba moja la Malengo ya Maendeleo ya Milenia linaainisha nia ya kuondoa umaskini uliokithiri na njaa. Uendelezaji wa mtangamano, unachangia katika kukuza biashara, uwekezaji, na kufungua fursa nyingine kiuchumi, na hivyo kuwawezesha Watanzania kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano wa Afrika Mashariki, na kuchangia katika kuyafikia malengo yaliyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Maendeleo ya Milenia. Katika kutekeleza azma hii Tanzania inatarajia kunufaika kiuchumi na kijamii hasa kutokana na kupanuka kwa soko, kuongezeka kwa ajira, uwekezaji, upatikanaji wa mitaji, kuboreka kwa miundombinu, kuimarisha ulinzi na usalama na kuendeleza ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama hatua ya kwanza ya mtangamano, Nchi Wanachama zilikubaliana kutekeleza Umoja wa Forodha. Hatua hii imefungua fursa za masoko hasa katika biashara ya bidhaa za kilimo na viwanda na usafirishaji. Katika kutekeleza Umoja wa Forodha Nchi Wanachama zimekubaliana kuondoa Ushuru wa Forodha kwa biashara mionganoni mwao, kwa bidhaa zinazozalishwa na Nchi Wanachama; kuweka wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zitokazo nje ya Jumuiya; kuweka vigezo vya Jumuiya vya kutambua uasili wa bidhaa; na kuondoa vikwazo visivyo ya kiforodha. Kuanzia mwaka 2005 Nchi Wanachama zilikuwa zinatekeleza kipindi cha mpito cha miaka mitano cha kuondoleana ushuru wa forodha katika biashara ya bidhaa mionganoni mwa Nchi Wanachama. Kipindi hicho kiliisha mwezi Desemba 2009. Kuanzia mwezi Januari mwaka 2010 biashara ya bidhaa zote zinazokidhi vigezo vya utambuzi wa uasili wa bidhaa, mionganoni mwa Nchi wanachama hazitozwi ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa kutoka nje ya Jumuiya zinatozwa ushuru wa forodha kwa viwango vitatu: asilimia sifuri kwa mali ghafi za viwandani na mitambo, asilimia 10 kwa bidhaa zilizosindikwa kwa kiwango cha kati na vipuri, na ushuru wa asilimia 25 kwa bidhaa zilizokamilika. Jumuiya pia ilikubaliana orodha ya bidhaa nyeti kutoka nje ya Jumuiya ambazo hutozwa ushuru zaidi ya viwango hivi vitatu kwa madhumuni ya kuzuia ushindani usio halali, na uendelezaji wa viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Umoja wa Forodha umekuwa wa mafanikio katika biashara ya bidhaa mionganoni mwa Nchi Wanachama. Mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la Afrika Mashariki yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Mauzo ya Tanzania katika soko la Jumuiya yalionezekwa kutoka Dola za Kimarekani Milioni 96.4 mwaka 2005 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 117.7 mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 22.1, na kuongezeka tena hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 173.1 mwaka 2007 sawa na ongezeko la asilimia 47.1. Mwaka 2008 mauzo yalionezekwa na kufikia Dola za Kimarekani milioni 315.5 sawa na ongezeko la asilimia 82.2. Katika mwaka 2009, mauzo yalipungua na kufikia dola za kimarekani milioni 263.7

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushuka kwa mauzo ya Tanzania katika Jumuiya mwaka 2009 kulitokana na mtikisiko wa uchumi ulioikumba dunia, na mabadiliko ya tabia nchi yaliyopelekea ukame na mafuriko. Mauzo yalipungua kwa asilimia 16.44. Anguko hili limetokana na kupungua kwa mauzo kwa baadhi ya bidhaa, ikiwa ni pamoja na nafaka ambazo zilipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 43.46 mpaka Dola za Kimarekani milioni 5.7, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 11.2, chumvi kutoka Dola za Kimarekani milioni 77.61 mpaka Dola za Kimarekani milioni 11.4 ikiwa ni anguko la asilimia 20.9, mauzo ya bidhaa za chuma yalipungua kutoka Dola za kimarekani milioni 34.15 mpaka Dola za Kimarekani milioni 5.7 ikiwa ni pungufu kwa asilimia 9, mauzo ya mafuta yalipungua kutoka Dola za Kimarekani milioni 37.25 mpaka Dola za Kimarekani milioni 17.1 ikiwa ni anguko la asilimia 6.38. Katika mwaka 2009/10 bidhaa ambazo Tanzania imeuza kwa wingi katika nchi za Afrika Mashariki ni pamoja na bidhaa za umeme na vifaa vya umeme, mazao ya mkonge, nguo, vifaa vya uchapishaji, mafuta ya mitambo, mazao ya mbao, samaki, kahawa, vifaa vya plastiki, vinywaji, chuma/nondo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa manunuzi ya bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya, Tanzania ilinunua bidhaa zenyenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 160.4 mwaka 2005 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 174.4 mwaka 2006. Manunuzi yалиshuka hadi kufikia dola za Kimarekani milioni 106.53 mwaka 2007. Mwaka 2008 manunuzi yaliongezeka hadi kufikia dola za Kimarekani Million 204.8. Mwaka 2009 manunuzi yaliongezeka hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 310.5. Mwenendo wa manunuzi ya bidhaa kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya. Bidhaa ambazo Tanzania inaagiza kwa wingi kutoka Nchi Wanachama ni pamoja na nondo, sukari, nafaka, mafuta ya kupikia, nguo, chupa za chai, vifaa vya umeme, madini, bidhaa za plastiki na vioo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia mwenendo wa biashara ya bidhaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, urari wa biashara baina ya Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeendelea kuimarika. Mwaka 2006 nakisi ya urari wa biashara kati ya Tanzania na Nchi Wanachama ilipungua hadi Dola za Kimarekani milioni 56.7 kutoka Dola za Kimarekani milioni 64.0 mwaka 2005. Aidha urari wa biashara kati ya Tanzania na Nchi Wanachama ulikuwa na chanya kwa Dola za Kimarekani milioni 66.6 kwa mwaka 2007 na milioni 110.8 kwa mwaka 2008. Hata hivyo, katika mwaka 2009 Tanzania ilipata nakisi ya urari wa biashara ya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 46.8 kutokana na sababu nilizokwisha eleza hapo awali. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa pamoja na jitihada nyingine za Serikali za kuvutia wawekezaji, utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha umechangia katika kukuza uwekezaji baina ya Nchi Wananchama.

Miradi iliyowekezwa hapa nchini kutoka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 2005 ilikuwa 35 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 39.65. Miradi mipyä katika mwaka 2006 ilikuwa 38 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 41.06. Katika mwaka 2007 miradi mipyä ilikuwa 27 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 50.88. Mwaka 2008 uwekezaji uliongezeka kwa miradi mipyä 77 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 310.35; na uliongezeka tena kwa miradi mipyä 31 yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 55.77 katika mwaka 2009. Sekta zilizoongoza katika uwekezaji kutoka Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika

kipindi cha mwaka 2005 hadi 2009 ni pamoja na Sekta za Uzalishaji; Kilimo; Utalii; Ujenzi; na Usafirishaji. Idadi na thamani ya miradi iliyowekezwa na Tanzania katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kama inavyoonekana katika Kiambatanisho Na 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ongezeko la uwekezaji baina ya nchi Wanachama nafasi za ajira zitokanazo na uwekezaji huu zimekuwa zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2005 ajira mpya zilikuwa 2,643. Kiwango cha ajira kiliongezeka katika mwaka 2006 kwa ajira mpya 5,379; 2,605 mwaka 2007; 1,424 mwaka 2008 na ajira mpya mwaka 2009 zilikuwa 1,687. Sekta zilizoongoza katika kuongeza nafasi za ajira ni pamoja na uzalishaji, kilimo, utalii, ujenzi na usafirishaji, Kiambatanisho Na. 6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2009 Jumuiya ya Afrika Mashariki ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha kwa nia ya kubaini mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojiteza katika kipindi cha mpito cha utekelezaji wa Umoja wa Forodha.

Tathmini hiyo imeonyesha kuwa Nchi Wanachama zimenufaika na Umoja wa Forodha kwa kukuza biashara mionganini mwao kuongezeza kwa mapato ya Serikali na uwekezaji. Aidha, tathmini imeonyesha kuwa mapato ya ushuru wa forodha hayakuathirika kama ilivyodhaniwa wakati wa uundaji wa Umoja wa Forodha. Hata hivyo, tathmini imebainisha kuwa vikwazo visivyo vya kiforodha bado ni changamoto kubwa katika biashara ya bidhaa baina ya Nchi Wanachama.

Kama nilivylitaarifu Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu ya Bajeti mwaka jana, Wizara pia imefanya tathmini ya ndani ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Lengo la tathmini hiyo ilikuwa ni kubainisha kwa kina mafanikio na changamoto zitokanazo na utekelezaji wa Umoja wa Forodha ili kujipanga kimkakati katika hatua zinazofuata za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Baada ya kuzidurusu taarifa za tathimini hizi mbili, Wizara imebaini kuwa vikwazo visivyo vya kiforodha bado vingalipo, mathalan vizuizi barabarani na urasimu usio wa lazima wa vyombo vinavyosimamia viwango vya ubora wa bidhaa nchini; gharama kubwa za uzalishaji kutokana na miundombinu isiyotosheleza na umeme; kutotumia fursa zitokanazo na michepoo ya bidhaa na huduma ambazo Tanzania ina uwezo zaidi ikilinganishwa na nchi nyingine wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kukabiliana na changamoto zilizojiteza katika miaka mitano ya utekelezaji wa Umoja wa Forodha, katika hatua za mtangamano zinazofuata. Aidha,

Wizara inaendelea na hatua za kuyawasilisha mapendekezo rasmi Serikalini ili kuandaa mikakati ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muhtasari wa mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuainisha sera na sheria zote kwa lengo la kukuza biashara na uwekezaji hususan katika maeneo ya nishati, kilimo, ardhi, mazingira, madini, kodi na masuala ya fedha;
- (ii) Kuimarisha vyombo vinavyosimamia biashara ili kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha katika biashara na kupunguza gharama za kufanya biashara;
- (iii) Kupunguza gharama za uzalishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za viwanda kwa kuongeza uwekezaji kwenye nishati, maji, mawasiliano na kuboresha upatikanaji wa mitaji yenyе riba nafuu;
- (iv) Kuwawezesha wazalishaji kuongeza ubora wa bidhaa ili kuhimili ushindani ndani na nje ya Jumuiya;
- (v) Kutekeleza mpango mahsusni wa kuongeza uwekezaji katika sekta ya miundombinu ili kujenga miundombinu ya kisasa itakayowezesha kuongeza tija na kupunguza gharama za kufanya biashara;
- (vi) Nchi Wanachama kuongeza utashi wa kudhibiti vikwazo visivyo vya kiforodha; na

Nchi Wanachama kutoa msukumo wa kuanzishwa kwa Ukanda Huru wa Kibiashara wa *SADC-EAC-COMESA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziara za Mipakani; katika kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Umoja wa Forodha hususan kubaini kero za wananchi katika kutumia fursa za soko la Afrika Mashariki, mwezi Septemba 2009 na mwishoni mwa mwezi Mei 2010 Wizara ilifanya ziara katika mipaka ya Manyovu, Mabamba, Ngara, Mtukula, Sirari, Rusumo, Namanga, Holili na Horohoro. Lengo la ziara hizo lilikuwa ni kutathmini namna Itifaki ya Umoja wa Forodha inavyotekelzw, kuwaelimisha watendaji juu ya umuhimu wa Itifaki hiyo, na kuwaelimisha wananchi kuhusu fursa zitokanazo na Umoja wa Forodha na Mtangamano kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyobainika ni uelewa mdogo hasa mionganoni mwa wafanyabiashara wa kati na wadogo kuhusu taratibu zilizopo za Umoja wa Forodha, hususan taratibu za Uasilia wa Bidhaa (*Rules of Origin*). Ili kurahisisha utambuzi wa bidhaa kwa wafanyabiashara wadogo na wakati, Jumuiya ya Afrika Mashariki imeweka utaratibu rahisi zaidi wa cheti rahisi cha Utambuzi wa Uasili wa Bidhaa (Simplified Certificate of Rules of Origin) kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wanaosafirisha bidhaa zisizozidi thamani ya Dola za Kimarekani 500. Kutokana na uelewa mdogo wafanyabiashara wetu wadogo hawajatumia fursa hii kupata unafuu wa kodi. Aidha vikwazo visivyo vya kiforodha, hususan vituo vingi vya ukaguzi; matumizi ya njia zisizo halali (njia za panya); vizuizi katika biashara ya mazao; na uelewa mdogo kuhusu pasi za kusafiria za Jumuiya ya Afrika Mashariki bado ni changamoto.

Ili kupambana na changamoto hizi, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine kwa lengo la kuboresha na kuimarishe huduma, ikiwa ni pamoja na kuanzisha Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani (*One Stop Border Posts-OSBPs*), kutekeleza mradi wa kuboresha viwango utakaowezesha vituo vya uzalishaji hapa nchini kupata hati ya utambuzi ya Shirika la Biashara Ulimwenguni kwa Kiwango cha ISO 2000 kinachotambuliwa na WTO. Aidha, baadhi ya Mashirika yanayoshughulikia viwango ikiwemo Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) yamefungua ofisi za kanda, na kuweka maafisa wao mipakani. Hatua hizi zimeleenga katika kusogeza huduma karibu na wananchi. Wizara inaendelea pia kutoa elimu kwa Umma kwa lengo la kukabiliana na hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza Mpango wa Ubina baina ya Serikali na Sekta Binafsi (*Public – Private Partnership – PPP*), Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi (kampuni ya Sky Sea Ltd.) iliandaa ziara katika nchi za Zambia, Malawi, Uganda, Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo-DRC iliyofanyika kuanzia tarehe 7 hadi 20 Machi, 2010.

Lengo la ziara hii ilikuwa ni kuwashawishi wafanyabiashara wa nchi hizo na Serikali zao kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Ziara hii ilikusudia kutangaza maboresho katika Bandari ya Dar es Salaam, hatua za kiforodha na kutangaza Miundombinu ilivyoboreshwana kupelekeea kushuka kwa gharama za kufanya biashara na kukuza fursa za biashara; kutoa fursa ya kuongea na wafanyabiashara wa nchi hizo; na kuendeleza mahusiano mema baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na majirani zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongezeka na kuboreka kwa huduma ya usafirishaji wa mizigo kwenda nchi jirani kutaiwezesha Tanzania kufanya biashara ya huduma zinazohitajika katika kupokea na kusafirisha mizigo. Aidha kuongezeka kwa watumiaji wa Bandari na barabara zetu kutaongeza pato la taifa, ajira na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hii ilibainisha changamoto zinazokwaza wafanyabiashara kutoka nchi hizo kutotumia kikamilifu bandari ya Dar es Salaam.

Vikwazo hivyo ni pamoja na: usalama mdogo hususan udokozi na uvamizi barabarani, vikwazo visivyo vya kiforodha (Vizuizi vingi barabarani), matatizo yanayosababishwa na mawakala wa forodha, uwezo mdogo wa reli ya kati na reli ya TAZARA, ucheleweshaji katika kupakia na kupakuwa mizigo. Pamoja na changamoto hizi, ziara iliwezesha kutoa taswira mpya kuhusu hali ya sasa ya ubora wa huduma katika Bandari ya Dar es Salaam na hivyo kuwahamasisha wafanyabiashara kurejea katika bandari ya Dar es Salaam. Baaada ya ziara hii, Wizara ilikutana na watendaji wa vyombo vinavyohusika na uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kukubaliana kuunda Kamati ya Kitaasisi ikishirikisha wadau toka sekta ya umma na sekta binafsi ili kupendekeza namna ya kutatua changamoto zilizosalia kwa kuainisha hatua za kuchukua na wahuksika kwa kila hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishaji wa Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani (*One Stop Border Posts-OSBPs*); uanzishaji Vituo vya Pamoja vya Utoaji Huduma Mipakani (*One Stop Border Posts-OSBP*) unalenga kurahisisha taratibu za uhamiaji na forodha kwa kutoa huduma hizi upande mmoja wa mpaka kwa pamoja bila kulazimika kuititia taratibu kama hizi upande wa pili wa mpaka. Aidha, aina zote za udhibiti zinazofanyika mpakani kwa utaratibu wa sasa zitaendelea kufanyika kwa ukamilifu katika upande mmoja badala ya kulazimika kufanyika katika pande mbili. Kwa mfano, katika mpaka wa Namanga, ukaguzi wa mpakani kwa wale wanaotoka nchini Tanzania kwenda nchini Kenya utafanyika katika upande wa mpaka wa kuingia nchini Kenya kwa pamoja na ukaguzi wa kuingia nchini Kenya. Kwa upande mwengine ukaguzi wa kuingia nchini Tanzania utafanyika katika upande wa mpaka wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii itawezesha biashara, uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kusafiri ndani ya Jumuiya, na usafirishaji shehena kufanyika kwa urahisi na kwa gharama nafuu baina ya Nchi Wanachama wa Jumuiya. Kwa kuanzia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Rwanda zimesaini Hati ya Makubaliano ya Uanzishwaji wa Kituo cha Huduma za Pamoja Mpakani katika kituo cha Rusumo. Uanzishwaji wa kituo hicho unakwenda sambamba na ujenzi wa daraja la Rusumo ambalo ni kiungo muhimu kati ya Tanzania na Rwanda ambapo Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la *Japan – JICA* limekubali kugharimia ujenzi wa kituo hicho na daraja jipya la Rusumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vingine vinavyotarajiwa kuanzishwa ni Namanga, Horohoro/Lungalunga, Sirali/Isebania, Mutukula na Holili/Taveta. Tayari uchambuzi yakinifu unaendelea kwa vituo vya Namanga na Holili. Aidha, rasimu ya sheria ya uanzishwaji wa vituo vya huduma za pamoja vya mpakani katika Afrika Mashariki imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao Kuboresha Huduma za Viwango na Ubora; katika kutekeleza Ibara ya 13 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya inayosisitiza ushirikiano katika masuala ya ubora wa viwango vya bidhaa. Wizara imekuwa ikishirikiana na Shirika la Viwango nchini na wadau wengine katika program na mikutano ihusuyo masuala ya viwango vya ubora wa bidhaa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ili kuhakikisha kujenga mazingira yaliyo sawa Nchi Wanachama zimeandaa Sheria ya Ubora na Viwango vya mwaka 2006. Sheria hii imewianisha taratibu za ukaguzi, viwango, vifaa vya upimaji na ugezi baina ya Nchi Wanachama ili kuwezesha watumiaji wa sheria hii kutekeleza mfumo unaofanana. Bidhaa ambazo viwango vyake vimewianishwa hadi sasa kutokana na sheria hii ni 1500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama katika mwaka wa fedha 2009/2010 zimetekeleza mradi wa *Trade Capacity Building: Enhancing the Capacity of Quality Infrastructure and TBT and SPS Compliance*, unaodhaminiwa na UNIDO kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi. Chini ya mradi huu viwanda na kampuni kumi za uzalishaji nchini zinatarajia kupata Hati ya Utambuzi wa Kiwango cha ISO 2000 inayotambuliwa na Shirika la Biashara Ulimwenguni (WTO); viwanda na kampuni hizo ni *Afri Tea and Coffee Blenders*, *Wakulima Tea Company*, *Mikoani Traders (Azania)* na *Power Food Industries* vilivyopo Dar es Salaam; *Tanzania Fish Development Company (TFDC) Vegetable Oil Company (Voil)* na Tanperch vya Mwanza; *Kagera Tea, Kagera Fish* na *Bukoba Milk Company* vya Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uanzishaji wa Soko la Pamoja la Afrika Mashariki; katika kutekeleza Ibara ya 76(1) na 104(2) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanzisha Soko la Pamoja la Afrika Mashariki ambayo ni hatua ya pili ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iliongoza na kuratibu ujumbe wa Tanzania katika majadiliano ya Itifaki ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Majadiliano hayo yalianza mwezi Aprili 2008 na kukamilika mwezi Oktoba mwaka 2009. Majadiliano hayo yalifanyika kwa umakini kwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Tanzania na Jumuiya yamezingatiwa. Kufuatia kukamilika kwa majadiliano haya, Itifaki ya Soko la Pamoja ilisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano wao wa Kilele uliofanyika Mwezi Novemba, 2009 jijini Arusha. Hadi sasa nchi zote Wanachama zimesharidhia Itifaki na kuwasilisha katika Sekretarieti Hati za kuridhia ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya msingi yanayohusishwa katika Soko la Pamoja ni:-

- (i) Soko huru la bidhaa ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Goods*); utekelezaji wa Soko huru la bidhaa utaiwezesha Tanzania na nchi nyingine wanachama kupata Soko la uhakika kwa bidhaa mbalimbali, zikiwemo bidhaa za kilimo na viwanda katika Jumuiya;
- (ii) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kusafiri katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Free Movement of persons*);
- (iii) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kufanya kazi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Workers*): utekelezaji utawawezesha Watanzania kuajiriwa katika sekta mbalimbali zilizofunguliwa na Nchi Wanachama;
- (iv) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kufanya biashara ya huduma katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Services*): utekelezaji wa hatua hii unawahakikisha uhuru wa soko la biashara ya huduma katika sekta zilizofunguliwa na Nchi Wanachama kwa kuondoa vikwazo hatua kwa hatua, na kutoanzisha vikwazo vipy;
- (v) Uhuru wa raia wa Afrika Mashariki kuwekeza mitaji katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Free Movement of Capital*): utekelezaji wa hatua hii utawawezesha kuondoa vikwazo kwa raia wa Afrika Mashariki kuwekeza kwenye soko la mitaji katika nchi

nyingine ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki hatua kwa hatua kwa mujibu wa ratiba ya utekelezaji;

(vi) Haki ya raia wa Afrika Mashariki kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara na uchumi katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Right of Establishment*).

utekelezaji wa hatua hii unawahakikishia raia wa Afrika Mashariki haki ya kuanzisha na kuendesha shughuli za biashara na kiuchumi katika nchi yoyote mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bila ubaguzi kwa misingi ya utaifa au taratibu za uanzishaji Kampuni hatua kwa hatua.

(vii) Aidha, Nchi Wanachama zimekubaliana kuainisha sheria na maeneo yanayolindwa kwa wananchi wa nchi husika na kuyawasilisha katika Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya Itifaki ya Soko la Pamoja kupata nguvu ya kisheria kwa lengo la kukubaliana jinsi ya kufungua maeneo hayo katika siku za usoni; na

(viii) Haki ya ukazi kwa raia wa Afrika Mashariki katika nchi yoyote ndani ya Jumuiya (*Right of Residence*): utekelezaji wa haki hii unawawezesha raia wa Nchi Wanachama watakaopata ajira au kuanzisha shughuli za kiuchumi kuishi katika nchi yoyote mwanachama, kulingana na taratibu zilizokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maeneo haya utafanyika hatua kwa hatua ili kutoa nafasi ya maandalizi na pia kupunguza athari hasi za utekelezaji. Aidha, Nchi Mwanachama hailazimiki kutoa ajira kwa wageni katika sekta ya umma; na pia sheria na sera za Nchi Wanachama zitaendelea kutumika katika maeneo yaliyokubalika, mathalan katika masuala ya ardhi, na ukazi wa kudumu. Kutokana na makubaliano ya kutumia sheria za nchi wanachama katika maeneo haya, Mwanaafrika Mashariki atakapotaka kuanzisha shughuli ya kiuchumi katika Nchi Mwanachama atatakiwa kufuata sheria za ardhi na uwekezaji za nchi husika ili kuweza kupata eneo la kufanya biashara/shughuli za kiuchumi. Majadiliano na maandalizi ya Itifaki ya Soko la Pamoja yalihusisha sekta na wadau mbalimbali toka Sekta ya Umma na Sekta binafsi.

Napenda kuchukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha kukamilisha majadiliano ya Itifaki ya Soko la Pamoja hususan, katika maeneo yaliyokuwa na utata yaani ardhi, hati za kusafiria na ukazi wa kudumu. Maamuzi yaliyofikiwa yamezingatia maslahi ya Tanzania, kama niliviyokwishaeleza, masuala haya yataongozwa na sheria husika za Nchi Wanachama.

Aidha, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau wote waliohusika katika mchakato huu uliohusisha maandalizi na majadiliano ya kina ambayo yaliwezesha

kukamilisha Itifaki hii kwa kuhakikisha kuwa maslahi ya Tanzania na Jumuiya yamezingatiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 151 cha Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kinazitaka Nchi Wanachama kukamilisha Itifaki na hatimaye kuridhiwa na Nchi Wanachama kwa mujibu wa taratibu zao.

Aidha, Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalitaka Bunge kuridhia itifaki ambazo kwa masharti yake zinahitaji kuridhiwa. Kulingana na matakwa haya ya kisheria, Bunge lako Tukufu liliridhia Itifaki ya Soko la Pamoja hapo tarehe 19 Aprili 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kukubali kuridhia itifaki hii. Hatua hii imetoa heshima kubwa kwa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya, kwani Tanzania imeweza kuridhia Itifaki hii kwa wakati, na kutoa chachu kwa nchi nyingine wanachama kukamilisha mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hii iliyofikiwa viro Viambatanisho ambavyo majadiliano yake bado yanaendelea na yapo katika hatua mbalimbali. Viambatanisho hivyo ni Mafao ya Hifadhi za Jamii (*Social Security Benefits*) na Taratibu za Uwianisho wa Mitaala na Utambuzi wa Sifa za Kitaalam (*Regulations for Harmonization of Curriculum and Mutual Recognition of Academic Qualification*) na vinatarajiwaa kukamilika ifikapo Julai 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa sasa inakamilisha maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja. Lengo la Mkakati huu ni kuainisha mikakati inayohitajika kuiwezesha Tanzania kujipanga katika kuzitumia kikamilifu fursa zitokanazo na Soko la Pamoja katika maeneo na sekte mbali mbali. Wizara imekwisha pokea rasimu ya kwanza ya Mkakati kutoka kwa mshauri mwelekezi. Wizara inaendelea kukusanya maoni ya wadau ya Rasimu. Mkakati huu unatarajiwaa kukamilishwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uanzishaji wa Sarafu Moja ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; kulingana na Kifungu cha 5(2) cha Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, uanzishaji wa Sarafu Moja ni hatua ya tatu ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Uanzishwaji wa Sarafu Moja unahitaji Nchi Wanachama wa Jumuiya kukidhi matakwa ya uwianishaji wa vigezo vyta uchumi mkubwa (*Macro-economic Convergence*) kati yao. Vigezo hivyo ni pamoja na uwiano wa ukuaji wa Pato la Taifa (*GDP*), kasi ya

upandaji mfumuko wa bei (*inflation*), viwango vya riba (*interest rate*), akiba ya fedha za kigeni, na kiwango cha kubadilisha fedha (*exchange rate*). Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zinatakiwa kuzingatia uwianishaji wa vigezo hivi baina yao kabla ya kuwa na sarafu moja ili kujenga uchumi imara utawezesha nchi wanachama kunufaika nchi wanachama kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza hatua hii, mwezi Septemba, 2009 Jumuiya ya Afrika Mashariki ilimteua Mshauri Mwelekezi kufanya utafiti utakaoiwezesha Jumuiya kuingia katika hatua hii. Mshauri Mwelekezi alikamilisha kazi yake na matokeo ya utafiti huo yaliwasilishwa katika Mkutano wa Ishirini wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika mwezi Machi 2010. Baraza la Mawaziri liliridhia matokeo hayo na kuagiza taarifa ya mshauri mwelekezi itumike kama mwongozo katika majadiliano ya Itifaki ya Sarafu Moja.

Aidha, Baraza liliagiza iundwe timu ya wataalam kutoka Nchi Wanachama kwa ajili ya majadiliano ya Itifaki ya Sarafu Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeshaanza mchakato wa kuunda timu ya wataalam. Timu hiyo itaipitia ripoti ya mshauri mwelekezi kwa kina na kuanda mapendekezo ili kuanda msimamo wa Tanzania. Majadiliano ya uanzishwaji wa Itifaki ya Sarafu Moja yanatarajiwa kuanza rasmi mwezi Septemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirikisho la Kisiasa, baada ya kukamilika kwa zoezi la kukusanya maoni ya wananchi kuhusu kuharakisha au kutoharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki katika nchi za Tanzania, Kenya, na Uganda, Burundi na Ruanda Wakuu wa Nchi Wanachama katika Mkutano wao maalum wa 6 uliofanyika Arusha, tarehe 20 Agosti, 2007 waliamua kuwa mchakato wa kukusanya maoni ufanyike pia kwa nchi za Burundi na Rwanda kufuatia nchi hizo kuijunga na Jumuiya.

Baada ya kupokea maoni toka nchi hizo mbili, Wakuu wa Nchi katika mkutano wao wa 11 uliofanyika Arusha, tarehe 20 Novemba, 2009, waliagiza Baraza la Mawaziri la Jumuiya kuunda timu ya wataalamu kufanya uchambuzi wa changamoto zilizotolewa na wananchi na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia agizo hilo, Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 20 uliofanyika tarehe 26 Machi, 2010 iliunda Timu ya Wataalamu ya watu kumi na tano, (watatu kutoka katika kila nchi mwanachama) kwa ajili ya kutekeleza agizo la Wakuu wa Nchi. Timu imekwishaanza kazi na inategemewa kuwasilisha ripoti yake mwezi Julai, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Kikanda, Utatu wa *EAC-COMESA-SADC (EAC-COMESA-SADC Tripartite Arrangement)*, mwaka 2008 Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, SADC na COMESA walikutana mjini Kampala kujadiliana jinsi ya kuimarisha ushirikiano mionganoni mwa Jumuiya hizo. Viongozi hao waliazimia

kuanza mchakato wa kuanzisha Eneo Huru la Biashara kwa lengo la hatimaye kuanzisha Umoja wa Forodha wa Nchi Wanachama za *SADC*, *COMESA* na *EAC*. Wakuu wa Nchi walielekeza kuwa uandaliwe mpango wa kuanzisha Eneo Huru la Kibiashara la Nchi Wanachama wa *EAC-COMESA-SADC*, (*EAC-COMESA-SADC Free Trade Area Road Map*), na mpangilio wa Kitaasisi. Kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara kutasaidia kupunguza gharama za kufanya biashara kwa kuwianisha taratibu za kiforodha, viwango vya ushuru wa forodha na kuondoa vikwazo visivyo vya kiforodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utatu huu utapanua wigo wa soko la bidhaa mbalimbali, utakuza fursa za ajira, na utachangia katika kuinua kipato cha wananchi na pato la Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti juu ya uanzishwaji wa Eneo Huru la Kibiashara umekamilika. Kufuatia kukamilika kwa utafiki huu, mpango wa kuanzisha Eneo Huru la Kibiashara la Nchi Wanachama wa *EAC-COMESA-SADC*, (*EAC-COMESA-SADC Free Trade Area Road Map*), na mfumo wa kitaasisi vimekwisha andaliwa na kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri la Sekta ya Biashara, Viwanda, Fedha na Uwekezaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kikao kilichofanyika tarehe 24 Juni, 2010. Mpango huo, na mfumo wa kitaasisi vinatarajiwa kuwasilishwa katika kikao kijacho cha Baraza la Mawaziri, na hatimaye katika kikao cha Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, *SADC* na *COMESA* kwa maamuzi.

Majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi kati ya Jumuiya ya Afrika ya Mashairiki na Umoja wa Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Kiuchumi (*Framework for Economic Partnership Agreement*) kati ya nchi za kundi la Afrika, *Caribbean* na *Pasifikasi (ACP)* na Umoja wa Ulaya (*EC*) yalianza mwaka 2002. Majadiliano haya yaliingia sehemu ya pili mwaka 2003 yakihusisha kanda mbalimbali za kiuchumi. Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kuzingatia maagizo ya Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2002 kwamba zijdili masuala ya *WTO* na *EU/ACP* kama kundi moja, ziliweka sahihi ya awali ya makubaliano (*initialing*) ya Mkataba wa Mpito wa Ubia wa Uchumi (*Framework for Economic Partnership Agreement (FEPA)*) na Umoja wa Ulaya (EU) tarehe 27 Novemba 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Mkataba wa Mpito nchi za EAC zilifungua masoko yake kwa bidhaa za Jumuiya ya Ulaya kwa asilimia 82.6 na kuweka asilimia 17.4 kwenye orodha ya bidhaa nyeti. Jumuiya ya Ulaya kwa upande wake ilifungua soko lake kwa bidhaa kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa asilimia 100 (*Duty Free Quota Free – DFQF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu wa mpito uliainisha katika Ibara ya 37 maeneo ya kuendelea na majadiliano ili kufikia mkataba kamili. Katika majadiliano haya yanayoendelea, nchi changa kimaendeleo kama Tanzania zinatarajiwa kunufaika na misaada itakayoziwesha kutatua changamoto za kiuzalishaji na kiusambazaji, na

kupatiwa misaada ya kiufundi na kifedha itakayoziezesha kuzalisha na kuuza katika soko la dunia; kupatikana kwa misaada ya kuboresha miundombinu kupitia mpango wa kitaifa na kikanda; na kurahisika kwa viwango vya uasili wa bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano ya Ubia wa Kiuchumi baina ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya yamekamilika katika maeneo ya utaratibu wa kupunguziana Ushuru wa Forodha, Viwango vya kulinda Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea katika biashara ya mazao ya kilimo, Vikwazo vya Kiufundi vya Biashara, Ushirikiano katika usimamizi wa shughuli za Kiforodha na Uwezeshaji wa Biashara. Aidha, makubaliano bado hayajafikiwa katika vipengele vifuatavyo vya Mkataba wa Mpito:

- (a) Upendeleo Maalum (*Most Favoured Nation*);
- (b) Ushuru na Kodi za Mauzo ya Nje (*Duties and Taxes on Exports*);
na
- (c) Ushirikiano wa kiuchumi na kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa kipengele cha kutoa upendeleo maalum katika Mkataba wa Ubia kama kinavyopendekezwa kunazibana nchi za EAC kutotoa upendeleo zaidi kwa nchi nyingine kuliko upendeleo utakaotolewa kwa EU. Msimamo huu unadhoofisha jitihada za nchi kutafuta ushirikiano wa kibiashara kati ya EAC na nchi zingine, hususani nchi zenye uchumi unaobukia haraka kama China, India na Brazil. Msimamo huu unadhoofisha pia azma ya kuendeleza South-South Cooperation. Aidha, msimamo huo unakinanza na matakwa ya WTO ya kuziwezesha nchi zinazoendelea (enabling clause,).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kuwepo kwa kipengele cha ushuru na kodi za mauzo ya nje katika Mkataba huu kutazuia nchi kutoza kodi kwenye bidhaa tunazouza nje ya nchi. Pale nchi Wanachama ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki itakapowabidi kutoza kodi kwenye bidhaa zinazouzwa nje itabidi kuomba kibali toka Baraza la EPA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Tanzania na nchi nyingine za EAC ni kuendeleza Viwanda na Biashara kwa nia ya kukuza mauzo nje. Hivyo hakuna nchi inayopendelea kutoza ushuru na kodi za aina hii. Hata hivyo, upo umuhimu wa kutojifunga moja kwa moja, ili kutoa nafasi ya kisera pale inapobidi kuweka ushuru wa aina hii, ili kukabiliana na mitikisiko ya kiuchumi (*economic shocks*), au kulinda/kuendeleza sekta fulani muhimu kiuchumi/kijamii, hususan kuendeleza viwanda vya usindikaji kwa uongezaji thamani katika mazao/bidhaa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pande zote mbili zimekubaliana kuingiza sura ya ushirikiano wa kimaendeleo katika Mkataba ya Ubia baina ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Ulaya kwa lengo la kuzipatia Nchi ya Jumuiya ya Afrika ya

Mashariki misaada ya kiufundi na itakayoziwesha kutatua changamoto za kiuzalishaji na kiusambazaji ili kuweza kuzalisha na kuuza katika soko la dunia. Hata hivyo, muafaka haukuweza kufikiwa kama sura hii ya ushirikiano wa kimaendeleo iingizwe kwenye Mkataba ya Mpito (*FEPA*), au katika Mkataba Kamili (*comprehensive EPA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kutofikia muafaka baina ya Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kamishna wa Umoja wa Ulaya katika mkutano wa pamoja uliofanyika tarehe 9 Juni, 2010, pande zote zilikubaliana kuendelea na majadiliano katika vipengele hivi vya Mkataba wa Mpito na maeneo mengine ya mkataba kamili wa Ubia wa Kiuchumi. Hivyo, badala ya kusaini Mkataba wa mpito kama ilivyotarajija awali, pande zote mbili zimekubaliana kuendelea na majadiliano kwa lengo la kukamilisha maeneo yote na kusaini mkataba kamili (*Comprehensive Economic Partnership Agreement*) wenyewe manufaa kwa pande zote mbili ifikapo mwezi Novemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji Wa Miundombinu Ya Kiuchumi Sekta ya Uchukuzi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inaelekeza uimarishaji wa miundombinu ili kuziwezesha sekta nyingine za uzalishaji. Kifungu cha 44(c) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kinaelekeza kuendelea kuchukua hatua za kuimarissha barabara zitakazounganisha nchi yetu na nchi jirani kwa barabara za lami na zinazopitika wakati wote.

Aidha, kifungu cha 45 (e) kinaeleza kuwa Serikali itachukua hatua za kuvutia uwekezaji katika miundombinu ya usafiri na uchukuzi wa reli, barabara, maji na anga katika Kanda za Maendeleo ili kuimarissha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani na kuwafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta ya miundo mbinu ya kiuchumi utaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijirografia kunufaika kiuchumi na kuendeleza fursa ya kuzihudumia nchi jirani zisizo na bandari. Tanzania ni nchi pekee inayopakana na nchi zote Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hivyo, kujipanga kutekeleza miradi ya miundombinu iliyoainishwa katika programu na mipango mbalimbali ya Afrika Mashariki hususan barabara, reli na bandari kutaifanya Tanzania kuwa kiungo na kitovu cha biashara katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma hii, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu na miradi iliyoainishwa katika sekta ya uchukuzi inayoiunganisha Tanzania na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama ifuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtandao wa Barabara kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa kuendeleza Mtandao wa Barabara katika Jumuiya (*The East African Road Network Project*) unaojumuisha kanda

(corridor) tano. Utekelezaji wa ujenzi wa mtandao wa barabara wa Jumuiya katika kanda hizo tano umefikia hatua mbali mbali kama ifuatavyo:-

Kanda ya kwanza (Corridor 1) Katika kanda ya kwanza ya Mombasa - Malaba - Katuna - Kigali-Kanyaru Haut-Bujumbura-Gatumba ikijumuisha Marangu –Tarakea, Chalinze – Segera na Segera – Himo hatua zifuatazo zimefikiwa:-

- (a) barabara ya Marangu – Rombo Mkoo inayojumuisha Mwika Kilacha (Km 32) ujenzi umekamilika kwa asilimia 52;
- (b) Rombo Mkoo – Tarakea (Km 32) ujenzi umekamilika kwa asilimia 92;
- (c) Tarakea – Kamwanga ujenzi wake umeishakamilika.
- (d) Chalinze – Segera (Km 125) ukarabati umekamilika kwa asilimia 70; (e) Segera – Same (Km 172) ukarabati unatarajiwa kuanza muda wowote; na
- (f) Same – Himo (Km 80) usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati unaendelea.

Kanda ya pili (Corridor 2) Katika kanda ya pili inayojumuisha Dar-es-salaam-Isaka-Lusahunga-Mutukula-Masaka, na Lusahunga-Nyakasanza-Rusumo –Kigali-Gisenyi hatua zifuatazo zimefikiwa:-

- (a) Barabara yote imejegwa isipokuwa Kagoma-Lusahunga (Km 154) inaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami;
- (b) Isaka – Lusahunga (Km 242) ukarabati unaendelea.

Kanda ya tatu (Corridor 3), Katika Kanda ya tatu ya Biharamulo - Mwanza - Musoma - Sirari - Lodwar – Lokichogio ambayo pia ni sehemu ya mtandao wa barabara katika ukanda wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Road Circuit) hatua zifuatazo zimefikiwa: -

- (a) Biharamulo – Bwanga (km 76.9) usanifu wa kina umekamilika;
 - (b) Geita – Usagara (km 90) zipo katika ujenzi;
 - (c) Nyanguge – Musoma – Sirari (km 184) zinahitaji ukarabati (*rehabilitation*). Kanda ya Nne (Corridor 4) Katika kanda ya nne ya Tunduma - Sumbawanga - Kigoma – Manyovu (Mugina) – Rumonge – Bujumbura – Ruhwa (Bugarama) – Karongi – Gisenyi Serikali ya Tanzania inagharamia upembuzi yakinifu wa barabara ya Sumbawanga – Tunduma na MCC watafadhilli ujenzi wa barabara hii.
- (a) Barabara ya Sumbawanga – Kanazi/Kibaoni (km 151) kazi ya ujenzi (upgrading) inaendelea, na

(b) Barabara za Kibaoni – Mpanda (Km 95), Mpanda – Uvinza – Kanyani/Kidakwe (Km 252), Kidakwe – Nyakanazi (Km 310) usanifu wa kina umekamilika.

Kanda ya Tano (Corridor 5), Katika Kanda ya Tano ambayo ni Tunduma - Iringa – Dodoma - Arusha - Namanga – Moyale hatua zifuatazo zimefikiwa:

(a) Barabara za Babati – Minjingu – (km 60), Minjingu – Arusha (Km 104) na Arusha – Namanga (Km 105) ziko katika ujenzi wa kiwango cha lami.

(b) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Dodoma – Babati.

(c) Iringa – Dodoma fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami zimepatikana kutoka kwa JICA na ADB. Mchakato wa kumpata Mkandarasi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ya Arusha – Namanga – Arthi River yenye urefu wa kilomita 104.4 kwa upande wa Tanzania na kilomita 136 upande wa Kenya hadi mwezi Juni 2010 ni kama ifuatavyo:-

(a) Kipande cha Kilomita 35 kilikuwa kimeshajengwa kwa kiwango cha lami, matabaka ya msingi (base) km 40, changarawe km 52 na madaraja (*Box Culverts*) 17 kati ya madaraja (*Box Culverts*) 37 yameshajengwa.

(b) Upembuzi yakinifu wa barabara ya Arusha – Holili – Voi yenye urefu wa kilomita 260 umekamilika na hivi sasa usanifu wa kina unaendelea.

(c) Barabara ya Malindi – Lunga Lunga na Tanga – Bagamoyo zipo katika hatua za mwisho za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

(d) Barabara ya Tanga – Horohoro Mkandarasi ameanza kazi ya ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha Sekta ya Usafiri wa barabara Nchi Wanachama zinaendelea pia na maandalizi ya Mkakati wa Uendelezaji wa Usafirishaji na Programu ya Maendeleo katika Sekta ya Barabara (*EAC Transport Strategy and Road Sector Development Programme*) inayotarajiwa kukamilika Mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mitandao ya miundombinu ya reli, barabara, bandari na mawasiliano kwa lengo la kuunganisha Tanzania na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutaiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha biashara kutohana na fursa yake kijiografia katika kupitishia bidhaa na mawasiliano kati ya nchi hizo, nchi za maziwa makuu na nchi za nje. Hivyo basi kipaumbele katika uendelezaji wa mitandao hii ni muhimu ili kunufaika na fursa tuliyonayo katika mtangamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nchi yetu kuitia mpango wa Kilimo Kwanza inayo fursa kubwa ya kuzalisha chakula na kuweza kutosheleza mahitaji ya chakula ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, utekelezaji wa mitandao ya miundombinu ya usafirishaji inayounganisha nchi yetu na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki utainufaisha nchi yetu kwa kusafirisha mazao hayo kwenda nchi nyingine wanachama wa Jumuiya na hivyo kuwawezesha Watanzania, hususan wakulima kuzitumia kikamilifu fursa za Kilimo katika Mtangamano wa Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtandao wa Reli, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimekamilisha maandalizi ya Mpango kabambe wa Maendeleo ya Reli wa Afrika Mashariki (*The EAC Railways Development Masterplan*) ambao umepitishwa mwaka 2009. Mtandao huu kwa upande wa Tanzania umeainisha njia zifuatazo: -

- (e) Liganga - Mchuchuma - Mtwara;
- (e) Mchuchuma - Mbambabay;
- (f) Liganga - Mlimba; Dar es Salaam - Mtwara;
- (g) Isaka - Kigali - Kabanga; Keza – Ruvubu – Gitega – Musongati;
- (h) Isaka - Kigali - Biharamulo - Bukoba - Masaka;
- (i) Tunduma- Sumbawanga- Mpanda - Kigoma;
- (j) Uvinza – Bujumbura; na
- (k) Mbegani (*Bagamoyo*) Port – *Kidomole*; na Tanga – Arusha – Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelezaji wa Mtandao wa Reli za Afrika Mashariki utasaidia Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupunguza gharama za kufanya biashara.

Hivyo kama njia mojawapo ya mkakati wa uendezaji wa reli, tarehe 11 na 12 Machi 2010, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki zilifanya Kongamano la Reli Jijini Dar es Salaam lililowashirikisha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Wabia wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lengo kuu la Kongamano hilo liliwa ni kuwakutanisha pamoja wadau wa reli na washirika wa maendeleo kuzungumzia namna ya kuboresha sekta hii Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano kuhusu kuunganisha reli kati ya Dar es Salaam na Isaka, na ujenzi wa reli ya Isaka-Kigali/Keza – Gitega – Musongati unaolenga kuziunganisha nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi na DRC na kuendeleza matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam yamekamilika. Aidha, upembuzi yakinifu wa mradi huu

umekamilika na hivi sasa mchakato wa kupata Washauri Elekezi kwa ajili ya Usanifu wa Kina, Meneja Mradi na Mkaguzi wa Mradi (*Project Auditor*) unaendelea kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali za Nchi Wanachama wa Jumuiya za Tanzania na Uganda zimekubaliana kushirikiana kujenga reli ya Tanga – Arusha-Musoma – *Port Bell/New Kampala*. Serikali hizi mbili zinatarajia kusaini hati ya makubaliano na kushirikiana katika kutafuta fedha za kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Usafiri wa Anga, Nchi wanachama zinatekeleza Itifaki ya kuanzisha Wakala wa Usimamizi wa Usalama wa Anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East Africa Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency-CASSOA*) tangu mwaka 2009. Katika kutekeleza Itifaki hii, Nchi Wanachama zinaendelea kuboresha usalama wa anga kulingana na viwango viliwyowekwa na Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri na Usalama wa Anga (*ICAO*); na zinaendelea kuwianisha kanuni za usalama wa anga za kimataifa (*East Africa Harmonized Safety and Security Aviation Regulations*) kulingana na viwango vya ICAO, baadhi ya kanuni zimekwishawianishwa na tayari zimeanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyolitaarifu Bunge lako Tukufu kuitia hotuba yangu ya bajeti ya 2009/2010, Nchi Wanachama kuitia CASSOA zimeanza kutumia mfumo wa gharama nafuu wa mawasiliano ya Anga (*Cheaper Navigation System*) unaotumia mfumo wa *Global Navigation Satellite System (GNSS)*. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika nchi yetu mfumo huu tayari unatumika katika viwanja vya Kimataifa vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam; na Kilimanjaro. Taratibu zinaendelea ili mfumo uweze kutumika katika viwanja vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Nchi Wanachama zinaendelea kuandaa mpango wa mafunzo ya pamoja ya marubani na waongoza ndege katika Nchi Wanachama ili kuendana na mabadiliko yanayotokea katika sekta ya usafiri wa anga duniani. Mafunzo haya yatawezesha kutoa leseni ya urubani ya Afrika Mashariki. Kwa upande wa Tanzania, jumla ya wataalam 43 wa masuala ya anga walipatiwa mafunzo katika maeneo ya ukaguzi na usalama wa anga, urubani na uongozaji ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama zimeanzisha mkakati wa maendeleo wa miaka kumi wa kuendeleza viwanja vya ndege viliwyopewa kipaumbele katika Jumuiya ili viwe vituo vya kimataifa na kikanda vya kuingilia na kutokea kwenye vivutio vya utalii kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa mtandao wa utalii katika Jumuiya.

Viwanja vya ndege vitakavyohusika katika mpango huu ni Arusha, Ziwa Manyara, Kigoma, Mafia na Loliondo. Katika mwaka 2009, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imekamilisha maandalizi ya upembuzi yakinifu na kuwasilisha katika Sekretariat ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa ajili ya kutafuta mshauri mwelekezi kwa usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Nishati, Kifungu Na. 43 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kinaainisha kuwa Serikali itachukua hatua zenye lengo la kuongeza upatikanaji wa nishati na hasa umeme, ili kuongeza uhakika wa upatikanaji, na usambazaji wake na kuwafikia wananchi wengi. Ushirikiano katika sekta ya nishati unalenga kuimarisha uwezo wa Nchi Wanachama kuzalisha na kusambaza umeme kwenye Kanda ya Afrika Mashariki.

Mheshimwia Spika, katika kutekeleza mpango huu mji wa mpakani wa Lungalunga nchini Kenya unapatiwa umeme kutoka mji wa Horohoro nchini Tanzania; mji wa Namanga nchini Tanzania unapatiwa umeme kutoka mji wa Namanga (Kenya). Aidha, Mkoa wa Kagera unapata umeme kutoka Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembizi yakinifu kwa ajili ya mradi wa kuupatia umeme mji wa Mutukula nchini Tanzania kutoka mji wa Mutukula nchini Uganda umekamilika. Vilevile Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea na mazungumzo kati yake na Serikali ya Uganda kuhusu mradi wa kuzalisha umeme wa Murongo/Kikagati (mpakani mwa Uganda na Tanzania) kwa lengo la kuwezesha uwezekaji unaotarajiwa kuzalisha umeme utakaoweza kusambazwa katika vijiji vilivypo katika mipaka hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na upungufu wa nishati ya umeme, Nchi za EAC na SADC zimekubaliana kuanzisha mpango wa kuunganisha umeme ambao unalenga kuunganisha mifumo ya kitaifa ya umeme ujulikanao kwa jina la *Southern Africa Power Pool*. Kwa kuanzia mpango huu utaunganisha nchi za Zambia, Tanzania, na Kenya ambapo Tanzania itapokea umeme wenye msongo wa 400 KV kutoka mji wa Pensulo nchini Zambia. Umeme utapita katika miji ya Mbeya, Iringa, Dodoma, Singida, Arusha na hatimaye mji wa Nairobi nchini Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mawasiliano, katika Kifungu cha 46 (d) cha Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 Serikali inaagizwa kuhakikisha kwamba inaongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo na kuanzisha mfuko maalum wenye lengo la kupeleka huduma za Simu na Internet hadi vijijini. Aidha, Kifungu cha 46(e) cha Ilani kinaielekeza Serikali kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano kikanda na kimataifa (*ICT hub through marine optic fibre system*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelekezo hayo ya Ilani ya Uchaguzi, Serikali na Nchi Wanachama zipo katika hatua za kuendeleza Mtandao wa Mawasiliano wa Jumuiya (*EAC Broadband Infrastructure Network*) ambapo zimekamilisha utafiti wa mtandao wa mawasiliano baina ya Nchi Wanachama. Kwa sasa Jumuiya inaendelea na juhudhi ya kutafuta rasilimali kwa ajili ya kutekeleza mtandao huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*The National ICT Backbone Infrastructure Network*) umeendelea kutekelezwa ambapo katika kipindi cha mwaka 2009/2010 Tanzania imetandaza mkongo

wenye urefu wa zaidi ya Kilometra 2000 na hivyo kuifanya Tanzania kuwa na mkongo wenye urefu wa kilometra zaidi ya 5000. Zoezi la kuufikisha Mkongo huo katika mipaka ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uko katika hatua za mwisho. Mipaka iliyofikiwa hadi sasa na mkongo huo ni Rusumo (Rwanda); Mtukula (Uganda); Kabanga (Burundi); na Namanga, Sirari na Horohoro (Kenya).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudini za kukamilisha kuunganisha nchi yetu na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tayari nchi yetu imeunganishwa na Mikongo ya Kimataifa ya baharini ya *SEACOM* na *EASSy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganishwa kwa Mtandao wa Mkongo wa Taifa na Mitandao ya Mikongo ya baharini ya *SEACOM* na *EASSy* ni fursa pekee ya kijiografia ambayo inaiwezesha nchi yetu kuwa kitovu na lango la mawasiliano kikanda na kimataifa na hivyo kufikia lengo letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Zanzibar, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2009/2010 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimeainisha Miradi itakayotafutiwa fedha kwa wafadhili kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa miradi minne kati ya miradi minane iliyoainishwa kutafutiwa wafadhili kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki imepewa kipaumbele, na tayari imeandalowiwa andiko na kufanyiwa usanifu na tathmini ya gharama za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizofikiwa kwa miradi hii iliyoainishwa ni kama ifuatavyo: -

(l) Mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika uwanja wa Ndege wa Zanzibar umepata ufadhili wa Benki ya Exim ya China;

(m) Mradi wa Uwanja wa ndege wa Karume Pemba ulipelekwa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na walishauri uingizwe katika miradi ya Kitaifa. Mradi huu umeshaingizwa katika miradi ya kipaumbele ya Kitaifa.

(n) Mradi wa The Wind Power Plants: Majadiliano yamekamilika na Jumuiya ya Afrika Mashariki imekubali kusaidia katika kufanya upembuzi yakinifu chini ya mpango wake wa Nishati Mbadala wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sekretarieti imekwisha wasilisha maombi ya fedha za upembuzi yakinifu chini ya mpango wake wa Nishati Mbadala wa Jumuiya ya Afrika kwa Washirika wa Maendeleo;

(o) Mradi wa Agriculture and Food Security: Jumuiya ya Afrika Mashariki itasaidia kufanya upembuzi yakinifu chini ya usimamizi wa EU (EDF). Sekretarieti inasubiri majibu kutoka EDF kuhusu ufadhili wa mradi huu;

(p) Mradi wa Uimarishaji wa Karantini za Mazao na Mifugo/Magonjwa ya Wanyama (*Animal Disease Free Zone*): Mradi huu uliwasilishwa katika Sekta husika na kufanikiwa kupewa gari moja (*Land Rover*) kwa ajili ya ukaguzi wa homa ya mafua ya ndege.

(q) Mradi wa the Establishment of East African Roll on Roll off Services between *Ports of Dar es Salaam/Zanzibar Town/Pemba/Mombasa* utaingizwa kwenye Mkakati unaoandaliwa wa uendelezaji wa usafirishaji na programu ya maendeleo katika sekta ya barabara. Mkakati huu unatarajiwaka kukamilika mwaka 2011.

(r) Mradi wa *Development of Zanzibar New Maruhubi Hub Port and Deep Sea Fishing Infrastructure – Dry Dock Construction* utaingizwa kwenye programu ya uendelezaji wa Bandari na usafiri Majini ambapo programu hiyo itajadiliwa kwenye kikao cha nane cha Baraza la Mawaziri la Sekta ya Usafiri, Mawasiliano na Hali ya Hewa mwezi Agusti, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Uzalishaji, Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao wa 11, uliofanyika tarehe 20 Novemba, 2009, mjini Arusha waliagiza uandaliwe mkutano kwa ajili ya kujadili mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula, lengo likiwa ni kukabiliana na upungufu wa chakula katika Nchi Wanachama, ikihusisha pia uwezekano wa kusafirisha chakula kutoka katika maeneo yenye ziada kwenda maeneo au Nchi Wanachama zenyepungufu wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maagizo haya Wizara iliratibu ukamilishwaji wa Mpangokazi wa Usalama wa Chakula wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sera ya Mabadiliko ya Tabianchi [*EAC Action Plan on Food Security and Climate Change Policy*]. Uwepo wa Mpango huu na utekelezaji kwa ufanisi kwa Sera ya Kilimo Kwanza kutaiwesha Tanzania kutumia vema nafasi yake ya kijiografia kuwa ghala na kitovu cha usalama wa chakula katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 35 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inaelekeza Serikali kuchukua hatua kuhakikisha kuwa Sekta ya Utalii inatoa mchango mkubwa katika uchumi wa nchi yetu na nchi za Afrika Mashariki kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendana na mahitaji ya Soko la Pamoja, sekta ya utalii imetakiwa kutoa nyota za viwango kwa mahoteli, nyumba za wageni na migahawa (*Classification of Accommodation, Establishments and Restaurants*).

Zoezi hilo kwa upande wa Tanzania limefanyika Dar es Salaam, Arusha, na sehemu ya Mkoa wa Pwani. Ili kuwa na nguvukazi ya kutosha katika kukamilisha zoezi hilo, imetayarishwa mitaala na wakufunzi wa kutoa mafunzo ya kufanikisha zoezi la kutathmini hoteli/mgahawa na kutoa nyota. Baraza la kisekta limeagiza mitaala hiyo ifanyiwe uhakiki ili iwe ya Jumuiya kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza kasi ya kukamilisha zoezi hilo, Jumuiya imetayarisha mitaala na wakufunzi wa kutoa mafunzo ya kufanikisha zoezi la kutathmini hoteli/mgahawa na kutoa nyota.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2005, hususan katika Kifungu cha 32(h) ambapo msisitizo umewekwa katika ubora wa mifugo na sio wingi, Serikali imeelekezwa kuchukua hatua za kuendeleza mikakati ya kukuza Sekta ya Mifugo kupitia ugani, tiba, kinga, usambazaji wa maji na uboreshaji wa malisho.

Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara yangu inaendelea kuratibu majadiliano na maandalizi ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Kusimamia Biashara na Viwango vya Ubora wa Mazao ya Wanyama na Mimea (*EAC Draft Protocol on Sanitary and Phyto Sanitary*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha ubora wa mifugo na kupambana na magonjwa ya mifugo, Nchi Wanachama zinatekeleza mradi wa kupambana na kuenea kwa magonjwa ya mafua ya ndege (Avian Influenza) na homa ya mapafu ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta za Huduma za jamii Sekta za Elimu, Utamaduni na Michezo, Afya na Sayansi, ushirikiano katika nyanja ya kijamii umejikita katika Elimu, Utamaduni na Michezo, Afya na Sayansi. Katika Sekta ya Elimu, Nchi Wanachama zinaendelea kukamilisha zoezi la kuwianisha mfumo na mitaala ya elimu.

Uwianisho huu ni muhimu kwani utawezesha kukamilisha maandalizi ya kanuni za uwianisho wa mitaala na utambuzi wa sifa za kitaalamu (*regulations for harmonization of curriculum and mutual recognition of academic qualification*) ambacho ni mionganini mwa viambatanisho wa Itifaki ya Soko la Pamoja ambavyo majadiliano yake yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatua hii ni muhimu katika utekelezaji wa Soko la Pamoja, hususan kwenye eneo la ajira kwani itawezesha Nchi Wanachama kuwa na vigezo sawa katika kutambua sifa za waombaji wa nafasi za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa ikishirikiana na Nchi Wanachama katika kuhakikisha kuwa wanafunzi wa Sekondari katika Jumuiya wanaielewa Jumuiya yao kwa kuwashirikisha katika mashindano ya kila mwaka ya uandishi wa Insha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwaka 2009/2010 maudhui ya mashindano ni ‘Ni kwa namna gani matumizi ya Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yatakavyoweza kuchochaea au kuhamasisha mchakato wa kuwaunganisha watu wa Afrika Mashariki’. Kwa sasa Nchi Wanachama zipo katika mchakato wa kukamilisha mashindano haya. Kupitia Bunge lako tukufu naomba niwasihii walimu na wanafunzi wa Tanzania kushiriki katika mashindano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara 117 ya Mkataba wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki inazitaka Nchi Wanachama kushirikiana katika masuala ya afya. Katika kutekeleza matakwa hayo, Nchi Wanachama zinaendelea na mipango ya pamoja ya kudhibiti magonjwa ya kuambukiza kwa binadamu na wanyama mipakani. Aidha, Nchi Wanachama zinaendelea na mchakato wa kuwianisha mifumo ya udhibiti wa ubora wa madawa kwa lengo la kufanikisha nia ya Nchi Wanachama ya kununua madawa kwa pamoja kwa jumla ili kurahisisha udhibiti na kupata bei nafuu kutokana na ununuzi wa jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania, kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inaendelea na mchakato wa kuridhia Itifaki ya Kamisheni ya Afya, ambayo ilipitishwa na mkutano kumi na saba wa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea na kuwianisha taaluma katika sekta ya afya. Katika kutekeleza hili, Nchi Wanachama zipo katika mchakato wa kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Kikanda ya Uwianishaji wa Taaluma ya Waugazi na Wakunga (*Regional Guidelines for Harmonization of Nursing and Midwifery Education and Practice in the East African Community Partner States*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Masuala ya Jinsia, Watoto na Maendeleo ya Jamii, kwa kipindi kirefu kumekuwepo na juhudzi za makusudi za kuwafanya watu wenye mahitaji maalum kushirikishwa katika shughuli mbalimbali za Jumuiya. Jumuiya iliandaa mkutano uliowakutanisha watendaji, watu wenye ulemavu na Wabunge wa Jumuiya uliofanyika Jijini Kampala, Uganda tarehe 19 - 20 Februari, 2010. Katika mkutano huo, ilikubalika kuwa masuala ya watu wenye mahitaji maalumu (*People with Disabilities*) yapewe kipaumbele katika Mtangamano wa Afrika Mashariki. Ilipendekezwa kuwa Jumuiya iandae Sera ya Afrika Mashariki ya watu wenye mahitaji maalumu (*EAC Policy on Persons with Disabilities*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya inaendelea na maandalizi ya Mkakati wa miaka minne wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii. Rasimu ya Mkakati huu imekwishaandalishi na taratibu za kukamilisha mkakati huu zinaendelea.

Mradi wa Mazingira na Matumizi Endelevu ya Ziwa Victoria (LVEMP II)- 2/6/2010

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya imeanza kutekeleza mradi wa usimamizi mazingira ya Ziwa Victoria Awamu ya Pili (*Lake Victoria Environment Management Programme - LVEMP II*). Hati ya Makubaliano kwa ajili ya mradi huu ilitiwa sahihi tarehe 22 Mei, 2009 kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia.

Awamu hii ya pili ya Mradi itatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na inalenga kuimarisha mfumo wa utendaji kwa kujenga uwezo wa usimamizi wa *Programu (Strengthening Institutional capacity for managing the program)*; kuthibiti uchafuzi wa

udongo; kuhifadhi na kusimamia vyanzo vya maji; na kuboresha maisha ya jamii inayolizunguka eneo la Mradi. Jumla ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya mradi ni Dola za Kimarekani 90.0 milioni ambapo mgawanyo kwa kila Nchi Mwanachama ni kama ifuatavyo: Kenya Dola 27.5 milioni, Uganda Dola 30.0 milioni na Tanzania Dola 32.5 milioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa shughuli za mradi huu zilizokwishafanyika ni pamoja na: kuanzisha ofisi ya kuratibu mradi; kutambulisha malengo na shughuli za mradi kwa wadau mbalimbali, kutoa elimu na semina kwa vyombo vya habari; kuboreshaji uwezo wa taasisi zinazosimamia raslimali za maji na uvuvi katika Ziwa Victoria; kuanza maandalizi ya kuhuisha sera, sheria na kanuni zinazosimamia uendelezaji wa bonde la Ziwa Victoria baina ya Nchi Wanachama; kutoa mafunzo ya ukusanyaji taarifa za awali kuhusu sekta zote saba za Mradi, ambapo zoezi la kukusanya takwimu za awali (*Baseline study*) linaendelea; ufuutiliaji wa ubora wa maji katika Ziwa Victoria na kuweka takwimu kwenye *Database* kwa ajili ya uchambuzi na kuainisha maeneo ya kufanya utafiti. Utafiti huo unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Julai 2010; kukamilisha maandalizi ya mpango wa kukarabati maabara ya maji ya Bukoba unaotegemewa kuanza Julai, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Siasa, Ulinzi na Usalama, Kifungu cha 107 cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kinaelekeza Serikali kuchukua hatua za kuendelea kufuata Katiba ya nchi, sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kidemokrasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza agizo hili, Serikali na Nchi Wanachama zimekubaliana kuunda Itifaki ya Utawala Bora ya Jumuiya. Itifaki hii itachukua nafasi ya Mfumo wa Utawala Bora wa Jumuiya uliokubalika hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuratibu na kusimamia maandalizi ya Itifaki ya Utawala Bora ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Itifaki hiyo inajengwa kwa kuzingatia nguzo kuu tano za Utawala Bora ambazo ni: Kuheshimu Katiba; Utawala wa Sheria na haki za kisheria; Kulinda na Kudumisha Haki za Binadamu na kutoa fursa sawa kwa wote; Mfumo wa Kupambana na Rushwa na Kuheshimu Maadili na Mgawanyo wa Mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 110 (b) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 inaielekeza Serikali kuchukua hatua katika kupambana na rushwa kwa kujenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa wananchi uwezo, ari na ujasiri zaidi katika kupambana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma. Katika kutekeleza azma hii, Wizara imeratibu na kushiriki katika kukamilisha majadiliano ya uundaji wa Itifaki ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Itifaki hii inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao kijacho cha Baraza la Mawaziri wa Jumuiya kwa ajili ya kuisaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuratibu na kusimamia Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama zimekamilisha majadiliano ya uundaji wa Itifaki ya Uratibu wa Sera za *Nje* (*EAC Protocol on Foreign Policy Coordination*).

Itifaki hii itaziwezesha Nchi Wanachama kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na nchi nyingine duniani kwa kuwezesha balozi za Nchi Wanachama kutoa huduma za kibalozi pale ambapo nchi nyingine mwanachama haina huduma hizo kama itakavyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Nchi Wanachama kupata nafasi za uwakilishi katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa, na pia wananchi kutoka nchi za Afrika Mashariki kupata ajira katika Taasisi na Mashirika ya Jumuiya za Kimataifa, Nchi Wanachama zinaendelea kushirikiana kuwaunga mkono wananchi kutoka Nchi Wanachama wanaowania nafasi za ajira katika Mashirika na Taasisi za Kimataifa. Makubaliano hayo yamewesha Nchi Wanachama kupata nafasi za uwakilishi kama ifuatavyo: Tanzania International *Oceanographic Commission* na nchi ya Uganda imepata *International Civil Aviation Organization International Hydrological Programme*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu huu umewevesha jumla ya wananchi 13 kutoka Nchi Wanachama kupata nafasi za ajira katika Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa kwa kipindi cha kuanzia mwezi Agosti, 2009 hadi kufikia mwezi Juni, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kuendelea kutoa rai kupitia Bunge lako Tukufu kwa Watanzania wanaoomba nafasi za kazi kwenye Taasisi na Mashirika ya Kimataifa kuwasilisha majina yao kwenye Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili tuweze kushauriana kwa lengo la kuungwa mkono na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Kifungu cha 125 unahimiza ushirikiano wa karibu katika masuala ya ulinzi na usalama. Ili kutekeleza kifungu hiki Nchi Wanachama wa Jumuiya, mnamo mwaka 2001, zilisaini Hati ya Makubaliano ya Ushirikiano katika nyanja ya Ulinzi (*Memorandum of Understanding on Cooperation in Defence*). Katika kutekeleza hati hii ya makubaliano, pamoja na masuala mengine, Nchi Wanachama zimekubaliana kuwa na mazoezi ya pamoja ya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 majeshi ya Nchi Wanachama yameendesha mazoezi mawili ya pamoja ambayo yalibeba dhima za: huduma za kibinadamu (*humanitarian Mission*); majanga (natural disasters); shughuli za

misafara (*convoy operations*); udhibiti wa halaiki (*crowd control*); kuhifadhi silaha (*weapon handling*); na vizuizi vya magari (*vehicle checkpoints*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kwanza lilijulikana kama Exercise Mlima Kilimanjaro na lilifanyika mwezi Septemba 2009 katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga hapa nchini Tanzania. Zoezi la pili lilijulikana kama *Exercise Natural Fire 10* na lilifanyika Kitgum, Uganda mwezi Oktoba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Kifungu cha 111(d) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kinachohimiza kuongeza uwezo wa Taifa wa kupambana na ujambazi na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa kupambana na kuzagaa kwa silaha haramu ndogo ndogo na za kati. Mradi huu, unaoghamariwa na Shirika la Misaada ya Ujerumani (GTZ), unashughulika na kukusanya na kuharibu silaha haramu ndogo na nyepesi; kuhuisha sheria za umiliki wa silaha ndogo ndogo na nyepesi mionganii mwa Nchi Wanachama; kuzijengea uwezo kiutendaji ofisi za madawati simamizi (*National Focal Persons*); na kuelimisha wananchi juu ya madhara ya silaha ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mradi huu tarehe 25 Mei 2010 jumla ya silaha ndogo ndogo 2,600 zilizokusanywa katika Mikoa ya Kigoma na Kagera na kuharibiwa mjini Bukoba katika zoezi lililoshuhudiwa na viongozi wa Serikali, wananchi na wadau wengine. Silaha hizi ni zile zilizokusanywa na zilizosalimishwa kwa hiari kutoka kwa wananchi na wakimbizi waliokuwa kwenye makambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutambua na kudhibiti chanzo cha kusambaa kwa silaha ndogo ndogo na za kati katika Jumuiya, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanza zoezi la kuweka alama silaha. Tayari Nchi Wanachama zimepatiwa vifaa vya kusaidia kutekeleza zoezi hili. Kwa upande wa nchi yetu, zoezi hili limekwishaanza na linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005 katika Vifungu 113 na 114 inaielekeza Serikali kuchukua hatua za kujenga uwezo wa kudhibiti na kukabiliana na majanga makubwa kama Tsunami, tetemeko la ardhi, tufani, mvua za kimbunga, mafuriko, na ukame mkubwa. Kwa kutambua gharama na hasara kubwa zitokanazo na majanga ya aina hii, Nchi Wanachama zilikubaliana kuunda Mfumo wa Kupashana Habari za Tahadhari za Majanga wa Jumuiya (*EAC Early Warning Mechanism*).

Wizara inaratibu na kushiriki katika majadiliano ya kuunda mfumo huo. Rasimu ya mfumo huu imekamilika na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi ili uanze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa umma ili kujenga uelewa na kuimarisha ushiriki wa Watanzania katika masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, na hivyo kuwawezesha kunufaika na fursa zilizopo katika Jumuiya, Wizara imeandaa Mpango Kabambe wa Elimu kwa Umma, ambao ulizinduliwa mwezi Mei 2010. Kulingana na mpango huu, elimu itatolewa kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na

vipindi vya redio, runinga, makala, machapisho, semina, mikutano, mabango, na makongamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza mpango huo, Wizara imetoa elimu kwa umma sehemu mbali mbali za Tanzania Bara na Zanzibar kwa lengo la kuelimisha kuhusu hatua zinazofikiwa katika kuendeleza Mtangamano wa Jumuiya, fursa na changamoto zilizopo pamoja na maamuzi mbali mbali yanayofikiwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Machi, 2010 Wizara iliendesha semina mjini Dodoma kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya, kwa lengo la kutoa elimu, na kuunda mfumo wa ushirikiano baina ya Wizara na TAMISEMI. Mfumo husika utakaowezesha Wizara kuzitumia Sektretarieti za Mikoa na Halmashauri katika kutoa elimu kwa umma katika maeneo yao. Utaratibu huu utajenga mfumo endelevu wa kutoa Elimu kwa Umma ambapo wataalamu mahsuswi watakaoteuliwa toka katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri watakuwa viungo baina ya Wizara na Maeneo yao. Wataalamu watapatiwa elimu ili waitumie katika kutoa elimu kwa umma katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2010 Wizara ilitoa elimu kwa Makatibu Wakuu na Makatibu Tawala wa Mikoa, huko Dodoma. Aidha, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kama vile Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wafanyabiashara, viongozi na watendaji mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya warsha na semina katika mikoa ya Kigoma, Mwanza, Kagera, Dodoma, Shinyanga, Tabora, Kilimanjaro, Iringa, Morogoro, Rukwa, Mbeya, Ruvuma; na mikoa yote ya Zanzibar. Aidha, Wizara imefanya ziara katika mipaka ya Namanga, Sirari, Holili, Holoholo, na Mtukula kwa lengo la kuwaelimisha wananchi na watendaji kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na fursa zitokanazo na Mtangamano. Semina na ziara hizi zimevezesha pia kutambua changamoto zilizopo na kuandaa mikakati ya kupambana na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Agosti 2009, Wizara ilishiriki katika maonyesho ya Nanenane yaliyofanyika kitaifa mjini Dodoma na kuweza kutumia fursa hiyo kuelimisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maonyesho ya Nguvu kazi na Jua kali, kifungu cha 50(e) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kinabainisha kuwa Serikali itawawezesha wananchi kiuchumi ikiwa ni pamoja na kukuza ujasiri amali. Ilani inaelekeza Serikali kubuni mipango ya kuwapa fursa wajasiri amali Watanzania wanaoinukia. Katika kutekeleza hilo, Wizara imeendelea kuratibu maonyesho ya Jua kali/Nguvu kazi ambayo hufanyika kila mwaka kwa mzunguko katika Nchi Wanachama. Maonyesho hayo huwashirikisha wafanyabishara ndogo ndogo kutoka Nchi Wanachama na kutoa fursa ya kubadilishana uzoefu wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2009 maonyesho hayo yalifanyika mara mbili, jijini Dar es Salaam ikiwa ni utaratibu wa kawaida na pia mjini Arusha ikiwa ni sehemu ya maadhisho ya miaka kumi ya Jumuiya. Katika Maonyesho hayo Wajasiriamali walipata fursa ya kupata soko la bidhaa zao kama nguo za batiki, vinyago, vyakula vilivyosindikwa, asali, bidhaa za ngozi, madawa yatokanayo na miti shamba, vifaa vya ujenzi na bidhaa zilizotengenezwa kwa vyuma kama majiko ya kuokea mikate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko Wa Maendeleo Wa Afrika Ya Mashariki (*Eac Development Fund*), kulingana na Ibara 87 ya Mkataba ya Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na maamuzi ya Baraza la Mawaziri katika Mkutano wao wa kumi, Nchi Wanachama zimekubaliana kuanzisha Mfuko wa Maendeleo wa Afrika ya Mashariki (*EAC Development Fund*). Lengo la Mfuko huu ni kugharamia programu na miradi ya maendeleo ya kikanda, hususan miradi ya kuendeleza miundombinu. Rasimu za Sera na Itifaki za kuanzisha mfuko huu zimekamilika na majadiliano yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kulingana na aya ya 136(i) ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Makao Makuu ya Jumuiya yatajengwa mjini Arusha, Tanzania. Wizara imendelea kusimamia kwa karibu ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kulingana na maamuzi haya. Usimamizi huu wa karibu umewezesha kukamilishwa taratibu zote za maandalizi, ikiwa ni pamoja na upembuzi yakinifu, kumpata mkandarasi, na kupata raslimali zinazohitajika. Kufuatia kukamilishwa kwa hatua hizi za maandalizi, Wakuu wa Nchi Wanachama waliweka jiwe la msingi la Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya mwezi Novemba, 2009. Kwa sasa ujenzi unaendelea vizuri. Inatarajiwa kuwa ujenzi utakamilika ifikapo Februari, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Pinda (Mb), alitembelea ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya tarehe 31 Mei, 2010. Ninaomba kuchukua fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kutembelea ujenzi huu, kwani ziara hiyo imethibitisha dhamira ya Serikali katika kuendeleza mtangamano wa Afrika ya Mashariki na imetoe hamasa katika kasi ya ujenzi wa Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhisho ya Miaka Kumi ya Jumuiya, Jumuiya Afrika Mashariki ilishereheke kutimiza miaka kumi ya Jumuiya mwezi Novemba, 2009. Wizara iliratibu maadhisho hayo ya miaka kumi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyofanyika tarehe 20 Novemba, 2009 mjini Arusha. Katika maadhisho hayo, pamoja na mambo mengine Wakuu wa Nchi waliweza kuweka jiwe la msingi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya Afrika Mashariki, na kuweka saini Itifaki ya Soko la Pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Afrika Mashariki kwa mujibu wa Ibara ya 23 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya

Afrika Mashariki ni chombo chenye mamlaka ya kuhakikisha kuwa Mkataba wa Jumuiya unazingatiwa kwa ukamilifu na kutoa tafsiri sahihi juu ya utekelezaji wa Mkataba huo pale inapohitajika. Mahakama hiyo imegawanyika katika vitengo viwili:

Kitengo cha Awali (*First Instance Division*), na Kitengo cha Rufaa (*Appellate Division*). Kila Kitengo cha Mahakama kina Majaji watano (5) ambapo kila Nchi Mwanachama ina Jaji mmoja katika kila kitengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa mujibu wa Ibara ya 27 ya Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mahakama ya Afrika Mashariki ina mamlaka ya kutoa ushauri (*Advisory Opinion*) kwa Jumuiya juu ya tafsiri na matumizi sahihi ya Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; kutatua migogoro ya kikazi baina ya Jumuiya na waajiriwa wake; kusuluuhisha migogoro kwenye Mikataba inayohusisha Jumuiya au Taasisi zake; na pia kusuluuhisha migogoro inayotokana na kipengele cha usuluhishi (*Arbitration Clause*) kinachoipa mamlaka Mahakama kusuluuhisha migogoro kwenye Mikataba ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2009/10 Mahakama ya Afrika Mashariki imeweza kutoa maamuzi katika kesi saba (7) kama inavyoonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la Afrika Mashariki kwa mujibu wa Ibara ya 49 ya Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Afrika Mashariki ni chombo cha Jumuiya ambacho majukumu yake makuu ni pamoja na; kutunga sheria za Jumuiya; na kujadili na kupitisha Bajeti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza jukumu la kutunga sheria za Jumuiya, Bunge la Afrika Mashariki katika mwaka 2009/2010 lilijadili na kupitisha Miswada Sita kama inavyoonyeshwa katika Kiambatanisho Na. 8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Bunge la Afrika Mashariki lilijadili na kupitisha Maazimio yafuatayo: Utekelezaji wa Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu haki za watu wenye mahitaji maalum; Uanzishaji wa Mamlaka ya Reli ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; Kupinga ukeketaji wa wanawake; kuipongeza Tanzania kwa kuwapa uraia Warundi 162,000; na Azimio la Kuunda Mfumo wa kisheria wa kuhakikisha Usalama wa Chakula na Mabadiliko ya Tabianchi katika Jumuiya. Aidha, Waheshimiwa Wabunge walipitisha hoja ya kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya kwa Hotuba yake nzuri kwenye Bunge la Afrika Mashariki iliyotoa mwongozo katika uendelezaji wa mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya katika kutekeleza majukumu yao ya kuendeleza na kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka, Utawala na Maendeleo ya Raslimali Watu ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kikamilifu, Mwezi Januari mwaka 2009 ilifanya marekebisho ya muundo kwa kuunda Idara za Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii; na Idara ya Siasa, Ulinzi na

Usalama, kila Idara ikiwa na Mkurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi wawili. Aidha, Idara ya Uwekezaji, Biashara, na Sekta za Uzalishaji iliboreshawa kwa kuongezewa nafasi za Wakurugenzi Wasaidizi wawili. Muundo huu mpya wa Wizara uliidhinishwa na Serikali mwezi Januari, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mabadiliko hayo Muundo mpya wa Wizara una Idara tano (5) ambazo ni Biashara, Uwekezaji na Sekta za uzalishaji; Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Kijamii; Siasa, Ulinzi na Usalama; Sera na Mipango; na Utawala na Rasilimali Watu. Aidha, muundo wa Wizara unajumuisha Vitengo sita ambavyo ni Sheria; Uhasibu na Fedha; Ukaguzi wa Ndani; Ununuzi; Habari, Elimu na Mawasiliano; na Usimamizi wa Mifumo ya Kompyuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia marekebisho ya muundo wa Wizara, katika Mwaka 2009/2010 Wizara imejaza nafasi tatu (3) za Wakurugenzi, nafasi sita (6) za Wakurugenzi Wasaidizi, na nafasi mbili (2) za Wakuu wa Vitengo. Aidha, Wizara iliajiri watumishi wapya kumi na moja (11) ikiwa ni katika kada za Mtafiti Daraja la II, Afisa Tawala Daraja la II, Msaidizi wa Kumbukumbu, Katibu Mahsusii Daraja la III, Mhasibu Daraja la II, Dereva Daraja la II na Afisa Usafirishaji Daraja la II.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 watumishi watatu (3) walipandishwa vyeo na vilevile watumishi ishirini na tano (25) walithibitishwa kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga na kuimarisha uwezo wa watumishi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu, Wizara imeandaa mpango wa mafunzo. Kulingana na Mpango huo jumla ya watumishi 40 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika mwaka wa fedha 2009/2010. Mafunzo yaliyotolewa kwa watumishi hao ni katika nyanja za biashara ya kimataifa, uchambuzi sera, uongozi, menejimenti, majadiliano, uchumi, uhasibu, ununuzi, ugavi, ukatibu muhtasi, ukutubi na fani nyingine za utoaji huduma. Aidha, mafunzo ya Utunzaji wa kumbukumbu yametolewa mwezi Mei, 2009 kwa watumishi wa kada za wasaidizi wa kumbukumbu, makatibu muhtasi, pamoja na wasaidizi wa Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Januari, 2010 Wizara kupitia Chuo cha Eastern and Southern African Management Institute (ESAMI) iliandaa mafunzo ya majadiliano (*Negotiation Skills*) na mafunzo ya kuongoza mikutano kwa watumishi waandamizi wa Wizara na sekta mbalimbali nichini. Lengo ikiwa ni kuwajengea uwezo wa majadiliano ya kikanda na kimataifa, na kujipanga katika kipindi cha uenyekiti wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Zoezi hili lilihusisha watumishi Arobaini (40) kutoka Wizara na Idara mbalimbali na watumishi tisa (9) walitoka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza jukumu la kuboresha utoaji wa huduma mbalimbali Wizara ilikamilisha Mkataba wa Huduma Bora kwa Mteja ambao ulizinduliu rasmi Januari, 2010. Mkataba huo unaainisha ahadi za Wizara katika kutoa huduma bora kwa wadau wa ndani ya Wizara na wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoahidi katika hotuba yangu ya bajeti iliyopita, ili kusimamia mwenendo wa maadili ya watumishi wa Umma, Wizara imeunda Kamati ya Maadili ambapo katika mwaka 2009/2010 Wajumbe wa Kamati walipewa mafunzo ya maadili. Aidha, inatarajiwa kuwa mafunzo kama hayo yatafanywa kwa watumishi wote kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la Mfumo wa wazi wa mapitio ya tathmini ya utendaji kazi (MWAMTUKA) au *OPRAS* ni agizo muhimu linalogusa utendaji katika utumishi wa Umma. Wizara imeendesha semina ya mafunzo kwa watumishi kuhusu namna ya kupanga malengo yanayopimika (*OPRAS*) na kuyawianisha na Mpango Mkakati wa Wizara. Wizara inatarajia kuanza kutumia Mpango wa *OPRAS* katika mwaka huu wa fedha (2010/2011).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha huduma za mawasiliano, Wizara inaendelea na maandalizi ya mpango Mkakati wa Matumizi ya Teknohana na ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Sera ya Mawasiliano ya Wizara (MEAC ICT Policy). Mpango Mkakati na Sera hii vinatarajia kukamilika na kuanza kutumika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupambana na maambukizi ya virusi vya ukimwi, katika mwaka 2009/2010 Wizara katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kupambana na janga la UKIMWI, iliendesha mafunzo kwa watumishi kuhusu kupima kwa hiari na namna ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI ambapo watumishi 47 walipima afya zao kwa hiari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa mapato na matumizi Wizara imeendelea kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika mapato na matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Fedha za Umma. Aidha, Wizara imejizatiti katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ili kuhakikisha kwamba malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. Hii ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zilizoidhinishwa katika bajeti zinatumika kwa kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mwaka 2008/2009 kutohakikisha kwamba fedha zilizoidhinishwa katika bajeti zinatumika kwa kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kifungu cha 110(d) cha Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 kinalekeza Serikali kuzidi kuziba mianya ya rushwa katika utendaji wake. Katika kutekeleza hili, Wizara imeendelea kusimamia manunuvi kwa kuzingatia Sheria ya Manunuvi Na. 21 ya mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2009/2010 Wizara iliandaa mpango kazi wa manunuvi wa mwaka, mikataba ya manunuvi, daftari la mali ya serikali, kufanya manunuvi ya vifaa na utoaji huduma na kutambua vifaa chakavu na kuviondosha

katika daftari la Serikali, kama ilivyo katika Sheria ya Manunuzi ya Umma Na. 21 ya mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya ununuzi na ugavi ni moja ya maeneo yanayotumia fedha nyingi za Serikali. Hivyo Wizara imeendelea kujenga uwezo katika eneo hili, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa Kamati ya Zabuni ya Wizara ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Mwezi Novemba, 2009 wajumbe wa Bodi ya Ununuzi ya Wizara (MTB) pamoja na watumishi sita (6) kutoka Kitengo cha Uhasibu, Sheria ya Ukaguzi wa Ndani walipatiwa Mafunzo ya Sheria ya Ununuzi. Mafunzo hayo yalitolewa na Mamlaka ya Rufaa ya Manunuzi (*Public Procurement Appeals Authority (PPAA)*). Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/10 watumishi wawili katika kitengo cha ugavi wamepata mafunzo katika Chuo cha ESAMI kuhusu usimamizi wa mikataba ya manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imeendelea kutekeleza maagizo ya Wakuu wa Nchi Wanachama kuhusu kulipa kwa wakati michango ya nchi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010, Mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ulikuwa shilingi 7,847,000,000/=. Mchango huu umekwishalipwa kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kimeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kupanuka kwa Muundo na kuongezeka kwa majukumu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kiasi cha mchango wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kimeongezeka toka shilingi 7,847,000,000/= mwaka wa fedha wa 2009/2010 hadi shilingi 8,613,743,600/ katika mwaka wa fedha 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika mwaka wa fedha 2009/2010, zipo changamoto ambazo Wizara ilikabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano ya kisekta, na utekelezaji wa miradi na programu za Jumuiya ni jukumu la sekta husika. Changamoto iliyopo ni Sekta husika kuhuisha na kukasimia masuala ya Jumuiya katika mipango ya Sekta husika. Kwa kuwa uelewa kuhusu masuala ya Jumuiya bado ni mdogo, wadau hufikiria kuwa shughuli zote za Jumuiya zinasimamiwa na kutekelezwa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki na hivyo kutoweka shughuli za Jumuiya katika mipango yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii, utekelezaji wa masuala ya kisekta hulegalega kutokana na kutohuishwa katika mipango ya kisekta na kutengewa fedha ipasavyo, na hivyo kutosimamiwa kikamilifu na sekta husika kama inavyotarajiwa. Hii ni changamoto kubwa kwa Wizara ambayo inalo jukumu la uratibu wa masuala ya Jumuiya kwa ujumla ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa maamuzi, miradi na program mbalimbali za Jumuiya zinatekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Tanzania katika shughuli za mtangamano unaowawezesha Watanzania kulinda maslahi ya Tanzania, na kunufaika na fursa zitokanazo na mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unategemea sana uelewa walio nao. Changamoto kubwa ni kuwawezesha Watanzania kuelewa na kupanua elimu waliyo nayo kuhusu mtangamano wa Afrika ya Mashariki ikiwa ni pamoja na fursa zilizopo na jinsi ya kuzitumia, lakini pia kuhusu changamoto zilizopo na jinsi ya kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na Aya ya tano wa Mkataba ya Uanzishwaji kwa Jumuiya, mtangamano wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki utatekelezwa hatua kwa hatua. Maandalizi ya hatua ya pili ambayo ni Soko la Pamoja yamekamilika, na maandalizi ya hatua ya tatu ambayo ni Sarafu Moja yameanza. Kila hatua huongeza fursa ikiwa ni pamoja na fursa za kiuchumi (soko, biashara, ajira, uwekezaji), na kijamii. Aidha, hatua hizi huongeza changamoto kwa Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii, changamoto katika utekelezaji wa hatua hizi ni upatikanaji wa raslimali za kutosha kukabiliana na ongezeko la majukumu, ikiwa ni pamoja na kuandaa mikakati endelevu ya kuliwezesha Taifa kunufaika ipasavyo. Dhana ya kupanuka kwa majukumu na umuhimu wa kujipanga na kuweka mikakati madhubuti kwa kila hatua na umuhimu wa kuongeza raslimali kulingana na hatua za mtangamano haijalewaka ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikilinganishwa na Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya, Tanzania imejaliwa kuwa na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo na kuweza kuwa mzalishaji na mlishaji wa Jumuiya. Changamoto iliyopo ni kuhakikisha kuwa tunatekeleza vema sera ya Kilimo Kwanza ili kutuwezesha kuwa ghala na kitovu cha usalama wa chakula katika Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jiografia Tanzania inayo kila nafasi ya kuwa kitovu cha usafirishaji. Changamoto ni kujipanga kimkakati kwa kuimarisha miundombinu, hususan barabara, reli na bandari ili kutumia fursa hii ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiforodha, (*Non Tariff Barriers – NTB*) vimeendelea kuwa changamoto katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha. Naendelea kutoa wito kwa wafanyabishara wote kuwasilisha malalamiko yatokanayo na vikwazo visivyo vya forodha ili Wizara iweze kuchukua hatua husika na hivyo kuwawezesha wafanyabishara wetu kunufaika kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto zilizobainishwa hapo juu, Wizara imeandaa mikakati ya kukabiliana nazo kama ifuatavyo:

- (a) Wizara imeendelea kuzishirikisha sekta mbalimbali katika mtangamano na katika kuchambua masuala yahusuyo Jumuiya;
- (b) Wizara imeendelea kufanya tafiti na chambuzi mbalimbali ili kuainisha fursa za mtangamano na kuandaa mikakati;

- (c) Wizara inaandaa vikao vya maandalizi ya wadau kabla na baada ya vikao vya Jumuiya ili kuweza kujipanga na kuhakikisha kuwa maslahi ya Taifa yanalindwa, na kuwezesha maamuzi yaliyofikiwa na Jumuiya yanatekelezwa kwa wakati kama ilivyopangwa;
- (d) Serikali imeunda Timu ya Kitaifa ikihusisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yenyeye jukumu la kuainisha na kutoa ushauri kuhusu vipaumbele vya kitaifa katika mtangamano, na kufuatilia utekelezaji wake;
- (e) Wizara imeandaa mpango endelevu wa kutoa habari na Elimu kwa Umma, na Mkakati wa Utekelezaji wa Soko la Pamoja; na
- (f) Wizara imeandaa Mpango Endelevu wa mafunzo utakaowezesha kujenga uwezo wa watumishi na kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau mbalimbali itaendelea kutekeleza majukumu yake katika mwaka 2010/2011 kwenye maeneo ya kipaumbele kama ifuatavyo:-

- (a) Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtangamano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Mkakati wa Utekelezaji wa Sera hiyo;
- (b) Kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja na kuanza utekelezaji wa mkakati huo;
- (c) Kuongoza na kuratibu majadiliano ya uanzishwaji wa Sarafu Moja ya Afrika Mashariki;
- (d) Kuratibu zoezi la kuwianisha sheria, kanuni na taratibu zilizopo nchini ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja;
- (e) Kuratibu utekelezaji wa Mitando ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Jumuiya (Barabara, Reli, Mkongo wa Taifa, na Mpango wa Uzalishaji na Usambazaji wa Nishati);
- (f) Kuratibu utekelezaji wa Programu za kisekta, katika sekta za kiuchumi na kijamii;
- (g) Kuratibu maandalizi ya Itifaki na sheria mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Itifaki ya uanzishwaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Afrika Mashariki (*East African Development Fund*), Itifaki ya Ulinzi; na Itifaki ya Amani na Usalama;
- (h) Kuratibu ukamilishaji wa uanzishwaji ukanda huru wa kibiashara wa kikanda kati ya EAC-SADC-COMESA (*Roadmap for the EAC-SADC-COMESA Tripartite Free Trade Area*);

- (i) Kutekeleza Mpango Kabambe wa Kutoa Elimu kwa Umma;
- (j) Kukamilisha uchambuzi wa changamoto za uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa; na
- (k) Kujenga uwezo wa Wizara kiutendaji ikiwa ni pamoja na kununua vitendea kazi na kutoa mafunzo kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi Ya Fedha Kwa Mwaka 2010/2011 ili Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki iweze kutekeleza majukumu na malengo yake kwa mwaka 2010/2011, naomba sasa nitoe hoja kuwa Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 13,088,958,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizo shilingi 12,324,182,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), shilingi 764,776,000/= na ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi (PE).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.meac.go.tz.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii nimeambatanisha majedwali mbalimbali. Naomba viambatanisho hivyo vichukuliwe kama vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011
Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa**

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:
Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyotolewa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili la Awamu ya Nne kwa umahiri mkubwa na hivyo kuliwezesha kuwa chombo tegemeo la wananchi katika kutetea maslahi ya Taifa lao. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa mchango mkubwa walioutoa katika kuishauri Serikali kwa kipindi hiki cha miaka mitano ya kwanza ya Bunge la Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri wa Serikali ya Awamu ya Nne. Chini ya uongozi wake Taifa letu limeendelea kupata heshima kubwa katika nyanja za uchumi, siasa, jamii na diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashukuru pia Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda (Mb.) na Waziri wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Mustafa Mkulo (Mb.), kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa mwongozzo wa masuala muhimu ya Taifa yakiwemo yanayoihusu Wizara yangu.

Halikadhalika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, chini ya uongozi madhubuti wa Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa ushauri wao mzuri waliokuwa wakiutoa mara kwa mara kwa Wizara yangu. Kamati hii imetoa mchango mkubwa sana katika kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufasaha na ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru viongozi wenzangu na wafanyakazi wote ninaoshirikiana nao Wizarani na kwenye Balozi zetu nje kwa utendaji wao mzuri wa kila siku.

Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi (Mb.), Katibu Mkuu, Ndugu Sazi Salula, Wakurugenzi na Mabalozi wetu walioko nchi za nje kwa kukamilisha bajeti hii kwa ubora na kwa wakati. Vilevile nawashukuru kwa kazi nzuri na ya kizalendo ya kutetea maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, familia yangu nayo imeendelea kuwa muhimili mkubwa kwangu. Kwa kunivumilia kwa kutokuwa na nayo karibu kwa muda mwingi kutokana na majukumu yangu jimboni na duniani. Napenda kwa namna ya pekee nimshukuru Mke wangu Dokasi Membe kwa wanangu Cecilia, Richard na Denis kwa upendo na uelewa wao nawashukuru sana. (*Makofî*)

Napenda pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mtama na hasa ujumbe uliofika leo wa kikosi cha kazi kwa upendo wao mkubwa kwangu na kwa moyo wao na kwa kunishauri na kwa kuniomba tena nigombee Ubunge katika kipindi hiki.

Ninaahidi kuendelea kuwatumikia kwa ari zaidi, kasi zaidi na nguvu zaidi iwapo nitapata nafasi tena katika kipindi hiki tulichonacho. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niungane na Wabunge wenzangu kutoa mkono wa pole na rambirambi kwako na kwa familia ya marehemu Mbunge mwenzetu Sigifrid Seleman Ng'itu aliyekuwa Mbunge wa Ruangwa, aliyefariki dunia katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010. Tuendelee kumuombea marehemu ili Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho, nitumie nafasi hii pia kuagana na Waheshimiwa Wabunge wenzetu na kuwatakia kila la heri katika harakati zao za kutetea Majimbo yao likiwemo la kwangu. Inshaalah Mwenyezi Mungu akitupa uhai na ikiwapendeza wapiga kura wetu tutakutana tena mwezi Novemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja ya nchi 189 zilizoridhia malengo ya milenia ya mwaka 2000 kama sehemu ya makubaliano ya kimataifa ya pamoja yaliyopitishwa na Mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Malengo ya Milenia yanazitaka nchi zilizoendelea na zinazoendelea kushirikiana kwa pamoja kuondoa umaskini, njaa, maradhi, afya ya mama na mtoto, elimu ya msingi kwa wote, fursa sawa kwa jinsia zote na suala la mazingira na maendeleo. Aidha, Tanzania inatekezeza malengo hayo kwa kuyaainisha katika mipango yake ya maendeleo ikiwa ni pamoja na MKUKUTA, MKUZA, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 kwa Tanzania Bara na 2020 kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati dunia ikielekea mwaka 2015 ambao ndio ukomo wa kufanikisha malengo ya milenia, kuna wasiwasi kuwa nchi nyingi hazitafikia baadhi ya malengo hayo. Mionganoni mwa malengo ambayo hayajafikiwa ni pamoja na lengo namba 4 na 5 kuhusu Afya ya Mama na Mtoto.

Kwa kutambua hilo Mheshimiwa Ban Ki-Moon, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa alimualika Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuhudhuria mkutano maalum uliofanyika New York, Marekani Aprili 14 hadi 16, 2010 wa kujadili mkakati mpya wa kufanikisha malengo haya mawili. Mkutano wa kutathmini utekelezaji wa malengo ya milenia utafanyika wakati wa kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwezi Septemba mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla hali ya amani na usalama barani Afrika inaendelea kuimarika. Hivi karibuni tumeshuhudia matukio muhimu yenye kuleta matumaini kwamba Afrika bila migogoro inawezekana. Kwa mfano, Sudan imefanya uchaguzi mwezi Aprili 2010. Uchaguzi huo ni hatua muhimu katika juhudzi za kutafuta amani ya Sudan kwa sababu ni uchaguzi wa kwanza wa kidemokrasia kufanyika baada ya miongo miwili ya utawala wa kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchaguzi huo Chama cha National Congress Party (NCP), chini ya uongozi wa Mheshimiwa Omar Al Bashir kiliibuka na ushindi Sudan ya Kaskazini. Aidha, Chama cha *Sudan People's Liberation Movement* (SPLM) kinachoongozwa na Mheshimiwa Salva Kiir nacho kiliibuka na ushindi Sudan ya Kusini. Ushindi wa viongozi hao ni msingi muhimu wa utekelezaji wa Mkataba wa Amani ya Sudan ya Kusini. Ni matarajio yangu kwamba uchaguzi huo utatoa fursa kwa wananchi wa Sudan ya Kusini kupiga kura ya maoni iliyopangwa kufanyika mwaka 2011 kuhusu hatma ya eneo lao. Tunaitakia Sudan kila la kheri na fanaka katika zoezi hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyolarifu Bunge lako tukufu mwaka jana Tanzania imetimiza ahadi yake kwa kupeleka batalioni moja ya askari wa kulinda amani kuungana na vikosi vya nchi nyingine huko Darfur chini ya Umoja wa Mataifa. Kutokana na hali ya Darfur kuimarika, uhusiano baina ya Chad na Sudan ambaa ulikuwa umeathiriwa na mgogoro wa Darfur, nao umeimarika. Rais Omar Hassan Al-Bashir wa Sudan na Rais Idriss Deby wa Chad, walikutana Khartoum tarehe 9 Februari, 2010 na kukubaliana kuimarisha uhusiano kati ya nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo niliyyataja, bado bara la Afrika linakabiliwa na changamoto zinazotishia ustawi wa usalama na amani, hususan, katika nchi za Burundi, Somalia, Niger, Guinea na Madagascar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini Burundi, mategemeo ya kufanyika uchaguzi wa kidemokrasia kufuatia utekelezaji wa Mkataba wa Kusitisha Mapigano kati ya Serikali ya Burundi na kikundi cha PALIPEHUTU FNL, yamepata pigo, baada ya vyama 12 vya upinzani kikiwemo cha FNL, kujiondoa kutoka kwenye uchaguzi wa Rais. Hatua hiyo imetokana na vyama hivyo kutoridhishwa na matokeo ya uchaguzi wa madiwani uliofanyika tarehe 24 Mei 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki imekuwa msitari wa mbele katika kuvishawishi vyama hivyo kuendelea na mchakato wa uchaguzi, na wakati huo huo kutumia njia za kidemokrasia za kushughulikia malalamiko ya uchaguzi. Katika kutekeleza azma hiyo, nilitembelea Burundi tarehe 18 Juni 2010 ili kuwasikiliza viongozi wa kisiasa wa nchi hiyo.

Aidha, tarehe 25 Juni 2010 niliongoza ujumbe wa Mawaziri wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenda kuwasihii viongozi wa kisiasa wa Burundi kuweka mbele maslahi ya nchi yao na kushiriki katika uchaguzi, hasa ikizingatiwa kwamba jukumu la kuleta amani nchini Burundi ni la wananchi wa Burundi wenywewe. Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan Tanzania inassaidia tu kufanikisha juhudhi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Somalia inakabiliwa na matatizo makubwa matatu. Tatizo la kwanza ni kukosekana kwa Serikali imara nchini humo. Hali hiyo imesababisha kuwepo na mapigano na mauaji ya mara kwa mara. Waathirika wakuu wa mapigano hayo ni raia na maafisa wa Serikali ya mpito ya Shirikisho ya Somalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili ni baa la njaa linaloikumba Somalia kutokana na kuzorota kwa hali ya amani na usalama nchini humo. Hali hii imesabisha

watu zaidi ya milioni 3.6 ambao ni nusu ya idadi ya watu wa nchi hiyo kuathirika na njaa na hivyo kuhitaji misaada ya kibinadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la tatu ni kuendelea kwa vitendo vya uharamia katika mwambao wa Somalia. Uharamia huo umezidisha gharama za bima na usafirishaji hivyo kuathiri shughuli za upelekaji wa chakula na misaada mingine ya kibinadamu pamoja na biashara za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudzi za kukabiliana na mgogoro nchini Somalia, Umoja wa Afrika umepeleka askari 5,268 kutoka nchi za Burundi na Uganda. Askari hao wanafanya kazi katika mazingira magumu na ya hatari katika kuzilinda taasisi za Serikali ya Mpito ya Somalia na kusimamia utoaji wa misaada ya kibinadamu. Kasi ya kutafuta ufumbuzi wa mgogoro wa Somalia katika ngazi ya kimataifa bado haijaza matunda. Umoja wa Mataifa, una jukumu la kushiriki kikamilifu katika juhudzi za kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa mgogoro huo. Ninayo furaha kulieleza Bunge lako tukufu kuwa hivi karibuni Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa amemteua Balozi wa kudumu wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa Dkt. Augustine Mahiga, kuwa mwakilishi wake katika masuala ya Somalia. Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Balozi Mahiga kwa uteuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa ahadi ya Tanzania ya kuwafundisha askari elfu moja (1,000) kutoka Somalia bado iko palepale punde nchi hiyo itakapokuwa tayari kuleta askari hao nchini Tanzania. Aidha, ninatoa wito kwa Jumuiya ya Kimataifa kutekeleza wajibu wake katika kushughulikia mgogoro unaoikabili Somalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hila zilizofanywa na Rais wa Niger, Mamadou Tandja za kubadilisha katiba ya nchi hiyo kwa lengo la kubakia madarakani, wanajeshi walifanya mapinduzi na kuiangusha Serikali yake. Hata hivyo, Umoja wa Afrika umelaani mapinduzi hayo, kwa sababu yanakwenda kinyume na misingi ya demokrasia na utawala bora. Napenda kuchukua fursa hii kutoa wito kwa Serikali ya kijeshi ya Niger kuharakisha mchakato wa kuitisha uchaguzi ili kurejesha utawala wa kikatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yanayoikabili Guinea na Madagascar kimsingi yanafanana kwani yanatokana na kubadili Serikali bila kufuata misingi ya demokrasia na utawala bora. Kwa bahati nzuri, viongozi wa Serikali ya Kijeshi ya Guinea na Upinzani kwa pamoja wamefikia makubaliano ya kuunda Serikali ya Mpito itakayokuwa madarakani kwa kipindi cha miezi sita ili kusimamia uchaguzi wa kidemokrasia. Hatua hii imetoa matumaini ya kurejesha amani nchini Guinea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Madagascar mgogoro wa uongozi nchini humo bado unaendelea. Mwezi Novemba, 2009 pande zinazopingana zilikubaliana kuunda Serikali ya Mpito chini ya Bwana Andry Rajoelina lakini juhudzi hizo zilikwama

kutokana na Bwana Rajoelina kukataa makubaliano hayo. Hata hivyo, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Rais Mstaafu wa Msumbiji, Mheshimiwa Joaquim Chissano ambaye ni Msuluhishi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) anaendelea na juhudi za kutatua mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Afrika unaendelea na mchakato wa kubadili Kamisheni ya umoja huo kuwa Mamlaka kufuatia maagizo yaliyotolewa na Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika, kwenye kikao chao kilichofanyika Sirte, Libya mwezi Julai 2009. Rasimu ya mapendekezo ya katiba ya Umoja wa Afrika kuanzisha Mamlaka hiyo imekamilika na itawasilishwa kwenye kikao cha Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika kitakachofanyika Kampala, Uganda mwezi Julai, 2010 chini ya mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Bingwa Mutharika, Rais wa Jamhuri ya Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) inaendelea kutoa kipaumbele katika kuimarisha na kuharakisha ushirikiano katika maeneo ya biashara; maendeleo ya miundombinu inayokuza ushirikiano; usalama wa chakula; mazingira na maliasili; rasilimali watu; huduma za kijamii; siasa; ulinzi na usalama; takwimu; sayansi na teknolojia na jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kupanua soko la bidhaa na kukuza fursa za uwekezaji, nchi shiriki zimeendelea kutekeleza makubaliano ya Soko Huru la SADC lililoanza tarehe 1 Januari 2008. Kwa sasa asilimia 85 ya biashara kati ya nchi wanachama wa SADC inaendelea kufanyika bila ushuru wa forodha. Aidha, nchi shiriki zimeanza kuondoa ushuru kwa bidhaa zilizobakia ili ifikapo mwaka 2012 biashara ya bidhaa katika nchi za SADC ifanyike bila ushuru wa forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika inaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki na Soko huru la pamoja la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA) katika kuanzisha Soko Huru la Pamoja ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imeendelea kujijengea heshima kubwa katika mahusiano yake na Umoja wa Mataifa kutokana na kushiriki kwake kikamilifu katika masuala mbalimbali yahusuyo Umoja huo. Umoja wa Mataifa umeendelea kuiona Tanzania kama mdau muhimu na kuihusisha katika masuala yake mbalimbali. Hili limethibitishwa na ziara nyingi za viongozi wa juu wa Umoja huo na Mashirika yake zilizofanyika hapa nchini katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Tanzania imewapokea Katibu Mkuu wa Umoja huo Mheshimiwa Ban Ki-Moon, Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Asha Rose Migiro, Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (*UNDP*) Bi. Helen Clark; Kamishna Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wakimbizi (*UNHCR*) Bwana António Guterres; Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu Idadi ya Watu Duniani (*UNFPA*) Bi.

Thoraya Obaid na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (*WHO*) Dr. Margaret Chan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizi sio tu zimeendelea kuijengea heshima nchi yetu katika medani ya kimataifa bali zimedumisha uhusiano uliopo kati ya nchi yetu na Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoileza Bunge lako tukufu katika hotuba yangu ya mwaka jana, mradi huu wa ‘*One UN*’ umetekelawa kwa mafanikio makubwa sana nchini Tanzania na napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Tanzania imekuwa ni nchi ya kwanza kuwasilisha mapendekezo juu ya kile kinachojudikana kama “*common and coordinated country programme*” kwa Mashirika na Mifuko yote ya Umoja wa Mataifa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yaliwasilishwa kwenye Mkutano wa pamoja wa Bodi Tendaji (Executive Boards) za mashirika ya UNDP, UNFPA, UNICEF na WFP uliofanyika huko New York Marekani tarehe 15 Januari mwaka huu. Mapendekezo haya ambayo yametokana na uzoefu wetu tulipata katika kutekeleza Mradi huu hapa nchini yalipokelewa na kuungwa mkono na wajumbe karibu wote wa bodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mradi huu ambalo bado halijakamilika ni lile la ujenzi wa ofisi moja ambapo Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau muhimu tunaendelea kutafuta sehemu ambayo itajengwa Ofisi hiyo. Maeneo kadhaa yamependekezwa na majadiliano na wahusika yanaendelea ili kuweza kupata sehemu muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa mkutano wa kumi na tano wa Umoja wa Mataifa unaojihusisha na masuala ya mabadiliko ya tabia nchi (*UNFCCC*) ulifanyika Desemba, 2009 Copenhagen Denmark. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ilishiriki kikamilifu katika majadiliano ambayo yanopelekea kupatikana kwa Mkataba Mpya wa Mabadiliko ya Tabia nchi. Kinyume na matarajio ya wengi, hasa nchi zinazoendelea, makubaliano hayakufikiwa kutoptana na kuwepo kwa tofauti nyingi katika masuala anuai yahusuyo mabadiliko ya tabia nchi. Badala yake Mkutano huo uliibuka na kile kilichojudikana kama Makubaliano ya Copenhagen (*Copenhagen Accord*). Pamoja na kuwa Makubaliano haya yana mapungufu hasa katika kujumuisha yale ambayo nchi zinazoendelea zimekuwa zikiyapigania, naliarifu Bunge lako tukufu kuwa Tanzania ni mionganoni mwa nchi ambazo zimetia saini makubaliano hayo. Hatua hii tumeichukua kwa kutambua kuwa fursa ya kuendeleza mchakato wa majadiliano hayo ipo na kwa matarajio

kwamba tutafikia muafaka kwenye Mkutano ujao unaotarajiwa kufanyika huko mjini Cancun, Mexico.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilishiriki kikamilifu katika kufanikisha ushiriki wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Madola uliofanyika huko Port of Spain, nchini Trinidad and Tobago tarehe 27 hadi 29 Novemba 2009. Kaulimbiu ya mkutano huo ilikuwa ni “Ushirikishi kwa ajili ya Maendeleo Endelevu yenye Usawa” (*Partnering for a more equitable and sustainable future*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano huu ulijadili matatizo ya kiuchumi yaliyoikumba dunia, kuyumba kwa bei za mazao ya kilimo na matatizo ya mabadiliko ya tabia nchi ambayo kwa kiwango kikubwa sana yanaziathiri zaidi nchi zinazoendelea kuliko zilizoendelea. Azimio la Mkutano huu liligusia ushirikiano katika maeneo ya udhibiti wa uchumi, madeni, sayansi, teknolojia na uvumbuzi, kuboresha ushirikiano na uratibu na jukumu la Jumuiya ya Madola katika mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge lako tukufu linavyoolewa, Wizara yangu na Balozi zetu nje imekuwa ikitekeleza Sera ya Mambo ya Nje yenye msisitizo mkubwa katika nyanja za uchumi. Hivyo, kwa muda wa zaidi ya miaka kumi sasa Wizara imeweza:

- (i) Kuitangaza vyema nchi yetu kuhusu fursa zinazopatikana katika uwekezaji, biashara na utalii;
- (ii) Kuzungumza na mifuko na mashirika mbalimbali ya fedha ya kimataifa ili kuendelea kupata misaada;
- (iii) Kuratibu na kushiriki mikutano na makongamano kwa lengo la kuhamasisha wawekezaji, wafanyabiashara na watalii kuwekeza au kutembelea Tanzania.
- (iv) Kuingia katika mikataba mbalimbali ambayo inalenga kukuza ushirikiano wa kijamii na kiuchumi.

Madhumuni ya juhudhi zote hizi ni kutafuta mbinu ya kukuza uchumi wetu ili hatimaye Tanzania iondokane na bajeti tegemezi, hasa ikizingatiwa kuwa misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inapungua au kusitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Serikali kuitisha mpango kabambe wa KILIMO KWANZA, wenyе nguzo kumi, Wizara yangu na Balozi zake nje tumejipanga kikamilifu katika kufanikisha utekelezaji wa KILIMO KWANZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza diplomasia ya uchumi, kuimarisha ujirani mwema na kukuza ushirikiano, viongozi wetu wakuu wa kitaifa ambao ni Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Aman Abeid Karume, na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, walifanya ziara katika nchi mbalimbali duniani zikiwemo nchi za bara la Afrika, Mashariki Kati, Mashariki ya Mbali, Ulaya, Asia na Marekani. Aidha, viongozi wetu walipata fursa ya kufanya mazungumzo na wakuu wa Taasisi mbalimbali duniani zikiwemo, Shirika la Kilimo na Chakula (FAO), Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziara hizo zililenga kuimarisha mahusiano na ushirikiano na nchi ama taasisi hizo na kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa kutangaza fursa za uwekezaji na vivutio nya utalii vilivyopo nchini Tanzania. Kwa mfano, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete akiwa nchini Jordan alifanya mazungumzo na mwenyeji wake Mfalme Abdullah II bin Al Hussein na kukubaliana kushirikiana katika sekta za elimu, afya, kilimo, biashara na ulinzi. Aidha, viongozi hao wawili walikubaliana kuanzisha ushirikiano baina ya bandari ya Aqaba na bandari ya Dar es Salaam na kuanzisha shirika la meli kwa njia ya ubia kwa mtaji kutoka nchini Jordan. Ushirikiano huo unategemewa kusimamiwa na Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano baina ya Tanzania na Jordan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, wakati wa ziara ya kikazi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda nchini Japan, serikali ya Tanzania na Japan zilitiliana saini makubaliano kuhusu mkopo wa Yeni za Japan bilioni saba na milioni mia moja kumi na tisa (7,119,000,000.00) ambazo ni sawa na shilingi bilioni mia moja na sita, milioni mia saba themanini na tano (106,785,000,000.00) kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Tunduru hadi Namtumbo na kutoka Iringa hadi Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu nchini Vietnam imekuwa na mafanikio makubwa katika kusaidia kutekeleza mpango wa KILIMO KWANZA. Vietnam imeonesha nia ya kushirikiana na Tanzania kuendeleza kilimo cha kisasa pamoja na kuwekeza katika sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa njia ya utalii wa mikutano, nchi yetu iliandaa kwa ufanisi mkubwa mkutano wa Jukwaa la Uchumi la Dunia Kanda ya Afrika (*World Economic Forum for Africa*) uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Mlimani City Dar es salaam kuanzia tarehe 5-7 Mei 2010. Mkutano huu ulifanyika kwa ufanisi mkubwa na napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine katika kufanikisha mkutano huu wa kihistoria ambao kwa mara ya kwanza umefanyika Afrika Mashariki na umeijengea heshima kubwa nchi yetu mbele ya jumuiya ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhusiano na ushirikiano mzuri uliopo kati ya nchi yetu na Japan, Tanzania ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa pili wa ufuatiliaji wa

makubaliano ya Mkutano wa Nne wa Kimataifa wa Tokyo Kuhusu Maendeleo ya Afrika (TICAD IV) ambao ulifanyika mjini Arusha tarehe 2 na 3 Mei 2010. Mkutano huu ulitoa fursa muhimu kwetu kuendelea kupata misaada kutoka Japan. Aidha, taasisi zetu zinazohusika na utalii, biashara na uwekezaji zilifaidika kutohuna na mkutano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na wajibu wa kufanikisha uanzishwaji na uratibu wa Tume mbalimbali za Kudumu za Pamoja za Ushirikiano (*JPCs*) ambazo ni msingi wa kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na nchi mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara imefanikisha kuanzishwa kwa Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano na Jordan. Mkataba huo umewekwa saini tarehe 23 Februari, 2010 mjini Amman, Jordan wakati wa ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Jordan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Makubaliano (*MoU*) ya kuanzisha Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano baina ya Tanzania na Oman yaliwekwa saini na mimi mwenyewe nilipofanya ziara nchini Oman, tarehe 14 Oktoba 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, rasimu ya Mkataba wa kuanzisha Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano baina ya Tanzania na Saudi Arabia ipo tayari na inasubiri kuwekwa saini. Wakati huohuo mazungumzo ya awali ya kuanzisha Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano baina ya Tanzania na Jamhuri ya Kiarabu ya Syria yameanza. Wizara inategemea kuwa Mkataba wa kuanzisha Tume hiyo utawekwa saini ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza sera yetu inayosisitiza diplomasia ya uchumi, umuhimu wa nchi au taasisi kuingia katika mikataba ya nchi na nchi, kikanda ama kimataifa ni kuhakikisha ya kuwa makubaliano yaliyomo katika mikataba hiyo ikiwemo kulinda haki za binadamu, mazingira ama masuala ya biashara na uwekezaji vinalindwa. Hivyo, kwa kuzingatia wajibu huu Wizara yangu imeshiriki kwenye majadiliano yaliyopelekea kutia saini mikataba mbalimbali katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, suala la kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi ughaibuni(*Diaspora*) na kuweka utaratibu utakaowawezesha kuchangia maendeleo ya nchi yao liko katika hatua nzuri. Wizara imeendelea kuhamasisha na kuhimiza Balozi zetu nje ziwezeshe Watanzania wanaoishi ughaibuni kushiriki kikamilifu katika kuchangia shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi hivi sasa, Watanzania wengi waishio ughaibuni wameonesha nia ya kuanzisha jumuiya pale ambapo hazipo na pia kuimarisha zilizopo. Kwa mfano, jumuiya ya Watanzania walio Uingereza inaendelea kuimarika na inaratibu pia masuala ya Watanzania wanaoishi nchi nyingine za Ulaya, hususan Uhlanzi na

Ubeltiji. Mwezi Mei, 2010 Watanzania wanaoishi Kenya na Rwanda nao wamefufua jumuiya zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeshiriki katika mikutano na semina mbalimbali zilizoandalisha na nchi na mashirika wafadhili kwa madhumuni ya kunufaika na utaratibu na uzoefu wa nchi na mashirika hayo katika kupata idadi ya raia wanaoishi ughaibuni. Benki ya Dunia, Umoja wa Ulaya na Shirika la kimataifa linaloshughulikia Uhamiaji (*IOM*) wameonesha nia ya kushirikiana na Tanzania katika kufanikisha azma hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kama msimamizi mkuu wa masuala ya Itifaki ya nchi, imeendelea kutoa huduma ya kiitifikasi na kikonseli. Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara imeratibu uwasilishaji wa hati za utambulisho kutoka kwa mabalozi wa Canada, Brazil, Iran, Bangladesh, Jamhuri ya Korea, Zambia, Rwanda, Marekani, Japan, Algeria, Palestina na Afrika ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za kikonseli, Wizara imendelea kurahisisha upatikanaji wa viza kwa maafisa na watendaji wa Serikali, Vyama vya Siasa na Taasisi nyingine zinazostahili huduma hiyo.

Wakati huo huo Balozi zetu nje zimeendelea na utoaji wa viza kwa raia wa nje wanaoitembelea Tanzania na kusaidia kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili Watanzania waishio nje ya nchi. Aidha, Wizara imeendelea kutatua matatizo na kulinda maslahi ya Watanzania wanaofanya kazi kwenye Balozi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeendelea kutekeleza jukumu kubwa la kusimamia utawala na maendeleo ya utumishi Wizarani na katika Balozi zetu nje katika kuboresha maslahi, elimu na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivi sasa, uwezo wa Wizara kwa upande wa rasilimali watu ni jumla ya watumishi 409. Kati ya watumishi hao; 205 wako Makao Makuu; 15 wako Ofisi ya Mambo ya Nje Zanzibar; na 189 wako katika Balozi zetu nje. Aidha, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya wa kada na fani mbalimbali 53 na watumishi 16 wa kada mbalimbali ikiwa ni ajira mbadala. Matarajio yangu ni kwamba, ajira hizi zitakamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

Kwa upande wa mafunzo, watumishi hupelekwa mafunzoni kwa ajili ya kuongeza ujuzi katika taaluma zao. Katika kutekeleza hili, mwaka wa fedha wa 2009/2010, watumishi 24 walipelekwa mafunzoni. Kati yao 13 walipelekwa kozi ndefu na 11 kozi fupi. Vilevile, Wizara imepandisha vyeo na kuwateua watumishi 17 kuwa Wakurugenzi Wasaidizi na inatarajia kuwapandisha vyeo watumishi 50 wa kada mbalimbali ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la majengo ya ofisi na makazi katika balozi zetu nje bado ni changamoto kubwa. Ili kufanikisha mkakati wa Wizara wa kuepukana na mzigo wa gharama za pango, Wizara imekamilisha kazi ya ununuzi wa Jengo la Ubalozi Jijini Washington, D.C. Jengo hilo litatumika kama ofisi za ubalozi na kitega uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara imeanza mchakato wa kununua Jengo la Ubalozi Jijini New York. Mpaka sasa kiasi cha shilingi 13,522,276,250 zimekwishapelekwa New York kama malipo ya awali. Matarajio yangu ni kwamba, kazi hii itakamilika katika mwaka huu wa fedha na hatimaye ubalozi wetu wa kudumu Umoja wa Mataifa utakuwa na ofisi katika jengo letu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara inaendelea na mazungumzo na Mifuko ya Taifa ya Hifadhi za Jamii kwa ajili ya ufadhili wa ujenzi wa majengo London, Nairobi, Maputo, Abuja na Kigali. Baadhi ya majengo haya yatakuwa ofisi na mengine vitega uchumi ili kuiongezea Serikali mapato na kuiwezesha Wizara kujiendesha yenyewe. Aidha, zoezi la kukarabati baadhi ya majengo ya ofisi na makazi ya watumishi wa Balozi zetu nje linaendelea. Ni matumaini yangu kwamba, Wizara yangu itaendelea kutengewa fedha za kutosha kukamilisha zoezi hili na napenda kutoa taarifa na kushukuru mapema kwamba, katika safari hii tutaomba shilingi bilioni 40 kwa ajili ya shughuli hizi. (*Makofii*)

Ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano wa Mwalimu Julius Nyerere unaofadhilliwa na Serikali ya China, umeanza rasmi Jiji Dar es Salaam. Ujenzi huu unafanywa na Kampuni ya *Fujian Construction Engineering Group* iliyoteuliwa na Serikali ya China. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu udhibiti wa mapato na matumizi ya Wizara; kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu imeongeza ufanisi katika masuala ya usimamizi wa bajeti ya fedha kwa ujumla ambapo kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Balozi tano (15.6%) zilipata Hati Safi za Ukaguzi wa Hesabu ikilinganishwa na Balozi tisa tu (9.4%) zilizopata Hati kama hizo kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Zaidi ya hapo, Balozi 23 (71.9%) zilipata Hati Safi zenye Masuala ya Msisitizo ikilinganishwa na Balozi 19 (59.4%) kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Aidha, Balozi tatu (9.4%) zilipata Hati zenye Shaka ikilinganishwa na Balozi nane (25%) kwa mwaka wa fedha 2007/2008. Ni Ubalozi mmoja tu (3.1%) ambao ulipata Hati isiyoridhisha ikilinganishwa na Balozi mbili (6.2%) kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na ubalozi huo tumeanza kuushughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kueleza hatua kadhaa ambazo zimechukuliwa na Wizara yangu ili kupanua wigo wa makusanyo ya maduhuli. Hatua hizo ni pamoja na kumiliki majengo ya Ofisi katika baadhi ya Balozi zetu badala ya kupangisha, kusimamia vyema vyanzo vya mapato yanayotokana na viza pamoja na kuimarisha Balozi zetu za Heshima katika kukusanya na kuwasilisha maduhuli yanayotokana na viza. Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ipo katika mchakato wa kufunga

mashine za viza kwenye Balozi za Heshima za Milano nchini Italia na Copenhagen nchini Denmark. Ni matarajio ya Serikali kwamba, mashine hizo zitafungwa kwenye Balozi zote za Heshima, kwa kuanza na zile zenye makusanyo makubwa ya maduhuli, kwa kadiri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara yangu itaendelea kusimamia vyema bajeti yake na kuhakikisha kwamba, Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha na Manunuzi zinazingatiwa ipasavyo wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu shughuli za uendeshaji wa Mahakama ya Afrika iliyopo Arusha. Hivi karibuni, Wizara yangu imewasilisha jina la Jaji wa Mahakama Kuu kuwa mionganini mwa wagombea wa nafasi tano za Majaji wa Mahakama hii. Uchaguzi wa kujaza nafasi hii utafanyika Kampala, Uganda mwezi Julai 2010. Hii ni fursa ya pekee ya kuitangaza nchi yetu kupitia mgombea mahiri na mwenye wasifu wa aina yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, bado Wizara yangu inakabiliwa na changamoto ambazo tunaendelea kuzishughulikia ili kuboresha mazingira ya kazi ya Mahakama hiyo ya Afrika. Changamoto hizo ni pamoja na kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za kudumu za Mahakama hii pamoja na makazi ya kudumu ya Rais na Msajili wa Mahakama hiyo. Jitihada zinaendelea ili kuhakikisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na makazi ya viongozi hao yanapatikana mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu litakumbuka kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mojawapo ya nchi za Kiafrika zinazoshiriki katika mchakato wa kuimarisha Utawala Bora kwa kujitathmini, yaani *African Peer Review Mechanism (APRM)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Aprili, 2010, Serikali yetu ilitegemea kukamilisha hatua za mwisho za mchakato huu, kwa kupokea ujumbe kutoka Sekretarieti ya Mpango wa Kujitathmini (*APRM*) iliyoko Afrika Kusini, ukiongozwa na Prof. Adebayo Adedeji. Lengo la ujumbe huo lilikuwa kuhakiki Taarifa ya Tanzania kuhusu utekelezaji wa misingi ya Utawala Bora nchini Tanzania, ambayo ingejadiliwa kwenye kikao cha Wakuu wa nchi za Umoja wa Afrika kitakachofanyika Kampala nchini Uganda mwezi Julai, 2010. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa bajeti na nchi yetu kuwa katika maandalizi ya Uchaguzi Mkuu, ziara ya Profesa Adedeji haikuweza kufanyika na imeahirishwa. Tunategemea kuwa, zoezi hili sasa litahitimishwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi zilizo chini ya Wizara; Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC) kimeendelea kufanya kazi nzuri na kuyaweka majengo na mazingira yake kuwa katika hali nzuri kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Kituo kimeweza kukaribisha wastani wa mikutano 150 kwa mwaka. Kati ya mikutano hii; 40%

ya mikutano ni ya kimataifa na 60% ni ya kitaifa. Idadi hiyo ya mikutano imeweza kuleta wageni wa mikutano wapatao 17,726 Mjini Arusha kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matunda ya ujio wa wageni nchini kwa ajili ya mikutano si kwa manufaa ya Kituo tu, bali hugusa sehemu mbalimbali za jamii kama usafiri, kodi ya viwanja vya ndege, biashara ya hoteli za kitalii na za kawaida, mauzo katika maduka ya kitalii na ya kawaida, kutembelea Hifadhi za Taifa na hata kupanda Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio ya Kituo ni kuendelea kuongeza idadi ya mikutano kila mwaka kwa kujitangaza zaidi na kutoa huduma bora zaidi. Azma hii inalenga kuifanikisha kaulimbiu ya Kituo ambayo ni “*We bring the World to Tanzania.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sehemu ya kujizatiti kupambana na ushindani wa kibiashara, Wizara ipo katika mchakato wa kuanzisha kituo kipy cha mikutano Mjini Arusha kitakacho julikana kama *Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK-ICC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia kimeendelea na jukumu la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za diplomasia, uhusiano wa kimataifa na mikakati ya kutatua migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, Chuo cha Diplomasia kimepanga kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 170 hadi 350, kuajiri wahadhiri waandamizi wapya wawili ili kukidhi ongezeko la wanafunzi na kuongeza vyumba vya madarasa. Aidha, jitihada zinafanyika ili kupata fedha kwa ajili ya fidia ya eneo la ekari elfu moja lililopatikana katika Kijiji cha Buma, Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya ujenzi wa chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara yangu ilipangiwa kutumia kiasi cha shilingi 88,002,643,100.00; kati ya fedha hizo, shilingi 63,917,282,800.00 zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida; shilingi 20,269,113,100 zilikuwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo na shilingi 3,816,247,200.00 zilikuwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Balozi zake, ilitegemea kukusanya kiasi cha shilingi 9,863,298,000.00. Hadi kufikia tarehe 14 Juni, 2010 kiasi cha shilingi 11,766,233,131.00 kilikuwa kimekusanywa. Kiasi hiki cha fedha ni sawa na ongezeko la asilimia 19.3 ya makusanyo ya fedha zote za maduhuli zilizokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 18 Juni, 2010, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 75,161,804,951.00 kutoka Hazina kama sehemu ya mgao wake wa bajeti. Kiasi hiki cha fedha ni sawa na asilimia 85.4 ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, pamoja na mambo mengine, Wizara yangu imepanga kutekeleza malengo makuu muhimu kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

- (i) Kuendelea na juhudzi za kuitekeleza diplomasia ya uchumi kwa dhamira ya kuiletea nchi yetu maslahi ya kiuchumi na maendeleo ya jamii.
- (ii) Kuendeleza Sera ya Ujirani Mwema na Nchi jirani.
- (iii) Kuendelea kushiriki na kuimarisha ushirikiano wa kikanda (EAC, SADC, Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Nchi Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM)) kwa maslahi ya Taifa kwa nia ya kukuza uchumi na maendeleo ya jamii.
- (iv) Kuendelea kudai mageuzi ya Umoja wa Mataifa, hususan katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, kwa lengo la kuongeza sauti na heshima ya nchi zinazoendelea.
- (v) Kuendelea kuzishinikiza nchi tajiri kutekeleza ahadi yao ya kutenga asilimia 0.7 ya Pato la Taifa la nchi zao kwa ajili ya misaada kwa nchi maskini.
- (vi) Kuendelea kulitangaza jina la nchi yetu na kuiletea heshima mionganini mwa mataifa.
- (vii) Kuendeleza mchakato wa kuitambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Ughaibuni na kuboresha mazingira ya kazi, mawasiliano na pia kuhakikisha umiliki wa nyumba za ofisi na makazi katika balozi zetu.
- (viii) Kuendeleza kuboresha mazingira ya kazi, mawasiliano na maslahi ya wafanyakazi ili kuongeza ari ya utendaji kazi.
- (ix) Kuhakikisha tunaongeza umiliki wa nyumba za ofisi na makazi katika Balozi zetu nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza kikamilifu kazi zilizotajwa hapo juu, Wizara yangu imepangiwa kiasi cha shilingi 112,336,928,000.00 kwa mwaka wa fedha 2010/2011. Kati ya fedha hizo; shilingi 67,836,928,000.00 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 44,500,000,000.00 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Aidha, shilingi 3,796,136,000.00 ni kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi. Kati ya bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara, shilingi 1,000,000,000.00 ni kwa ajili ya mchakato wa APRM, shilingi 2,000,000,000.00 ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika na Haki za Binadamu na Watu na shilingi 1,615,767,628.00 ni kwa ajili ya fedha za mishahara na matumizi ya kawaida ya Chuo cha Diplomasia. Aidha, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 12,732,300,000.00 kama maduhuli ya Serikali. Kwa maana ya utekelezaji wa Bajeti, kiasi hiki cha maduhuli tayari kimehesabiwa kama sehemu ya matumizi ya kawaida ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Labda nianze kwa kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Mawaziri, kwa uwasilishaji mzuri ambao wameufanya mbele yetu kwa muhtasari. Kama tunavyoolewa kwamba, *Hansard* itakuwa na maelezo kama walivyoyawasilisha kwenye vitabu vyao.

Sasa ninachukua fursa hii kuwataka Mwenyekiti wa Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa sababu yeye atakuwa ana-cover hizi Wizara mbili, msemaji wake sasa aweze kuja hapa na kutupa maoni ya Kamati kuhusiana na Wizara hizi mbili. Baada ya hapo, nitataka upande wa Kambi ya Upinzani nao Wasemaji Wakuu wa Kambi kwa Wizara hizi mbili kila mmoja aweze kuja kutoa maoni ya Wizara husika na baada ya hapo tutakuwa na matangazo ya wageni halafu tutaendelea na michango. Sasa kwa kuanza naanza kumwita Mwenyekiti au Mwakilishi wake; namwona Mheshimiwa Juma Hassan Killimbah tafadhalii. (*Makofii*)

MHE. JUMA H. KILLIMBAH (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuwakilisha Taarifa ya Kamati, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa utukufu, kwa kunijalia katika majaliwa yake, kutekeleza wajibu wangu kwa kipindi cha miaka mitano ya Ubunge wangu kwa Jimbo la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote, kwa kutulea na kutuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ya uhai wa Bunge hili. Nyote nawaombeenii *Inshallah*, Mwenyezi Mungu awajalie mrejee katika Bunge hili na nafasi hizo mlizonazo mtazirejea tena. (*Makofii*)

Nitumie fursa hii, kuwashukuru sana Wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Iramba Magharibi, kwa ushirikiano walionipa kwa kuwakilisha kwa kipindi cha miaka mitano. Ushirikiano wao ndiyo uliotufanya hivi sasa tupige hatua kubwa za kimaendeleo ndani ya Jimbo la Iramba Magharibi. Kipekee, namshukuru sana mke wangu Hajira na wanangu Siti, Latifa, Esta, Mambala, Badi na Shimba, kwa kunivumilia muda wote wakati nikitekeleza majukumu yangu ya kuwatumikia Wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na mapato na matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kuliomba Bunge hili liipokee na kujadili na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kulitaarifu Bunge letu kuwa, Kamati katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, imekuwa ikifuatilia kwa karibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2009/2010. Kamati ilitembelea Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Mjini Arusha. Ilipokea Taarifa ya kukagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya hiyo. Aidha, Kamati imekuwa ikipokea na kujadili Taarifa ya Hali ya Uhusiano wa Nchi za Afrika Mashariki, iliyokuwa ikiwasilishwa kwenye Vikao vya Kamati na Mawaziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 02 Juni 2010, Kamati ilikutana kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, iliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ina Fungu moja ambalo ni Fungu 97.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa jinsi ya Wizara ilivyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dhima, Dira na Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Aidha, Kamati ilielezwa kiasi cha fedha zilipokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa Malengo ya Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Kwa mujibu wa maelezo, fedha zote zilizopokelewa kutoka Hazina zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya bajeti kama ilivyofafanuliwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge hili kuwa, Kamati iliridishwa na mtiririko wa fedha toka Hazina na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010. Ni matumaini yetu kwamba, Wizara hii itaendelea kuwa madhubuti katika kutekeleza majukumu yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua makadirio ya Wizara hii, Kamati ilitoa maoni ya ushauri katika maeneo mbalimbali ya ushirikiano kwa Nchi za Afrika Mashariki. Napenda kuliarifu Bunge kuwa, Serikali imefanikiwa katika kulinda maslahi ya msingi ya nchi kwa kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri imeonesha kuwa, nchi yetu haidaiwi michango ya Uanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na imeendelea kufuata na kutekeleza kwa vitendo, Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004 na Kanuni zake katika kukabiliana na vikwazo mbalimbali vya kibashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kwamba, Wizara hii imepanga kutekeleza majukumu muhimu ikiwemo maandalizi ya Sera ya Taifa ya Mtengamano, kukamilisha Mikakati ya Kitaifa, utekelezaji wa Itifaki wa Soko la Pamoja na kuanza utekelezaji wake na kutekeleza mpango kabambe wa kutoa elimu kwa umma kuhusu mtengamano kwa Jumuiya hii. Aidha, Wizara inalenga kukamilisha uchambuzi wa changamoto za uanzishwaji wa Shirikisho la Kisiasa ili kufanikisha azma ya Serikali na malengo yake ya Mwaka wa Fedha 2010/2011. Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki imekadiriwa kutumia kiasi cha shilingi bilioni kumi na tatu, milioni themanini na nane, mia tisa hamsini na nane milioni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili kwa kina taarifa na utekelezaji wa majukumu na mpango wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Baada ya kupitia kifungu kwa kifungu, ninapenda kuliarifu Bunge hili kwamba, Kamati inaunga mkono maombi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kutoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika hatua zake zote ili kupanua uelewa wa Wananchi na kuwapa nafasi nzuri ya kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zitokanazo na ushirikiano huu.

(ii) Kwa kuwa Tanzania imeridhia utekelezwaji wa Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja, Serikali iendelee kuandaa mazingira sahihi na mkakati madhubuti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Mpango wa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Baada ya kupitia kifungu kwa kifungu, napenda kuliarifu Bunge hili kwamba, Kamati inaunga mkono maombi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 na kutoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iendelee kutoa Elimu kwa Umma kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika hatua zake zote ili kupanua uelewa wa wananchi na kuwapa nafasi nzuri ya kushiriki kikamilifu kwa kutumia fursa zitokanazo na ushirikiano huu.

(ii) Kwa kuwa Tanzania imeridhia Utekelezwaji wa Itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Itifaki ya Umoja wa Forodha na Itifaki ya Soko la Pamoja, Serikali iendelee kuandaa mazingira sahihi na mikakati madhubuti ya kitaifa itakayowawezesha Watanzania kunufaika kikamilifu na utekelezwaji wa itifaki hizi.

(iii) Suala la umiliki wa ardhi ndani ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki libakie kuwa ni suala la Taifa husika.

(iv) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki tujifunze kutoka mifano ya ushrikiano wa nchi nyingine Duniani kama vile Ushirkiano wa Nchi za Ulaya.

(v) Kwa kuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ina ushirkiano mzuri kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kiuchumi na kisiasa, diplomasia, itumike kuishawishi nchi hiyo ili ijiunge Uanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi, kwa jinsi unavyoliongoza Bunge hili tangu kuchaguliwa kwako katika nafasi hiyo. Uongozi wako umekuwa kielelezo katika Sekta ya Uhusiano na Ushirkiano wa Kimataifa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi wanavyokusaidia kuongoza vikao.

Ninapenda pia kumshukuru Waziri wa Ushirkiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Diodorus B. Kamala; Naibu Waziri wa Ushirkiano wa Afrika Mashariki; Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed; na Wataalam wa Wizara hiyo, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Stergomena L. Tax, kwa ushirkiano wao na kazi nzuri sana katika kutetea maslahi ya Taifa na kusimamia na kuendeleza utekelezaji wa Mkataba wa Ushirkiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa kazi nzuri na ushirkiano mkubwa walioutoa katika kufanikisha kazi hii. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi - Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Ndugu Stella Mlambo, Katibu wa Kamati, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Taarifa hii kutoka kwa wakati.

Baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ushirkiano wa Afrika Mashariki, jumla ya Shilingi 13,088,958,000 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Juma Hassan Kilimbah. Waheshimiwa Wabunge, ili twende katika mpangilio mzuri, baada ya maoni haya ya Kamati, nitamwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara hii atoe kabisa maoni yake, halafu baadaye nitamwita tena Mwenyekiti ili utaratibu uende vizuri kwa sababu hizi ni Wizara mbili tofauti.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika, naam Mheshimiwa!

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, akitaka kuwasilisha Hotuba yake, alisema ile anayoisoma ni *summary*.

MWENYEKITI: Kanuni unayoitumia?

MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni 68(7). Kasema ile anayoiwasilisha ni *summary*, hotuba kamili imegawiwa kwenye hivi vitabu. Lakini baada ya kuisikiliza ile hotuba, kuna mambo mengi sana ambayo yamo kwenye ile *summary* kuliko hii hotuba iliyogawiwa. Kwa maana hiyo, ingekuwa ni vyema na hiyo *summary* sasa ili kufaidika tuipate, tupate uwezo wa kuchangia. Naomba mwongozo wako.

MWENYEKITI: Ahsante. Nadhani nitakuwa nimekuelewa, lakini nafikiri Mheshimiwa Waziri alipozungumza alisema atatoa muhtasari; kwa hiyo, hapo ulipokuwa unaongea wewe nilidhani labda huo muhtasari umekuwa mkubwa kuliko hotuba iliyowasilishwa, kumbe ndani ya muhtasari kuna vitu huvioni humo, lakini kwenye Hansard vinaingia hivyo vitu. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri ili kama ana uwezo wa kukupatieni huo muhtasari wake, basi utolewe kopi ili muweze kuupata muweze kuchangia. Baada ya hapo, sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara, Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji.

MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI (K.n.y. MSEMADI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa fursa ya kutoa Maoni haya kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, lakini pia kwa Niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ushirikiano wa Umoja wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 99(7), Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sifanya hivyo, naomba nitoe pole kwa wale wote waliofikwa na misukosuko ya kimaisha, ikiwemo vifo vya wanafamilia au kupata ajali na kuumia. *Inshallah* Mwenyezi Mungu atawapa subira kwa mitihani hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, yaani Burundi, Kenya, Uganda, Rwanda na Tanzania bado haijakomaa na kwa maana hiyo ushirikiano huu bado unahitaji usimamizi mkubwa sana. Jaribio hili la ushirikiano wetu linataka uangalizi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti kubwa zilizopo baina ya nchi tano hizi kijamii, kiuchumi na hata kisiasa, bado zinaufanya umoja huu kuwa mgumu. Lazima tujielekeze katika mikakati ya kuweka pamoja utaratibu wa Sheria za Jamii na Soko la Pamoja. Ibara ya 76(1) ya Mkataba wa Jumuiya imeainisha nyanja za ushirikiano katika Soko la Pamoja kuwa ni pamoja na uhuru wa watu kwenda watakako, uhuru wa kutoa huduma kibiashara na uhuru wa kuhamisha mitaji. Vikwazo hivi bado viro na pale tutakapojaribu kuvitatua, ndiyo tutaongeza wigo wa suala zima la ushirikiano baina ya nchi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, hali ya dunia hivi sasa ipo katika mwelekeo wa nchi zilizo majirani na au kupakana, kuunda Jumuiya za Kiuchumi kwa nchi hizo. Hoja zitolewazo ni kuwa, kuongeza wanachama katika Jumuiya ni kuimarishe umoja. Lakini je, hatuoni kuwa nchi zetu zina mitazamo tofauti ya kiuchumi, kimila, kisiasa, kiusalama na kwamba hii inaweza kutuongezea matatizo mbalimbali katika nchi zetu kuliko kufikia lile lengo letu tulilolikusudia? Kwa nini hatukukaa kwanza na kutafakari kwa kina matatizo tuliyonayo? Haraka hizi ni za nini? Kwa nini tufanye haraka kwa gharama za Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza ni kuwa, wakati bado nchi zetu hizi zinakumbwa na matatizo mengi ya ndani na mengine yakiwemo yale yaliyosababisha kuvunjika kwa Jumuiya hii hapo awali, Wakuu wa Nchi zetu wameamua kuingiza wanachama zaidi katika Jumuiya hiyo na kufanya sasa kuwa na wanachama watano, yaani Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda na Tanzania. Je, isingelikuwa vyema kwanza tukatatua matatizo tuliyonayo sisi wenyewe kabla ya kujibebesha matatizo ya wengine? Sasa tunashabikia suala la kuunda Shirikisho la Kisiasa haraka sana kama inavyowezekana; kwa nini Viongozi wetu hawafikirii kutatua matatizo ya ndani kwanza na kuboresha hali ya kiuchumi kwa kila nchi kabla ya kufikiria kuingia katika Shirikisho? Je, tunaunganisha nguvu au tunaunganisha matatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 104(2) ya Mkataba wa Jumuiya, inatoa uhuru wa kuishi popote katika Jumuiya. Hili pia nalo lina matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu sana kwa suala la ardhi tukaliacha holela. Haitokuwa vyema kwa Wanachama wa Jumuiya kutoka nchi jirani kujipatia ardhi ya Tanzania bila kuwepo na utaratibu wowote wa kisheria. Suala hili Wananchi wa Tanzania hawalihitaji kuwemo ndani ya Soko la Pamoja. Hivyo ni lazima tujifunge mkanda ili tuhakikishe ardhi ya Tanzania haichukuliwi ovyo ovyo na wasiokuwa Watanzania. Kwa maana hiyo, Sheria za Ardhi ni lazima zirekebishwe na au kubadilishwa ili rasilimali hii bado iwe mikononi mwa Watanzania wenyewe. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa kutuhakikishia kuwa, suala la ardhi

lilijadiliwa na kukubaliwa kuwa kila nchi itafuata sheria zake za ardhi na kwamba, haitoruhusiwa kwa mgeni kupata ardhi katika nchi ambayo si yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mtandao wa Miundombinu utasaidia sana ukuaji kiuchumi wa Nchi Wanachama wa Afrika Mashariki hasa katika zile barabara zilizoko katika mlango (*Corridor* Nambari 1 mpaka 5). Hata hivyo, jambo moja la kusikitisha ni kuwa, harakati hizi za miundombinu inaelekeea kabisa kuwa suala la mwambao wa Pwani ya Afrika Mashariki, umesahaulika kiuchumi na kimaendeleo. Je, ni kweli kuwa hakuna uwezekano wowote wa kuunganisha Mtwara – Dar es Salaam – Zanzibar – Bemba – Tanga – Mombasa – Lamu kwa kuwa na usafiri wa uhakika wa *speed boat* kama zilivyobuniwa Barabara za Mombasa – Kigali – Himo (*Corridor No. 1*), Dar-es-Salaam – Kigali – *Corridor 2*, Biharamulo – Lodwan – Lokichogio *Corridor No. 3*, Tunduma – Gisenyi (Rwanda) – *Corridor No. 4* na Tunduma – Namanga – Moyale – *Corridor No. 5*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzetu wanaoishi pbeni mwa Ziwa Victoria nao wanafaidika na ushirikiano huu wa pamoja kwa kuwa na Mradi wa Kuendeleza Bonde la Victoria, ambao lengo lake ni kuwasaidia raia wa nchi hizi wanaoishi pembezoni mwa Ziwa hilo. Hivi sasa kuna mpango wa kuinua uchumi wa wakazi wa maeneo ya Ziwa Victoria kwa kutambua maliasili za uwekezaji zilizopo na zinazoweza kutumika bila ya kuharibu mazingira kwa kuuwezesha umma kuwekeza na kutunza mazingira na miradi ya wakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya pia yanaweza yakafanyika kwa watu wanaoishi Mwambao wa Afrika ya Mashariki. Je, ni kitu gani kilichozaui hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari zilizopo katika mwambao wa nchi zetu, zinahitaji maboresho na matengenezo ya hali ya juu ili kusaidia nchi hizi kuimarika kiuchumi. Pia panahitajika usafiri wa uhakika wa kuziunganisha bandari hizi pamoja na miji iliyomo katika maeneo hayo. Kauli za aina hii ziliwahi kutolewa na Mheshimiwa Waziri; sijui kwa sasa hatua hizo zimefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha nao una matatizo yake. Bado kuna baadhi ya nchi kama vile Kenya, hazifanyi wajibu wake kama wanavyotakiwa wafanye chini ya Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya hiyo. Mifano ipo mingi:-

(i) *Internal Tariff Elimination* ambayo ina lengo la kuondoa ushuru wa forodha mionganoni mwa nchi wanachama haujatekelezwa vizuri na hivyo kuleta matatizo mionganoni mwa jamii ya Wanaafrika Mashariki.

(ii) *Elimination of Non Tariff Barriers* ni tatizo lingine kubwa; kwa mfano, Viwanda vya Tanzania vinapangiwa *quoter* ya kupeleka Kenya na pia kutozwa ushuru ambapo hili ni kinyume na utaratibu wa itifaki wenywewe. Je, Serikali imechukua hatua gani hadi sasa ili kuvihami viwanda vyetu na hivyo kutoa motisha kwa Watanzania katika kuimarisha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya Soko la Pamoja la Afrika Mashariki, inasisitiza uundwaji wa soko hilo kwa hatua na pia kuweka maeneo muhimu ya soko hilo katika nyanja tofauti kama vile soko huru la biashara, uhuru wa raia kusafiri au kufanya kazi popote atakapo kwa mujibu wa utaratibu na sheria zilivyowekwa kama ibara za 76(1) na 104(2) za Mkataba wa Jumuiya zinavyoainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni muhimu sana lakini lazima tuweke msisitizo wa uratibu wa pamoja, yaani *co-ordination*, mionganoni mwa Wizara zetu ili tuweze kufanikiwa vizuri. Pamoja na kwamba, Itifaki hii ya Soko la Pamoja imechukua sura mpya kuanzia tarehe 1 Julai, 2010, bado Wananchi walio wengi mijini na vijijini, hawajaelimishwa vya kutosha kuhusu soko hili la pamoja na jinsi gani wanawenza kufaidika na ukubwa wa soko hili lenye jumla ya watu milioni 120. Ingawa Soko la Pamoja linahusisha soko la bidhaa, mitaji, ajira na huduma, bado Watanzania walio wengi wanajiuliza Soko hilo la Pamoja liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Kenya, Mheshimiwa Mwai Kibaki, katika Siku ya Madaraka, aliwahutubia Wananchi na kuwaelimisha juu ya maana ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na ni vitu gani Wakenya watafaidika navyo. Kambi ya Upinzani inasikitika kuona kuwa, Waziri mwenye dhamana alizunguka Nchini Uingereza, Miji ya London na Reading, kuwaelimisha Watanzania wanaoishi huko (*Tanzania-diáspora*), juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Soko la Pamoja, lakini anashindwa kufanya ziara kama hiyo hapa Tanzania!

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali hii, tunaishauri Serikali ifanye jitihada za makusudi, kuielimisha jamii ya Watanzania kuhusu maana halisi ya Soko la Pamoja na jinsi gani linaweza kuwa na faida kwa Watanzania kama Washirika wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Inashangaza kuona kwamba, katika masuala ambayo ni vipaumbele ndani ya nchi yetu kama kilimo na elimu, kuna upungufu mkubwa wa wataalam. Kilimo (kuna upungufu wa maafisa ugani zaidi ya asilimia 60). Vilevile kuna upungufu wa walimu wa sayansi. Nchi yetu haikuyazingatia hayo katika makubaliano ya utekelezaji wa Soko la Pamoja na ndiyo maana yamepangiwa kuanza utekelezaji wake mwaka 2015. Kwa kuwa makubaliano hayo siyo Msahafu wala Biblia, tunaishauri Serikali iliangalie upya suala hili ili tuendane na utekelezaji wa vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema katika hotuba zetu za nyuma kwamba, Zanzibar bado ni mtoto yatima katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Mambo kadhaa ambayo siyo ya Muungano, ambayo kikatiba zetu yanapaswa kushughulikiwa na Zanzibar yenyewe au na Tanzania Bara yenyewe, sasa yamo katika orodha ya Afrika Mashariki; ambayo kwayo yanashughulikiwa na Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti mbili za Afrika ya Mashariki zilizopita, Zanzibar imewasilisha mapendekezo ya miradi inayoweza kutekelezwa na Zanzibar chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Miradi hii ni pamoja na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa; uwekaji wa vituo vya umeme wa upepo; ujenzi wa Bandari ya Maruhubi; magonjwa ya wanyama; uongezaji wa ubora wa mazao; uanzishwaji wa *Roll on Roll off*

services kati ya Bandari ya Zanzibar, Dar-es-Salaam na Mombasa; na Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Karume na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar, ambao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umejitafutia wafadhili; je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuambia kwa uhakika ni mradi gani mwingine kati ya hiyo niliyoitaja angalau umefikia asilimia kumi ya mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa jibu ni hapana; basi upungufu huu unazidi kuweka mazingira ya Zanzibar kama ni ya kutengwa na kwa maana hiyo kuleta picha mbaya ndani ya Muungano wetu na katika shirikisho lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, tatizo hili Mheshimiwa Waziri ameliona; na viyi atawezza kulitattua?

Mkataba wa Jumuiya ulisainiwa Novemba 30, 1999 na ukaanza rasmi tarehe 7 Julai, 2000. Kuna mambo yamebadilika na ambayo ni vyema yakaangaliwa upya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji huu wa kisiasa pamoja na kuingiza wanachama wapya wawili na tukiangalia mazingira yalivyo, sisi tuna imani kubwa kuwa, sasa ni wakati wa kuutazama upya mkataba huu kwa njia ya kurekebisha baadhi ya vifungu ambavyo kwayo tunaamini kuwa, vimepitwa na wakati au vinahitaji mabadiliko. Hii ni kuisaidia zaidi Jumuiya yetu kwa maana ya kuifanya iwe imara zaidi kuliko hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, ikiwa tutayatekeleza vyema masharti ya mkataba wake, basi itawasaidia sana wanachama na kuwachochea wafanyabiashara binafsi. Tunaweza kusema Jumuiya hii inaweza kabisa kuwa “*people centred* na *private sector drive*.” Hivyo ni muhimu kwa Jumuiya hii kuwa:-

- (a) Wanachama wake (yaani nchi wanachama) zinaaminiana na kuheshimu uhuru wa kila nchi;
- (b) Kuendeleza mbele ujirani mwema na kuishi bila ya kugombana;
- (c) Kupigania Utawala Bora pamoja na kila mwanachama kuwa mstari wa mbele katika kutatua mgogoro wa mwenzake unapotokea;
- (d) Kujitahidi kugawana sawa sawa faida zinazotokana na ushirikiano huo; na
- (e) Utaifa wa Afrika Mashariki lazima uwekwe mbele kuliko utaifa wa nchi kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiyaweza hayo, ninaamini kuwa, Jumuiya yetu inaweza kuwa Jumuiya ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana wewe na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ahsanteni. (*Makofii*)

MHE. WILSON M. MASILINGI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007, Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114 (11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2009/2010, na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na kuliomba Bunge hili liipokee na kuijadili Taarifa hii na hatimaye kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa salama za rambirambi kufuatia ajali ya ndege ya kivita ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyotokea hivi karibuni na kusababisha vifo vya maafisa wa jeshi na hivyo kuleta majonzi kwa familia na wanajeshi na makamanda wote wa jeshi. Salamu za rambirambi zimfikie Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Waziri wa Ulinzi, Mkuu wa Majeshi yetu ya Ulinzi Generally David Mwamnyange, familia za marehemu wote wawili Major na Luteni na wote walioguswa na msiba huu. Mungu awape nguvu na roho za marehemu azilaze mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujiridhisha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati ilifanya ziara nje ya nchi na mikutano mbalimbali na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa ili pamoja na mambo mengine kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara na hali ya uhusiano wa nchi yetu na jumuiya ya Kimataifa. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukurani za dhati kwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne kwa usikivu na kutekeleza mapendekezo na ushauri wa Kamati uliolenga kuimarisha na kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii katika ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulijulisha Bunge hili kuwa tarehe 04 Juni 2010, Kamati ilikutana kupokea na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011 iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard K. Membe. Taarifa hiyo ilihu Fungu 38 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Katika kikao hicho, Kamati ilielezwa kuhusu mambo yafuatayo:-

- (i) Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara;
- (ii) Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2009/2010;

- (iii) Malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2010/2011; na
- (iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inamshukuru na inampongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri na uongozi bora katika kudumisha mahusiano mazuri na nchi zote za Afrika Mashariki, Maziwa Makuu na Mataifa mengine Duniani. Aidha, Mheshimiwa Rais amesaidia sana katika kutatua matatizo ya kifedha ili kuiwezesha Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutekeleza majukumu yake, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na ndiyo sababu hakupata mpinzani ndani ya Chama cha Mapinduzi na namtakia ushindi wa kishindo kwa sababu Muleba Kusini hana mpinzani.

Nawapongeza pia Mheshimiwa Bernad Kamilius Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa utendaji mzuri wa majukumu yao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuendeleza heshima ya nchi yetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuteuliwa kwa Dr. Asha-Rose Migiro kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na hivi karibuni uteuzi wa Dr. Augustino Mahiga ambaye alikuwa Balozi wetu wa kudumu Umoja wa Mataifa New York kuwa mwakilishi wa Katibu Mkuu katika masuala ya Somalia, ni ushahidi wa mafanikio ya diplomasia ya nchi yetu. Tunampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na atufikishie shukrani zetu na pungezi kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2009/2010, Kamati ilielezwu jinsi Wizara ilivyotekeliza majukumu yake kwa kuzingatia dhima, dira na malengo ya Bajeti kwa Mwaka 2009/2010. Aidha, Mheshimiwa Waziri alieleza kiasi cha fedha zilizopokelewa kutoka hazina kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Mwaka 2009/2010. Kwa mujibu wa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, fedha zote zilizopokelewa kutoka Hazina zilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa malengo ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge hili kuwa Kamati imeridhishwa na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010. Ni matumaini yetu kuwa Wizara hii itaendelea kuimariswa kifedha na wataalam ili kuwa madhubuti katika kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuendeleza utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi na kuimariswa taswira njema ya nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Wakati wa kupitia na kuchambua makadirio ya matumizi ya Wizara hii, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imetoa ushirikiano mkubwa na inaendelea kutekeleza ushauri wa Kamati. Taarifa ya Mheshimiwa Waziri ilionyesha kuwa kwa kuzingatia ushauri wa Kamati, Serikali imefanya yafuatayo mionganoni mwao muda hautoshi kuorodhesha yote:-

(i) Mtiririko wa fedha kutoka hazina umeimarishwa na kupunguza tatizo la kuchelewesha malipo;

(ii) Serikali imenunua majengo kwa ajili ya Ofisi zetu za Kibalozi na nyumba za wafanyakazi Marekani;

(iii) Mabalozi wapya wameteuliwa kujaza nafasi zilizokuwa wazi. Kamati inamshukuru Mheshimiwa Rais na inawapongeza Waheshimiwa Mabalozi walioteuliwa kuiwakilisha nchi kama ifuatavyo:- Mheshimiwa Balozi Alex C. Massinda – Canada; Mheshimiwa Balozi Begun Karim Taji –Ufaransa na Mheshimiwa Balozi Mohamed M. Mzale-Ubelgiji;

(iv) Utaratibu umewekwa ili kuwawezesha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya shughuli za kiuchumi na kijamii hapa nchini; na

(v) Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na nchi za Mashariki ya Kati, China na Mashariki ya mbali kwa kuweka msisistizo katika Balozi zetu kuendeleza Diplomasia ya Uchumi ikiwa ni pamoja na kutangaza fursa zilizopo nchini katika maeneo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere, Julius Nyerere *International Conference Centre* ni ushahidi mwingine wa mafanikio wa diplomasia hii tunakupongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa afikishe shukrani zetu kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kueleza makadirio ya mapato na matumizi, Kamati ilielezwu malengo ya Wizara katika eneo la Ushirikiano wa Kimataifa na diplomasia ya uchumi. Ili kutekeleza ipasavyo mipango ya Wizara, Mheshimiwa Waziri alitueleza kuwa jumla ya Sh. 112,336,928,000/= zinaombwa. Kati ya fedha hizo Sh. 67,836,928,000/= zinaombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 44,500,000,000/= ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni maoni na ushauri wa Kamati. Kamati inayo maoni na ushauri kwa Serikali kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iendeleze utaratibu wa kidiplomasia ili kuendeleza na kuimarisha usalama wa nchi yetu;

(ii) Kuhusu tatizo la muda mrefu la kukosekana kwa Serikali katika nchi ya Somalia na kusababisha tatizo la uharamia Pwani ya Bahari ya Hindi, ni vema Serikali iendelee kusaidia katika njia za kidiplomasia ili kutafuta suluhisho la kudumu;

(iii) Pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua yake ya kuendelea kununua majengo kwa ajili ya Ofisi za Balozi za nchi yetu na nyumba za watumishi nje ya nchi,

tunashauri kuwa Serikali iendelee kutekeleza uamuvi wa kununua, kujenga na kukarabati majengo ya Balozi zetu;

(iv) Balozi zetu ziwezeshwe zaidi kushiriki kikamilifu katika maonyesho ya Biashara *Trade Fairs* zinazoendeshwa katika nchi hizo ili kutangaza vivutio vya uchumi vya nchi yetu; na

(v) Ili kuепusha kuathiri bajeti na utekelezaji wa majukumu nyeti ya Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimatatifa ni vema Fungu la gharama za safari za viongozi wa Kitaifa nje ya nchi lihamishiwe kwa kudumu Hazina au Wizara ya Fedha na gharama ziwe zinalipwa moja kwa moja kutoka hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Nachukua nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Mwenyekiti na kupitia kwako kumpongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge letu Tukufu na Naibu wake kwa jinsi waliovyoongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa wakisaidiana na Wenyeviti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru tena kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Benard K. Membe; Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Mheshimiwa Balozi Seif A. Iddi; Waheshimiwa Mabalozi na wataalam wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Sazi Salula, tumesoma wote pamoja karibu miaka 30 iliyopita, kwa ushirikiano wao na kazi nzuri katika kutetea maslahi ya Taifa. Mheshimiwa Sazi Salula ukiendeleza umahiri wako maadili mema, uchapakazi wako mzuri sana uliopelekea kupandishwa vyeo haraka haraka unafanya kazi na waungwana Mheshimiwa Benard Membe na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete utafika mbali, ongeza kasi zaidi na zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu na Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri, ushirikiano na umakini mkubwa katika kuchambua bajeti ya Wizara ambayo tunaitolea taarifa. Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mwenyekiti; Mheshimiwa Musa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mjumbe; Mheshimiwa Mohammed A. Abdulazi, Mjumbe; Mheshimiwa Col. Mst. Saleh A. Farrah, Mjumbe; Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mjumbe; Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mjumbe; Mheshimiwa Hassan C. Kigwagilo, Mjumbe na Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mjumbe, ambaye nampongeza kwa sababu amewasilisha taarifa kwa niaba ya Kamati kuhusu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki na ameiwasilisha kwa umahiri mkubwa, nampa pongezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa William J. Kusila, Mjumbe; Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mjumbe; Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. John S. Malecela, Mjumbe; Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mjumbe; Mheshimiwa Col. Mst. Feteh S. Mgeni, Mjumbe; Mheshimiwa Ali

A. Mohamed, Mjumbe; Mheshimiwa Dkt. Ibrahim S. Msabaha, Mjumbe; Mheshimiwa Balozi Abdi H. Mshangama, Mjumbe; Mheshimiwa Thomas A. Mwang'onda, Mjumbe; Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mjumbe; Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, Mjumbe; Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mjumbe; Mheshimiwa Muhammad I. Sanya, Mjumbe; Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe na Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mjumbe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashililah na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Katibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo, aliyesaidiwa kwa sababu ya matatizo ya kiafya na Ndugu Hussein Athuman kwa kuratibu vikao na shughuli za Kamati hadi taarifa hii kutoka kwa wakati. Tunamwombea Katibu wetu ambaye anategemea kujifungua, ajifungue salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina shukrani maalum. Natoa shukrani za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kunipa ushirikiano mkubwa sana tangu nilipochaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati. Mashirikiano kati ya Bunge na Serikali yameonyeshwa kwa mfano na Mheshimiwa Rais kwa namna nyingi natoa mfano, amenialika nikasafiri naye kwenda Libya, India, China, Japan na muda wote alikuwa ananitambulisha kwa upendo sana na kuwa karibu naye na hata wakati mwingine kubaki na yeye na Mheshimiwa Benard Membe katika vikao vya siri na viongozi wa nchi. Hiyo ni imani kubwa na heshima kubwa kwa Bunge, nawashukuru Mheshimiwa Rais na Waziri Mheshimiwa Membe.

Namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa ushirikiano alioutoa kwangu na Kamati pale mambo yalipokuwa magumu na ikabidi tufanye mawasiliyan ya karibu na Serikali kunyoosha mambo, ahsante sana Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa ushirikiano wako ambao ulikuwa unatoa kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Mawaziri wote ambao tumekuwa tunawasimamia wakiwemo Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mambo ya Ndani ya Nchi tumeshamshukuru, Ulinzi wa Jeshi la Kujenga Taifa tayari. Nimshukuru Spika na Katibu wa Bunge safari ilizobidi tusafiri nje kufanya ukaguzi zilishughulikiwa na kuratibiwa vema sana. Nitoe shukrani za dhati kabisa pia kwa Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama kutoka Kambi ya Upinzani wameonyesha uzalendo mkubwa hawakutoa siri za Kamati na muda wote usingeweza kutofautisha nani Mbunge wa CCM na nani Mbunge wa Kambi ya Upinzani. Ni pongezi za dhati na moyo huu wa kizalendo uendelee hivyo hivyo na hata tuliposafiri nje na Mheshimiwa Khalifa Khalifa hakukuwepo mvutano wa aina yoyote. Tulikuwa tuna msimamo mmoja kwa diplomasia ya nje na heshima ya nchi yetu ilidumishwa kutokana na ushirikiano huu, muudumishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa kunipa imani na ushirikiano mkubwa nilipokuwa naongoza Kamati hii hadi mukutano huu wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Waziri wa Utawala bora pia alikuwa anawasilisha taarifa za usalama wa Taifa letu, zilizokuwa zinawasilishwa wakisaidiana na Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa na Naibu wake wa Idara ya Usalama wa Taifa Mkurugenzi Mkuu Othman na Naibu wake Ndugu Luzoka. Tunawapongeza sana kwa uzalendo wao na ushirikiano wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za dhati kabisa na za kipekee nawashukuru Waziri wa Ulinzi na Mkuu wa Majeshi kwa kunipa heshima kubwa kuwa Mgeni Rasmi mwishoni mwa mwaka jana katika kuzindua maonyesho ya kumbukumbu ya miaka 45 ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na hiyo ni heshima ambayo nilipewa na sitawasahau. Anayekupongeza hadharani na wewe unamshukuru hadharani. Aidha, Mheshimiwa Rais kunikumbuka siku ya Malaria Mnazi Mmoja akanipongeza nashukuru. Bila yeze Muleba tulikuwa tumeshakwama, akatukwamua, Mheshimiwa Kikwete, Rais, tunamwombea kwa Mungu, hatuna cha kumlipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niwashukuru Wabunge wote na ninyi mlikuwa mnaniwa ushirikiano wote tukikutana tunacheka na kupiga michapo na nitawamisi sana kama sitarudi lakini Mwenyezi Mungu atuwezeshe kurudi wote tuendelee kukutana na kushirikiana *Inshallah* Mungu atasikia dua zetu tuwe na afya njema na wapiga kura wataendelea kuwa na imani na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Shilingi 112,336,928,000/- kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kabla sijaunga mkono hoja kwa kumshukuru Mheshimiwa Dr. Kamara ambaye naye amewasilisha hotuba yake kwa umahiri mkubwa na ambayo nayo pia tumeshaunga mkono kama Kamati na kwa kazi nzuri na ushirikiano alionipatia na Wajumbe wa Kamati yetu kwa umahiri mkubwa, namwombea ashinde kwa kishindo, arejee Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Kwa heri ya kuonana Mwenyezi Mungu akipenda. Ahsante kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani kwa niaba ya kambi ya Upinzani kwa kunipa fursa hii ili kutoa maoni ya kambi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kwa mujibu wa kanuni za Bunge kifungu cha 99(7), toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa neema na rehema kwa kutujaalia afya njema na uzima. Aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo la Gando kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono kwa dhamana hii nzito waliyonipa ya kuwawakilisha katika chombo hiki nyeti. Kwa umuhimu wa kipekee ni kwa wanachama wa Chama Cha Wananchi (*CUF*) Jimbo la Gando kwa kunipa kura za ushindi katika uchaguzi ndani ya Chama kuwa mgombea wa nafasi hii kwa kipindi kijacho cha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wetu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa kwa kutoa mwongozo sahihi kwa Kambi kwa mujibu wa kanuni za Bunge. Pia niwashukuru wenzangu wote katika Kambi ya Upinzani kwa msaada na maelekezo mazuri waliyonipa wakati wa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sijatenda haki kama sitamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaonipa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sera mpya ya mambo ya nje, suala la manufaa kiuchumi ndilo lililopewa kipaumbele cha kwanza kama dira ya maamuzi yetu kuhusiana na siasa za Kimataifa. Ni wazi watumishi waliokabidhiwa majukumu ya kutekeleza sera hii wana changamoto kubwa ya kuhakikisha tunapata vyanzo vingi vya uwekezaji na nafasi za kuuza bidhaa zetu kwa thamani iliyo bora kwetu. Lakini vilevile ni sera hii ndiyo inayopaswa kutulinda na hatari za wawekezaji uchwara na wasio waaminifu. Kwa miaka kadhaa sasa tumeshuhudia mmiminiko wa wawekezaji uchwara wanaotumia mapungufu yetu kutuingiza katika mikataba yenyе kuhatarisha maslahi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka Waziri atueleze inachukua muda gani, pale kampuni ya Kitanzania kupata taarifa za kampuni ya nje inayotaka kufanya nayo biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limekuwa tatizo kwa balozi zetu kutupatia taarifa, hivyo wakati mwingine tunashirikiana na makampuni feki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watendaji na Wawakilishi wetu Wizarani. Taswira hii ya nchi yetu katika nyanja za siasa, uchumi na utamaduni itapewa hadhi pale tu timu hiyo ya wanadiplomasia itakapokuwa imeundwa kwa umakini zaidi. Umakini ninaouzungumzia hapa ni pamoja na kujali taaluma na sifa binafsi za kiutendaji (*personal integrity*) katika kuteua timu ya wanadiplomasia hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya siasa za Kimataifa hivi sasa yanatalazimisha kuacha mara moja mtindo wa kuteua Mabalozi na Wawakilishi wengine wa nchi yetu kwa kuzingatia kujuana. Hatuwezi kuendelea kunyamaza huku tukiona watu mbalimbali ambao tayari wamelisababishia Taifa letu hasara kwa namna moja ama nyingine, kubwa katika majukumu waliyokuwa nayo mwanzoni ama wananyamaza kimya au wanapewa jukumu la kuongoza na kulinda maslahi ya Watanzania nje ya nchi yetu. Au watendaji ambao tayari wanakaribia umri wa kustaafu lakini bado

wanachaguliwa kuliwakilisha Taifa nchi za nje. Je, ni kweli uteuzi kama huo unaleta tija kwa Taifa letu au ni kulitia hasara Taifa ya kumsafirisha mtu huyo na familia yake na baada ya muda mfupi inaingia gharama za kumrudisha. Kwa utumishi wa ndani mwisho wa utumishi ni miaka 60 hivi kwenye sekta hii ya Ubalozi tunaweza kwenda mpaka miaka 100? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wote duniani wanaiangalia nchi ya Uchina kama eneo nyeti (*strategic post*) kwa maslahi ya kiuchumi duniani, hivyo wanahakikisha wawakilishi wanaowatuma huko ni mahiri na wallobobe katika fani za diplomasia na uchumi wa dunia. Hivyo, Tanzania kama nchi tumeshindwa kuliona hilo na ndio sababu kubwa bidhaa zenyе ubora hafifu zinaingizwa nchini kwa wingi toka uchina, hii haina maana kuwa uchina hawatengenezi bidhaa zenyе ubora wa hali ya juu, suala ni kuwa wawakilishi wetu wameshindwa kutoa mwongozo kwa Watanzania na wenye viwanda wa Uchina juu ya bidhaa zinazotakiwa kuingia Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaitaka Wizara iweke watendaji walio na uchungu wa maendeleo ya nchi yao, kuliko kupeleka watendaji ambao wanakwenda kufikishia muda wao wa kustaa fu tu na kujilimbikizia mali na kusahau wajibu wao kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika enzi hizi za ushindani mkubwa wa kimaslahi, uajiri lazima uangalie ujuzi na uwezo wa kitaaluma utakaowawezesha watumishi kupigania na kutetea maslahi ya wananchi wetu kwa kutumia hoja zenyе nguvu, zenyе kulenga ufanisi mkubwa. Matokeo yake Wizara hii imegeuka *strong room* ya siri zisizo siri ambazo hata Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu aliwahi kuhoji ni madudu gani yanayofichwa huko? Hii inatokana na ukweli kuwa Wizara bado inao baadhi ya watendaji wasio na upeo wa juu wa fani ya diplomasia na siasa za Kimataifa na hivyo kutokuwa tayari kuwa wazi ili wananchi wahoji utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia. Chuo cha Diplomasia kilichopo Kurasini, Dar es Salaam ni moja ya taasisi zinazofanya kazi chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Katika ripoti ya mafanikio ya Wizara hii katika Serikali ya Awamu ya Tatu, imeelezwa kuwa, chuo kimefanikiwa kwa kuongeza programu zake kutoka nne hadi tisa. Programu hizo zinalenga masuala ya *Management of Foreign Relations, Economic Diplomacy, Defense and Security management, Strategic studies, Conflict Resolution, Peace Studies, Protocols and Public Relations na International Relations and Diplomacy*.

- Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji, ni jinsi gani chuo hicho kinasaidia katika kufanya tafiti mbalimbali katika programu hizo na jinsi ambavyo zinasaidia katika kuandaa miongozo ya mahusiano ya Kimataifa ya Wizara hiyo pamoja na kujiunga au kujitoa katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda? Kuikubali au kuikataa mikataba mbalimbali ya Kimataifa, ambayo viongozi wetu wanatia saini kwa niaba ya nchi na kuileta Bungeni kui-ratify tu?

- Chuo kinawezeshwa vipi ili kiweze kutimiza majukumu makubwa kilichopewa?

- Watumishi wa chuo hicho kama Walimu au Wahadhiri wanaandaliwaje ili wabebi majukumu hayo mazito na kuendana na mabadiliko yanayotokea hivi sasa ulimwenguni? Na haki na maslahi yao yanaangaliwa vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Chuo hicho cha Diplomasia kiwe *think tank* ya Wizara kwa kufanya tafiti mbalimbali kutanabaisha hali ya kiuchumi na kisiasa ya Kimataifa ili watendaji wa Wizara waweze kupata ushauri kutoka kwa watafiti wa chuo hicho pamoja na kuanda semina mbalimbali kwa watendaji wa Serikali ili kuboresha taaluma zao katika masuala ya uhusiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ilikwishatoa ushauri kuhusiana na masuala kadhaa yafuatayo yatekelezwe ili kuboresha matumizi ya chuo hiki. Chuo hiki kiongezewe hadhi mara moja na kuwa chuo kikuu shiriki cha UDSM yaani *University of Dar es Salaam School of Diplomacy* ambacho kitabobebe katika kutoa shahada za juu za masuala ya kidiplomasia na strategia. Je, ushauri huo tuliookwishautoa umefikiriwa? Kama ndio, utekelezaji wake umefikia hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa *APRM* umeridhiwa na nchi hii kwa muda mrefu sasa. Uongozi wa kusimamamia Ofisi hii ikiwemo Baraza la Usimamizi la Taifa ambalo linasimama kama Bodi ya Wakurugenzi lipo na watumishi wake wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kujiunga na mpango huu, Tanzania imeingia katika orodha ya nchi ambazo zimeonekana siyo tu kuwa zenye mkakati wa kuondoa kero za utawala bora bali iliyo tayari kukosolewa. Hayo yalisemwa na Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya M. Kikwete Septemba 11, 2009 wakati akizindua Baraza la Usimamizi la Taifa la *APRM*. Alieleza dhamira ya wazi ya Serikali yake na yake binafsi kuhakikisha Tanzania inatumia mradi wa *APRM* kuchangia maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na dhamira hiyo nzuri ya Mheshimiwa Rais wetu kuona mradi huu unakuwa msaada katika dhamira yake ya kuimarisha utawala bora nchini, takwimu za bajeti ambazo Wizara husika imekuwa ikizipanga kwa ajili ya mradi wa *APRM* zimekuwa chini ya nusu ya mahitaji kama yanavyopangwa na Baraza la Usimamizi la Taifa la *APRM* na hata wakati mwengine pale inapoidhinishwa bajeti si kiasi chote hutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limekuwa likitenga fedha hapa Bungeni ili kufanikisha mpango huu. Kambi ya Upinzani inasikitishwa na hali halisi ambayo watumishi wa mpango huu hawawezeshwi. Kwa msingi huo tunamtaka Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje alieleze Bunge lako Tukufu hali halisi ya utendaji wa kazi wa *APRM* hapa nchini ikiwa ni pamoja na hatua iliyofikiwa na kwa nini hadi sasa nchi yetu bado haijaridhia kuja kuhakiki taarifa ya awali ya tathmini ya utawala bora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makusudi Wizara haithamini kazi iliyokwishafanyika na Kambi ya Upinzani inaona hayo ni sawa na matumizi mabaya ya rasilimali za Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaona kuwa athari za kutokutoa fedha za kutosha kulingana na mahitaji ya Baraza kufanya kazi zake, athari yake shughuli walizojipangia kulingana na ratiba yao zinashindwa kutekelezwa na hivyo mradi kuonekana ni gharama kubwa kuu-*maintain*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mchakato wa Tanzania kuwa na Uraia wa Nchi Mbili (*Dual Citizenship*) Mheshimiwa Waziri ameutaja sasa hivi na sisi tumefurahi tu kuutaja. Kambi ya Upinzani inasikitika kwa uamuvi wa Serikali kuamua kuwa uamuvi wa kuwa Watanzania wanaweza kuwa na uraia wa nchi mbili bado ni kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani kama mdau mkuu wa hoja hii kwani kwa muda mrefu imekuwa ikisisitiza uanzishwaji huu. Katika kuongelea hoja hiyo tumekuwa tukiainisha manufaa ambayo yanaweza kupatikana kutoka kwa Watanzania au raia wengine ambao wanahitaji uraia wa Tanzania. Hasa hasa manufaa ya kiuchumi, katika mpango wa uchumi mbadala tulishauri kuwepo kwa kitu kinachoitwa *Diaspora bond* hii ni kwa Watanzania wanaoishi nje, lakini kuwa Watanzania ambao wamekwishachukua uraia wa Mataifa mengine zaidi ya Tanzania na hivyo kisheria sio Watanzania lakini bado wanapenda kushiriki katika maendeleo ya Tanzania. Hivi nchi yetu ina hofu gani juu ya jambo hili? Woga huu ni kwa maslahi ya nani hasa? Sasa wakati umefika wa jambo hili kufanya mara moja, tunaomba tujue ratiba kama alivyosema Waziri katika hotuba yake, tunaomba tupate ratiba ya utekelezaji wa nia hiyo nzuri ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi ya Serikali. Kulingana na hali halisi ya kiuchumi inayoikabili nchi yetu. Wakati umefika sasa wa kupunguza matumizi katika mambo mengi zikiwemo safari za nje, uwakilishi wetu kwenye mikutano ya Kimataifa uendane na mahitaji ya mikutano yenyewe ili kubana matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi zetu zimekuwa na masuala kadhaa yanayohusu kutokufuata kanuni za matumizi ya fedha. Lakini kwa ufupi tu, Balozi zilitumia fedha zaidi ya makisio yaliyoidhinishwa jumla ya shilingi 16,073,916,142 isivyotakiwa, upotevu huu ni mkubwa sana na kwa bahati mbaya makosa yanayosababisha upotevu huu yanajirudia mara kwa mara, hii ni kwa kiasi kikubwa inachangiwa na kutofuata ushauri unaotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anaoutoa mara kwa mara katika taarifa zake, Dola za Kimarekani 182,401, Paundi za Kiingereza 79,568, Euro 286,080, Dinari 126,138.87 na Faranga za Uswisi 1000. Jumla kuu ya fedha zote ni shs. 16,073,916,141.95

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu huu ni mkubwa sana na kwa bahati mbaya makosa yanayosababisha upotevu huu yanajirudia mara kwa mara, hii kwa kiasi kikubwa inachangiwa na kutokufuata ushauri unaotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa

Hesabu anaoutoa mara kwa mara katika taarifa zake. Hivyo basi, tunaitaka Serikali iwe makini zaidi katika kufuatilia maagizo yanayotolewa na Mdhhibitii Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushauri kwa Wizara jinsi ya kupunguza matumizi. Kambi ya Upinzani inatoa ushauri ufuatao ili kupunguza gharama:-

- Kwa baadhi ya nchi hutumia utaratibu wa kuteua Mabalozii wa Heshima (*Honorary Councilors*).

- Sehemu ambazo tuna uwakilishi lakini ni kwa uhusiano wa kisiasa tu na hakuna faida za kiuchumi, tunaweza kupunguza Mabalozii katika nchi hizo.

- Serikali ijithabidi sana kununua majengo yake ili kujiwekea rasilimali ugenini kitu ambacho kinafanyika na pia kubana matumizi kwa sababu majengo ya kukodi yana gharama kubwa kama ambavyo tunaona katika sehemu mbalimbali duniani.

- Wakati nchi yetu ina matatizo ya fedha, bado wapo Watanzania wenzetu wanaofuja fedha kwa maslahi yao hawa wachukuliwe hatua mara moja.

- Hali ya makazi ya baadhi kwa Mabalozii wetu ni mbaya na ya kutisha sana, hivyo hatua za dharura zichukuliwe na Serikali za kufanya ukarabati wa nyumba hasa zile za makazi ya Mabalozii na Maafisa wa Kibalozi ili kuepuka hatari ya ndugu zetu kuangukiwa na majengo.

- Kwa zile sehemu ambazo nchi yetu inamiliiki maeneo ya kujengwa, Serikali ikope katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii ili kujenga majengo hayo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri.

- Aidha, Serikali yetu iingie mikataba na watu binafsi wenye uwezo na utaalami wa kuweza kujenga ili ilipe baadaye kwa utaratibu maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda nikushukuru wewe binafsi, nimshukuru sana Mheshimiwa Spika na Ofisi yake kwa ujumla kuwa msaada na mabadiliko makubwa waliyoyaleta kwenye Bunge letu. Bunge hili sasa lina heshima kubwa ndani ya nchi na nje ya nje ya nchi yetu na naamini wale ambaa labda wanadhani kuwa maneno yanaweza kulidhalillisha Bunge hili basi maneno hayasaidii kwani Bunge hili litaimarika, Ofisi ya Spika itaimarika na naamini Spika wetu kwa sababu ana nia njema na nchi yetu na Bunge hili atarudi na huenda atatuongoza tena katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nawatakia kheri Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote na Mwenyezi Mungu anasema wale wanaotakiana kheri basi yeye huwabariki katika kheri, tutakiane kheri sote ili turudi kuwatumikia Watanzania hapo Novemba, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana tena kwa kunipa fursa na baada ya kuyatoa hayo machache kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sasa hatujaelekea kwenye wachangiaji wa hoja hizi mbili ambazo zimewasilishwa mbele yetu naomba nichukue fursa hii kuwatangaza wageni ambao wamefika hapa Bungeni leo hii.

Kwanza kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Bernard K. Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambao ni Bwana Sazi B. Salula, Katibu Mkuu wa Wizara; Balozi Mohamed Mzale, Mkurugenzi Idara ya Mashariki ya Kati; Balozi H. Mrango, Mkurugenzi Idara ya Ushirikiano wa Kikanda ambaye hayupo; Balozi Francis Malambugi Mkurugenzi Idara ya Afrika; Balozi Begum Taj Mkurugenzi Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa; Balozi Anthony Italilo, Mkurugenzi Mkuu wa Itifaki; Balozi Mohammed Hamza, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje Zanzibar; Bwana Katinda E. Kamando, Mkurugenzi Idara ya Sera na Mipango; Bwana Shaban Mnubi, Mkurugenzi Idara ya Utawala na Raslimaliwatu; Bwana Savo Mung'ong'o, Mkurugenzi Fedha na Utawala *AICC*; Bwana Mawazo Kaducha, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Ulaya na Amerika; Bi. Riziki S. Mngwali, Kaimu Mkurugenzi wa Chuo cha Diplomasia; Bwana Rogatius Shao, Kaimu Mkurugenzi Idara ya Asia na Australia; Bi. Rehema Twalib, Katibu Mtendaji wa Mchakato wa Afrika wa Kujitathmini Wenyewe *APRM* yaani *African Pier Revies Mechanism*. Karibuni sana. (*Makofî*)

Aidha, Mheshimiwa Waziri ana wageni wake binafsi ambao ni: Bwana Tasilo Membe ambaye ni mdogo wake, Bwana Joseph Kulwa Kahama, Ndugu Renata Marie, Ndugu Sophia Wandiba, Ndugu Filsan Ainan Abdulahi na Ndugu Dunga Ludovick. Karibuni sana. (*Makofî*)

Vilevile kuna Wakuu wa Vitengo mbalimbali wanne ambao wameambatana na msafara huu wa Wizara, wako wageni 20 kutoka Jimbo la Mtama, naomba wasimame wote kwa pamoja. Karibuni sana. (*Makofî*)

Pia wapo jumla ya Maafisa 44 kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Vile vile kuna mgeni wa Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ambaye ni mkewe Bi. Asha Suleiman, huyu ni Mke wa Mheshimiwa Mbunge lakini pia huwa anamwakilisha Mheshimiwa Mbunge kumfanyia kazi zake za Ubunge pale Jimboni Mheshimiwa anapokuwa hayupo. (*Makofî*)

Kuna Wajumbe wa Bodi ya *United Nation Association (UNA)* Tanzania ambaye ni Ndugu Tatu Mnanga Issa na Ndugu Sillesi Malli Karibuni sana. (*Makofî*)

Sasa ni wageni kutoka Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wageni wa Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Balozi Juma Mwapachu, Katibu Mkuu Jumuiya ya Afrika Mashariki, hayupo!

Waheshimiwa Wabunge kutoka Tanzania ambao wanaiwakilisha Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Fortunatus Masha, Mheshimiwa Said Ghalib Bilali, Mheshimiwa Kabourou Aman, Mheshimiwa Didas Masaburi, Mheshimiwa Sebtuu M. Nassor, Mheshimiwa George Nangale, Mheshimiwa Kate Kamba, Mheshimiwa Janeth Mmari na Bwana Jucandunus Filbert. (*Makofi*)

Aidha, Mheshimiwa Waziri ana wageni wake binafsi kama ifuatavyo; Bi. Adelaida Kamala ambaye ni mke wake, Ndugu Karenrose Kamala ambaye ni mtoto wake, Ndugu Catherine Kamala pia mtoto wake, Ndugu Glory Rwekaza ambaye ni Mpwa wake na Ndugu Frank Theodory. Karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Pia wapo jumla ya Wakurugenzi Wakuu wa Idara na Maafisa 27 kutoka Wizara hiyo ambao wameongozwa na Dr. Stergomena L. Tax ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara na Bwana Uledi Mussa ambaye ni Naibu Katibu Mkuu. Karibuni sana.

Wageni wengine ni wa Mheshimiwa Halima J. Mdee ambao ni wanafunzi watatu kutoka Merriwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka ambao ni Walimu 30 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwa pamoja naomba msimame, naona hawapo watakuwa *Basement*.

Vilevile kuna kikundi cha watoto wa Kanisa la Morovian 28 wakiongozwa na Walimu wao pamoja na walezi, kwa pamoja naomba msimame. Karibuni sana na hongereni sana kwa hilo vazi lenye rangi ya bendera ya Taifa.

Vilevile kuna jumla ya wanafunzi 40 kutoka Shule ya Upili Sekondari ya Wasichana Msalato, kwa pamoja naomba msimame. Karibuni sana muangalie jinsi tunavyoendesha shughuli za Bunge na mmepependeza sana.

Mwisho wa matangazo lakini Waheshimiwa Wabunge kuna tangazo la semina, Ofisi ya Katibu wa Bunge inawatangazia kuwa kutakuwa na semina kwa Wabunge wote siku ya Jumapili tarehe 04/07/2010 saa 4:30 katika ukumbi wa Pius Msekwa. Semina hiyo itahusu Shirika la Nyumba la Taifa kuwa na mpango wa uanzishaji Mji mpya wa Kigamboni na itaratibiwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na kwa taarifa hii Mheshimiwa Waziri pia ameniandikia kwamba itifaki itazingatiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo sasa tutakuwa tunafuatiwa na wachangiaji sita wa mwanzo ambao wako hapa mbele yetu ili waweze kujiandaa na utaratibu ambao watachangia:-

Mchangaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Basil Mramba ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Kabwe Zitto na mtu wa sita, katika orodha hiyo atakuwa Mheshimiwa Said Amour Arfi. Tuanze na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed tafadhali!

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kwanza kuchangia, kwanza niwapongeze Mawaziri wote kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwasilisha hotuba zao. Lakini kwa sababu ya muda niende moja kwa moja kwenye mada tu na niseme tu kwanza nawapongeza ndugu zetu wa Ghana, jana walicheza mpiga mkubwa sana, walituonyesha kwamba Waafrika tunaweza kama tukiandaliwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na moja ambalo nataka kulisema ni suala zima la kuendeleza mchakato wa kutambua Jumuiya ya Watanzania wanaoishi Ughaibuni. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amesema kwamba wanaendelea na *programme* hiyo, lakini jambo hili limechukua muda mrefu, lakini baya zaidi hakuna mwongozo hasa namna gani Balozi zetu zinaweza kufanya kazi na hawa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza kwenda kwenye nchi, kwa mfano, nilikuwa Canada hivi karibuni, nikakuta kuna vyama viwili pale yaani kuna vyama vya Watanzania wanaotoka Zanzibar na wanaotoka Bara, basi ikabidi tukae pale tuone kwamba wanawezaje kuungana wakaanzisha kitu kimoja. Sasa nasema hakuna miongozo maalum ya kuweza kuwaongoza hawa vijana wetu, ni namna gani waweze kuanzisha taasisi zao ambazo zitaratibiwa na zitazisaidiwa na Serikali, mwongozo huo hakuna kwa Mabalozi wala kwa vijana wenyewe mpaka hivi sasa. Kwa hiyo, tunasema tu lakini hakuna mwongozo madhubuti uliotolewa. Kwa hiyo, naomba la kwanza kufanyika iwe ni mwongozo madhubuti utakaotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile waelezwe faida watakazipata huko kwao, wengine wamekuja hapa kutaka kufanya au kuanzisha biashara lakini wamepata vikwazo wameondoka na wana uwezo mkubwa tu wa kufanya hayo. Kwa hiyo, nasema bado hakuna utaratibu na *coordination* nzuri baina ya Balozi, Wizara na Taasisi nyingine za Serikali kutambua umuhimu wa hawa vijana wetu. Nchi kama Kenya inapata si chini ya bilioni 700 kila mwaka kwa *Diasporas* lakini sisi hatupati kitu kwa sababu hatuna utaratibu mzuri. Kwa hiyo, cha kwanza naomba hilo lifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili tumetangaza hii Sera ya Diplomasia ya Kiuchumi, lakini nafikiri bado ni nadharia kwa sababu hakuna ubalozi unaoweza kuwaambia wewe katika nchi yako unayotuwakilisha sisi kama nchi Tanzania tunategemea hapo utufanyie mambo kadhaa, hakuna! Kwa hiyo, kila mmoja anaogelea

vile anavyoweza mwenyewe. Leo unakwenda pale anakwambia Waziri karibu hapa unaalikwa mahali Fulani, unakutana na Wafanyabiashara unaondoka, ndiyo yamekwisha!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuwe na malengo kwa kila nchi kwa sababu Tanzania tumefungua Ubalozi mahali fulani basi hapo malengo yetu ni haya na haya, ndiyo wenzetu wanavyofanya, sasa sisi hatuna tunaogelea tu. Kwa hiyo, Mabalozi wetu kule na wao wanaogelea tu na bahati mbaya hakuna utaratibu wa kuleta taarifa, halafu taarifa zikafanyiwa kazi na wao wanakuwa *disappointed* wanaona aha! Hata nikipeleka zinakaliwa na *Desk Officer* mmoja basi yamekwisha. Kama tumebadilisha sera basi ni lazima kuwe na mkakati wa utekelezaji, sasa hakuna mkakati wa utekelezaji, kwa hiyo, Balozi aliyekuwepo pale hajui afanye nini anafanya ya jumlajumla na hili si jambo jema, pengine amngoje tu Rais, pengine akienda kutembelea pale awakusanye wafanyabiashara wakutane ndiyo kazi kubwa anaweza kufanya, lakini kumbe kuna mengi zaidi anayoweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo linaweza kufanyika ni kwamba nchi yetu inafanya biashara na nchi mbalimbali, wafanyabiashara wa Tanzania wamesafiri kutoka hapa mpaka Marekani na Rais, pamoja na Wakurugenzi wa Taasisi ya EPZ. Wakurugenzi wale wanaelezea *EPZ facilities* zilizopo Tanzania lakini wafanyabiashara Watanzania wanaotoka Tanzania hawajui wanazisikia mara ya kwanza Marekani. Sasa kumbe wewe mwenyewe ndani hukujitayarisha kwa watu wako wenyewe ambao unahitaji watu hao waingie ubia na wale unaowapelekea, wao hawana taarifa lakini mgeni ndiyo ana taarifa. Tumeelezwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tulipokwenda kutembelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna kasoro nyingi sana za kijiandaa sisi wenyewe ndani, taasisi zetu bado hazijafanya kazi ya kuwaelimisha Watanzania fursa zilizopo Tanzania, wageni wanazijua zaidi fursa zilizopo Tanzania kuliko Watanzania wanavyojua fursa zilizopo ndani ya nchi na hivyo hivyo Mabalozi wetu wana hali hiyo. Kwa hiyo, nafikiri kuna haja ya kuandaa mkakati hasa wa hii Sera tunaitkelezaje na tutapata manufaa gani kwa Balozi ambaye yupo kwa mfano, Uingereza? *Role mission* yetu katika programu ya maendeleo ya kiuchumi unakutaka ufanye nini, kwa *private* sekta, sekta gani utawasiliana nayo na tuwe na utaratibu wa *communication* hapa kwetu unaletewa taarifa unakaa nayo tu, sisi hapa tulipo ndani unaandika barua miezi mitatu hujibiwi, sijui Balozi ye ye anajibiwa lini? Sasa kasoro hizi kama hatutaziondoa kwenye ushindani wa kibiashara hatuwezi kufanikiwa. Hilo lilikuwa jambo la pili ambalo nilitaka niliseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni hili suala la *Dual Citizenship*. Tumelizungumza muda mrefu na nashukuru Waziri amelizungumza kwa sauti kali sana. Ile hamasa uliyoitia pale imetupa matumaini kwamba Bunge linalokuja la mwanzo kabisa tutakuta Sheria iko tayari. Tunasema hivyo kwa sababu kama leo tumefungua mipaka ya Afrika Mashariki, wana wa Afrika Mashariki watembea na *Identity Card* zao watakuwa

tayari wametambuliwa. Lakini Mtanzania aliyeo nje ana uwezo mkubwa wa kutaka kufanya *investment* hapa kwetu, lakini imekuwa ni tabu maana mnam-*treat* kama mgeni na yeze anafanya hayo kwa uchungu kwamba hii ni sehemu ya nchi yangu niliyozaaliwa. Sasa nafikiri haya tuyaangalie katika dunia ya leo haya mambo ya uraia yatakwisha tu mbele ya safari kwani dunia itakuwa ni kisiwa kimoja tu, muhimu ni *identity* yako inayokuonyesha unatoka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilifikiri hili Mheshimiwa Waziri ajitahidi tutakapokuja mwezi Januari naamini wengi tatarudi hapa na kama hatutarudi itakuwa ni bahati mbaya tu lakini wengi watarudi, angalau hilo liweze kuanza mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nilitaka kuzungumzia Afrika Mashariki kidogo. Makampuni ambayo yapo kutoka Kenya, nilikuwa naangalia page 102 ya jedwali namba 4, makampuni yaliyoko Kenya mpaka 2009 yalikuwa 193, Makampuni ya Tanzania yaliyofungua biashara Kenya ni 15, nafikiri na Uganda yako 15 ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuko mbali sana, jana Rais Kibaki nimemsikia akisema ni makampuni zaidi ya mia mbili na zaidi tayari yanafanya biashara Tanzania, sisi bado tuko makampuni 15, unajua sababu yake ni nini? Sababu zake ni tatu:-

Ya kwanza, ni lile lile kwamba Watanzania wenye hawajajua fursa zilizopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, hawajajua kabisa. Tunaona kama kuna siasa tu lakini zile *benefit* za kiuchumi katika soko hili kubwa la watu milioni 100, bado Watanzania wengi hawajalifahamu hata wale wafanyabiashara. Hilo la kwanza.

Ya pili, bado hatujajenga taasisi za kuweza kuwasaidia hao wachache amba wanataka kufanya hiyo biashara, wenzetu wa Kenya wameshajenga *Financial Institutions* ambazo tayari zina uwezo wa kusaidia. Juzi hapa tulikuwa tunazungumza kwenye Madini kwamba ukienda kwenye benki zetu wanakwambia sisi hatuna uzoefu wa kukopesha watu wa madini, ukitazama Tanzania hakuna mkoaa ambaa hauna Madini hata Dar es Salaam lakin benki zinakwambia hatuna uzoefu wa kukopesha watu wa madini, kwa hiyo hawakopeshwi.

Ukienda benki ukawaambia unataka kukopeshwa kwa ajili ya uvuvi wanakuambia sisi hatuna uzoefu wa mambo ya uvuvi, wanachojua wao ni biashara ya kununua na kuuza, hatuna benki za uwekezaji. Kenya kuna *Financial Institution* ambazo ni *very strong* ndiyo maana makampuni yao yameweza kufanya biashara ndani ya Kenya na nje ya Kenya. Sasa hili kama viongozi wa Serikali hamjaka mkali-*address* na *Central Bank* bado tutakuwa tunapiga hadithi tu hapa na hata siku moja hatutaweza kuingia kwenye ushindani wa kibiashara kama *Financial Institution* zetu haziko tayari kuweza

kuwaondoa Watanzania katika umaskini. Ndiyo maana sisi tukasema katika bajeti yetu angalau 20% ya *deposit* ya benki hizi zielekezwe kwenye sekta mbalimbali, ukiweka sekta 15 au 10 iende madini, tano iende madini, sekta nyingine iende uvuvi na kadhalika.

Huu ndiyo utaratibu peke yake unaweza ku-stimulate uchumi na kuwaingiza Watanzania kuingia katika soko hili, vinginevyo urari wa biashara tutajisifu Watanzania kwamba tuna *export* lakini yatakuwa ni Makampuni ya Kenya yaliyopo hapa, yanazalisha ndiyo *yana-export* na wao wataweza kujenga mtaji wao kwa sababu ile *corporate tax* baada ya kutoa faida wanayopata itakwenda kwenye nchi yao. Hiyo ndiyo *result end* yake. Kwa hiyo, ni kweli tutapata ajira na kadhalika lakini kwa kweli yale manufaa hasa ambayo Watanzania kama kuurithi uchumi wao hautatokea hata siku moja katika Tanzania. Hilo lilikuwa ni jambo moja ambalo nataka niliseme.

Ya tatu ni hili, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ukiangalia kesi zote zilizokwenda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatokea Kenya, Watanzania na wengine hawajui hasa manufaa na kazi za Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki lakini Kenya wao wameshapeleka kesi zaidi ya tano. Kwa hiyo, sisi hatujui hata kuvitumia hata hivi vyombo ambavyo tunavyo hivi sasa. Kwa hiyo, Serikali inachangia lakini hatuoni faida ya mchango tunaoutoa. Sasa hili nasema ni tatizo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba vilevile kwamba tunao Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini utaratibu wetu wa kuwapata Wabunge kwa kila Bunge una tofauti. Sasa hamwezi kujenga umoja wakati hamja-*harmonise system* ya kuchagua katika chombo cha Umoja. Tuna *different system* ya kupata Wabunge hapa, Kenya na Uganda, hatuwezi kufanya hivyo. Kama ni Bunge la Afrika Mashariki utaratibu wake wa kupatikana uwe wa aina moja, kwa hiyo kama kuna kanuni za Tanzania tuzirekebishe zioane na kanuni za Kenya na wengine, tukubaliane kwamba hii ndiyo *modality* ya kuwapata Wabunge, hakuna kanuni nyingine kama unasema ni kutoka upinzani wawe watano kila mahali, utaratibu wake wa kupatikana uwe ni wa aina moja wote lakini hatujafanya hivyo na *area* nyingi hatujazifanya namna hiyo. Kwa hiyo, hatuwezi kushirikiana kama zile sheria na taratibu hamja-*harmonise* mkawa na utaratibu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho ni suala zima la demokrasia. Tuko katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, utaratibu wetu wa kuwapata viongozi kuingia katika madaraka ni tofauti kidogo. Tumeona matatizo ya Burundi, juzi ni wanachama wetu tupo pamoja nao, sasa haya kama hatujayaonyesha tukaya-*address* na tukamwambia mwenzetu umekuja katika umoja huu ndiyo utaratibu wetu, hutaki utatoka, nafikiri hatutafika mahali pazuri hata kidogo. Kwa hiyo, *harmonisation* ya *procedure* hizi za kuwapata viongozi na za kufanya biashara lazima ziwe *unified* ili Watanzania, Wakenya, Waganda na Warwanda wayafahamu bila ya hivyo tutapata matatizo makubwa.

Nashukuru sana Waziri ametutoa hofu katika suala zima la ardhi, naomba tuendelee na hilo kwanza bado mapema sana, suala la wataalam vilevile tuendelee nalo

lakini tusikae chini bali tufanye kazi. Jana tulikuwa tunaangalia takwimu za wasomi wa Kitzanzania, wasomi wa Kenya, wa Rwanda na Uganda, hali yetu ni mbaya sana, hali yetu nasema ni mbaya sana katika ushindani wa kielimu. Bajeti yetu ya kielimu ni mbaya tunahitaji kuli-*address* hili mapema sana na tuli-*address* kwa *operation* siyo kuli-*address* hivihivi kienyejenyeji iwe ni kwa *operation* kabisa. Huwezi ukakiacha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam miaka 30 leo bado kinachukua wanafunzi 15,000 au 16,000, huwezi! Leo Tanzania tulitakiwa angalau *minimum* tuwe tunatoa wanafunzi 150,000 lakini hatujafika huko wenzetu Kenya wameshafika angalau 100,000. Hii ni hatari katika ushirikiano.

Kwa hiyo, nafikiri suala la elimu ni suala la msingi kuliangalia ndani ya Tanzania tunafanya nini ili tuondoke tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, sasa nitamwita Mheshimiwa Basil Mramba atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji na Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni ajiandae.

MHE. BASIL P. MRAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Leo nazungumza habari za Afrika Mashariki na nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ingawa leo hayupo hapa nadhani yuko kwenye shughuli ngumu na Watalaaam wote kwa hotuba nzuri yenyenye mambo mengi na mazuri ambayo yanafanya katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze pia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii lakini niseme waziwazi kwamba Mkao wa Kilimanjaro ni mdau wa mstari wa mbele kwenye Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Ukisoma hotuba ya Wizara ya Maji, Miundombinu na hii ya Afrika Mashariki utagundua jambo moja kwamba Mkao wa Kilimanjaro unarukwa kwenye kufaidika na miradi ya Afrika ya Mashariki. Kwa lugha nyingine Kilimanjaro *Region is being marginalised not by design* siyo kwa makusudi lakini kwa namna mambo yanavyofanywafanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nianze kwa kusema kwamba ingekuwa jambo zuri sana kama viongozi wa Mikoa ya mstari wa mbele Kagera, Mara, Kilimanjaro na Tanga tunaopakana na nchi hizi za Afrika Mashariki tushirikishwe katika maamuzi kabla maandalizi ya mambo ya kujadili na kuamua katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Siyo lazima viongozi wa kisiasa, wanaweza wakawa pia wataalam tulionao huko mkoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mifano ya kuonyesha kwa nini nasema hivyo. La kwanza, kwenye hotuba hii ya *Pool* Afrika Mashariki tuangalie ile *Southern Power Pool* ukurasa wa 58 wa hotuba hii ambaa baadaye inatarajiwa umeme utatoka Kusini mwa Afrika kuelekea Nairobi. Umeme huu umeruka Moshi na Rombo ambapo ndiyo njia

fupi zaidi ya kwenda Nairobi kwa umeme au kwa barabara. Kabla sijasahau nishukuru sana Wizara kwa namna ambavyo imekuwa ikifuatilia suala la barabara kati ya Mkoa wa Kilimanjaro na Kenya. Hapo mmeefanya vizuri na nawapongeza, tatizo tu ni kwamba barabara ile haijaanza kutumika kwa sababu vyombo husika havitaki nadhani au havifanyi haraka yoyote kutoa leseni za vyombo vya usafirishaji. Leseni bado ni tatizo na Waziri anajua baadhi ya hizo leseni sitaki kuzusha hapa nitazungumza naye huko nje. Kwa barabara mmeefanya vizuri na barabara ndiyo pekee mradi wa East Africa ambao umekwenda vizuri kwa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende la pili, usafiri wa anga. Wakati Kenya wanajiandaa kujenga Kiwanja cha Ndege pale Taveta mpakani na Holili Tanzania, sisi Tanzania hata kile Kiwanja cha Moshi cha siku nyingi kabla ya uhuru hakina mwenyewe sasa hivi inavyoonekana, ambapo watalii wakiumia mahali karibu pa kuwapeleka ni ama *KCMC* ambapo ni dakika 15 kutoka Kiwanja cha Moshi ama Nairobi ambapo wangepandia Moshi kwa haraka zaidi wakitokea mlimani huko ambapo wamepata ajali za namna mbalimbali wakielekea Nairobi kuliko kwenda *KIA* ama Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali ya Tanzania haitaki kiwanja hiki cha Moshi Mheshimiwa Waziri kitumbukize kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu kina mantiki kwenye utalii na kwenye biashara za Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni reli. Kuna *Railway Master Plan* hapa nimeisoma katika ukurasa wa 56, lakini lile suala linalopigiwa kelele hapa kila siku na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo kwamba tuangalie Reli ya Mombasa, Taveta, Moshi mpaka Arusha kwa sura hii ya Afrika Mashariki na kwa kuzingatia kwamba Tanzania sisi tuna mpango wa kujenga *Inland Port* pale Holili, kama tungeangalia vitu hivi kwa pamoja reli hii ya Mombasa, Holili, Moshi mpaka Arusha ingekuwa ni mradi wa Afrika ya Mashariki. Kwa sasa hivi sioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano, *ICT*. Sijui kama ni ajali kwamba Mikoa ya Mara na Arusha imeshaunganishwa na Mkongo wa Taifa yaani imeshaunganishwa na Kenya. Mkoa mzima wa Kilimanjaro haujaunganishwa na Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi wakati wa hotuba ya Waziri wa Mawasiliano, niliambiwa kwamba kuna awamu ya pili inayokuja na mimi naendelea kuuliza hii awamu ya pili itaruka tena Mkoa wa Kilimanjaro? Kama ni hivyo ndio *marginalisation* ninayoizungumzia ambapo kwa *ICT* Mkoa wa Kilimanjaro uko tayari zaidi kuunganishwa na Kenya kuliko Mikoa mingine yote ambayo tayari imeshaunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye masuala mengine ya ujirani mwema, nadhani Mheshimiwa Waziri hajui ni *unfair* mimi kuzungumza kwenye hotuba hii lakini

nafikiri ni vizuri sasa ajue kwamba kwa miaka mingi toka wakati ule Mheshimiwa Lowassa akiwa Waziri wa Maji, kwa miaka hiyo yote kumekuweko na majadiliano yasiyokwisha kati ya Kenya na Tanzania kuhusiana na matumizi ya maji ya Ziwa Chala. Kuna Ziwa liko Wilaya ya Rombo theluthi mbili na liko Kenya theluthi moja, lina maji mengi mazuri, Tanzania tunataka kuyatumia, Kenya wanataka kuyatumia kwa sababu majadiliano haya hayaishi Kenya wameshaanza mradi na mwezi Oktoba utekelezaji unaanza. Sisi tumekuja kugundua kwamba wao wamekwenda mbali sana wanataka kuanza mradi wa umwagiliaji mashamba upande wa Kenya Wilaya mbili. Sisi ambapo hata maji ya kunywa kutoka kwenye Ziwa hilo bado hatujayapata, tunaendelea kusema tutazungumza, sisi tutazungumza wao watatekeleza na hiyo ni sehemu ya *marginalisation*. Mambo ya Mkoa *can take its time*. Tutasubiri tu, tutazungumza na tutazungumza, ni lini tutamaliza mazungumzo ili maji haya yaweze kutumika kwa matumizi ya binadamu au umwagiliaji kama Kenya kwa namna ambayo inaleta haki kwa nchi zote mbili? Nimeambiwa majadiliano yataendelea lakini sijui yataendelea mpaka lini? Hili ni jambo la Wizara ya Mambo ya Nje na kwa kiasi naona sasa ni jambo la Afrika ya Mashariki na kwamba Waziri ulishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la hawa wanyama Tembo kutoka Kenya, yamezungumza sana hapa jana lakini Wilaya ya Rombo tunaathirika sana. Kenya hawajali Tembo wao, wanakuja wanakula mazao wanarudi na hawana pasipoti, hawahitaji *visa* wala kadi za usafiri zinazozungumzwa. Kwa nini tusifanye mazungumzo ya pamoja kati ya Tanzania na Kenya kudhibiti Tembo hawa wanaozunguka Mlima Kilimanjaro? Wako Wilaya ya Siha, Hai, Rombo na hakuna tunachojadiliana nao, Tembo hawa sio wa Tanzania ni wa Kenya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kabla sijamaliza, naomba Mheshimiwa Waziri haya uyazingatie. Mimi naona ukiangalia moja moja iko *marginalisation by default* inayoendelea kati ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Mikoa hii ya Kaskazini hasa Mkoa wa Kilimanjaro. Mimi nadhani sio makusudi lakini nataka sasa uelewe kwamba hilo jambo lipo na siku litakapoingia kwenye siasa, sisi wa Kilimanjaro tutalizungumza kisiasa na sidhani kama itakuwa ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie juu ya *EPA*. Mimi nilisaini ule mkataba wa awali wa *EPA*, *EPA* hii ya uchumi. Ushauri wangu kwa sasa hivi, maana naona muda unakwisha, ni kwamba lolote mtakaloamua liwe WTO *compliant*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, nakushukuru na naomba tena kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bismillahi Rahman Rahim.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kabla sijachangia katika mada zetu hizi zilizokuwa mbele yetu, naomba nitamke wazi kwamba naunga mkono hotuba zote mbili ile ya Afrika Mashariki na ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nataka nitumie fursa hii kwa dhati kabisa, kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Muyuni, kwa kuniwezesha mpaka leo niko hapa na napenda kuwaarifu kwamba bado uwezo ninao, nia ninayo na tutakuwa pamoja na nategemea *Inshallah* wataniunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nakuja kwenye upande wa Afrika Mashariki. Kama tunavyoolewa wazungumzaji wengine wamesema kwamba Utaifa wa Afrika Mashariki uwekwe mbele kuliko Utaifa wa nchi. Hii ni kauli ambayo mmoja katika wasemaji aliizungumza katika kikao chetu hiki na kidogo ikanipa moyo wa kutaka kujua kama hii ndiyo hali halisi ilivyo kwa upande wa Afrika Mashariki na tuna malalamiko ya kusema kwamba sasa sisi Zanzibar kuna mambo si ya Muungano na yamewekwa kwenye Afrika Mashariki sijui hapa Mheshimiwa Waziri ikiwa kama leo tunazungumza Utaifa wa Afrika Mashariki halafu tunakuja na hoja kubwa ya kuzingatia, Zanzibar ifikiriwe vipi katika suala hili? Ningombwa Mheshimiwa Waziri anapokuja kujumuisha hapa atufanulie, je, kwa upande wa Zanzibar haya masuala ya Afrika ya Mashariki na hizi dhana za kwamba Utaifa wa Afrika Mashariki uwe mbele kuliko Utaifa wa Nchi za Afrika Mashariki, ningombwa anifafanulie kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu ajira ya wafanyakazi wanaohusiana na Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Afrika ya Mashariki. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kipengele cha 56, ukurasa wa 29 alitutajia takwimu za wafanyakazi katika ofisi zetu hizi na katika takwimu hizi utaona kwamba kuna idadi ndogo sana ya wafanyakazi kutoka Zanzibar. Je, katika suala hili tunaona ipo haja kwamba sasa hivi umefika wakati kwamba ni lazima kuwepo uwiano wa wafanyakazi wa Zanzibar na wafanyakazi kutoka Tanzania Bara? Kwa sababu katika idadi ya wafanyakazi 205 waliotamkwa katika hotuba hii, kuna wafanyakazi 15 dhidi ya wafanyakazi 189. Najua kwamba Zanzibar ni ndogo lakini kweli uwiano huu kidogo unaleta picha na sura kweli ya Kimuungano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwamba sasa hivi Mheshimiwa Waziri na Wizara zote mbili ya Afrika ya Mashariki kwa sababu, ingawa hakuna takwimu lakini nategemea pengine nako hali itakuwa hii hii na hii ya Mambo ya Nchi za Nje kwa Zanzibar imefika wakati sasa tukae kitako na kuzingatia wakati wanapokuja kwenye ajira ni lazima kuwe na uwiano wa kuona kwamba Zanzibar walau inatengewa watu wake au nafasi zake za kusema kwamba Zanzibar iwe na watu hawa. Utaratibu huu wa kapu wa kusema kwamba kila mmoja aombe naona itafikia wakati Zanzibar kusiwe hata na wafanyakazi ikiwa leo tuna wafanyakazi 15 tu waliokuweko katika ofisi hii sijui huko tunakokwenda tutakopokuwa dunia kama kisiwa tutakuwa katika hali gani? Kwa hivyo, ningombwa sana hapa akalizingatia suala hili na Serikali ikazingatia kuhusu ajira, kuwe na uwiano kati ya sehemu mbili hizi za Muungano kati ya Zanzibara na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ninapenda kuichangia. Nashukuru sana Mheshimiwa Waziri alipokuja kutoa hotuba yake, alizungumzia kuhusu hali ya majengo ya ofisi zetu za Ubalozi. Nimeshukuru sana na kwa kweli nilikuwa na azma ya kuwa mkali kidogo katika suala hili, lakini nashukuru kusikia kwamba Serikali

imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi. Ni suala la aibu, kwa Tanzania ilivyo sasa na kwa heshima ya Tanzania na kwa hali ya majengo na ofisi zetu zilizokuweko nchi za nje, kwa kweli inasikitisha sana. Kwa sababu hii hali ya Ubalozi katika nchi za nje sio aibu ya Mambo ya Nje, lakini hii ni aibu ya nchi nzima, kwa hivyo, ninaomba sana Serikali izingatie kwa dhati kabisa kuhakikisha kwamba majengo na ofisi pamoja na nyumba za wafanyakazi wa Ofisi za Ubalozi katika nchi za nje zinakuwa katika hadhi ya Kitanzania ili na sisi tuweze kuona kwamba Tanzania nayo inaonyesha sura ya kwamba ni moja ya nchi katika Afrika ambayo imepiga hatua mbele katika maendeleo na siasa zinazohusiana na Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio katika majengo tu lakini na kwa wafanyakazi. Katika muda ambao nimebahatika walau kwenda nchi za nje na kukutana na wafanyakazi, nimeshudia kwa kiasi fulani katika maelezo, kwa kweli wanaishi katika hali ambayo hairidhishi. Ninaomba sana Serikali ijitahidi angalau kuwaona hawa wafanyakazi wanayo kazi ngumu. Inafikia hatua leo mtu katika ofisi ya Ubalozi anatumia fedha zake mwenyewe kuikopesha Serikali au kujikopesha au kuikopesha Ofisi ya Ubalozi ili mambo yaende. Nadhani mambo kama haya, kuna haja kamili ya kukaa kitako na kuyazingatia kwa dhati kabisa na kuona kwamba tunaepukana nayo kabisa ili kuwapa heshima wafanyakazi wetu hawa katika Ofisi za Ubalozi ili na wao wajisikie kwamba ni moja katika sehemu ya Taifa hili na ni moja katika vijana au jamii iliyokuwa inapenda kuona kwamba nchi yetu hii ya Tanzania nayo inakuwepo katika hadhi ya kuvutia na kupendeza kama dunia nzima inavyoolewa msimamo wa Tanzania katika mambo ya uhusiano wa nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nizungumzie kuhusu Afrika Mashariki. Juzi tu tumesema kwamba tumeanza Soko la Pamoja lakini kwa kweli tukitazama suala la taaluma kwa wananchi kuhusu suala hili bado taaluma ni ndogo. Kwa hivyo, ninaomba sana Serikali ifanye juhudhi zaidi ya kutoa elimu kwa sababu wengi hasa katika vijijini hawajafahamu nini taratibu na mwenendo na hali halisi ya hili suala zima la Muungano au Shirikisho la Afrika ya Mashariki. Tunazungumza tu Soko la Pamoja, Fedha ya Pamoja lakini kuna wengi bado hatujakuwa na elimu ya kutosha. Kwa hivyo, ninaomba sana Wizara izidishe kutoa elimu, tukishirikiana na sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa jumla ili kuweza kuhakikisha kwamba elimu hii inafahamika zaidi na kuwaondoshea woga Watanzania ili tuweze kwenda sambamba na mabadiliko haya ya dunia pamoja na mabadiliko yetu katika hii Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, sina la ziada isipokuwa naunga mkono hoja zote mbili, ya Wizara ya Afrika ya Mashariki na ile ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ahsante sana, shukrani. (*Makofî*)

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda niunge mkono hotuba hizi mbili za Waheshimiwa Mawaziri wa Afrika Mashariki na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kuunga mkono, napenda vilevile niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri. Ni kweli na ni dhahiri kwamba tunafanya kazi na hawa Mawaziri wanafanya kazi katika mazingira kidogo magumu sana. Lakini kwa kipindi ambacho nikianzia na Mheshimiwa Dr. Kamala, amekuwa Waziri wa Wizara hii ya Afrika Mashariki, tumetambua kwamba ushiriki wa Tanzania umeongezeka kwa kiwango gani na ndiyo maana mijadala mingi inayoendeshwa sasa hivi, mashauriano mengi yanayoendelea sasa hivi, yanaonesha jinsi Watanzania tunavyoweza kubadilika sasa hivi katika mchakato mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili, nimpongeze sana Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Bernard Membe, mwanzoni niliona kwamba pengine Wizara hii ilikuwa pana kwake licha ya kwamba ni Mwanadiplomasia aliyekuwa amebobe, lakini jinsi ambavyo ameanza kukaa kwenye kiatu hicho na kuanza kuenea, ni jinsi gani kwa kweli ameweza kujifunza na kuendesha shughuli za Wizara hii pana ambayo ndio sura ya nchi nje ya nchi, yeye na Mheshimiwa Dr. Kamala, kwa kweli wamekuwa wasaidizi wazuri sana wa Mheshimiwa Rais katika kuelezea na kusimamia masuala muhimu sana kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia muda, vile vile niseme kwamba napongeza sana kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Rais. Kwa sababu heshima ya Mtanzania, leo hii ukiwa nje ya nchi, tuna heshima kubwa sana ni kwa sababu tumekuwa na viongozi ambao kweli wametambua umuhimu wao na wametambua maslahi ya nchi na ndiyo maana hata leo hii Mtanzania unazidi kupata heshima kubwa sana nje ya nchi. Japokuwa sisi Watanzania hapa hatutambui hilo, lakini naomba nikiri kwamba kwa wanaotoka nje ya nchi wanaweza kuwa mashuhuda kwamba Tanzania inashiriki vipi katika masuala mbalimbali na hata safari anazofanya Mheshimiwa Rais nje ya nchi zina faida kubwa sana kwa Watanzania wenzangu. Si rahisi kukaa tu ndani ukaona nchi inasonga mbele, haiwezekani, lazima haya yafanyike. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Mawaziri wa Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye sura ya Afrika Mashariki, kuna makandokando mengi sana ambayo Watanzania lazima tuongeze juhudhi, kama tulikuwa tunatembea, tukimbie, vinginevyo tutabaki nyuma. Kwa sababu dunia ya leo sivyo ilivyo, kila kukicha inabadilika. Mheshimiwa Mramba hapa amesema kuhusu suala la Kilimanjaro kwamba inatengwa *by default* na kadhalika lakini nadhani suala zima ni sisi tunashiriki namna gani katika kutumia fursa tulizonazo lakini pili ni kwa namna gani sisi tunakuwa mbele, tutekeleze badala ya kuwa tunasema tunapanga, tunapanga, tunapanga. Nchi kama Rwanda imetoka mbali sana, historia ya Rwanda kama tunavyoijua lakini leo hii walipofikia kiuchumi ni tofauti na sisi. Sisi tuna rasilimali zote lakini nadhani tunahitaji kupata msukumo utakaoongeza mtekenyo wa kufanya sisi Watanzania tutekeleze zaidi badala ya kupanga zaidi. Kama ni kupanga tumeepanga vitu vingi sana, tunachotaka sasa hivi ni utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Afrika Mashariki ukiangalia kwa mfano kwa Mkoa wa Mwanza, Mwanza peke yake ukisema hapa sasa ndio niwekeze zaidi na iwe moja ya *hub* katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mwanza ni karibu na Kenya,

Uganda, Rwanda na ni karibu na Burundi lakini hata DRC ni ukanda ule ule, lakini ni aibu hata leo ukienda Serikali haijawekeza vya kutosha Mwanza. Katika miradi mingi inayofanyika, Mwanza inaachwa pembedi, lakini kumbuka Mkoa wa Mwanza una Mikoa mingine kandokando karibu sita sasa hivi. Sasa Mikoa yote hii ukiangalia ina watu zaidi ya milioni 10 lakini ukiangalia kutoka Mwanza kwenda Serengeti ni kilomita 130, Mwanza kwenda Entebbe, Uganda, ni mwendo wa nusu saa kwa ndege, Mwanza kwenda Nairobi ni mwendo wa dakika 45 kwa ndege, vivyo hivyo kwenda Rwanda na Burundi. Lakini ukiangalia Mwanza ambayo ndiyo *hub* ya Mkoa wa Mara, Kagera, Mkoa mpya wa Geita utakaoanzishwa, Mkoa mpya wa Simiu utakaoanzishwa, Shinyanga na hata Tabora na Kigoma wanategemea sana Mwanza lakini Serikali haijawekeza vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba katika mikakati hii ya Afrika Mashariki, hebu mjaribu kuangalia ni namna gani *hub* ya Mwanza inatumika kwa maslahi na ustawi wa nchi hii na hasa kiuchumi. Leo hii ukifungua reli hii au barabara hii inayokwenda Kanda ya Ziwa, umefungua uchumi mkubwa sana. Tumekalia uchumi sisi Watanzania, mizigo inapaswa kusafirishwa kwenda nchi jirani kuititia Mikoa hii ya Kati pamoja na Mikoa ya Magharibi na Kanda ya Ziwa, ni mingi sana ambayo ni sehemu kubwa sana ya kuongeza uchumi katika nchi yetu. Kwa hiyo, naomba majadiliano haya na masikilizano haya yalenge zaidi kuboresha miundombinu ambayo ni muhimu kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Soko la Pamoja wasiwasi kwa Watanzania lakini napenda kutoa wito kwa Watanzania wenzangu na kusema kwamba lazima tukubali kubadilika. Hakuna namna tunaweza tukakaa sisi kama kisiwa lazima tukubali kubadilika na kubadilika ni kuanzia kubadilika kifikra. Pamoja na hivyo, sasa Serikali itusaidie kuelemisha wananchi, itusaidie kuhakikisha kwamba Watanzania wanakwenda sambamba hatua kwa hatua. Katika hili, tunahitaji kupata elimu ambayo inatolewa kwa kiwango fulani lakini nadhani kuna haja ya kuongeza mchakato wa utoaji wa elimu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Afrika ya Mashariki, kuna tatizo moja kwa upande wa Balozi zetu. Watanzania walioko nje ya nchi katika Balozi zetu, wanakaa wakati mwengine miezi miwili au zaidi ya miezi miwili hawana mishahara, hawana fedha za kujikimu au za kuendesha gharama za Ubalozi. Hii ni aibu kwa nchi yetu. Mimi naomba hivi, kama kuna uwezekano, Bajeti hii ya Balozi zetu itengwe na iwe inatumwa angalau miezi mitatu au sita kabla ili kuondoa usumbufu huu. Sisi tunaozunguka kule inatupa ugumu sana, unakwenda kwenye Ofisi ya Ubalozi wanakwambia hata chai hawana, wanasema hata mishahara hawajapokea, kodi ya nyumba wanadaiwa, umeme wanakatiwa. Ni aibu sisi kama Watanzania, hebu heshima hii tuiendeleze. Mheshimiwa Waziri unayehusika umewasiliana na mimi na kukueleza na kukuomba kwamba hebu mtafute mfumo ambao utawezesha Balozi zetu zipate fedha kwa muda unaotakiwa na kuondoa usumbufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho kinanigusa sana ni suala la hizi safari za nje. Safari za nje mara nyingi tunawapeleka wawakilishi wengi kupita mahitaji yenye na hii ni gharama kwa nchi. Hebu tuangalie ni watu gani wanakwenda, aina ya watu na majukumu yaliyo mbele yetu ili kupunguza mizigo mkubwa kwa Taifa letu. Tunalipa fedha nyingi sana kugharamia gharama za safari za nje na hii ukiangalia

tunaposema tufunge mkanda ni pamoja na mambo kama haya. Naomba sana Waziri anayehusika, hili suala aweze kulifanyia kazi na pengine inapobidi tuchukue hatua za makusudi kabisa wa kajaribu kuokoa fedha nyingi katika njia hii. Sina wasiwasi na Mheshimiwa Membe, nafahamu ni mchapa kazi, ana timu nzuri, ajipange vizuri na hii itatupa nafasi nzuri sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nilikuwa na ombi moja, sambamba na suala zima la uwekezaji, Balozi zetu zihusike sana katika mazungumzo ya kibiashara, zisaidie kuwavuta wawekezaji kuja nchini mwetu na hata misafara inayokwenda nje ya kidiplomasia ni bora zaidi ijikite katika masuala ambayo ni ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa fursa ya kuchangia hotuba hizi mbili, Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara ya Afrika Mashariki na ninafuraha kwamba kwa mchango wangu wa leo hasa kwa Wizara ya Afrika Mashariki, itakuwa katika Bajeti zote tano za Wizara ya Afrika Mashariki nimechangia toka Bunge hili lianze. Hii ni kwa sababu mimi ni Mwanaafrika Mashariki, ni mpenzi mkubwa wa Afrika Mashariki kwa sababu mimi *principally* ni *Pan-africanist*. Kwa hiyo, nafurahi kwamba leo nimetimiza ndoto yangu ya kuhakikisha kwamba nachangia katika Hotuba zote za Wizara ya Afrika Mashariki. Nashukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili ya jumla, la kwanza ni la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Wakati Waziri anatoa taarifa kuhusiana na hali ya usalama kule Niger, nadhani kwa sababu ya *principle* ile ile ya *African Union* kupinga mapinduzi, lugha ambayo kidogo imetumika katika hotuba ya kwamba aliyejewa Rais wa Niger, alifanya hila nadhani si lugha ya kidiplomasia zaidi, kwa sababu ni lugha ambayo ina-support yale mapinduzi, sidhani kama ni sahihi na ninaomba Waziri aweze kuliangalia hilo na kulirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni katika makubaliano, kwenye ukurasa wa 25, makubaliano kati ya Serikali yetu na Serikali ya Oman ambapo katika hotuba Waziri anasema: “*memorandum* ile iliwekwa saini na mimi mwenywewe”, nadhani pale ingekuwa “iliwekwa saini na Waziri wa Mambo ya Nje kwa sababu *document* hii ni *official* sio *personal*, ya Mheshimiwa Membe, hayo ni mawili madogo ya ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni la Kigoma, Balozi wetu wa Tanzania nchini Ujerumani alifanya kazi kubwa sana, akazungumza na Serikali ya Ujeruman, akazungumza na Serikali ya Jimbo la *Niedersachsen* kuhusiana na kuwa na mahusiano maalum na Tanzania. Lile Jimbo la *Niedersachsen* lina historia na Mkoa wa Kigoma kwa sababu katika Jimbo lile kuna Mji unaitwa *Papenburg*, ndiyo Mji ambao ni Makao Makuu ya Kampuni ambayo ilitengeze meli ya MV Liemba mwaka 1910, miaka 100 iliyopita na meli hiyo mpaka sasa bado inaelea ndani ya Ziwa Tanganyika. Kwa hiyo, wale watu wakawa na *interest* ya kutunza ile *heritage* kati yetu sisi na Wajerumani na

Balozi akafanya kazi nzuri sana tukapata ujumbe wa Serikali ya *Niedersachsen* kuja Tanzania kupitia Wizara ya Mambo ya Nje kwa ajili ya kuwa na mahusiano maalum na mpaka sasa hivi Serikali ya Ujerumani katika Bajeti yake imetenga *Euro milioni* 9 kwa ajili ya kuanza mchakato wa kuifanyia marekebisho MV Liemba ili iwe *hotel* ya kitalii na badala yake kujenga meli ndogo mbili na kuzileta katika Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kuhudumia wananchi kuchukua nafasi ya MV Liemba. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia hotuba ya Waziri kwa sababu jambo hili linaratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje, hakuna hata neno moja kuhusiana na suala hili na katika mahusiano ya Kidiplomasia nchi mbalimbali zina mahusiano na Mikoa mbalimbali ya nchi zingine. Kwa mfano, nchi ya Rwanda ina mahusiano na Jimbo moja la Kusini la Ujerumani na katika *model* hiyo hiyo ambayo tulikuwa tumechukua lakini kwa sababu Jimbo lile ni dogo, Tanzania ni kubwa sana tukawa tumeona kwamba iwe ni Mkoa tu wa Kigoma na Mkoa ambaa una mahusiano rasmi na Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Waziri alitolee ufanuzi kwa sababu ni jambo ambalo linaratibiwa na Wizara yake, kukaa kimya tunapata simanzi kidogo labda Wizara ya Mambo ya Nje haitoi kipaumbele kwa mambo ya Kigoma ingawa Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje anatoka Kigoma. Kwa hiyo, ninaomba suala hili liweze kuangaliwa vizuri na Waziri aweze kulitoa ufanuzi na kwa sababu *project* hii kwa watu wa Kigoma ni muhimu sana, itaongeza utalii na itatunza historia tuliyonayo kati yetu sisi na hao ndugu zetu kutoka Ujerumani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili dogo pia la kidiplomasia, nimepata taarifa kwamba Serikali ya Morocco inafanya *lobbying* ili Serikali ya Tanzania ianzishe mahusiano ya Kibalozi na nchi hiyo. Naomba Serikali ikumbuke kwamba mwaka 1984, *African Union* wakati ule *OAU*, ilitoa uamuzi rasmi wa kukubaliana na Morocco kujitoa *OAU* kwa sababu ya suala la Western Sahara na sisi *principle* yetu katika mambo ya nje ni kukaa na wanyonge, wanaoonewa, wanaonyanyaswa na wanaokandamizwa. Kama suluhisho la Western Sahara halijapatikana, Serikali yetu wala isijibu hata simu kutoka Serikali ya Morocco na wala hata siku moja tusiweke kipaumbele katika *the so called* Diplomasia ya Uchumi tukaacha *principles* zetu ambazo zimekuwa zikituongoza miaka yote kama Tanzania na kutujengea heshima mbele ya Mataifa mengine, heshima ya kusimama na wanyonge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afrika Mashariki, juzi tumeingia katika Soko la Pamoja. Kwa sisi wapenzi wa *integration*, ni hatua nzuri sana na muhimu sana. Kuna malalamiko mengi sana ya Watanzania kutoandaliwa na ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba Watanzania wanaandaliwa. Kwa miaka miwili, mitatu, urari wa biashara kati ya Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki umekuwa ni mzuri sana. Lakini kwa mujibu wa Taarifa ambayo Wizara ya Afrika Mashariki imeitoa sasa inaonesha kwamba mwaka 2009, mauzo yetu nje kwa nchi za Afrika Mashariki yamepungua sana na hasa mauzo yetu na nchi ya Kenya. Mwaka 2008, tuliuza bidhaa zenye thamani shilingi bilioni 235, mwaka 2009 imeshuka mpaka shilingi bilioni 177 na ukiangalia urari wa biashara kwa ujumla ndani ya eneo zima la Afrika Mashariki tuna

urari ambao ni hasi bilioni 46.8 (-46.8 bilioni) wakati mwaka 2008 tulikuwa na urari wa *positive* bilioni 110 (+110 bilioni).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara haijatolea maelezo suala hili, tatizo limekuwa wapi, maana tulikuwa tuna Ushuru wa Forodha tumeanza nao, tumepata uhuru sisi wa kuuza mazao yetu Kenya wakati wao wanapouza kwetu wanauzua na Kodi. Kuanzia tarehe moja milango imefunguka zaidi kwamba tunauza na wao wanauzua kwetu kama kawaida. Mwaka mmoja tu kabla hatujaanza, *actually* miezi sita tu, kabla ya hatujaanza Soko la Pamoja, tayari urari wetu wa biashara umeanguka vibaya mno. Tatizo liko wapi na Wizara haijaaeleza? Katika hotuba yote hii, kitabu kikubwa kweli zaidi ya kurasa 101, ukiachana na hizo takwimu, Wizara ya Afrika Mashariki haijatuambia ni nini ambacho kimetokea. Tulikuwa na *trend* nzuri, inakwenda vizuri, ghafla imeanza kuporomoka na sasa hivi tumeshafungua milango hali itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe changamoto kwa Serikali kwamba lazima kuwe na juhudi maalum ya kuanzisha *think tanks* kwa ajili ya *studies* kuhusiana na jinsi gani ambavyo nchi yetu inaweza ikafaidika zaidi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu kutegemea tu Serikali kutoa maelekezo kusema kwamba tutauza hiki na hiki, haitoshi. Tujifunze katika nchi zingine ambazo zina mahusiano kama haya. Jumuiya ya Ulaya, unakuta kila nchi wana *private think tanks* ambao kazi yao ni kufanya *studies*, kitu kama hiki tayari tungkuwa na *a back up study* kwa nini tuna *drop*, nini kimetokea, labda uzalishaji ndani ya Tanzania umeshuka na uzalishaji wa sehemu nydingine umeongezeka. Kwa sababu kwa nini tunanunua zaidi wakati tulikuwa tunauza zaidi kutoka kwa wenzetu? Kwa hiyo, naomba Serikali ijaribu kuangalia hata kama itatokana na Bajeti ya Serikali, tupate wataalam, waanzishe *private think tanks* tuwasaidie, kazi yao wawe wanakaa na kutoa *studies* na makala mbalimbali na kuonesha nafasi yetu katika eneo hili la Jumuiya ya Afrika Mashariki ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika suala hili la Jumuiya ya Afrika Mashariki, nimelizungumza sana toka mwaka 2006 na *privately* nilizungumza na Mheshimiwa Membe, kwamba ndani ya *region* sasa hivi imeonekana kwamba sisi sauti inakuwa ndogo zaidi. Tukienda kupiga kura leo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, *a free vote* tutapigwa kura na Burundi tu, Kenya, Rwanda na Uganda wanapiga kura wenyewe. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba sauti yetu ndani ya *region* inashuka. Sasa kuna njia mbalimbali, kwanza *ku-improve* mahusiano na hizo nchi nydingine. Lakini sisi tuna mahusiano maalum na Comoro, kwa nini hatufanyi juhudhi maalum Comoro ikaingia ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ni soko letu lile na tuna mahusiano nao. Kuna Wacomoro wengi wanaishi Zanzibar, kwa nini hatufanyi hicho kitu? Sisi tuna mahusiano maalum na Mashariki ya Congo, watu milioni 25 Mashariki ya Congo wanalishwa na Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Rukwa. Kwa nini hatufanyi juhudhi maalum za kutaka hii *Common Market i-extend from Indian Ocean to Atlantic Ocean?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hiki *for the last four years* kwa nini Serikali haoni umuhimu huo? Diplomasia ya sasa inahitaji muwe wengi ili mnapoenda kwenye maeneo mbalimbali mpate sauti za wengi. Haiwezekani sisi tuwe tunaenda kwenye vikao tunaweza tutapigwa kura na Burundi tu na kwa sababu tunawasaidia

katika mambo ya amani. Tena Mheshimiwa Membe, kule wamelipua gari letu, Ubalozi wa Tanzania nchini Burundi haujatoa kauli na itabidi tuwaonye kidogo hawa na wala tusiruhusu *rebels* ambao wamekataa kushiriki kwenye uchaguzi, kutuvuruga, sisi watu wa Kigoma tumechoka kupokea wakimbizi. Tumechoka kabisa kabisa. Kwa hiyo, mtu ye yote ambaye analeta hatari ndani ya *member country* wa *East Africa* ashughulikiwe mara moja. Wala tusimpe muda, wala tusimpeleke kwenye Meza ya Mazungumzo, tumeshawapa muda, uchaguzi umeitwa, wamekataa kushiriki uchaguzi, *we must forward ahead.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Kamala, mpaka wa Kagunga haujakwenda na kuna mazungumzo pale. *TANESCO* tumeomba watuletee umeme kutoka Burundi, kwa vyovyote vile lazima itakuwa ndani ya kimahusiano ya Afrika Mashariki. Naomba Mheshimiwa Waziri azungumze na wenzetu wa Burundi tuharakishe mchakato wa kuleta umeme pale Kagunga. *TPA* wametujengea Bandari pale Kagunga, Halmashauri imejenga soko pale, tunataka mpaka ule uwe kama mpaka wa Namanga au mpaka wa Tunduma. Naomba Waziri autembelee na tumwombe Mheshimiwa Rais aende akazindue ile Bandari pale ambayo imejengwa na *TPA* na kama *TANESCO* watakuwa wamefanikiwa kwa msaada wako, tuweze kupata umeme, kijiji kile kiweze kushamiri na watu wa Kigoma *wa-enjoy* hiyo *Common Market*. Kwa sababu sisi tuna mipaka na nchi mbili na tunawauzia zaidi na kwa vyovyote vile Tanzania itafaidika zaidi kama ikiutumia Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya biashara na nchi ya Burundi na baadaye kama mtakubaliana na ushauri wangu na nchi ya Congo na tuweze kuhakikisha kwamba tunajenga Jumuiya iliyoimara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu yalikuwa ni hayo, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu, muumba wa mbinu na nchi, kwa neema na fadhila zake na utukufu wake. Nikushukuru nawe kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia katika hoja hizi mbili ambazo zimewasilishwa. Lakini nitangulize tu kwanza *ku-declare interest* kwa sababu nataka nijikite sana katika suala la utawala bora yaani *African Peer Review Mechanism (APRM)* kupitia Kambi ya Upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu, Mheshimiwa Dr. Jakaya Kikwete, kwa nia njema na kwa utashi wake mwenyewe, aliona kwamba ipo haja ya makusudi ya nchi yetu ikajitathmini na kisha kutathminiwa katika maeneo mbalimbali ambayo yanachangia sana kuleta vurugu katika Afrika na hili ni Azimio ambalo viongozi wa nchi za Kiafrika walikubaliana na Bunge letu pia likaridhia na niishukuru Serikali kwamba imeanzisha mchakato huu ili tuweze kujitathmini kama Taifa tuweze kuona mafanikio na upungufu tulionao ili tuweze kujisahihisha. Serikali ilisema kwamba itabeba gharama za kuendesha mchakato huu. Niishukuru Serikali kwamba imejitahidi kutimiza wajibu wake na kiasi kidogo sana ambacho tunasaidiwa na Mashirika ya Kimataifa, Shirika la *UNDP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu tulitaka mchakato huu na tathmini hii iwe ni mali yetu sisi wenyewe kama Watanzania, Serikali haikutaka *APRM* iweze

kupewa michango na taasisi nyingine ambazo zinaweza zikatulazimisha kufanya yale wanayoyataka wafadhili. Kwa nia njema kabisa ya Serikali ili iweze kujitambua na kisha kuwa tayari kuja kutathiminiwa na wengine ili tuweze kuja kufikia malengo tuliyokuwa tunayakusudia. Mchakato huu ni muhimu sana kwa maslahi na ustawi wa Taifa letu na kwa nia njema umejikita mahali pazuri lakini kwa sababu moja au nyingine mchakato huu umesimama na tatizo kubwa ni pesa. Kama tuliamua kama Taifa tujitazame, tujiangalie na tujitathmini tuone tumefanya nini katika kipindi cha toka tumejitawala mpaka sasa, wapi tumekosea na wapi tunahitaji tujisahihishe, ilikuwa ni lazima sana Serikali ikawekeza ili mchakato huu ukakamilika katika muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba kwa mara tatu mfululizo tumeshindwa kama nchi kuja kutathminiwa na wenzetu kwa visingizio mbalimbali. Inatia aibu sana kama Taifa, inatia mashaka makubwa sana katika macho ya wenzetu ambao sisi tulikubali kwamba tupo tayari kujitathmini na kisha tukakiri kwamba tutakuwa tayari kuja kutathminiwa, tunapoonesha hofu ya kuja kufanyiwa uhakiki wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeypata mafanikio makubwa sana ambayo tumeyapata katika kipindi toka tumejitawala, yapo mafanikio ambayo ni ya kuigwa mfano katika Afrika hasa amani na utulivu, lugha ya Kiswahili ilivyoweza kutuunganisha Watanzania na mifano mingi tu ambayo ni ya kipekee ambayo haijawahi kutokea katika Afrika tumefanikiwa katika hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, upo upungufu mwingi ambao unapaswa ushughulikiwe mapema zaidi. Kama Serikali ingekuwa tayari kwa ratiba ambayo ilikuwa imepangwa na tathmini hii ikawa imepitiwa, ninaamini kabisa baada ya Uchaguzi Mkuu, Serikali itakayoingia madarakani ingekuwa na vitu vingi sana ambavyo ingeanza kuvifanyia kazi. Inatia mashaka kabisa kwamba baadhi ya dosari ambazo zinaonekana, hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na hivyo kuendelea kubakia palepale na matatizo yanaweza yakawa yenyе kujirudiarudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee mfano katika Chaguzi mbili za nyuma zilizopita ya mwaka 1995/2000 na hata 2005, kwa kule Visiwanı kila baada ya matokeo kutangazwa kunakuwa na malalamiko na wakati fulani ikapelekeea mpaka baadhi ya Watanzani kupoteza maisha yao. Kwa nia njema kabisa, dosari hizo zilionekana na yakatolewa mapendekezo ya ni namna gani ya kuweza kuziondoa dosari hizo ikiwa ni pamoja na upungufu wa wazi uliomo katika Tume zetu za Taifa za Uchaguzi yaani *NEC* na *ZEC* lakini kwa sababu tathmini hii haijapitiwa na kuhakikiwa, tunaingia tena katika uchaguzi bila dosari hizo kuwa zimerekebishwa, hii inatia mashaka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mengi mazuri ambayo yangeweza kutusaidia kama Taifa na hasa tunapoangalia maeneo ya Utawala Bora katika huduma za Kijamii. Tumeypata mafanikio makubwa sana katika maeneo mbalimbali na katika nyanja mbalimbali kwa mfano elimu, tuna shule nyingi tumejenga lakini zina upungufu mwingi ambao pia umeainishwa katika taarifa hiyo. Sasa ingeweza kuisaidia sana Serikali kuweza kuangalia ni hatua gani za haraka zichukuliwe katika maeneo mbalimbali ambayo pengine yangeweza kubadilisha hali ya maisha na ustawi wa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitahidi kufanya mashauriano na Kamati ya Bunge na viongozi mbalimbali wa Wizara pamoja na maelezo waliyoyatoa lakini bado nitaendelea kwa unyenyekevu kabisa kumwomba Mheshimiwa Waziri alitilie uzito suala hili na kuangalia ni namna gani atasaidia kwa juhudzi zake mwenyewe kufanya mchakato huu uweze kukamilika katika muda muafaka. Mpaka ifikapo April, 2011 ambayo wanadhani kwamba hiyo *Country Review Mission* ndiyo itakuwa ni miezi 21 toka taarifa kuandaliwa, kwa maana hiyo hata hiyo taarifa itakuwa haina maana tena, fedha tuliyotumia itakuwa imepotea. Kwa hiyo, nirudie tena kuiomba na kuinasih Serikali kwamba jambo hili ni kwa maslahi ya Taifa letu kwa ajili ya kujenga umoja wa Taifa letu, ni kwa ajili ya kuangalia tulipokuwa tumekosea kama Taifa ili tuweze kujisahihisha. Kwa maendeleo ya watu wetu, narudia tena kuomba Serikali iangalie itafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoiwakilisha sasa hivi kwamba Serikali kupitia Wizara yake imetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya *APRM* lakini ninapenda nimkumbushe tu Mheshimiwa Waziri na alitolee tamko hili kwamba hiyo shilingi bilioni moja ambayo imetengwa kwa ajili ya *APRM*, *APRM* inadaiwa zaidi ya shilingi 840 milioni kama ada na michango ambayo haijalipwa mpaka sasa hivi. Kwa maana hiyo, kama watalipa hilo deni watakuwa hawana fedha za kufanya kazi, Wizara itaisadia vipi ili mchakato huu uweze kukamilika na kuleta maslahi na maendeleo kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofii*)

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Naomba nitangulize shukrani na pongezi kwa Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu wao, kwa kazi nzuri walioifanya pamoja na wataalamu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaelekeza mchango wangu zaidi katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Dhana ya *Regional Integration* kama ilivyoanzishwa na kuendelezwa katika maeneo mengine na hasa nikichukua mfano wa *European Union* utakuta kwamba *Regional Integration* inajengwa juu ya misingi kadhaa, ustawi wa jamii, mara nyingi ni kitu cha msingi. Suala la ulinzi, amani na usalama, ni msingi mwagine mkubwa lakini pia kufanikiwa kama ustawi wa kiuchumi, ustawi wa kisiasa, hivi navyo vinaunda msingi mwagine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo letu la Afrika ya Mashariki, ukitazama nchi zote tano, unakuta kwamba kuna tofauti nyingi na kubwa tangu mfumo tunaoutumia wa kisiasa, Rwanda na Burundi zimekuwa katika mkondo mwagine wa kufuata zaidi tamaduni za Kifaransa, Uganda, Kenya na Tanzania zinifuata mkondo wa Kiingereza lakini vitu hivi ni sharti tuanze tu kuvitazama katika Shirikisho hili, ni tofauti zipi ambazo ni kubwa na hatupaswi kuzitofautisha lakini pia tunakamilishana katika nyanja zipi hasa katika uwanja wa demokrasia na siasa, uwanja wa kiuchumi na uwanja wa kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusema kwamba wakati umefika hapa Tanzania, hili linakuwa ni sehemu ya Jumuiya hii ya Afrika ya Mashariki, tuone kwamba sisi kama Taifa, tunu zetu zinazotufanya kuwa tofauti na Mataifa mengine ni zipi? Maana tukijenga juu ya tunu hizo za msingi kwetu hili litatuimarisha na kutufanya kuwa bora zaidi katika uanachama huu wa Afrika ya Mashariki. Ninadhani suala zima la lugha, ni lazima tulivalie njuga na kwa sababu hili ni moja kati ya yale yanayotufanya tuwe na tofauti katika nchi hii. Lakini muungano wetu wa kisiasa na umoja wetu na watu kuwa na picha ya Utaifa zaidi kuliko u-mimi na ukabila, ni baadhi ya tunu ambazo tunapaswa kwenda nazo katika Afrika ya Mashariki ndani ya Jumuiya ili hizi zitufanye kuwa tofauti na watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti zipo nyingi ukianza na suala zima la sarafu, tuna tofauti, shilingi kwa Uganda na Kenya, kwa upande wa wenzetu wa Rwanda na Burundi unakuta tuna tofauti kubwa lakini pia hii ni taswira ya uchumi. Pia tumetofautiana kiuchumi, kwa upande wa huduma za jamii, kuna haja Wizara inayohusika kuanza mjadala wa kuwa na *Common Community Policy*, angalau tukawa na sera zinazoshabihiana katika maeneo kadhaa ya msingi hasa katika suala la zima la soko. Tukiwa na Soko la Pamoja, ni lazima tukubaliane na misingi ya soko lakini pia katika uwanja wa kilimo, mifugo, uvuvi na rasilimali zingine za asili, ni lazima tuwe na makubaliano, ardhi isiwe sehemu na ninakubali na kumpongeza Waziri kwa msimamo tuliokuwa nao kama nchi, kutotumia ardhi kama bidhaa inayopelekwa pia kwenye soko hili la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vingine tunapaswa kujiuliza kama tuna Sera ya Pamoja, tunakuja katika suala la viwanda, miundombinu lakini pia hifadhi ya mazingira kwa sababu tukiwa na tofauti kubwa mno katika maeneo haya, tutaingia katika matatizo tena kama yale ya mwaka 1977, Jumuiya ilipovunjika. Tunapaswa kuandaliwa na sisi tuijandae kama nchi maana ni kweli kabisa kuwa kuna hofu kubwa na hofu yenyewe inatokana na udhaifu tuliokuwa nao kama nchi katika kuwekeza kwenye suala zima la elimu, suala zima la kuendeleza rasilimali watu na kwa sababu hiyo tunaona kwamba tunapoenda kushindana na baadhi ya watu wanaotoka kwenye nchi za Afrika ya Mashariki sisi tutapoteza. Wasiwasi huo upo lakini dawa ni kujaribu kugeuza vitisho hivyo na kufanya kuwa ni fursa kwetu ili tuweze kuwekeza na kujipanga vizuri kwenye uwanja mzima wa kuwaendeleza watu wetu. Uwanja wa kuendeleza rasilimali zetu, uwanja wa kuendeleza teknolojia na uwanja wa kuendeleza viwanda kwa sababu tishio linakuja kwamba katika Soko hili la Pamoja na kwamba soko la ndani limepanuka zaidi ya watu milioni 130 badala ya wale milioni 40 ambao tumekuwa nao lakini hicho tutakachokiwa ni kipi? Changamoto kwetu ni kujaribu kubainisha kwamba tunaingia kwenye hili Soko la Pamoja lakini tunaingia ili tuuze nini, maana kwa sasa ukitazama hasa kwenye mpaka wa Namanga kinachosafirishwa ni malighafi zaidi kwa sura ya magogo, mahindi, viazi, machungwa lakini kama tungeongeza thamani ya vitu hivi kwa kuwa na viwanda hapa kwetu, tungenufaika kabisa kama nchi. Kwa hiyo, nadhani tuanze kujipanga na kuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba yale tunayoenda kuyauza katika Soko hili la Pamoja ziwe ni bidhaa ambazo zimekamilika na thamani imeongezwa kwa sababu kwa njia hii watu wetu watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fursa zipo nyingi lakini Wizara ifanye kazi moja kubwa ya kubainisha fursa hizo lakini pia kuandaa *programme* maalumu ya mafunzo kuwajulisha Watanzania wengine kwamba fursa tunazo katika maeneo yapi na lazima tutazame suala zima la *comparative advantage*. Tunadhani kwamba sisi tuna maanufaa katika maeneo yapi na katika nyanja zifi maana siyo rahisi kuwa *absolutely advantage*. Kwa hiyo, ni vizuri tukajaribu kujenga juu ya maeneo yale ambayo tunaona kama nchi, kama wana Afrika ya Mashariki, tuna *comparative advantages* katika maeneo yapi na hili ni sharti liongozwe na tafiti za kisayansi zitakazotuelekeza kama nchi kwamba Sera zetu tuzielekeze mahali fulani au jitihada zetu tuzielekeze mahali fulani ili tuweze kunuifa katika Shirikisho hili la Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa suala la usalama, kwamba mipaka ya Burundi, Rwanda na DRC, ina matatizo, mpaka kati ya Kenya na Somalia una matatizo, kwa hiyo, kuna haja ya kuhakikisha kwamba katika mipaka hii ya nje, ulinzi na usalama unaimarishwa ili kusudi tuweze kuwezesha *movement* ya watu katika mipaka hii ya ndani kwa sababu tukiachia hii mipaka ya ndani ikawa huru na ni lazima iwe huru itakuwa na gharama ya kuhakikisha kuwa mipaka ya nje inaboreka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofî*)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hizi mbili ya Afrika ya Mashariki na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri, ni Wizara ambazo zimeshikwa na Mawaziri hodari sana. Mheshimiwa Membe pamoja na Mheshimiwa Dr Kamara pamoja na Naibu wao Mahiri amba ni Maaskari wa Miamvuli amba hakika tumeona wanafanya kazi nzuri, tumeona bidii yao, kwa kweli ninawapongeza sana. Vilevile nachukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Iringa pamoja na Mkoa wa Njombe hususani akina mama amba miaka mitano nyuma walinipa ridhaa ya kuingia katika jengo hili. Nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitawatambua asubuhi ya leo, ninasema ahsanteni sana hususani akina mama kutoka Wilaya ya Ludewa, Makete, Njombe, Kilolo, Mufindi, Iringa Mjini na Iringa Vijijini. Vilevile niwashukuru sana kwa ushirikiano wao na niseme tu kwamba ombi lao la kuniomba niendelee kuwa Mbunge kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, nimelikubali na hivyo tutashirikiana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba nianze na Wizara ya Afrika ya Mashariki. Nipongeze sana Wizara hii kwa kweli imefanya kazi kubwa, hatua nyingi ambazo zimechukuliwa katika ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, tumeanza kuziona zikizaa matunda, hatua ya Soko la Pamoja lakini vilevile ningeomba nikumbushie hatua muhimu ya kuwa na Sarafu Moja (*Monetary Union*). Hatua hii itasaidia sana kuharakisha maendeleo mbalimbali ya hizi nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ambapo mwanzo zilikuwa tatu Tanzania, Kenya na Uganda na sasa ziko tano Rwanda na Burundi zimeingia. Kwa hiyo, suala la kuwa na Sarafu Moja kama wenzetu

wa *European Union* litasaidia sana, kwa sababu tunapotoka nchi moja kwenda nchi nyingine, unapotoka Tanzania kwenda Kenya, unapobadilisha pesa pale tayari mwananchi inabidi alipe *tax* na vitu mablimbali, sarafu hizi zimetofautiana. Kwa hiyo, mimi ninaomba tu-*fast truck* ili hatua ya kuwa na Sarafu Moja (*Monetary Union*) ifike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, ni muhimu tukaweka mikakati mbalimbali hususani kuhusiana na suala la kuwa na Soko la Pamoja. Wakati mwingine katika nchi yetu tunakuwa na huduma mbalimbali mfano za barabara, huduma za reli n.k. Kwa mfano, ndege kutoka mashirika mbalimbali mfano *British Airways*, *Kenya Airways* na mashirika mengine mengi ya nje yanakuja Tanzania. Mashirika haya yanapokuja Tanzania, kuna wakati nilikuwa maeneo yale, unakuta ndege ina-*land*, inalipa *landing charges* baada ya hapo watu wetu wanaingia mle ndani kusafisha yaani (*cleaning*) wamevaa *gloves* kusafisha, *cleaning of the Airline*, baada ya kumaliza kusafisha zile *Airline* inaondoka. *British Airways* kuna Watanzania kadhaa wamelipa *ticket* maana yake zile *ticket* wanapokwenda kulipa ni kwamba unapeleka uchumi wako kwa ile nchi kama ni *British* maana yake ni Uingereza, kama ni *Gulf Air* unapeleka ile hela yako nchi ya Kiarabu, maana ni Shirika la Kiarabu kama ni Emirates, Dubai, sisi Tanzania hatuna *Airline and you can imagine* mtu mmoja wakati mwingine to one destination anatumia mpaka dola za Kimarekani 7000, unakuta Watanzania 10 wanapanda *Airline*, sasa ni kiasi gani wanapata lakini sasa wakija ku-*land* na kuondoka, ni muhimu tukawa na mikataba. Tuwe na *Memorandum of Understanding*, Mashirika haya yakija ku-*land* basi hata maji wanashindwa kununua? Kilimo Kwanza, Ushirikiano wa Kimataifa, Wizara ya Miundombinu tusaidiane wasije tu kuwa wana-*land* na kuondoka, tunaingia kusafisha meza, tunapukutapukuta, haya, ahsanteni sana, hapana let us trade with them, tuwe aggressive, tupigane kama kahawa, tuna kahawa, korosho tunazo, kwa hizi *Airline* tuna soko la uhakika sana. Kwa hiyo, mimi ningewaomba sana wataalamu wetu mtusaidie, Viongozi wetu Mawaziri wanafanya kazi vizuri sana na wameshawapa wataalamu wetu Ilani, tuna Ilani tumesema tutaweka mikakati na wameweke mikakati, kwa hiyo, wataalamu wetu tunaomba mtusaidie *Memorandum of Understanding* kwenye hizi *Airline* siyo wanakuja tu wanachukua uchumi wetu wanaondoka, hapana let us trade with them.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hayana *test*, vitu kama kahawa, Chai ya Tanzania, *Arabic Tea* tunayo, mashirika haya ya nje chai yao hata *test* haina. Imebadilika tu rangi lakini sisi tuna *Lemon Tea* kutoka Mufindi pale, tuna viwanda vya chai, tunavyo vitu vina *test* na vina afya kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, nilidhani tunaposema tunakuwa na Ushirikiano wa Kimataifa, Soko la Pamoja, ni vema tukawa tunaweka mikakati lakini nipongeze sana jitihada ambazo zimefanyika na Wizara tunakuta masoko ya bidhaa mbalimbali yanaenda vizuri kwa mfano tuna-supply umeme, chumvi, magunia, mafuta, sabuni, kwa kweli maeneo haya tunafanya vizuri sana. Kwa hiyo, ninaomba kutoa mawazo kwamba kuna masoko mengine yako very clear kila Shirika likija lina *trade* katika bidhaa fulani haya ni masoko ambayo yako clear, mnachukua dola zenu, tunaendelea na maisha Bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo pia ningeomba kulisemea ni juu ya mtandao wa reli ambao tutakuwa nao katika Wizara hii ya Afrika ya Mashariki. Katika mtandao wa reli, *master plan* imeshaandaliwa na reli hiyo itapita maeneo ya Liganga, Mchuchuma, Mtwara na Mbambabay. Kwa hiyo, kwa kupitia mchango wangu huu, nitashukuru sana nikiwa kama mdau wa eneo hilo, nkipata hiyo *master plan* ili tuweze kubadilishana mawazo lakini pia tutafurahi kujua baada ya *master plan, project* hii inatarajiwa kuanza lini? Maana suala la Mchuchuma na Liganga, tumekuwa tukilisikia muda mrefu sana kwamba litaanza mara moja na jitihada zimekuwa zikifanyika, tunaishukuru Serikali kwamba jitihada zimeshaanza kufanyika maeneo hayo. Lakini suala la miundombinu ni lazima lipewe kipaumbele. Kwa hiyo, nishukuru sana Serikali na Wizara lakini tuendelee kuwa na ushirikiano wa karibu sana na wadau wa hilo la Mchuchuma na Liganga katika harakati za kuwa na reli maana ndipo tutakapoweza kufanikisha uzalishaji wa madini yanayopatikana huko Ludewa, Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masuala ya Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri sana na Naibu wake, Mheshimiwa Balozi Seif, tumeshuhudia tunaposema Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kweli nchi yetu ni ya kwanza, nchi zingine ndiyo zinafuata kwenye ushirikiano wowote. Iliwahi kutokea, alikuja mtu mmoja wa nchi za nje, ikatokea Trafiki amesimamisha gari lake, yule mgeni akamtemeaa mate Trafiki yule, kwa kweli sisi Watanzania ilituuma sana. Sasa tunasema hawa watu wa nje wanakuja nchini kwetu, hawatuheshimu lakini tunashukuru Wizara ilichukua hatua na kumrudisha yule mtu mara moja tena ilikuwa ni kwa faida ya maisha yake. Kwa hiyo, nimponeze sana Waziri kwa hatua zile. Mimi binafsi sikupendezwa maana huwezi kwenda Uingereza au Marekani ukafanya kitu hicho, unapita tu kwa Askari wao, unamtemeaa mate, lazima hizo nchi zinazokuja ziwe na adabu kwa nchi yetu ya Tanzania wasifike na kufanya mambo kienyejenyeji muda wa Ukoloni umeisha. Sasa hivi tumewaambia kwamba Waafrika tunaweza na Marekani Rais wa pale sasa ni Mwfrika na nchi zingine zijue kuwa Waafrika sasa hivi uwezo wanao, nguvu na sababu za kuongoza na kutawala tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni juu ya Balozi, nchi nyingi sana wameanza kufunga Balozi zao Tanzania, sasa hili ningeomba Wizara ijaribu kuangalia kwa nini wafunge, wanatuwekea Balozi ndogo, matokeo yake Watanzania wakitaka kwenda Canada au Australia, ni lazima huyu Mtanzania aende Kenya. Anapoenda Kenya anapanda *Kenya Airways* maana ule uchumi anapeleka Kenya, *ATC* yetu ndiyo tunaiona hivyo. Anakwenda, anawachangia halafu akifika kule alale, ale, tayari uchumi wa nchi jirani unaongezeka sisi kwetu hizi Balozi zinazofungwafungwa hizi *if they want to trade with us*, kama wanahitaji *relation*, wawe na Balozi zao Tanzania. Sasa kieleweke kwa nini wanafunga Balozi, wanatuwekea nchi za jirani inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu ni bora wangemuweka Afisa kwenye Balozi zao, unakuta wanaotaka *visa* wakati mwingine kuna watu mbalimbali 20, sasa wale watu 20 kila mmoja achukue tiketi yake kwenda Kenya, *what is this?* Wangemuweka Afisa mmoja basi *a-collect Visa* za Watanzania, Afisa wao mmoja wa Ubalozi aende akawashughulike arudi lakini *otherwise this is not fair* yaani siyo halali kabisa wanataka kushirikiana na sisi lakini hapo hapo wanafunga Balozi, wanatuwekea Balozi Ndogo, huu

Ushirikiano wa Kimataifa ukoje? Kwa hiyo, nilidhani hilo Mheshimiwa Waziri atusaidie kuongea nao kwamba kama wanahitaji ushirikiano na Tanzania basi hapo tuheshimiane, Balozi zao ziwe Tanzania, wasiweke kwenye nchi jirani, basi wafunge Ubalozi wa Kenya na nchi nyingine walete Balozi zao hapa ili wale wawe wanakuja hapa kwetu. Kwa hiyo, kwa hilo, nilidhani kuwa ni lazima tuwe *strict*, tuwe makini sana. Kwa kufanya hivyo, itatusaidia kuwa na ushirikiano mzuri na nchi hizo waelewe kabisa kuwa sisi tuko makini maana abiria wengi sana wanatoka Tanzania kwenda kufanya kazi za kiofisi, biashara n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni la Balozi ya Israeli, muda mrefu sana tumekuwa tukiulizia kwamba ni vyema tukawa na Ubalozi wa Israeli. Kadri siku zinavyozidi kuendelea, watu wengi sana wamekuwa wakienda nchi mbalimbali, Israel, Palestina, sasa nchi zingine zimekuwa na Balozi lakini Ubalozi wa Israeli Tanzania bado. Kwa hiyo, hii pia ni mionganoni mwa zile nchi ambazo Balozi zao ziko Kenya kama Canada na nyingine. Kwa hiyo, maeneo hayo ningeomba niweke msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya kusema hayo, niwapongeze sana Mawaziri wetu na Manaibu wao, kwa kazi nzuri na nizidi kuwaombea kwa Mungu na hata kwa wapiga kura, waweze kuwapitisha, waweze kurudi, ili waendelee kuwaendeshea gurudumu letu hili la maendeleo ya nchi yetu, tuweze kwenda kwenye ile nchi ya ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa heshima na taadhima, naomba niunge mkono hoja. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, kwa kutuhitimishia wachangiaji. Kwa bahati tulibahatika kuwa na wachangiaji saba ambao wamekamilika kwa mchango wa Mheshimiwa Chana.

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JUMA H. KILLIMBAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Bernard Membe (Mb), Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Balozi Seif Iddi (Mb), Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kazi nzuri ya kuandaa na kuiwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maoni kadhaa kuboresha bajeti ya mwaka 2010/2011. Jengo la zamani la Ubalozi wetu wa Washington DC, atafutwe mjenzi kwa njia ya *Build Own and Transfer (BOT)*, ili alikarabati na baadaye alitumie kwa muda fulani kabla ya kulirejesha kwa Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za watumishi wa Balozi za Washington DC na New York zikarabatiwe, Wizara/Serikali isipuuze. Kadhalika Kodi ya Pango kwa

watumishi mbalimbali ipelekwe kwa wakati kwani upo usumbufu mkubwa wanaoupata watumishi kutokana na kufungiwa nyumba na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara ya watumishi kwa Balozi zetu ipelekwe kwa muda muafaka yaani kila robo ya mwaka kwa utangulizi, kuwacheleweshea mishahara watumishi wa Balozi nje ya nchi, ni adhabu kubwa na ni jambo lisilostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ipeleke fedha kwenye Balozi zetu kwa ajili ya maadhimisho ya Sikuu za Kitaifa mfano Siku ya Uhuru na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Waziri mwenye dhamana ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, pia nimpongeze Mheshimiwa Mohamed Aboot Mohamed, Naibu Waziri wa Afrika Mashariki, nimpongeze Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa maandalizi ya Bajeti ya 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao ushauri katika maeneo machache kwa nia ya kuboresha utendaji wa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Soko la Pamoja (*Common Market*) bado nasisitiza juu ya Wizara kuendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi wa Tanzania juu ya mtangamano kuhusu jjumuiya Soko la Pamoja ni kweli kabisa Watanzania walio wengi hawajui kabisa hali halisi ya Soko la Pamoja, sio hilo tu hata ufahamu kuhusu Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kunaweza kukaleta athari za hasara kubwa mionganoni mwa wananchi wa Tanzania ambapo upo uwezekano mkubwa fursa nyingi kuporwa na baadhi ya wanajumuiya mfano mzuri ushindani wa bidhaa mbalimbali katika soko la ajira na fursa zingine nyingi ambazo hazijachangamkiwa na Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi pamoja na Mkataba wa Jumuiya kueleza wazi wazi juu ya kila nchi mwanachama kutumia sheria za nchi yake kuhusiana na masuala ya ardhi lakini lazima taha dhira iwepo juu ya kudhibiti wanajumuiya baadhi yao wanaoweza kujipenyeza na kwa kuwa jamii ya wananchi wa Afrika Mashariki inafanana sana wakatumia udhaifu huo kujipenyeza vijijini na kupora ardhi kwa kununua kwa bei hafifu na baadaye ikawa mali yao. Pia wanaweza kutumia fursa ya kofia ya uwekezaji. Sheria ya Uwekezaji ione na kubaini wanajumuiya wa aina hii na ni nchi ipi wana tabia ya tamaa ya kupora mali ya nchi mwanachama wenzake. Wizara ishauri Jumuiya kuharakikisha ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya katika Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Napongeza ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na nchi mbalimbali. Nampongeza Rais kwa kukubalika katika nchi mbalimbali na hata Marais wa huko kufika Tanzania, nampongeza sana. Naamini mwaka 2010 hali itakuwa ya kupendeza zaidi na ya kukubalika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja ambalo linaninyima raha kabisa katika kipindi changu cha Ubunge kuanzia 2005-2010, nalo ni suala la kuwapa uraia wakimbizi na wakimbizi hawa kupata vitambulisho vya uraia. Wao wangepata utambulisho wa kuishi Tanzania si kuwa raia wa Tanzania. Waruhusiwe kupiga kura, kupata uongozi, hapo ndipo nashindwa kuelewa kabisa. Sasa naomba kupata ufanuzi ingawa najua yapo mambo ya ndani, nitaridhika sana kupata ufanuzi labda nitafarijika. Najua hawa ni watendaji, wanajituma kwa kilimo, biashara lakini bado hawana sababu ya kupata uongozi hapa nchini na ukizingatia ugomvi wao ni wa kisasi, kikabila na nchi yetu haina ukabila na hata kubaguana, hawa wasije kuleta virusi hivyo Tanzania.

MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, naomba kutoa pongozi nyingi kwako, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii, kwa utendaji kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Mabalozi na Maafisa wa *Foreign* popote walipo. Mheshimiwa Waziri, wewe binafsi unatupa moyo sana kwa utendaji wako mzuri na jinsi unavyoikeni nchi yetu katika nafasi ya juu Kimataifa yaani “*International Personality*” ya Tanzania inaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kote tulikotembelea tumepokewa na kukarimiwa vizuri sana na Mabalozi pamoja na Maafisa wao yaani tumepata “*Consular Assistance*” (*First Class*) kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iongeze malipo ya fedha za tahadhari katika Balozi zetu nchi za nje. Aidha, Mabalozi na Maafisa hawa walipwe motisha kubwa ili wafanye kazi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri umekuwa taabu sana katika Balozi hizi. Tunaomba Serikali ikubali na kuhakikisha kuwa Balozi zinakuwa na usafiri wa kutosha na wa kuaminika. Mimi nimeshuhudia ukosefu wa usafiri katika Balozi hizi hadi wanakodisha magari kibashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Wizara haitoshelezi. Heshima ya Taifa ni ghali sana. Kwa hiyo, Serikali isiwe na kigugumizi ila ikubali kuipa Wizara hii bajeti kubwa zaidi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hoja 100%. Ahsante sante.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali kwa kuondoa aibu inayopata nchi yetu kwa kutolipa madeni ya uanachama wetu katika Jumuiya ambazo sisi ni wanachama. Tunaomba jambo hili liendelezwe ili lisitokee tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mashirika yale ambayo yanatusaidia kama vile ya *APRM*, ni lazima tuoneshe nia yetu njema. Ninapenda kujua kama mwaka huu wa fedha mchango wetu kwa *APRM* utalipwa na kama mwaka huu kuna fedha za

kuwezesha *APRM* kufanya kazi zake hapa nchini bila vikwazo vya kifedha. Mwaka wa fedha uliokwisha, Serikali haikuiwezesha *APRM* kufanya kazi zake vizuri kutokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iimarishe mahusiano na nchi zote ili kuendeleza diplomasia ya uchumi. Uchumi ndio siasa ya sasa, hivyo Serikali iharakishe kufungua uhusiano na Morocco. Tunapoteza nini au tunapata faida gani kwa kuwa na uhusiano au kutokuwa na uhusiano wa kidiplomasia na Morocco?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia bado kina matatizo ya ardhi pale kilipo. Naomba kujua kama Serikali imefanya mawasiliano na Serikali ya Msumbiji, kama Msumbiji haitaki kuendelea na Chuo cha Diplomasia, kwa nini hawakiachii ili Tanzania ibadili hati za ardhi? Aidha, naipongeza Serikali mwaka huu, Chuo angalau kitabhatika kupata nyongeza ya fedha za kukiendesha. Ni matumaini yangu kuwa Chuo cha Diplomasia kitakuwa “*Centre of Excellency*” kwa masomo ya Diplomasia nchini.

MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa uwasilishaji mzuri wa hotuba, imesheheni hali halisi ya siasa yetu ya nje kama ilivyoelekezwa na Ilani ya CCM ya mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa uwasilishaji mzuri. Hotuba yake imetoa hali ya ushirikiano na mwelekeo wa Afrika Mashariki kwa siku zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubalozi wa Tanzania nchini Ujerumani ulifanya juhudzi za kuanzisha mahusiano maalumu kati ya Tanzania (Kigoma) na Jimbo la *Niedersachsen* (*Lower-Saxon*). Mahusiano hayo maalumu yanatokana na historia iliyopo kati ya Mkoa wa Kigoma na Mji wa Papenburg huko *Niedersachsen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia hii inatokana na kwamba meli ya MV Liembe ilitengenezwa na Kampuni kutoka Mji huu (Meyer-weft). Kumekuwa na ziara ya viongozi wa mji huu mnamo mwezi Februari ambapo walitembelea Mkoa wa Kigoma na kutembelea MV Liembe. Ziara hii iliratibiwa na Wizara na Ubalozi wetu huko Ujerumani. Hata hivyo, suala hili halimo kabisa katika hotuba ya Waziri na hii maana yake ni kuwa suala hili halina umuhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Ujerumani tayari imeteua *Consultant (KFW)*, kwa ajili ya kuangalia jinsi ya kutunza *heritage* hii kati ya nchi zetu mbili.

Imetengwa bajeti ya £9m kwa ajili ya *project* hii ya MV Liemba. Naitaka Wizara ya Mambo ya Nje, ihakikishe kuwa mahusiano haya yanaendelezwa na mradi huu unafanikiwa. Naomba Mheshimiwa Waziri alitolee kauli suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia Serikali inafanya mpango na nchi ya Morocco ili kuanzisha mahusiano ya Kibalozi. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa kuna msimamo wa *O.A.U/AU* toka mwaka 1984 kuhusiana na suala la Sahara Magharibi. Tusipinde “*Principles*” zetu kwa vigezo vya “Diplomasia ya Uchumi”. Heshima yetu Afrika imejengwa na misimamo yetu ya kutetea wanyonge lazima tuendelee kutetea wanyonge duniani kote.

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, kwani Wizara hii ni ufunguo na dira sahihi ya utandawazi. Napenda kumpongeza Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Membe pamoja na Naibu wake kwa kuongoza Wizara hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda kutoa angalizo langu kwa Wizara hii, kwani kuna wawekezaji wengi amba ni wababaishaji amba wanatoka nje na kuja hapa nchini kuwekeza, lakini wanatumia upungufu wetu kutuingiza katika mikataba yenye kuhatarisha maslahi na usalama wa Taifa letu. Ni vema basi Wizara hii ikafanya uchunguzi kujua ni nchi gani wanatoka na huko wamewekeza nini na wanaingizia nchi hiyo faida gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujua, nilipokuwa Afrika Kusini nilipata habari kwamba Balozi wetu huko alivamiwa na kupigwa, kuporwa gari na baadhi ya vitu vyake na hali yake ilikuwa mbaya, anaendeleaje? Je, wahalifu hao walipatikana na Afrika Kusini inasema nini kuhusiana na suala hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza Mabalozi wetu kwa kuitangaza vema nchi yetu kuhusu fursa zinazopatikana katika uwekezaji, biashara na utalii. Hivyo basi, tunawaomba watendaji wetu hapa nchini waweze kusimamia vema yale yote ambayo Mabalozi wetu wanayafanya kazi, ili kuendana sawa na kazi na matokeo yake, ili kulipatia faida Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuchangia hoja ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwanza, napenda kumpongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Mheshimiwa Kamala na Naibu wake Mheshimiwa Mohamed Abood kwa kazi yao nzuri na kwa kuwa makini kwa kutoa na kupanga mipango ya kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nami napenda kutoa angalizo kuwa nchi ambazo tumeingia nazo katika Jumuiya, kila moja ina tamaduni zake, siasa na utaratibu wake na katika baadhi ya nchi ni nchi ambazo hazina amani, ni nchi za vurugu na vita vya mara kwa mara. Hivi hii hatuoni kama inaweza kutuletea matatizo mbalimbali katika nchi yetu na kutofikia lengo ambalo tumekusudia? Kwanini hatukukaa na kutafakari kwa kina matatizo tuliyonayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kuwa sisi ndani ya Tanzania hatujamaliza kero zetu za Muungano na sasa tunataka kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Je, kama nako kutakuwa na kero ina maana tutakuwa kazi yetu ni kujadili kero, nazo utatuzi wake zinachukua muda mrefu sana kwani hata Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulikuwa na mkataba wa Muungano. Mimi binafsi naona tumeingia haraka katika Jumuiya na kwa gharama za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia upande wa ardhi na Serikali pia kutoa ardhi kwa wawekezaji na kutojali wananchi wao kama ambavyo jana Mheshimiwa Mwanawetu alivyokuwa akichangia kuhusu mwekezaji mzungu ambaye anataka kuchukua baadhi ya vijiji zaidi ya 19. Hivi kama hili linawezekana leo, kesho itashindikana nini kupewa ardhi Mkenya au Mganda hata Mrundi pia? Watanzania tulio wengi hatuna uzalendo hasa wanaopewa nafasi za kuongoza vitengo kama ardhi. Hata hapa ndani kesi za ardhi ni nyingi, kanyang'anywa huyu na kupewa mwingine kinyume na taratibu, maeneo ya wazi kuuzwa kwa bei kubwa na Watendaji wa ardhi. Hii inaonyesha kuwa hatuna uwezo wa kutunza ardhi yetu. Kama sisi kwa sisi hatuoni haya kufanyiana kinyume, je, kama kaja raia jirani na kaja kamili atanyimwa kweli ardhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania tumezoea kuishi kwa amani na uvumilivu, hivyo basi wananchi wetu tusije kuwaingiza mashakani kwani wananchi hawa ni wanyonge na hawajazoea vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali kuwa makini zaidi kwani maji ukishayavulia nguo huna budi kuyaoga. Basi tuyaoe yakiwa na uvuguvugu na sio ya moto au ya baridi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nitumie nafasi hii, kumpungeza Mheshimiwa Waziri, Naibu na Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kuiweka nchi yetu katika ramani ya dunia. Tusione vikielea vimeundwa, yote ni matokeo ya kazi nzuri ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Kwa miaka mingi tumekuwa tukiomba Wizara hii ione namna ya kuimarisha ofisi zetu za Kibalozi nje ya nchi. Uimarishaji wetu si kwa ajili ya majengo tu na idadi kubwa ya watumishi bali kwa kuwa na watumishi wenye mwelekeo wa kuiweka nchi yetu itoe huduma safi na nzuri kwa ajili ya kuwavutia wageni waje huku na kuwekeza. Pale tuliomba tuzichunguze na kuzipanga upya Balozi zetu ili tubaki na chache tu za muhimu ili tusipoteze fedha kwa kuwa na Balozi zisizokuwa na umuhimu wa pekee kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais, kwa jinsi anavyopanga ziara zake nje ya nchi, kwa kuzingatia safari zenye manufaa kwa Taifa. Tutaendelea kumshauri Waziri wetu, Mheshimiwa Membe, awe anapata nafasi ya kutosha kuelezea vyombo vya habari juu ya mafanikio ya safari hizi za Rais ili wanaobeza safari za Rais, wasipotoshe umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aendelee kutoa elimu kuhusu mchakato wa nchi yetu kuwa na uraia wa nchi mbili. Nadhani linalohitajika ni elimu ya kutosha kwa watu wetu. Bado wengi wanaipotosha dhana hii ambayo ingeeleweka vizuri, tungefaidika sana na mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Diplomasia kingeweza kufanya mambo mengi kama kitapewa kila aina ya msaada wa kitaalamu na kifedha. Chuo hiki kingeweza hata kutupatia utafiti wa miongozo sahihi ya mahusiano na nchi mbalimbali. Matatizo ya nchi mbalimbali na suluhisho la matatizo ya nchi hizo yangeweza kutupatia ukweli wa hali halisi ya mambo mengi. Naomba Waziri alione hilo, ni muhimu sana kwa maendeleo ya mahusiano ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kwa moyo wa dhati nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kazi kubwa sana waliyoifanya kwa hali ya viwango vya juu hadi kufikia hatua hii ya ushirikiano wa nchi zetu za Afrika ya Mashariki. Mmeweka historia na mtakumbukwa sana kwa kazi nzuri mliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kazi nzuri hii, tusiibezo bali tuienzi. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mafanikio ya utekelezaji wa itifaki ya soko la pamoja. Ni kweli bado watu wetu wengi hawajapata nafasi ya kuelezwala ili lieleweke vizuri. Soko la pamoja ndiyo msingi wa kukuza uchumi na maendeleo ya kijamii. Ni vizuri tuanze na uundwaji wa soko kwa kuzingatia hatua mbalimbali ili lieleweke vizuri. Wizara husika lazima ziratibiwe mapema ili masuala ya mitaji, ajira yawekwe wazi. Fursa lazima ziwekwe wazi na tuandae taasisi za kushughulikia masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa vyombo vya fedha hapa nchini navyo viandalifi ili visaidie azma hii ya soko la pamoja. Hili ni suala ambalo lazima lipewe umuhimu wake ili upande mmoja uonekane umejiandaa vizuri kuliko wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na mpango uliletwa na UN- Habitat kwa nchi zinazozunguka Ziwa Victoria ili wapate huduma ya maji kwa miji kumi kwa kila nchi. Lakini hadi leo inaonekana wenzetu wa Kenya wameendelea vizuri katika kutumia msaada huo. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili maana huu ni mradi wa ukombozi kwa wakazi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mpango wa *Kagera Basin Development Projects* ambazo zilikuwa ziendeze miradi ya kilimo (Ngoni) umeme (Rusumo) na kadhalika, ambao ulikuwa uwe wa nchi za Tanzania, Rwanda, Burundi na sehemu ya Uganda, sijui umeishia wapi maana huu mradi ulikuwa uwe suluhisho kwa uchumi wa nchi yetu kupitia kwa wenzetu wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri alifuatilie suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyolishughulikia suala zima la jumuiya yetu. Kweli tumepata Waziri. Namtakia kheri, mafanikio katika uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili.

MHE. MOSSY S. MUSSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na uwasilisho mzuri wa Mheshimiwa Waziri, naipongeza Wizara na watumishi wake wote. Kwanza napongeza sana *protocol*, kwa uwajibikaji wake ambao Watanzania tunajivunia sana kwa mipangilio yao mizuri katika hafla za Kimataifa na Kitaifa kwani siku zote wamekuwa “*smart*” katika fani yao ya utumishi uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, naomba kidogo nichangie katika kile ambacho siridhiki nacho, ni kule kutokuhusika vizuri katika matukio ya vifo vyta Watanzania wanaouwawa nje ya nchi. Wizara imekuwa nyepesi kusimamia mazishi, kusafirisha mwili na sio kukemea au kutoa kauli nzito kwa kufuata misingi ya kidiplomasia. Mifano ambayo tunaiona kwa nchi za wenzetu kama Marekani, Israel, Kenya, ambao huonyesha “*seriousness*” katika matukio kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa mbunifu mkubwa wa mambo ambayo hutegemea kuvuma lakini tumekuwa wazito kufuatalia mambo yetu, mfano, Sullivan ilikusanya wageni ambao sio tu walishiriki m Kutano ule mzuri walishangaa Tanzania kuwa na rasilimali nyingi na huku tukiendelea kutaka misaada toka nje. Hii inaonyesha dhahiri kwamba nchi yetu haiuzwi vizuri nje na hata kama ikiuzwa bsi inakuwa kwa njia ya kimchezomchezo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Diplomasia, lazima kipewe kipaumbele kabisa kwa kuwapata Wanadiplomasia bora kama walivyo hawa wanaokaribia kustaa fu wazuri, waadilifu, *smart*, wa kweli, hofu yangu ni kuja kuwaingiza vijana wasio na sifa nzuri kutokana na *background* yao kutokuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nashauri Wizara hii itoe kipaumbele kwa watumishi wake hasa walio na umahiri mkubwa wa kufanya kazi Ikulu kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais katika shughuli zake mbalimbali hata zile za habari na usimamizi wa safari za ndani n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kushauri majengo ya Wizara hii yabadilishwe kufuatana na unyeti wake, iondokane na *style* hii ya sasa ya magofu na hasa lile la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima wa afya na nikawenza kuandika maoni yangu katika hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii nataka kujua mpaka hivi sasa Tanzania ina Balozi ngapi zinazokodi majumba huko nje? Ikiwa zipo ni kwa nini hatujengi au kununua nyumba zetu wenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nataka kujua kuwa katika Balozi zetu kuna Balozi yoyote inayokodi gari? Ikiwa zipo ni Balozi gani hizo na kwa nini tufanye hivyo? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Waziri nataka kujua katika Ushirikiano huu wa Afrika Mashariki sisi Pemba tutanufaika kwa miradi gani na itaanza lini miradi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu habari za Afrika Mashariki kwa Watanzania wa kawaida wanafikishiwa vipi? Mbona mimi naona wananchi wengi hawaelewi mambo hayo yanavyoendeshwa wanapata habari mwisho mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri unieleze unafikisha vipi taarifa hizi hata hiyo elimu unayotoa unawapa viongozi tu lakini kwa wananchi wenyewe huja eleza umewafikia vipi? Ili na wao waweze kuelewa na isiwe wanasikia tu kuwa leo Tanzania inaingia katika soko la pamoja na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE.JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Hoja yangu kwa Wizara hii ni kutaka haki itendeke kwa kampuni ya *General Business and Equipment Suppliers Company Limited* ya mjini Itigi (Jimbo la Manyoni West), kwamba Kampuni hii ilinyang'anywa magari makubwa mawili yaliyosheheni *gypsum* iliyokuwa inasafirishwa kwenda Kiwanda cha Saruji cha Cimerwa, Cyangugu Rwanda 1995. Malori hayo yalikamatwa na Serikali ya Rwanda. Baadaye walipokwenda Mahakamani kule kule Rwanda kampuni hii walipewa haki kwamba warudishiwe malori yao na mali au walipwe fidia ya thamani ya mali na malori hayo. Kiwanda cha Cimerwa ni cha Serikali ya Rwanda (*joint venture* na China).

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kushindwa kutekelezewa haki yao kule Rwanda, kampuni ya *General Business and Equipment Supplies Company Limited* ilifungua kesi hapa nchini dhidi ya Serikali ya Rwanda ikashindwa na Mahakama Kuu kuagiza kuwa mali za Serikali ya Rwanda zikamatwe kufidia hasara iliyoisababishia kampuni hii. Hapa ndiyo ikawa mgogoro baada ya Serikali ya Rwanda kutoshirikiana ili kukazia hukumu ya Mahakama. Miezi miwili iliopita nilimwona Mheshimiwa Waziri wetu na kumkabidhi nyaraka za malalamiko ya kampuni hiyo aweze kusaidia kidiplomasia na kwa kutilia maanani itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili haki

itendeke kwa kampuni husika ambayo ni ya Watanzania wanaosaidia kuwapatia vijana wetu ajira kwa kuchimba *gypsum* inayotumika hapa nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua suala hili limefikia hatua gani na kama limepewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. JUMA A. NJWAYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja. Aidha, napenda kuwapongeza Waziri wa Nje Mheshimiwa Bernard Membe, Naibu Waziri wake Balozi Seif Ali Idd na watendaji wote wa Wizara kwa kuitumia nchi yetu vizuri. Hata hivyo nina mchango ufuatao:-

Mosi, Balozi zetu nje zina matatizo ya majengo ya makazi na ofisi, ni vyema uwepo mpango wa kila mwaka kujenga ofisi za uhakika ambao utaandamana na umiliki wa majengo hayo. Huu ni uwekezaji kwa kiasi fulani na hivyo llichya ya uhakika wa majengo na mahali pa kazi (ofisi) lakini ni rasilimali ya msingi nje.

Pili, bado tatizo la Mabalozi wetu kuchelewa mishahara halijapata suluhisho la kudumu. Ni vyema hali hiyo ikarekebishwa kwa ajili ya kuchochea motisha na imani pia heshima ya nchi yetu nje.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa kwamba Serikali imekuwa inaendelea kuimarisha uhusiano wa kiuchumi na nchi mbalimbali kwa kuweka msisitizo katika Balozi zetu kuendeleza Diplomasia ya Uchumi ikiwa ni pamoja na kutangaza fursa zilizopo nchini katika maeneo ya uwekezaji. Haya ni mabadiliko ya kiutendaji ya Balozi zetu ambazo kwa siku za awali zilikuwa zinajielekeza zaidi katika shughuli za ukombozi kwa nchi ambazo bado zilikuwa zinatawaliwa na wakoloni. Ni uamuzi wa busara sana kwamba sasa Balozi zetu zielekeze shughuli zao za kazi kuchangamkia fursa za kiuchumi ili nchi iweze kufaidi fursa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi wetu wengi wamekuwa wanachangamkia ipasavyo fursa hizo ikiwa ni pamoja na kutangaza maeneo ya utalii maeneo mbalimbali ya uwekezaji pamoja na kutafuta misaada mbalimbali kuwa nchi rafiki ili iweze kutumika kukwamua hali duni ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudhi hizi za Mabalozi wetu kama hazikupata ufuatiliaji mzuri kutoka taasisi husika ndani ya nchi, juhudhi zao zinaweza zisizae matunda. Kumekuwa na taarifa kadhaa kwamba baadhi ya watendaji wa Serikali hapa nchini ama wamekuwa hawataki, hawapendi au wanazembea kufuatilia juhudhi ambazo zimeanzishwa na Balozi zaidi katika masuala mbalimbali ambayo kama yalihitimishwa yanaweza kuleta manufaa makubwa kwa nchi yetu. Mfano mzuri ni suala la Ubalozi wetu mdogo uliopo Dubai ambao ulijitahidi kutafuta msaada kutookana na agizo la Mheshimiwa Rais kulitafutia msaada Shirika la Ndege la Tanzania (ATC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Ali Ahmed Saleh, alichukua juhudhi hizo na yeye mwenyewe akaja nchini akifuatana na Mwakilishi wa Mfalme wa nchi moja miongoni mwa nchi za *Emirates* ambayo ilikubali kulifufua Shirika letu la ATC, bahati mbaya baada ya viongozi hawa kuwasili nchini kwanza hawakupata mashirikiano mazuri lakini pia walipigwa dana dana ya hapa na pale na hatimaye viongozi wa ATC waliwatelekeza na lile lengo lililokusudiwa halikutimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuona kwamba juhudhi ambazo zinachukuliwa na Balozi zetu katika kuchangamkia fursa za kiuchumi kwa manufaa ya nchi yetu zinaheshimiwa na kupewa umuhimu unaostahili ili yale malengo yaliyokusudiwa yapatikane, vinginevyo kama viongozi wetu wazembe wataendelea kutuaibisha na kutunyima fursa za kiuchumi kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ya Rwanda iliipatia Tanzania ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba za Balozi. Ardhi hii sasa ni muda mrefu haijaendelezwa kiasi kwamba nchi ya Rwanda imetishia kulitwaa eneo hilo ili lirudi Serikali kwao kwa matumizi mengine. Namwomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni hatua gani itachukua kuhakikisha eneo hilo la ardhi linaendelezwa kwa lile lililokusudiwa au iwapo ardhi hiyo imeshatwaliwa na Serikali ya Rwanda kwa matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 1 Julai, 2010, Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimeingia katika utekelezaji wa Itifaki ya Soko la Pamoja. Ni dhahiri kwamba, Itifaki hii inasisitiza uundwaji wa Soko la Pamoja hatua kwa hatua ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo muhimu ya Soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumeingia kutekeleza Itifaki ya Soko la Pamoja katika hali ambayo Watanzania bado hawana elimu ya kutosha kuhusu Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usio na shaka kwamba, nchi yetu kama itachangamkia ipasavyo fursa zilizomo katika Itifaki hii, tutaweza kufaidika. Pia ni ukweli usio na shaka kwamba, iwapo Watanzania wataingia katika Itifaki ya Soko la Pamoja pasina elimu ya kina na ya kutosha kuhusu suala hili. Watanzania tutakuwa wasindikizaji tu na hatimaye tutabaki kuwa soko la bidhaa za nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina budi kuandaa mazingira madhubuti na sahihi, ikiwa ni pamoja na kuwaelimisha Wananchi wa mijini na vijijini kuelewa jinsi watakavyoweza kufaidika na Soko hili la Pamoja. Kwa kufanya hivyo, kutawafanya Watanzania nao kuwa na fursa sawa na nchi nyingine wanachama katika kufaidika na fursa za Soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa mambo muhimu ambayo yanapaswa kusimamiwa na Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki ni utulivu wa kisiasa katika Nchi Wanachama. Sote tumekuwa tunasikia yanayotokea katika Nchi za Rwanda na Burundi zikiwa zimo katika mchakato wa kufanya chaguzi za kuchagua Maraisi na Wabunge. Kumekuwa na mambo kadha yanayofanywa na viongozi walioko madarakani, ambayo kwa namna moja au nyingine, yanakwenda kinyume na haki za binadamu na demokrasia ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hayo yakinende huko Rwanda na Burundi, nchi yetu imekaa kimya haikemei na wala haisemi lolote kuhusiana na yanayotendeka huko. Ningependa kujua iwapo Tanzania inafahamu madhila ya kisiasa yanayofanyika hivi sasa huko Rwanda na Burundi na ni hatua gani inachukua kuona kuna utulivu wa kisiasa katika nchi hizo na kwamba, haki za binadamu na mienendo ya kidemokrasia yanaaheshimiwa ipasavyo.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa wa Watanzania wengi juu ya Muungano wa Afrika Mashariki bado ni mdogo sana. Wananchi hawaelewi ni vipi Jumuiya ya Afrika Mashariki itawasaidia kuondokana na umaskini uliokithiri vijijini. Hii kwa vipi soko la pamoja la ajira, bidhaa na kadhalika litakavyoweza kubadilisha hali ya biashara yetu ya sasa. Elimu kwa wananchi bado ni ndogo. Waziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki anatakiwa kuandaa wataalamu waende vijijini wakatoe elimu, haitoshi tu kuwa na majadiliano kwenye *television* au kuongea na waandishi wa habari. Ni wananchi wangapi wa vijijini wanazo hizo *television*? Ni wangapi wana muda wa kufuatilia nini kinajadiliwa kwenye vipindi vyta *television*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la ajabu kwa Waziri kwenda kuongea na Watanzania walio nje ya nchi kuhusu soko la pamoja wakati hapa ndani elimu hiyo haipo. Hapa siyo kujenga hisia kwamba kwa kuwa wananchi wanaulizia masuala ya hilo soko la pamoja eti wanalelewa, siyo kweli, hawaelewi ndivyo maana wanauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Soko la Pamoja la Ajira hapa naona sisi Watanzania bado hatuko tayari kwa hilo, hata kwa miaka mitano ijayo yaani 2015 kwa *speed* yetu na uwezo wa kujenga uwezo wa watu wetu bado hatuwezi kuingia kwenye ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hapa Tanzania zaidi ya robo tatu ya watumishi au watendaji wa mahoteli makubwa ni Wakenya kuanzia Meneja, Wakurugenzi hadi wahudumu na wapishi ni kutoka nje kama Kenya. Hapa bado tulikuwa hatujafungua soko la pamoja, je, tukifungua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye mambo kwa mipango na tafiti makini kabla ya kuamua chochote kwa niaba ya Watanzania tusiende kwa hisia wala kubahatisha ili Taifa lifaidike na Jumuiya ya Afrika Mashariki lazima tuwe na wasomi wa kutosha watakaoweza kuingia kwenye soko hilo, vinginevyo sisi Watanzania tutakuwa wafugaji wa mahoteli huku nafasi za juu zikichukuliwa na watu wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu yoyote kwa Rais kusafiri nje ya nchi huku ameongozana na watu 26, hapa ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi. Watu 26 kila moja kwa hiyo, safari moja anatumia siyo chini ya shilingi milioni 10 kwanza tiketi, posho, malazi, chakula na kadhalika na wanakwenda wote kwa ajili ya kazi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya ziara za nje ya nchi kwa yejote lengo ni kujifunza kwa wenzetu kwa hatua za maendeleo waliyopiga ili na sisi tuweze kujua jinsi

ya kusogea. Suala la kujiuliza kweli wakirudi wanaandika taarifa za safari? Je, kama zinaandikwa zinafanyiwa kazi? Nina wasiwas i kama zinafanyiwa kazi kwa sababu tangu tuanze kutumia wataalum nje kujifunza wamejifunza mengi sana lakini bado tunakwenda taratibu sana na yale mazuri tunayokuja nayo tunayaweka kabatini. Kwa hesabu za haraka ndani ya mwaka mmoja tunatuma siyo chini ya wataalamu mia moja kutoka Idara, Vitengo na Wizara mbalimbali tunachopata kinalingana na fedha tunazotumia kutunza wataalamu wetu.

MHE.PROF. PHILEMON M. SARUNGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpungeza Rais Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuanzisha Wizara hii kwa lengo la kuharakisha ndoto za muda mrefu za wananchi wa Afrika Mashariki kuungana na kujitetea maendeleo yao. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kutekeleza malengo na mipango ya Watanzania kushiriki katika ushindani wa kibashara kutoa elimu kwa umma wa Tanzania kutumia changamoto zilizopo katika Jumuiya yetu. Waziri alipokuwa Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri ametetea maslahi ya Taifa letu kwa nguvu zake zote. Namuombea Mwenyezi Mungu amuwezeshe kurudi tena Bungeni pamoja na Naibu Waziri kufanikiwa katika mchakato wa kumpata Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo napenda kuchangia kwa kutoa ushauri na maombi kama ifuatavyo; katika ukurasa wa 24 hadi 25 kuhusu ziara ya mpakani mwezi Septemba, 2009 na Mei 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri au ombi, Wilaya mpya ya Rorya inayo mpaka kati yake na nchi ya Kenya katika kituo kilichoko Kijiji cha Kirongwe, Barabara ya mpakani imeboreshwa na ujenzi wa barabara ya lami hadi mpakani imeanza kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi watendaji na maafisa wa Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki watembelee mpaka huu kama walivyofanya katika mipaka mingine mwezi Septemba, 2009 na Mei, 2010. Naomba Waziri atoe tamko hapa Bungeni leo hii. Asipofanya hivyo, babu na bibi zake wa Wilaya ya Rorya hawatakuwa tayari kumpa baraka zao na atashindwa uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 25 wa hotuba ya Waziri kuhusu vituo vya pamoja vya utoaji huduma mpakani (*one stop border post*). Ushauri au ombi, pamoja na azma ya Wizara kuhakikisha kuwa katika kijiji cha mpakani na Kenya kijiji cha Kirongwe (Rorya) kitaanzishwa kituo cha utoaji huduma mipakani, hali halisi hakuna dalili yoyote upande wa Tanzania, Serikali ya Kenya imeanza kuporomosha majengo upande wao wakati upande wa Tanzania hakuna dalili yoyote ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi sasa waanze ujenzi katika kituo cha uhamiaji kilichoko kijiji cha Kirongwe kuanzia mwezi huu wa Julai, 2010. Kama alivyotamka Naibu Waziri katika kupima viwango wananchi wa kijiji cha Kirongwe na vitongoji vyake wapewe kipaumbele katika kupewa viwango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nampongeza tena Mheshimiwa Waziri na timu yake.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongozi kwa Waziri, Naibu wake na wataalamu kwa maendeleo yaliyopatikana ndani ya EAC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iondoe programU na vipeperushi vitakavyoelimisha Watanzania juu ya fursa zilizopo katika soko la pamoja. Pia EAC iandae *master plan* ya elimu viwanda na miundombinu ili kupunguza tofauti kati ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa mipaka ya nje hasa mipaka kati ya Kenya na Somalia, Rwanda, Burundi na DRC uimarishwe na taarifa ya usalama itolewe na nchi husika mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, EAC iandae *social charter* itakayotumika kuboresha ustawi wa watu wote walio raia wa nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, EAC iandae *common policies* katika Nyanja za kilimo mifugo, uvuvi, viwanda na utunzaji wa mazingira.

MHE. EUSTACE O. KATAGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri na wote katika Wizara walioandaa Bajeti. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilishajiwa Bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utendaji, nawapongeza watendaji wote kwa jinsi wanavyoendesha Wizara hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umakini ninapongeza watendaji kwa umakini mkubwa katika majadiliano yote ambayo yamefanywa na nchi za ushirikiano na kuweza kulinda “interests” zetu watanzania hasa katika maeneo ya Ardhi, Ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umeme wa Murongo/Kikagati, tunashukuru mradi huu umebuniwa na pia *concept* ya kuwa ni muhimu mradi huu Tanzania ishiriki kama mbia na siyo kusubiri kuja kuuziwa umeme na Uganda. Tunaomba uharaka wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya lami Bugene, Nkwenda, Isingiro, Murongo, Kikagati (Uganga), Mbarara, tunaomba barabara hii inayounganisha sehemu hii ya Tanzania na Uganda iwekwe chini ya Afrika Mashariki na Wizara hii iishughulikie ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

MHE. BAKAR SHAMIS FAKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na kuweza kuchangia kuhusu hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wowote ule uwe mtu na mtu au nchi na nchi ni jambo jema sana, lakini ndani ya ushirikiano lazima pawepo kuaminiana, kukubaliana kwa dhati kabisa na pasiwepo na kutegana baina ya walioshirikiana. Swali je, katika ushirikiano huu wa Afrika Mashariki nchi wanachama wa Jumuiya hii wanaaminiana kwa dhati na je, hapana suala la kutegeana? Maana wananchi wengi hasa Watanzania bado wanao wasiwasiju ya ushirikiano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasija wa Watanzania walio wengi kuhusu ushirikiano wa Afrika Mashariki ni kuhusu kuingia kwa wananchi wa nchi wanachama na kujitafutia ajira nchi nyingine, pia kuhusu ardhi yao. Hivyo ni muhimu sana elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi ili waelewe ni kwa kiasi gani Serikali imejipanga kuhusu maslahi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kubwa ambalo mpaka sasa ni tete ni nafasi ya Zanzibar katika Jumuiya hii na hasa tukizingatia kwamba ziko baadhi ya shughuli zinahusika na Zanzibar tu na yale yanayohusika na Tanzania bara. Ni vyema Mheshimiwa Waziri kwa nia safi na kwa makini kabisa kuwaeleza Wazanzibar watanufaika au wananufaika vipi ndani ya Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Pamoja la Afrika Mashariki litasaidiaje katika kuuza elimu nchini na kusaidia katika dhana nzima ya Taifa ya Kilimo Kwanza. Ahsanteni sana.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kuanza kwa *Common Market*. Je, ni lini tutakuwa na *Monetary Union*?

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mheshimiwa Daktari Diodorus Buberwa Kamala, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kutoa pongezi kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Naibu Waziri, kwa bajeti yao nzuri ambayo imeainisha vyema kuboresha sekta zote za wizara hii bila kuwasahau watendaji wote

walioshiriki kuandaa hotuba hii. Niwaombee Mungu kaka yangu Mheshimiwa Bernard Membe na Naibu wake, wapiga kura wao wawape kura za kishindo ili warudi kuendeleza yale waliyoyaandaa, amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ninamwombea Mheshimiwa Daktari Kamala na Mheshimiwa Mohamed Aboud, wapate ushindi wa kishindo ili warudi tena Bungeni kuendeleza yale yote mazuri waliyoyaainisha kwenye hotuba hii nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa sana kusikia kauli ya Mheshimiwa Waziri wa Afrika ya Mashariki kuwa, suala la kumiliki ardhi litaendelea kuwa la Wananchi wa nchi husika. Hii iliwatia hofu sana Watanzania kwani ardhi ya nchi yetu ina mali nyingi sana; hivyo ni wazi kuwa nchi za wenzetu wanatamani hivyo wanataka kumiliki kijanja. Mungu aibariki Tanzania kwa uamuzi huu wa busara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza utaratibu wa nchi yetu kwa wageni kuja kuishi Tanzania, bali ninaomba sheria au utaratibu wa wageni kuamua kuishi Tanzania utazamwe upya kwani raia kutoka Nchi za Afrika Mashariki ni jirani zetu sana, hakuna haja ya kuwawekea sheria ngumu hasa suala la kufanya biashara, kuoau kuolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena kuunga mkono hoja hizi zote mbili kwa mikono miwili, nawatakia utekelezaji wenyetija kama walivyofanya kwa bajeti zote za miaka mitano.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara, kwa kuandaa bajeti nzuri na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, napenda kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 39 wa Kitabu cha Bajeti (Hotuba ya Waziri), amezungumzia hatua mbalimbali zilizofikiwa kuelekea Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, naunga mkono ushirikiano wa nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, napenda niweke bayana kwamba, siungi mkono Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki kwa sababu zifuatazo:-

- Bado mifumo ya kisiasa ya nchi hizi ni tofauti sana, kwa mfano, Nchi ya Uganda bado inatambua Uchifu na kuushirikisha katika mambo ya uongozi wa nchi.

- Nchini Uganda, Burundi, Rwanda na hata Kenya yenewe, bado hali ya usalama siyo ya kuridhisha hata kidogo.

- Bado Nchi ya Kenya ina mfumo wa siasa ambao unaweza kuuita wa kibabe na Uganda hali kadhalika.

- Mifumo ya umiliki ardhi ni tofauti sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo niliyoyaeleza hapo juu, naona si wakati muafaka wa kuendelea na jitihada za kuanzishwa kwa Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nchi zetu hizi zijifunze kutoka Umoja wa Ulaya (*European Union - EU*), ambao umeanzishwa miaka mingi sana lakini ajenda yao kubwa wakati wote imekuwa ni kuimarisha umoja wao kiuchumi zaidi kuliko umoja wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuendelee na jitihada za kuimarisha Jumuiya yetu kiuchumi kuliko Shirikisho la Kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa kuja na mpango wa elimu kwa umma. Suala hili la elimu kwa umma kwa Watanzania kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki, halikupewa umuhimu wa kutosha katika bajeti za huko nyuma. Siyo jambo la ajabu kuona kwamba, Wananchi wengi nchini (mijini na vijijini), hawajui kuwepo kwa Jumuiya hiyo pamoja na shughuli zake. Hivyo, ni matumaini yangu kwamba, hatua zote zinazochukuliwa na Wizara za kutoa elimu kwa umma kuhusu Jumuiya pamoja na shughuli zake, zitafanyika kama zilivyoainishwa katika Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Wizara, ukurasa wa 77.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Watanzania, napenda pia kujuu hatua ambayo ujenzi wa Ofisi kwa ajili ya Makao Makuu ulipofikia. Hili ni muhimu maana kukamilika kwa ujenzi wa Ofisi hizo, kutapunguza gharama za kukodisha majengo binafsi kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ardhi ni muhimu likabaki la nchi moja moja mionganoni mwa nchi zinazounda Jumuiya. Kama ambavyo Bunge hili limewahi kutahadharisha huko nyuma, tusifungue milango kwa nchi nyingine kuja kumiliki ardhi katika nchi yetu. Ni vizuri pia tujue kwamba, mifumo ya kumiliki ardhi mionganoni mwa wanachama ni tofauti sana. Kenya haina ardhi na mfumo wa umiliki ardhi ni wa kibepari; hivyo, Kenya ingeshabikia sana suala la ardhi liwe wazi kwa Wanajumuiya wote. Namshukuru Waziri kwa kulihakikishia Bunge kwamba, suala la ardhi litabaki kuwa la nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba ya Wizara na kuiwasilisha mbele ya Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati ya moyo wangu kabisa kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Benard Membe na Naibu wake Balozi Seifu Iddi kwa kuiwakilisha vizuri sana nchi yetu kwenye Jumuiya ya Kimataifa. Leo hii sura ya Tanzania na jina Tanzania si tu linajulikana duniani lakini pia jina hilo limetukuka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana kwa kazi hiyo. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwateua ninyi kuongoza Wizara hii muhimu sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa na sera nzuri ya mambo ya nje. Matokeo yake ni Watanzania wengi kuaminiwa na hivyo kuongoza taasisi mbalimbali Kimataifa, uteuzi wa hivi karibuni wa Balozi Dr. Maluga kuwa mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa nchini Somalia ni kielelezo cha sera nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Africa Peer Review Mechanism (APRM)*, napongeza nchi yetu kwa kujiunga na mpango huu. Mpango huu ambao naamini una malengo ya kujitathmini kiutawala bora na hivyo kuwa mionganoni mwa nchi, barani Afrika, ambazo zimenuia kuondoa kero za utawala na kuwa tayari kujikosoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utawala bora ni kigezo muhimu sana katika uendeshaji wa nchi zetu. Naamini kwamba nchi inayotambuliwa na Jumuiya ya Kimataifa kuongoza kwa kuzingatia utawala bora inapata si tu heshima kubwa lakini pia ni rahisi hata kuaminiwa kupewa mikopo na kufutiwa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri ili *APRM* Tanzania ifanye kazi nzuri basi fungu la pesa la kuendesha shughuli zake liimarishwe ili Baraza la Usimamizi la Taifa lifanye kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uraia wa nchi mbili (*Dual citizenship*), naunga mkono uraia wa nchi mbili. Naamini wapo Watanzania ambao walishachukua uraia wa nchi nyiningine, ambao kwa mujibu wa sheria zetu walishapoteza uraia wa Tanzania. Hivyo nashauri sheria yetu ya uraia irekebishwe ili Watanzania wenye uraia wa nchi nyiningine lakini bado wanataka kuwa na uraia wa nchi yao – Tanzania wasiruhusiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ni kubwa zaidi za kuwa na uraia wa nchi mbili kuliko hasara. Naamini wapo Watanzania waliofanikiwa sana kiuchumi huko nje lakini kwa sababu inawezekana walishapoteza uraia wa Tanzania wanaogopa kuwekeza Tanzania (nyumbani kwao). Lakini wakipewa uraia naamini kama ambavyo wao wanaamini mali zao zitakuwa salama zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gari la Tanzania kupigwa bomu huko Kigali, Rwanda. Hivi karibuni kulikuwa na habari za gari letu la Ubalozi wa Tanzania kupigwa bomu karibu na ofisi za Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba, kwa niaba ya Watanzania, Waziri atueleze tukio hili lina maana gani kwa Ubalozi wetu na Tanzania linaashiria nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia. Napenda kumpongeza sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyofanya kwa kipindi chote cha miaka mitano na pia kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini kumejitokeza wimbi kubwa la raia wa Kenya na nchi nyingine, kuuziwa ardhi bila kufuata sheria na taratibu za nchi yetu katika maeneo mengi ya Mkoa wa Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Je, kwa hali kama hiyo serikali inatoa tamko gani kwa Wananchi wanaowauzia raia wa nchi za nje kinyemela bila kufuata sheria za nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kulinda ajira za Wananchi wetu hasa katika eneo la wahudumu mbalimbali wa hoteli na watoa huduma za utalii, ambao wengi wao hawakupata mafunzo maalum ambayo hutoa mvuto kwa binadamu yeoyote kama ukarimu, unyenyekevu (*hospitality*). Je, serikali inasema nini juu ya kuandaa kozi fupi au semina zitakazowaelimisha Wahudumu wetu kuwa wakarimu na wanyenyekevu na waaminifu wakati wote wakiwa makazini kwao? Kwa kutofanya hivyo, kutasaidia vijana wetu kupata ajira na kushindana katika soko la ajira.

Mwisho, pongezi kubwa sana kwa Mawaziri wetu, Mungu atawarudisha wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. CASTOR R. LIGALLAMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na |Wakurugenzi wote kwa hotuba fasaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu uanzishwaji wa soko la pamoja Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zote tano za Afrika Mashariki, Tanzania ina fursa nyingi katika kulitawala soko hilo. Ni vizuri Wizara hii ikashirikiane kwa karibu na Wizara ya Kilimo, Viwanda, Biasha na Masoko katika kutumia nafasi hii kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara uzipishwe kwenye mikoa ambayo ina hali nzuri ya hewa. Miundombinu ya umwagiliaji itaongeza uzalishaji huu.

(ii) “*Rural Electrification*” iwe ni lazima kwa mikoa yenye uzalishaji mkubwa ili tuweze kuchocha “*agro-processing industries*” kule kule kwenye uzalishaji ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa. Katika hili Wizara inabidi ihushe na Wizara ya Nishati na Madini ili kuweka vipaumbele vya kusambaza umeme vijijini. Tusipofanya hivi, basi hatutauza bali tutanunua.

(iii) Pamoja na kwamba tumesema suala la ardhi litabaki kwa kila nchi husika, hiyo ni sawa kwa kauli, lakini Wizara inasemaje ikiwa mwanamke Mtanzania akiolewa na raia wa nchi mwanachama na lengo la ndoa hiyo ikawa ni kupata ardhi, Serikali inasemaje juu ya Mtanzania yule aliyeolewa juu ya kumiliki ardhi? Waziri atoe jibu katika hili.

(iv) Nchi kama Kenya ime-*exploit* siku nyingi masoko mbalimbali ya nje kama vile *AGOA*, Soko ambalo lina bidhaa nyingi za kuuza, lakini nchi yetu haikuchangamkia. Ili kukidhi uzalishaji mkubwa ili tu-*exploit* soko hili ni vyema:-

(a) Fedha za kilimo zisigawiwe kisiasa. Mfano, fedha za kilimo cha umwagiliaji kugawanywa mikoa yote bila kujali fursa zilizopo katika mikoa yenye uzalishaji mkubwa kwa bei nafuu.

(b) Miundombinu katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa iimarishwe ili mazao yafike sokoni yakiwa na hali nzuri.

(c) Mazao ambayo siyo *traditional crops*, yapewe kipaumbele hasa sasa ambapo tumeunda Bodi ya Mazao mchanganyiko. Mazao hayo ni kama cocoa, ufuta, mafuta ya alizeti, mawese, ndizi, mpunga, mahindi, viungo vya chakula na kadhalika.

MHE. MWINCHOUM A. MSOMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu kwa Watanzania juu ya mikataba na soko la pamoja ni muhimu sana na sio jambo la kuliepuka hata kidogo. Naiomba Serikali kupitia Wizara hii kulishughulikia kwa utashi mkubwa ili Watanzania waweze kuunga mkono juhudhi hizo za Serikali na kupata uelewa wa kutosha kwa maendeleo yao na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu kubwa ya Watanzania ni juu ya taratibu zitakazofuatwa katika maeneo ya ardhi, kwani baadhi ya nchi wanachama sera zao za ardhi haziwiani na sera zetu na vile vile nao pia wametuzidi kimapato na uzoefu wa matimizi ya ardhi. Tuweke bayana sera yetu ya ardhi kwa nchi wanachama ili kuepusha migongano au kutoa mwanya kwao kujipatia ardhi kiholela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya uongozi wa Rais wetu Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete hasa kwa juhudzi zake Mheshimiwa Kikwete za kuimarishe uhusiano Duniani na kuonyesha uongozi bora katika Diplomasia kuwa na usimamizi mzuri pia na Mheshimiwa Bernard Kamillius Membe, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa bila ya kumsahau Mheshimiwa Balozi Seif A. Idd, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia katika Wizara hii mambo makubwa yafuatayo:-

Kwanza, kama nilivyoleza awali nachukua fursa hii kutoa pongezi sana na nyingi kwa Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoendelea kuimarishe uhusiano baina ya nchi yetu na Mataifa mbalimbali duniani hasa Mataifa makubwa. Mataifa yamemkubali vyema na kung'ara katika viongozi na nchi za Afrika. Kung'ara kwake huko ni sambamba na kung'ara kwa Taifa letu la Tanzania. Tumuunge mkono kwa kudumisha nidhamu na kuongeza kiwango cha kuchapa kwa Watanzania wote katika nyanja za Kitaifa na Kimataifa. Ujasiri wake huo umepelekea kuteuliwa na viongozi mbalimbali wa Mataifa makubwa kwenye Kamati na Tume za Kimataifa hali ambayo inadhihirisha uwezo wake na kuaminika kwake na Tanzania kwa ujumla. Pongezi kwake.

Pili, uraia wa nchi mbili, ni muda mrefu sasa umeピtita tangu Serikali ilipoanza mchakato wa kuanzisha uraia wa aina hii kiasi kwamba Serikali inaonekana haiku makini katika kulishughulikia mpango huu. Tamko la mchakato wa kuwekwa utaratibu wa uraia wa nchi mbili umetamkwa Bungeni. Hivyo, naishauri Serikali kuongeza juhudzi ili hatimaye utekelezaji wake uanze.

Tatu, Chuo cha Diplomasia, naipongeza pia Wizara kwa kuchukua hatua ya kuipandisha hadhi *Diploma* inayotolewa na Chuo cha Diplomasia na kuifanya hivi sasa kutambulika rasmi katika taratibu zetu za mfumo wa elimu nchini hali ambayo itakifanya chuo hicho kuwa na hadhi zaidi na pia kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi Kitaifa na Kimataifa. Kwa kuwa chuo hiki kina hadhi Kimataifa naomba juhudzi za makusudi zichukuliwe kuwasaidia wanafunzi wanaomiliza masomo yao hapo chuoni, kupewa kipaumbele katika kuwapatia ajira Serikalini. Aidha, tufikirie kuanzisha kozi nyingine ya Digrii ya Uhusiano wa Kimataifa hapa chuoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili, ahsante.

MHE. MASOLWA C. MASOLWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sheria ya soko la pamoja kwa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki limeshaanza, ni vyema Watanzania tukaitumia fursa hii ipasavyo

badala ya kuendelea kulalamika. Serikali iendelee kuwaelimisha wananchi kwa nguvu zote ili waelewe ni kushiriki vizuri katika soko hili. Aidha, Serikali iwe inatoa tathimini ya mafanikio na changamoto za soko hili kila baada ya miezi sita kwa kuwa ndio tunaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa soko hili la pamoja limeainisha kwa upande wa wataalamu wanaohitajika. Ninaishauri Serikali kupitia Vyuo Vikuu hapa nchini kutoa elimu kwa wanafunzi wahitimu ili kuziomba nafasi hizo kwa nchi ambazo hazina wataalam hao. Hata hivyo, ni vyema nchi mwanachama zisiweke masharti magumu ya sifa za mtaalam anayehitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali pia kuwasaidia wataalam Watanzania watakaofanikiwa kupata kazi katika nchi mwanachama kuhusiana na usalama wao kupitia balozi zetu katika nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umiliki wa ardhi kwa watu wasiokuwa Watanzania ambao watakuja Tanzania kwa shughuli mbalimbali udhibitiwe na endapo mgeni huyo atabainika amemrubuni Mtanzania ardhi yetu afukuzwe mara moja nchini.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kabisa endapo Watanzania tutaitumia fursa hii ya soko la pamoja, watu wengi watanufaika ikiwa ni pamoja na Taifa letu kwa jumla kwa vile nchi yetu ina kila aina ya fursa. Serikali nayo kwa upande wake ni vyema ikaboresha miundombinu yote ili kuijeweka vizuri zaidi katika kukuza uchumi wetu kwa vile nchi takribani tatu za Jumuiya (Rwanda, Burudi na Uganda) zinategemea sana miundombinu yetu kwa kupitishia bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Lakini wakati tulionao sasa hautoshi kabisa kuwapa Waheshimiwa Mawaziri kuanza kuhitimisha hoja zao. Kwa hiyo, nitakalolifanya, nitasitisha shughuli za Bunge mpaka hapo jioni ili tutakapoingia sasa tutaanza na Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, ataanza kuhitimisha yeye halafu baada ya hapo tutaingia kwenye hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sina matangazo mahsus ambayo yanahitaji kutolewa, sasa nachukua nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni.

(Saa 6.47 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tulipoondoka mchana tulisema kwamba tutakaporudi tutaanza na Waheshimiwa Mawaziri kuhitimisha hoja zao. Tutaanza na Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili aanze kuhitimisha hoja yake, na kwa kuwa Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki hayupo Waziri, itabidi utumie nusu saa yako tu kuhitimisha hoja halafu tutaingia katika mafungu. Karibu sana.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa jinsi walivyochangia hoja yetu tulioifikisha mbele yenu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu makadirio na matumizi kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Masilingi - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, kwa jinsi ambavyo ameongoza Kamati yake wakati wote na jinsi ambavyo Kamati yake imetuelekeza na kutushauri ili kuhakikisha Tanzania inanufaika na ushiriki wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue waliochangia. Tumepata wachangiaji 10 kwa kuzungumza na wachangiaji 18 kwa kuandika. Waliochangia kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:-

Kwanza ni Mheshimiwa Killimbah - kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Fatma A. Fereji - kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed - Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, na Mheshimiwa Pindi Chana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Waheshimiwa waliochangia kwa kuandika, naomba na wao niwatambue. Kwanza ni Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Mwadini A. Jecha, Mheshimiwa Pindi H. Chana. (*Makofii*)

Wengine ni Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Janeth M. Massaburi, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Mkiwa A. Kimwanga, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti na Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wote walikuwa na hoja nzuri za kusaidia Wizara kuboresha utendaji wake wa kila siku, lakini vile vile wapo waliopenda kupata ufanuzi mbalimbali. Kwa kuzingatia muda mfupi, siwezi kuyajibu yote, naahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tutajitahidi kadri itakavyowezekana kabla ya kuahirisha kikao hiki cha Bunge ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupata majibu ya hoja zao kwa

maandishi. Kwa hiyo, nitajitahidi kupitia baadhi ya hoja muda ukiisha nitaomba radhi wale ambao sitawafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza kama nilivyo sema, wa kwanza alikuwa Mheshimiwa Killimbah aliyewakilisha maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Ametoa ushauri kama ambavyo wamekuwa wakitoa siku zote, wameshauri kwamba ni vizuri elimu ikaendelea kutolewa ili Watanzania waweze kuelewa fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naomba niseme kwamba suala la uelewa kuhusu masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tunalitazama kwa sura mbili. Sura ya kwanza ni sura ya ngazi ya Jumuiya. Ngazi ya Jumuiya, Baraza la Jumuiya ya Afrika Mashariki limeshaielekeza *Secretariat* ili kuandaa mpango wa kutoa elimu kwa umma ikiwa ni pamoja na kuandaa sera ya mawasiliano itakayokuwa inatusaidia kufikisha ujumbe kwa wahusika kwa haraka inavyowezekana. Kwa hiyo, ni katika ngazi ya jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ngazi ya Wizara kama Serikali, tumefanya mambo mawili yatakayotusa idia kutoa elimu kwa umma, jambo la kwanza tumeandaa mpango kama nilivyo eleza kwenye hotuba yangu, mpango wa kutoa elimu kwa umma ambao niliuzindua na tumeshaanza kuutekeleza kama nilivyo eleza.

Tulikuwa na mikutano na Wakurugenzi kuangalia jinsi tutakavyoweza kutekeleza hii elimu mpaka ngazi ya Serikali ya Vijiji. Tulifanya Semina pamoja na Makatibu Wakuu pamoja na Wakuu wa Mikoa na Maafisa Tawala. Yote haya tunayafanya kwa lengo la kuangalia ni kwa namna gani tunaweza kufikisha elimu kwa Watanzania wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo mbalimbali ambayo tumekuwa tukiyafanya na tutaendela kuyafanya kama vile kutembelea maeneo mbalimbali, kushiriki katika vipindi vyta televisheni na redio, kutoa matangazo kwenye magazeti na mambo mengine.

Tutaendelea kufanya hivyo, changamoto kubwa ni kupata *resources* za kutosha ili kufanya kazi hizo, lakini tutaendelea kuangalia ni kwa jinsi gani tunaweza tukawashirikisha na wadau wetu wengine, marafiki wetu katika masuala ya Afrika Mashariki tuone na wao wanaweza wakatusaidia namna gani kuweza kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma. Naomba nitambue ushauri huo wa Kamati na niahidi kwamba tutajitahidi kuufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile Kamati ilibainisha kwamba ni vizuri Serikali ikaweka mazingira mazuri ya kuwezesha Tanzania kunufaika na soko la Afrika Mashariki. Kama nilivyo sema kwenye hotuba yangu, tunakamilisha mkakati wa utekelezaji wa soko la pamoja. Mkakati huo ukiwa tayari, utatusaidia sana kujipanga vizuri kama nchi kuweza kunufaika na soko la pamoja la Afrika Mashariki.

Hatua hii tulivoichukua ya kuwa na mkakati wa utekelezaji wa soko la pamoja ni nzuri kwa sababu wakati tunatekeleza Umoja wa Forodha hatukuweka mkakati wa utekelezaji wa Umoja wa Forodha na ndiyo maana ilipofika kwenye kufanya tathmini

kila mtu alikuwa anajaribu kufanya anavyoona inafaa kufanya tathmini hiyo. Kwa hiyo, katika huu mkakati wa utekelezaji wa soko la pamoja tutaweka utaratibu wa jinsi ya kufuutilia kuona kila siku nini kinaendelea, na tutaweka na vigezo ambavyo mwisho wa siku tutavitumia kupima kama tunafanikiwa au hatufanikiwi katika utekelezaji wa soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za *EAC* ni vizuri zikajifunza kutoka nchi za Ulaya, tunashukuru kwa ushauri huo na tutaendelea kuufuutilia, na tulikuwa tukiutumia katika baadhi ya mambo.

Lakini suala la ardhi liwe la nchi husika kama ambavyo tumebainisha. Bunge hili Tukufu tulipokuja hapa kutoa semina wakati wa mazungumzo wa Soko la Pamoja, mlitushauri kwamba suala la ardhi lisiwe sehemu ya Itifaki ya Soko la Pamoja, lakini vile vili niseme tu hata tulipokutana na Kamati wakati wote Kamati ilitushauri tulizingatia suala hilo, tulilizingatia na suala la ardhi sasa litasimamiwa na sheria za nchi wanachama.

Ukienda Rwanda unataka ardhi, angalia sheria za Rwanda zinasemaje; ukienda Uganda angalia sheria za Uganda zinasemaje; ukienda Kenya angalia sheria za Kenya zinasemaje na ukija Tanzania, basi ujue kwamba Tanzania tunasema kwamba mgeni hatamiliki ardhi, ukifanya ujanja ujanja ukapata ardhi ujue siku za mwizi huwa mara nyingi zinahesabiwa. Pale tutakapochukua hatua na kusitisha na kutwaa ardhi hiyo uliyoichukua bila kufuata utaratibu na sheria za Tanzania, usianze kulalamika kwamba Tanzania haizingatia masuala ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati ni kwamba ingekuwa vizuri *DRC* na yenyeji ijiunge na Afrika Mashariki. Wizara inakubaliana na ushauri wa Kamati lakini na Mheshimiwa Zitto vile vili wakati anachangia amelizungumza hili. Ningependa kusema kwamba hivi karibuni Wizara yangu tuliandaa ziara ya kutembelea nchi zinazotumia Bandari ya Dar es Salaam kwa nia ya kueleza hatua ambazo tumezichukua kuboresha Bandari ya Dar es Salaam, lakini vile vili kusikiliza kero zao na kuona ni mambo yapi tunaweza kuyafanya ili kuzidi kuboresha huduma za Dar es Salaam; tulianzia Uganda, tukaenda Rwanda, Burundi, tukaenda *DRC* upande wa Mashariki tukaenda Malawi, tukaenda na Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kote huko walikuwa hawajui hatua tulizozichukua ili kuboresha bandari ya Dar es Salaam tukawaeleza, lakini na wao walikuwa na yao wakatueleza. Tuliporudi, tumeunda Kamati inayoshughulikia masuala ya *Non Tariff Barriers* na tumewaomba wahusika wachukue hatua kurekebisha mambo ambayo wenzetu wanayaona sio mazuri na yanayoweza kuwafanya wasitumie Bandari ya Dar es Salaam. Labda niseme kwamba inabidi tuone Bandari ya Dar es Salaam kama bidhaa.

Mimi naona Bandari ya Dar es Salaam kama bidhaa kuliko hata madini, ni bidhaa ambayo kila mtu anayehusika katika sakata hii, wale wanaosimama barabarani, wale watu waliopo kwenye mizani, wale watu wa *TRA*, watu wa Bandari wenyeji, Polisi, na wadau wote ni lazima wanaposhughulikia hawa watu wanaopitisha mizigo katika bandari ya Dar es Salaam washughulikie kama ambavyo mteja unakwenda benki kutafuta fedha zako, jinsi unavyopokelewa na kupewa kiti kizuri na kuhudumiwa kwa haraka.

Msimamo huo unatakiwa hawa wadau wote wanaoshughulikia masuala ya Bandari ya Dar es Salaam na wengine wote ni lazima wawe nao kwa sababu bandari ni bidhaa kubwa inayoliingizia Taifa fedha nyingi na lazima tuendelee kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile napenda niseme kwamba Mheshimiwa Fatma Fereji kwa niaba ya Kambi ya Upinzani na yeye ametoa ushauri kwamba, haikuwa sahihi kwa nchi za Rwanda na Burundi kujiunga kwa haraka na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Labda niseme tu utaratibu tunaotumia. Utaratibu tunaotumia ni kwamba ukitaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki unaleta maombi yako, ukishaleta maombi yako, tunakupa vigezo.

Kwa mfano, wenzetu wa Rwanda na Burundi tuliwaambia kwamba mnataka kujiunga Jumuiya ya Afrika Mashariki, mojawapo ya jambo la msingi ndani ya mkatuba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki ni kwamba lazima mzingatie utawala bora pamoja na demokrasia. Tukawauliza, mnalikubali hilo? Wakasema tunalikubali. Tukawaambia kwamba unajua hii Afrika Mashariki tunatumia Kiingereza na Kiswahili? Mnalikubali hilo? Wakasema tunalikubali. Tukawaambia unajua hapa sisi tunaheshimu suala la kufanya maamuzi kwa kuheshimu utaifa wa kila nchi, lakini vile vile na kwa kuaminiana mambo mengine? Kwa hiyo, vigezo vyote hivyo tuliwapitisha kwenye mtihani, tukafanya mahojiano na wakasema wanakubali, ndiyo maana wakaruhusija kuwa wanahama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuchukua nafasi hii kusema *European Union* ya sasa ambayo watu wengi huwa wanaitolea kama mfano. Kuanza kwake kulitokana na ile vita iliyokuwepo baada ya vita ya pili ya dunia. Kulikuwa na hawa watu wanaoamini kwenye masuala ya magharibi na mashariki, lakini kuna nchi zilizokuwa zikimiliki *atomic* na nchi zilizokuwa zikimiliki chuma, sasa ikaonekana ukimwachia mtu anayemiliki *atomic* usipokaa karibu naye na ukamdhiliti anatumiae *atomic*, siku moja unaweza ukakuta amekuvamia. Ikaanzishwa ushirikiano wa nchi zinazotumia *atomic* pamoja na zenye chuma kwa nia ya kudhibitiana mwaka 1953. Ilipofika mwaka 1957 ushirikiano ulipoanza kwa sababu ya kutoaminiana kwa sababu ya kuogopana, kwa sababu ya vita iliyokuwa imeenea Ulaya ndiyo umezaa *European Union* ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hata kama kungekuwa kuna matatizo ya hapa na pale kwenye hizi nchi, sio sababu ya kutoshirikiana, ni sababu ya kushirikiana kwa sababu mnapokuwa karibu zaidi mnawenza mkafanya kwa pamoja. Yale mazuri unayoyafanya wewe mwenzako atajifunza kwako, lakini mazuri anayoyafanya yeye utajifunza kwake, na mabaya unayoyafanya wewe utaacha na mabaya anayofanya yeye utamwambia mwenzako yaache haya hayatatusaidia kutupeleka mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni lazima tujue kwamba hatukuchagua wala hakumwomba Mwenyezi Mungu kukaa karibu na Burundi, hatukuchagua wala hatukumwomba Mwenyezi Mungu kukaa karibu na Rwanda, matatizo yanapotokea kule, Tanzania ndiyo inabeba mzigo wa Wakimbizi. Kwa hiyo, ni jambo zuri nchi zinapokuwa na matatizo, ninyi ndiyo mnayabeba, sio vibaya kushirikiana nao kwa karibu ili kuangalia

ni jinsi gani mnaweza mkazuia matatizo hayo yasitokee kwa manufaa yenu na kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Upinzani ulishauri kwamba kuna vikwazo visivyo vya kikodi, *Non Tarrif Barriers*, ni kweli tunakubali. Tulichokifanya kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, tumeweka Kamati kila nchi ya kuzuia vikwazo visivyo vya kikodi, lakini vile vile kila nchi kuna Kamati zinazoshughulikia Kamati zinazoshughulikia vikwazo hivyo. Wizara yangu ina Kamati inayoshughulikia na kuratibu masuala hayo. Wito ninaoutoa kwa Watanzania pale unapokumbana na vikwazo popote pale utujulishe ili tuweze kuwasiliana na wenzetu kwa haraka na kuchukua hatua hizo. Hivi sasa kwenye mtandao wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki fomu zipo, unawenza ukazitumia kuwasilisha taarifa na ukituletea taarifa tutaipata na kuifanyia kazi haraka. Wapo watu wengi ambao wametumia fursa hiyo na tumezifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Waziri kutoa elimu Uingereza lakini hapa Tanzania hajatoa elimu; ni kweli nilikuwa Uingereza hivi karibuni na ni kweli vile vile kwamba mbali na hiyo elimu nilioitoa kule kwa Watanzania wenzetu, lakini vile vile mtakumbuka kwamba wakati tupo kwenye mchakato wa kukusanya maoni ya Watanzania kwamba Tanzania twende haraka kwenye shirikisho ama tuende taratibu, nikiwa kama Naibu Waziri nilizunguka nchi nzima. Nilikwenda kila Mkoa na nilijitahidi kufika hata baadhi ya Wilaya, nikitoa elimu ya Afrika Mashariki. Ni kwa bahati mbaya labda hilo hawakuliona au wamesahau kwa sababu muda umepita mwangi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ni kweli nimekuwa nikifanya ziara mbalimbali ndani ya nchi na ninakumbuka kipindi kilichopita Kambi ya Upinzani maoni yao kwenye bajeti yetu walisema mbona Wizara hii inatembea sana kwenye nchi? Sasa leo hii hoja inasema mbona haujatoa elimu ya Afrika Mashariki sana kwenye nchi? Kwa hiyo, ukiunganisha hoja ya mwaka jana ya Kambi ya Upinzani ya kwamba mbona umezunguka sana hapa ndani ya nchi na inajibiwa na hoja iliyotolewa leo kwamba mbona umetoa na Elimu Ulaya? (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue nafasi hii vile vile kusema kwa ufupi kwamba ilikuwepo hoja kwamba Zanzibar inanufaika vipi, katika hotuba nimeeleza namna ambavyo Zanzibar inanufaika, lakini nirudie tu kwa haraka haraka kwamba kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki tutafanya upembuzi yakinifu wa mradi wa *The Wind Power Plants* wa Zanzibar. Lakini kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki kuna mradi wa usalama wa chakula kule Zanzibar ambao utafadhiliwa na fedha za *European Union* kwa utaratibu wa *European Development Fund (EDF)* lakini vile vile kama nilivyosema, tumetoa *Land Rover* moja kule Zanzibar kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa mafua ya ndege, tulipata moja kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini tukaona ni vizuri basi tuanze na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna huu mradi wa *East Africa and Roll off and Roll on* ambao utasaidia kuunganisha Pemba pamoja na maeneo mengine, Tanzania Bara pamoja na Mombasa, kwa sababu *roll off roll on* inaweza kubeba watu wengi kwa muda mfupi. Kama nilivyosema kuhusu maruhubi, *port and deep sea fishing*, ni kwamba sasa

ule mradi baada ya kuwasilisha *Africa Development Bank*, wakatushauri kwamba tuweke kwenye mipango ya Tanzania tunayoiwasilisha kule na tuupe kipaumbele, tutafanya hivyo kwa kutoa kipaumbele kwa mradi ule. Vile vile nilisema kuna jengo la *Airport* ya Zanzibar jengo la abiria ambalo mradi wa pamoja utagharimu zaidi ya dola milioni 70.4 ambazo ni fedha nyingi tu, tunatarajia hilo jengo litakuwa zuri. Miradi imefikia hatua hiyo na hii haitoshi. Kadri siku zinavyokwenda tutazidi kushaurina na kuongeza miradi mingine zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kutoka Kambi ya Upinzani kwamba Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni wa zamani na kwamba ni vizuri urekebishwe. Hivi sasa tupo kwenye mchakato wa kufanya mabadiliko mbalimbali katika mkataba huo.

Nimwombe mwakilishi wa Kambi ya Upinzani kama kuna jambo lolote ambalo mnaona kwamba ni lazima lifanyiwe marekebisho kwa maslahi ya Tanzania na maslahi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, nitafurahi sana kulipokea ili na lenyewe liwe sehemu ya mchakato wa pamoja wa mabadiliko tunayotarajia kuyafanya kwenye mkataba unaoendesha Jumuiya ya Afrika Mashariki kulingana na kifungu 150. Kwa sababu mabadiliko yanaweza yakafanyika kwenye mkataba kwa njia mbili, moja kwa nchi mwanachama kuwasilisha kwamba naomba tufanye mabadiliko haya au kuanzishwa na Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukimbilia shirikisho la kisiasa, katika hili naweza nikasema Tanzania ndiyo mara nyingi imekuwa ikiongoza hili kwamba twende namna gani kwenye shirikisho. Wenzetu waliotuzunguka walikuwa na mawazo kwamba hawaendi haraka, lakini tulipokusanya maoni Watanzania wakasema twende taratibu na hoja hiyo, mwisho wa siku ndiyo maamuzi ya wakuu wa nchi kwamba hebu sasa twende hatua kwa hatua.

Tufanye kila jambo kulingana na inavyoelekezwa kwenye mkataba na tufanye na mambo mengine yatakayotusaidia, siku moja tukifika huko, basi tufike huko kila mtu akiwa ameridhika akiwa hana sababu ya kujutia kwa nini amefika huko. Ndio maana wakuu wa nchi walipokutana kuhusu hoja ya twende namna gani kwenye shirikisho, waliagiza kwamba zile kero zote ambazo zilibainishwa wakati wa kukusanya maoni, hebu tuchague Kamati ya Wataalam watatu watatu kutoka kila nchi waweze kupitia himo changamoto na waje na ushauri kwamba mambo yapi tuyafanye kwa ajili ya kupiga hatua.

Nashukuru Mheshimiwa Basil Mramba kwa pongezi alizozitoa na akasema kwamba jamani sasa ni vizuri mkaiangalia Kilimanjaro kwa karibu. Nakubaliana naye kwamba lazima tujitajihidi kuiangalia Mikoa yote ambayo inapakana na nchi jirani, lazima tuiangalie kwa karibu.

Yote aliyojasema nimeyasikia na ametupongeza kwa upande wa barabara na nimwambie tu Serikali ya Kenya imetenga fedha kwa ajili ya bajeti ya mwaka huu kwa

ajili ya kujenga barabara ya lami Taveti Advoi ambayo itasaidia zaidi kuunganisha pale Holili. Niseme tu na mambo mengine tutaendelea kuyafanya ya kuimarisha ushirikiano.

Suala la mradi wa maji amelieleza hapa, tutalifuatilia tuone nini tunaweza tukafanya. Ametoa ushauri kuhusu *EPA* kwamba mambo yote tufanye, lakini yawe *WTO compatible*, nakubaliana na ushauri wake. Lakini tahadhari ninayoitoa hapa ni kwamba mawazo sasa tuweze kusaini mwezi wa Novemba lakini ikumbukwe kwamba *WTO* yenye *negotiations* bado hazijakamilika, kwa hiyo, bado zinaendelea. Kwa hiyo, kama tukiuchukua ushauri huu wa Mheshimiwa Mramba, maana tukitaka kutekeleza kwa asilimia 100 maana yake ni kwamba tuisaini *EPA* mpaka *WTO negotiations* ziwe zimekamilika. Sasa nisingependa kulizungumzia sana hili, lakini jambo la msingi ni kwamba mazungumzo yale lazima yawe *WTO compatible* kama ambavyo amesema.

Halafu Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji alitaka nitoe maelezo kwamba kwa nini tunasema utaifa wa Afrika wa Mashariki ndiyo uwe wa kwanza? Mimi sijasema hilo lilisemwa na Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, ulikuwa ni ushauri. Kwa hiyo, nisingependa kumjibia na sitaki kumuwekea maneno mdomoni kwamba alikuwa anamaanisha hiki, kwa sababu mimi mwenyewe najua kwanza hakuna utaifa wa Afrika Mashariki, hatujafika huko.

Lakini niseme tu, nadhani alichokuwa anasisitiza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ni kwamba wakati wote tuangalie kwamba Afrika Mashariki tunayojenga iweze kuwa imara. Lakini sidhani kama alitarajia kusema kwamba maslahi ya Taifa yasiwekwe mbele. Kwa sababu siku zote katika mambo ya ushirikiano maslahi ya Taifa kwanza mengine yanafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumza kidogo kwamba suala la wafanyakazi tulipoanza tulikuwa na wafanyakazi wachache sana na walikuwa nafasi za chini. Lakini hivi sasa tumejitahidi, tunaye Naibu Waziri anatoka Zanzibar. Lakini vile vile tuna Naibu Wakurugenzi wawili ambao wanatoka Zanzibar, tuna Afisa Habari Mkuu, tuna mchumi, tutaendelea kuongeza watalaam mbalimbali kutoka Zanzibar kadri zitakavyokuwa zikijitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu elimu, kuhusu soko la pamoja na hasa katika vijiji ni kwamba kama nilivyosema kwenye maelezo ya kwanza kwamba tuna mpango wa kufika mpaka ngazi ya vijiji. Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, nashukuru kwa pongezi ulizotupa na akasema kwamba Tanzania ina heshima kubwa nje ya nchi.

Ni kweli siyo nje ya nchi, hata Afrika Mashariki ndiyo maana Bunge lililokaa kule Rwanda hivi karibuni Bunge la Afrika lilipitisha azimio la kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete la kuapongeza Watanzania kwa kitu kizuri tulichokifanya cha kutoa uraia kwa watu 150 waliokuwa na uraia wa Burundi. Kwa hiyo, Bunge la Afrika Mashariki lilitoa azimio kuipongeza Tanzania na kumpongeza Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Katika azimio hilo walisema Tanzania imefanya jambo ambalo na nchi nyingine zinatakiwa kuiga. Lakini vile vile hivi karibuni tukiwa kule Nairobi kwenye Bunge la kupitisha bajeti Bunge la Afrika Mashariki vile vile likatoa hoja ya kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa hotuba nzuri aliyoitoa kwenye Bunge lile ambayo sasa hotuba hiyo ndiyo Wabunge wa Afrika Mashariki wameishika na wamesema wanaitumia kama mwongozo wa Afrika Mashariki. Kwa maneno mengine tunatoa uongozi hata ndani ya Afrika Mashariki.

Lakini vile vile Tanzania siyo kwamba tunafanya tu Afrika Mashariki, Waheshimiwa Marais wa *SADC*, *COMESA* na *EAC* walipokutana kule Kampala wakizungumzia umuhimu wa kuanzisha ukanda huru wa kibiashara lengo walitaka kuanzisha ukanda huru wa kibiashara, lakini Mheshimiwa Rais wetu akawaambia tusiishie kuanzisha ukanda huru wa kibiashara, hebu tupige hatua zaidi tuanzishe umoja wa forodha. Wakuu wote wa nchi kutoka *SADC*, *COMESA* na *EAC* walikubaliana na Mheshimiwa Rais wetu kwa asilimia 100. Kwa hiyo, tunatoa uongozi, tunatoa njia siyo tu Afrika Mashariki *hata SADC, COMESA na EAC*, Afrika hata nchi ya Afrika.

Nakushukuru Mheshimiwa Kabwe Zitto kwa hoja zako ulizozitoa, nimeshazizingumzia. Lakini wewe kama mchumi mwenzangu uliuliza, ukasema mbona mwaka 2009 bidhaa zimepungua. Inaonekana hatukuza zaidi kama tulivyouza mwaka uliotangulia. Kuna sababu mbalimbali, lakini sababu hasa kwa mfano mwaka 2009 tulipitisha uamuzi kwamba mazao ya nafaka za kilimo yasiende nje ya nchi.

Tulipopitisha uamuzi huo, kilichotokea mauzo ya nafasi yakapungua kutoka dola milioni 43.4 mpaka dola milioni 5.7. Kwa hiyo, sababu ya kupungua kule ni uamuzi tuliofanya sisi wa kuzuia kuuza mazao ya nafaka nje. Lakini sasa mwingine unawenza ukasema siyo uamuzi sahihi au ni sahihi, lakini kumbuka kunapokuwa kuna upungufu wa chakula kwenye nchi lazima mchukue hatua.

Tatizo lingine lililojitekeza ni kwamba chumvi. Chumvi mwaka uliotangulia tuliiza yenyе thamani ya dola milioni 77 lakini imeshuka kwa mwaka 2009 mpaka ikafika dola milioni 14.4 kutoka dola milioni 77 mpaka dola milioni 11.4. Sasa nilikuuliza watalaam wangu nikasema, sababu ni nini hapa? Wakanipa sababu ambayo siiamini, lakini niiseme ila nimepewa na watalaam wangu. Kwa hiyo, mkikuta siyo sahihi msiseme Mheshimiwa Mbunge kadanganya sasa. Watalaam wangu walichonishauri ni kwamba hii imepungua kwa sababu kwanza kulikuwa na tatizo la tabia nchi. Sasa inapokuwa kuna mabadiliko ya hewa kama wakati wote, sasa hakuna juu, kwa hiyo na utaratibu tunaotumia kutengeneza chumvi hatutatengeneza. Sasa sijui ni kweli au sio kweli. Lakini huenda ikawa kweli au isiwe kweli. Lakini hoja ni kwamba chumvi ilipungua.

Eneo lingine ni chuma. Chuma mwaka 2009 tuliiza bidhaa zinazotokana na chumvi dola milioni 34.5 ikapungua mpaka dola milioni 5.7. Sababu iko wazi, ni kwa sababu ya kuyumba kwa uchumi wa dunia. Uchumi wa dunia unapoyumba kitu cha kwanza kinachokuwa *affected ni contraction. Contraction* inavyoshuka ni dhahiri kama ulikuwa unaauza bidhaa za nondo lazima zitapungua.

Lakini kuna jambo moja naomba nilisema hapa tatizo lingine ambalo huenda lipo. Tuna tatizo la takwimu. Ukisoma ile *economic survey* ambayo ndio *official*, takwimu ambayo lazima tutumie inasema tumeuza dola milioni 262 *point something*.

Lakini watalaam waliobobea kwenye masuala ya uchumi tuliowapa kazi ya kutathimini mafanikio ya *customers union* wao ripoti waliyotupa wanatuambia Tanzania imeuza nje vitu vyenye thamani ya dola 627. Sasa mimi nilikuwa nimefikiria kwamba kwenye hotuba yangu niweke hilo, lakini watalaam wangu wakanishauri wakasema Mheshimiwa huwezi ukatoa takwimu ambazohaziendani na *official* takwimu za *economic national bureau of statistics*.

Sasa ambacho nimekiagiza, nimeagiza Katibu Mkuu pamoja na wasaidizi wake wawasiliane na wataalam wa takwimu na watalaam wa *BoT* ili waweze kushauri vizuri tuwe na takwimu nzuri zinazohusiana na masuala ya Afrika Mashariki. Haitakuwa jambo la busara, kwamba mtu anafanya utafiti anakuletea, unamwuliza *data* umetoa wapi? Anasema nimetoa *TRA*. Ukimwuliza hawa *National Bureau of Statistics* umetoa wapi takwimu? Anakuambia *TRA*. Ukimwuliza Benki Kuu umetoa wapi takwimu? Anakwambia *TRIA*. Lakini ukija kuangalia kila mtu ana takwimu zake. Kwa hiyo, lazima nikiri eneo hili lazima tulifanyie utafiti wa kina ili tuweze kujiridhisha.

Lakini lingine ambalo nilisema hapa pamoja na kwamba tunaona kwamba kwenye nafasi zilishuka, sio lazima kwamba ziwe zimeshuka kwa sababu ni kweli tulizua mahindi yasiende nje, lakini ni kweli kwamba watu walifanya magendo makubwa kwa kuuza mahindi nje. Kwa kuwa mtu unakuwa umemzuia, hawezu kuja akasema hiki ndiyo napeleka kwa sababu anajua akisema hivyo atakamatwa. Sasa haya ni mambo ambayo lazima tuyangalie. Naona na kengele imepigwa. Bado dakika sita.

Sasa niseme hivi, hoja zote zilizotolewa nitazifanyia kazi. Isipokuwa nimalizie kwa hoja moja ya jumla. Ni kwamba je, hii Afrika Mashariki soko la pamoja limeanza, tutaweza? Mimi nawaambia soko la pamoja limeanza na tutaweza kwa sababu, kwanza ukiziangalia nchi za Afrika Mashariki zote, ukiangalia eneo linalofaa kwa kilimo *arable land*, Tanzania tuna hekta 44 milioni, Kenya wana hekta milioni 10, Uganda wana hekta milioni saba, Rwanda wana hekta milioni mbili na Burundi wana hekta milioni moja.

Kwa maneno mengine, ukijipanga vizuri na tukitekeleza vizuri, Kilimo Kwanza ni dhahiri Tanzania tutanufaika na soko la chakula la Afrika. Hii watake wasitake hawana namna, ni kwamba Tanzania tutakuwa ghala la chakula la Afrika Mashariki.

Kwa bahati nzuri ukiangalia umoja wa forodha unasema mpunga kutoka nje ya Afrika Mashariki unatozwa kodi asilimia 75, mahindi kutoka nje ya Afrika Mashariki yanatozwa kodi asilimia 55. Tafsiri yake ni kwamba tunawalinda wakulima wa Afrika Mashariki. Lakini kumbe wakulima wa Afrika Mashariki mwenye ardhi ni Tanzania. Kwa hiyo, tunailinda Tanzania kwa kutumia Afrika Mashariki. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, kwenye uchumi na idadi ya watu ni jambo la msingi. Najua wachumi wengine huwa wanazungumzia suala la kupunguza idadi ya watu. Lakini mimi siamini katika hilo kwa sababu China inatamba katika dunia hii kwa sababu ya uwingi watu walionao. Mtu anapotaka kuweka kiwanda cha *CocaCola* akikiweka China kitakuwa cha manufaa zaidi. Ndiyo maana China pamoja na ukomonisti wake na mengine bado Marekani, bado Waingereza na wengine wanakwenda kule kuwekeza. Hii ni kwa sababu tu ya idadi ya watu.

Lakini vile vile sasa katika eneo hilo Afrika Mashariki Tanzania tuna *cooperative advantage*. Eneo lingine linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji Tanzania tuna hekta milioni 29 wenzetu Kenya wana milioni tatu, Uganda wana heka mbili, Rwanda wana hekta moja, Burundi wana ziro. Kwa hiyo, hata kama tukisema sasa tunamwagilia mwenye uwezo wa kumwagilia Afrika Mashariki na kulisha Afrika Mashariki ni Tanzania. (*Makofi*)

Lakini vile vile tukisema, sasa hebu tuangalie ni nchi ipi ina amani ambayo inafaa unapotafuta wawekezaji, basi itangazwe ikiwa ya kwanza? Kuna *peace index* ambayo haikutolewa na Tanzania wala mwana Afrika Mashariki inaeleza kwenye Afrika Mashariki, nchi ya kwanza yenye amani kuliko yoyote ile ni Tanzania, inafuatiwa na Rwanda, inakuja Uganda, inafuata Kenya, inamalizia Burundi. Kigezo hiki ni muhimu sana katika kuvutia wawekezaji na chenyewe kinatupa *comparative advantage*. (*Makofi*)

Ukija kwenye suala la *master power plan energy* ambayo tuna *master plan energy* ya *East Africa*, unakuta kwamba vyanzo vingi vya *energy* viko Tanzania. Hata ile miradi zamani ambayo ilikuwa ukipeleka Benki ya Dunia wanakwambia hiyo ni *not economically viable* kwamba *Stigler's Gorge* zamani tulipojaribu wali-calculate *IRR in turn rate of return* wakasema hii ndogo. Walipo-calculate increment in terms of return wakasema hii ndogo *pay back period* ni kubwa, wakasema mradi huu hatuwezi kuufadhili kwa sababu ni kidogo. Kwa sababu tutakuwa na umeme mwingi tusiokuwa na kazi nao.

Lakini kwa sasa tunapozungumza, umeme wa Afrika Mashariki ambao sasa tutaunganisha nchi zote kwenye *grid*, mradi huu ukiupeleka popote pale unauzu kama wa Afrika Mashariki, utapata fedha na utaweza kuuzia Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Tukienda kwenye *gas* huko, nisingependa kusema sana kwa sababu wakati uchunguzi bado unaendelea wa gesi, tuna gesi *cubic feet* bilioni 726 ambazo tukiziweza kupata zote tutakuwa na za kutosha kuzalisha hata *product* zinazotokana na gesi na mambo mengine. Kwa sababu hizo chache, nisingependa kuendelea kutangaza nyingine kwa sababu huenda wengine wasiziamini.

Kwa mfano ukiangalia Afrika Mashariki, rushwa inakwendaje kwenye Afrika Mashariki, inaonekana kwamba Rwanda rushwa iko chini zaidi, lakini nchi nyingine inayofuata kwa rushwa kuwa chini zaidi ni Tanzania, inayofuata nyingine ni Uganda, nyingine ni Burundi. Ya mwisho kabisa kwamba sasa kule rushwa inaonekana iko juu zaidi kuliko nchi yoyote ya Afrika Mashariki ni Kenya.

Sasa mambo haya lazima tuwe tunayaangalia na kuyatumia kuinadi Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Yote haya niliyoyasema ndio maana ukiangalia *GDP* inavyokua, kwa mwaka jana tu Tanzania *GDP* imekua kwa asilimia saba na inayofuata kwa *GDP* ni Uganda asilimia 6.4, inayofuata ni Rwanda asilimia sita, inayofuata kwa *GDP* kwa taratibu ni Kenya. Sasa ukiwa una mtu ambaye *GDP* yake inakuwa mara mbili zaidi yake, huna tatizo la kujua kwamba wewe ndiyo kigogo katika eneo hilo.

Lakini vile vile hata tukiangalia *GDP* ikoje Afrika Mashariki utakuta kwamba Kenya ni kweli *GDP* yao ni 30.5 milioni dola inayofuata ni Tanzania 22.4 dola, inayofuata kwa mbali sana ni Uganda 15, inayofuata kwa mbali zaidi 0.5 inayofuata kwa sababu ilikuwa lazima ifuate hakuna nyingine ni Burundi. Unapokuwa na mazingira kama haya huna sababu Tanzania kuwa mtu wa kwanza kuwa mwoga badala ya kuwa wa kwanza kuwa mstari wa mbele kwamba unaweza ukafanya kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimalizie na la sarafu moja. Niseme tu sarafu moja, yako mambo mengi ambayo tunajiandaa kuyafanya, lakini sarafu moja haiji kama zawadi. Ili uweze kupata sarafu moja lazima uhakikishe kwamba unafuata vigezo vya *macro economic convergence*. Eneo hilo tunafanya vizuri zaidi kuliko nchi nyingi ndani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Babu yangu amesema nisipomtaja hapa, basi mambo yatakwenda vibaya. Naomba niseme kwamba mchango wako nimeupokea na nimekutaja. Nimekutaja kwamba lile eneo lako nililolitembelea mwenyewe tutahakikisha tunaimairisha zile barabara na tutahakikisha tunachukua hatua za makusudi tuweze kuwa na *one border post* pale.

Mimi mwenyewe juzi nilikuwa Uingereza nimezungumza na *DFID* wameahidi kutupa bilioni dola 32 za kuimarisha mipaka. Kwa kuwa mimi ndio nimezileta kama Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri Afrika Mashariki, nitahakikisha kwamba sehemu yake inakwenda kwa Babu yangu ili na mimi mambo yangu yaweze kuniendea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nizungumze zaidi, lakini nachelea kupoteza muda. Lakini niseme tu na Mheshimiwa Pindi Chana na yeye vile vile amenialika niende kule na amesema nikienda atanipokea. Sasa mimi ni nani kualikwa na Mheshimiwa Pindi Chana halafu nisiende wakati amenihakikishia vile vile atanipokea na nitakaa vizuri kule! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niwahakikishie Wabunge wote kwamba hoja zenu tumezipokea na majibu yalikuwepo, lakini kwa kuheshimu muda, niishie hapo.

Lakini kabla sijaishia hapa, niseme tu, kabla hujasema Tanzania haitatamba katika Afrika Mashariki ni vizuri ukatembea ukaona nini Tanzania inafanya. Ukishatembea ukaona Tanzania inachokifanya kizuri usiishie hapo.

Tembea uone, uende Namanga kule ukifika Namanga utakuta Tanzania tunauza *transforma* na umeme. Ukishaona mambo hayo usiishie hapo. Nenda, zunguka uone kwenye Afrika Mashariki nzima, utakuta Afrika Mashariki nzima nchi yenyе amani ni Tanzania kuliko nchi yoyote ile. Ukishaona hiyo, usiishie hapo, zunguka tena uangalie Afrika Mashariki vyanzo vya nishati ya umeme utakuta Tanzania ndiyo inayoongoza Afrika kwenye kuzalisha Nishati na ina vyanzo vingi kuliko nchi yoyote.

Ukishaona hivyo usiishie hapo, zunguka uone mitandao ya barabara. Mitandao ya barabara ya Afrika Mashariki ni Tanzania tu yenyе sehemu kubwa ya mitandao hiyo na tumeweka lami mitandao hiyo kuliko nchi yoyote ile. Ukishaona hivyo usiishie hapo, tembea na uone na uzunguke utakuta kwamba nchi zote zilizotuzunguka zinategemea Tanzania tuzalishe na tuwalishe. Ukishaona Tanzania ndiyo ina ardhi kubwa ya kuweza kuwalisha wana wa Afrika Mashariki, ukishaona maajabu hayo yanayoendana na Kilimo Kwanza usiishie hapo, tembea na uzunguke, nenda nenda usiishie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba tunaingia kwenye soko la pamoja, lakini hatutaishia hapo, Tanzania tutatoa mwongozo na tutaongoza uchumi wa Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki hoja imetolewa na Mheshimiwa Waziri kwa jinsi majumuisho yako yalivyokuwa mazuri hoja yako imeungwa mkono na kundi lingine kubwa sana la Wabunge wa kawaida ambao siyo Mawaziri. Kwa hiyo, inaonekana muda haukuwa upande wako, lakini wengi wangependa kukusikiliza ukiendelea kutoa hayo uliyokuwanayo. Sasa tunaendelea na hatua inayofuata.

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 97- WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI

Kif.1001- *Administration and General* Tshs. 2,129,675,960/=

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nahitaji tu maelezo kidogo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na baadhi ya hoja ambazo amezielezea.

Kwanza kabisa hayo aliyokuwa anaelezea mwisho, ufanuzi wa nafasi ya Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ndio ambayo yamekuwa yakikosekana miaka yote, ndio maana Watanzania wengi wamejenga hisia kwamba sisi ndani ya Jumuiya ni wa mwisho, tuko chini kwa sababu Viongozi wa kisiasa mlikuwa hamchukui jukumu la kueleza ni *potential* gani ambayo nchi tunayo. Matokeo yake kila mtu sasa hivi kuanzia wasomi mpaka wamachinga wa kawaida wanaongea lugha hii, kwamba sisi tuko nyuma.

Sasa hii lugha hii ambayo umetoka kuizungumza ya kishujaa kabisa ya kueleza jinsi gani ambavyo Taifa letu liliyvo na *potential* ndio lugha ambayo Viongozi wote wa kisiasa tunapashwa kuizungumza. Kwa mujibu wa tafiti ambayo imefanywa na *Economic Intelligence Unit* inaonesha kwamba iwapo uchumi wa Tanzania utaendelea kukua kwa kasi inayokua sasa na chumi nyingine za nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea kukua...

MWENYEKITI: Mheshimiwa samahani...

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye hoja, nina dakika tano.

MWENYEKITI: Ndio, uende kwenye hoja usituhutubie.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye hoja au dakika tatu zangu zimekwisha?

MWENYEKITI: Njoo kwenye hoja Mheshimiwa.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa umeshanikatisha. *Economic Intelligence Unit* wanasema kwamba iwapo uchumi wa Tanzania utaendelea kukua kwa kasi hii inayokuwa sasa na chumi nyingine za Afrika Mashariki zikiendelea kukua kwa kasi hii hii ambayo inakua hivi sasa, ndani ya miaka mitatu Tanzania ndio itakuwa ndio *the biggest economy in the region*, ndani ya miaka mitatu na mambo yote ambayo umeyaeleza hapo.

Lakini tuna tatizo na ndio nataka alitolee ufanuzi Mheshimiwa Waziri, kwamba ni nini ambacho tunafanya hizi *potential* ambazo zipo zikawa zinaongoza maamuzi yetu na katika hoja ambazo nimezungumza hapa kwamba tujaribu kusaidia Watanzania wataalamu, waanzishe *think tanks* ambazo zitakuwa zina-*generate* taarifa na bahati mbaya kwamba hukuweza kulieleza hili, hili analionaje Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha kwamba hali ya nchi yetu katika *region* inafahamika na Watanzania wanajua na wachukue hizo fursa kuhakikisha kwamba tunaiweka Tanzania kuwa nchi kubwa zaidi na nchi yenye uchumi zaidi ndani ya *region*?

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Zitto kwa hoja aliyoitao. Naomba niseme kwamba nakubaliana naye kwamba umuhimu wa kuwa na *thinking tanks*, lakini niseme

tu ni hivi karibuni tumeanzisha Tume ya Mipango ambayo imepewa madaraka zaidi, lengo lake ni kujielekeza huko.

Lakini vile vile Wizara yetu hivi sasa tumepeleka maombi ya kubadilisha muundo wa Wizara, tunachokiomba vile vile tuwe na *research unit* ambayo itashughulikia kwenye kufikiria na kwenye mambo mengine. Lakini vile vile tumekuwa tukitumia taasisi mbalimbali kama *Economic Research Bureau*, kama *TISCO*, kama *ESRF* katika kufanya maamuzi mbalimbali.

Lakini vile vile niseme kwamba nilipowauliza watu wa mipango wakasema wanatumia na *private thinking tank*, lakini nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe kama ana jambo lolote anafikiri kwamba tukilifanya linaweza likatusaidia kuwa na kitu kizuri zaidi cha kusaidia, maana ukiwa *thinking tank* moja hamna nyingine inayotoa mawazo mbadala na yenewe ni tatizo.

Kwa hiyo, pamoja na hii iliyopo *officially* tunaweza tukaweka mazingira mazuri ya kuwa na *another alternative thinking tank* ambayo ni *independent* ambayo inaweza ikawa na yenewe inashauri. Nakaribisha mawazo yako na mengine yoyote yale kwa nia ya kufanya hivyo, kwa sababu tukifanya hivyo ndivyo tunazidi kujipanga vizuri kama nchi. Ahsante.

MHE. DR. HAJI MWITA HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, *sub-vote 1001* - mshahara wa Waziri. Nilipokuwa nachangia hoja inayohusu Afrika Mashariki nilitoa maelezo kuhusu utaifa wa Afrika Mashariki kwamba uwekwe mbele kuliko utaifa wa nchi na Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu hoja ali-quote kwamba hakusema ye na ni kweli kwamba sio ye ye ambaye ametamka, imetoka upande wa pili.

Sasa nilichokuwa nataka nifahamike ni kwamba kuwe na fikra au mawazo kwamba ikiwa kama sasa hivi sisi bado tunajifikiria kama nchi moja na ulimwengu, unajifikiria kuwa pamoja: Je, sisi kama Zanzibar bado tunalalamika kwamba nataka hiki, nataka hiki, niwe hiki, tutafika wapi, wakati watu wanazingatia suala la kuwa katika Taifa moja na kuwa pamoja na kuweza kujadili mambo yao yaende vizuri kama Taifa lililokuwa katika hali moja. Nafikiri nilikuwa nataka nitoe ufanuzi tu kuhusu hii *idea* ya utaifa wa nchi kuliko Utaifa wa Afrika Mashariki. Ahsante sana.

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Mbunge ila tu niseme duniani kote, nitumie mfano wa *European Union*, wakati wanaaza kushirikiana wako waliokuwa na mawazo kwamba ingekuwa vizuri *European Union* iwe *Federal* kwa haraka, kwamba iwe nchi moja. Lakini ukiangalia *European Union* kwa sasa imejikita zaidi kwenye uchumi, haijakwenda kwenye ile ya kupoteza utaifa pamoja na yote wanayoyafanya hayo.

Ukiangalia hata hapa Afrika Mashariki wako watu ambao wanafikiria kwamba labda tunakwenda taratibu kuelekea kwenye shirikisho, lakini ina-*involve* kupoteza uraia. Lakini kumbuka mwaka 1963, Mwalimu Nyerere alichelewesha uhuru wa Tanganyika kwa nia ya kutaka nchi nyingine zipate uhuru kwanza na kwa nia ya kutaka nchi nyingine

zkipata uhuru tuweze kuwa na sarafu moja, lakini nchi nyingine zilipopata uhuru tu, zikasahau kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa ametaka tuanze na sarafu moja. Walipopata uhuru tu kila nchi ikataka kuwa na sarafu yake.

Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kusema Tanzania sisi ni wana Afrika Mashariki wa kweli toka mwaka 1963 na alivyosema Mheshimiwa pale, suala la utaifa ni jambo la msingi kwa sababu utaifa ni utaifa tu. Haya mambo tuyape muda kadri siku zitavyokuwa tunakwenda ndio tutaona nini kitatokea.

Lakini kwa sasa kuanza kuzungumza kwamba sasa Tanzania haipo, Kenya haipo, Rwanda haipo, Burundi haipo, unaweza ukawa unajifurahisha tu, haya mambo tuyape muda kadri mambo yanavyokwenda, itafika siku moja tutazungumzia utaifa wa Afrika Mashariki. Lakini kwa sasa hebu tushughulike kwanza na kitu cha kuweka tumboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa hapa, umeme una matatizo, chakula kina matatizo, miundombinu ina matatizo, hayo ndio mambo kwanza ya msingi. Tukitaka kuyachanganya yote, watu wataona hata ushirikiano sio mzuri na itatuletea matatizo zaidi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Marekebisho yoyote)*

Kif.1002- <i>Finance and Accounts</i>	Tshs. 255,285,520/=
Kif.1003- <i>Policy and Planning</i>	Tshs. 8,062,579,320/=
Kif.1004- <i>Trade and Finance Investment</i>	Tshs. 874,618,680/=
Kif.1005- <i>Economic and Social Infrastructure</i> ...Tshs.	581,757,120/=
Kif.1006- <i>Political, Defence and Security</i>	Tshs. 312,023,360/=
Kif.1007- <i>Procurement Management Unit</i> ... Tshs.	133,987,160/=
Kif.1008- <i>Information, Education and Communication</i>	Tshs. 232,110,520/=
Kif.1009- <i>Management Information System</i> ... Tshs.	179,976,120/=
Kif.1010- Internal Audit Unit...	Tshs. 134,814,840/=
Kif.1011- <i>Legal Services Unit</i>	Tshs. 192,129,400/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Marekebisho yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Kif. 1001- <i>Administration and General</i>	Tshs. 0/=
Kif. 1002 - <i>Policy and Planning</i>	Tshs. 0/=
Kif. 1003 - <i>Trade, Finance and Finance</i>	Tshs. 0/=

(Bunge lilirudia)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Bunge limekaa kama Kamati ya Matumizi, limeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kifungu hadi kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote. Hivyo basi, naliomba Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio hayo. Naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya
Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa
Fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge)*

MWENYEKITI: Nachukua nafasi hii kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wako kwa kazi nzuri.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani aliyoinonesha kwangu kwa kuniteua kuwa Naibu Waziri katika Wizara hii kwa muda wote wa kipindi cha kwanza cha Utawala huu wa Awamu ya Nne.

Pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Rais - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa uongozi wake imara wa nchi yetu kudumisha kwake amani na utulivu katika nchi yetu, kumeweza kutuletea heshima kubwa ndani na nje ya nchi yetu, amani na utulivu wetu umeifanya nchi yetu kuwa msuluhishi wa migogoro ya majirani zetu na imesaidia sana utekelezaji wa Irani ya CCM. Namtakia Mheshimiwa Rais ushindi mnono na wa kishindo katika uchaguzi mkuu ujao chini ya utaratibu wa mafiga matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kumshukuru kwa kiwango cha juu Mheshimiwa Bernard Kamilius Membe - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa msaada wake mkubwa na wa dhati kwangu kwa kuniongoza vyema na kunielekeza ili kufanya kazi zangu kwa ufanisi. Kwa kweli nimefaidika sana kwa kufanya kazi chini ya uongozi na maelekezo yake.

Napenda pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Uongozi wake makini ndani ya Bunge hili. Aidha, napenda pia kukushukuru na kukupongeza wewe Mwenyekiti kwa namna ulivyoliongoza vyema Bunge hili leo.

Pia, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa namna walivyoliongoza Bunge letu hili katika kipindi hiki cha miaka mitano tutakayoimaliza hivi karibuni. Nawatakia kila la kheri warudi tena Bungeni ili watuongoze tena katika Bunge lijalo. Pia ninawashukuru Wabunge wenzangu wote kwa uhusiano walionipa katika Bunge hili, nawaombea kila la kheri na ninawaombea warudi tena Bungeni hapo mwezi Novemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wananchi wenzangu na wapigakura wangu wa Jimbo la Kitope. Nawashukuru kwa ushirikiano walionipa na kufanya kazi nao pamoja katika kuliletea Jimbo letu maendeleo.

Kwa pamoja, tumepiga hatua kubwa ya maendeleo katika Jimbo letu hilo, ni mategemeo yangu kwamba watanipa ridhaa yao tena katika kipindi kijacho cha mwaka 2010/2015 ili tuendelee kwa pamoja kuliongoza Jimbo letu na kuendeleza yale tuliyoyaanza na mwisho kabisa napenda kuzishukuru sana familia zangu kwa uvumilivu wao kwangu na kwa namna walivyonisaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Ni dhahiri kwamba michango yao itatusaidia sana katika kuboresha na kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi wa Watendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja ya rafiki yangu Mheshimiwa Shoka Khamis Juma ambaye ametaka kujua Tanzania ina Balozi ngapi zinazokodi nyumba huko nje na kama zipo kwa nini hatujengi.

Pili, magari. Wameulizia kwamba Balozi zina magari mangapi na magari mangapi inakodisha. Balozi 26 zinakodi jumla ya nyumba 107. Kati ya hizo, Ofisi za Balozi ni 15, nyumba ya makazi ya Balozi ni 12 na nyumba za maafisa ni 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina mpango wa miaka 15 ya kujijengea au kununua nyumba zake ili kuondokana na tatizo hili la kukodi nyumba.

Adiha, mpango huu kwa kiasi kikubwa unakwenda vizuri na huenda ukamalizika katika kipindi cha mwaka 2016/2017. Kila Ubalozi una magari mawili, moja likiwa la mwakilishi ambaye ni Balozi na nyingine kwa ajili ya huduma za Balozini.

Hivi karibuni kwa sababu ya kuondoa tatizo la magari tumewapelekea fedha baadhi ya Balozi ili ziweze kununua magari ili ziweze kufanikisha shughuli zao. Balozi ambazo tumezipelekea fedha hizo ni Balozi wa Washington, Abuja, Riyadh, New Delhi na Pretoria.

Kwa kuwapelekea fedha hizo, tunategemea kwamba matatizo ya magari yatawapungukia. Mheshimiwa Juma Killimbah alitoa ushauri kwamba jengo la zamani la Ubalozi wetu Washington lifanyiwe ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalipokea wazo hilo na kwa kweli tunajitahidi sana kufanya ukarabati huo na karibuni hivi ukarabati utaanza kwa jengo hilo na baada ya hapo, ye ye ameshauri kwamba tuwape watu wakarabati jengo lile on *BOT basis* yaani *Build, Operate and Transfer* lakini tutafanya hivyo na baada ya kumaliza kazi hiyo Wizara yangu italikodisha jengo hilo ili tuweze kupata mapato kwa ajili ya kuendeshea shughuli nyingine za Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Anna Abdallah amezungumzia juu ya suala la tatizo la ardhi kwa Chuo cha Diplomasia. Chuo cha Diplomasia kwa msaada wa Wizara kiko katika mchakato wa kupata ekari 1,000 katika kijiji cha Buma Wilayani Bagamoyo kwani ndugu zetu wa Msumbiji wanahitaji muda kwa sababu jengo tulilonalo sasa hivi lina jina la *Tanzania Mozambique Foreign Relations*. Kwa hivyo, litahitaji muda mrefu sana Msumbiji kuendeleza mchakato ili Msumbiji ijiteoe katika jengo tulilonalo hivi sasa. Hata hivyo tunajitahidi tuwe na chuo chetu baada ya kupata ardhi hii kubwa iliyoko Buma ili chuo hiki kiwe kikubwa na tuweze kukipanua.

Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, amezungumzia pia suala la chuo kiimashwe kitoe kozi za digrii na wahitimu wa chuo wasaidiwe kupata ajira. Chuo kinaendelea kuimashwa na kuendelezwa na si muda mrefu itaweza kutoa mafunzo kwa ngazi ya digrii. Ajira Serikalini ni kwa ushindani lakini wale wanaopitia mafunzo ya diplomasia wana nafasi nzuri zaidi katika ushindani katika sehemu mbalimbali Serikalini. Lakini wale wanafunzi ambao wanapitia Chuo cha Diplomasia wanakuwa na nafasi nzuri sana ya kupata ajira. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Pindi Chana amezungumzia juu ya suala la Balozi ambazo zinafunga Ofisi zake hapa Dar es Salaam na kuzipeleka nchi jirani. Tatizo la Balozi za nchi kufunga Balozi zake, siyo tatizo la Serikali yetu bali ni uamuza wa nchi hizo. Sisi tunajitahidi sana kila inapowezekana kujaribu kuhamasisha nchi nyingine kufungua Balozi zake nchini Tanzania. Mfano wa hivi karibuni nchi ya Uturuki

imefungua ubalozi wake hapa Tanzania na tunajaribu kuhamasisha nchi nyingine ziweze kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa pia mfano wa Canada, Canada haikufunga Ubalozi wake, isipokuwa imehamisha shughuli za *visa* kupeleka Nairobi na huu ni utaratibu wao ambao hatuwezi kuuingilia. Ni sawa sawa na Ubalozi wa Uingereza nao umefanya hivyo hivyo. Hilo siyo wazo la kufanya na hata na sisi tunaweza tukafanya hivyo hivyo. Sisi tumefunga Ubalozi wetu Netherlands. Lakini shughuli zake tumezihamishia Brussels. Hii inategemeana hali ilivyo na hali ya kifedha inavyohitajika katika kuendesha hizi Balozi na huduma zake. Mfano Uingereza inasema kwamba utoaji wa *visa* hapa Dar es Salaam una gharama na ndiyo maana wameandaa utaratibu wa kufanya *zones*. Siyo Tanzania tu iliyoondolewa Ubalozi, lakini nchi nyingi sana zimeondolewa Balozi zake na kupelekwa nchi nyingine kwa ajili ya kutoa *visa*. Kwa hiyo, hilo ni swali ambalo tusingeweza kuliingilia. (*Makofi*)

Pia Mheshimiwa Pindi Chana amezungumzia juu ya suala la lini Tanzania itafunga Ubalozi wake Israel. Mheshimiwa Mbunge kama nilivyoeleza maamuzi ya kufunga ubalozi au kutofunga ubalozi nchi fulani ni uamuzi wa nchi yenyewe na hii inategemea kwamba uhusiano wa nchi hiyo na nchi nyingine ukoje. Uhusiano wetu na Israel ni mzuri. Israel ina Ubalozi wake Tanzania, lakini Balozi wake yuko Nairobi na sisi tunao Ubalozi Israel lakini Balozi wetu yuko Egypt. Kwa hivyo, tunao ushirikiano mzuri na Israel na tunabertilishana Balozi lakini siyo kwa kuleta katika nchi isipokuwa Israel Balozi wake yuko Nairobi, na Tanzania Balozi wake wa Israel uko Egypt. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga amezungumzia juu ya suala la kuvamiwa na kuporwa kwa Balozi wetu aliyekuwa nchini Afrika Kusini, Mheshimiwa Emmanuel Mwambulukutu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Emmanuel Mwambulukutu alivamiwa mwaka 2007 na kuporwa lakini baadaye gari lake lilipatikana. Baada ya hapo Mheshimiwa Emmanuel Mwambulukutu alifanyiwa matibabu ya kutosha kuanzia mwaka 2007 mpaka 2008 wakati aliporudi nchini. Hali yake iko nzuri na yuko imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Janeth Massaburi ametaka kuwe na utaratibu wa kutoruhusu kila mtu kupita *VIP* pale *Airport*. Ningependa kusema tu kwamba hivi sasa tunajenga ukumbi mzuri wa *VIP* pale *Airport* utakuwa na nafasi kubwa na haya maoni ya Mheshimiwa Massaburi tutayatilia maana ni namna gani ya kuendesha ukumbi wetu huo mpya kwa ubora zaidi bila ya kuwaruhusu watu wa aina mbalimbali kuingia mle, kwa sababu ukumbi ule ni ukumbi wa *VIP* kama inavyosemekana. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na utaratibu maalum na watu maalum wa kuingia ndani ya ukumbi ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Massaburi pia ametaka kujuu kwa nini Ubalozi wa Uingereza umehamisha huduma zake za *visa* nchini Nairobi. Nimekwisha

eleza kwa nini Ubalozi wa Uingereza umehamisha huduma zake za *visa* kupeleka Nairobi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa amezungumzia juu ya suala la Chuo cha Diplomasia kupewa kipaumbele cha kuwapata Wanadipolomasia bora. Chuo cha Diplomasia kinajitahidi kukiendesha kwa ubora ili wapatikane wanadipolomasia wazuri. Tunamshukuru sana kwa ushauri wake huo na tutauzingatia na tutazidi kukipa kipaumbele Chuo chetu cha Diplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majengo ya Wizara yaboreshwe na hasa lile jengo la Zanzibar, kwa kweli ni kweli jengo la Ofisi yetu ya Zanzibar siyo zuri sana. Lakini tunajitahidi kwanza hivi sasa tunajaribu kutafuta uwezekano wa kutafuta kiwanja sehemu nyingine ili tuweze kujenga jengo jipya kama Wizara zingine za Muungano zilivyofanya. Hili tunaliendelea na Mungu akipenda tutajitahidi kuona kwamba tuna jengo zuri la Idara ya Mambo ya Nje Zanzibar ambalo linafanana na Wizara yenyewe. Lakini kwa sasa hivi tutajaribu kulikarabati lile jengo tulilopo sasa hivi ili pia lionekane bora na zuri zaidi kuliko lilivyo hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Raphael Chegeni yeche ametuambia kwamba Balozi zetu zижikite zaidi katika kuhimiza wawekezaji kuja nchini na hiyo ndiyo kazi yetu na ndiyo sera ya Mambo ya Nje. Tuna Sera ya Demokrasia ya Uchumi, kazi yake ni hiyo na tutajitahidi kuziwezesha Balozi zetu ziweze kufanya kazi hizo kwa ufanisi zaidi na kupata wawekezaji zaidi ku Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Basil Mramba amezungumzia suala la matumizi ya maji ya Ziwa Chala baina ya Tanzania na Kenya. Ningependa tu kusema kwamba kuhusu suala hili maoni ya Mheshimiwa Mbunge yamezingatiwa na yatafanyia kazi kuitia mikutano yetu ya Tume za Pamoja baina yetu na Kenya na inawezekana hali ikawa nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Sasa naomba nimwite mtoa hoja ili naye aje ahitimishe hoja yake hapa. Karibu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nichukue nafasi hii niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri ambayo wamechangia tangu asubuhi hadi jioni hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue waliochangia kwa kuzungumza, kwanza kabisa ni Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi. (*Makofi*)

Niwatambue pia waliochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Brigedia Jenerali Mstaafu Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Magdalena Sakaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, nawashukuru sana kwa michango mingi na nikiri kwamba inawezekana tusijibu maswali yote kwa sababu ya muda, lakini tutayajibu yale ambayo tuna majibu na muda unaturuhusu. (*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama alipokuwa anawasilisha taarifa yake alizungumzia suala la safari za viongozi. Safari za viongozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni za manufaa makubwa sana kiuchumi na Mheshimiwa Rais anazo safari za aina mbili kubwa. Kuna safari anazoalikwa na viongozi wa dunia wa nchi mbalimbali kutokana na michango yake mikubwa hasa katika fani ya *milleniaum* na Malengo ya Milenia (*MDG No. 4*) na *MDG No. 5* amekuwa anaalikwa na kuzungumza na kutoa mada huko. Lakini pia alikuwa anaheemea katika nchi mbalimbali, misaada na mikakati kadhaa ya maendeleo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopita ni kweli zimetumika pesa nyingi zinazokaribia shilingi bilioni 28 kwa viongozi wote wa juu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiit, safari hizi ni za muhimu, lakini Mheshimiwa Rais ametoa agizo la *ku-review* au kufanya tathmini ya idadi ya wanaoongozana katika msafara huu na Wizara yangu na hasa Idara ya *Protocol* inapitia upya agizo la Mheshimiwa Rais na nina hakika katika kipindi kijacho tutakuwa na takwimu maalum za idadi ya watu wanaoongozana na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Rais wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani walituuliza suala la wastaafu kuwa mabalozi na hata baada ya miaka 60 na hata miaka 100 wanaruhusiwa? Jibu ni kwamba tunayo makundi mawili ya mabalozi, kundi la kwanza *carrier diplomats*, watumishi waliozuka toka ndani ya Wizara, hawa inapofika miaka 60 kama watumishi wengine wa Serikali wanastaafu. Tunalo kundi la pili la *political appointees*. Wanasiasa kama tulivyo sisi humu ndani ya Bunge, wapo wenye miaka 65, wako wa miaka 70. Nina hakika kuna watu wanakaribia miaka 80 wapo na mabalozi nao hivyo hivyo. Wale wanaopata bahati ya kuwa *politically appointed* na Mheshimiwa Rais na wenyewe wanakuwa hawana kikomo cha umri mpaka pale inapompendeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama tulivyo Wabunge hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa swali Chuo cha Diplomasia tunakisaidiaje kutekeleza wajibu wake na kufanya tafiti? Ni kweli kabisa kwamba katika nchi kama

yetu Chuo cha Diplomasia kinatakiwa kiwe *think tank*, kiwe na watu mahiri wanaoifanya nchi na dunia. Lengo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Wizara yangu ni kukifanya Chuo cha Diplomasia kiwe *think tank*. Hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Rais tayari amemteua Balozi Mahundi ambaye ni *Doctor*, ana *Ph.D* ya *Strategic Studies* na *Conflict Management Prevention* na *Resolution*. Lakini pia tumeajiri Wahadhiri sita wakamamavu, wana akili na waadilifu na zinachemka. Hawa ndio watakuwa *think tank* ya masuala mengi ya utafiti ambayo tungependa watusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Chuo cha Diplomasia mwaka huu imepaa kwa asilimia 23 kutoka shilingi bilioni moja na milioni mia tatu kwenda shilingi bilioni moja na milioni mia sita, si haba. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tunalifikiria na tunalipa kipaumbele ili kukifanya Chuo cha Diplomasia kiwe chombo kinachoisaidia Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa swali kwamba Wizara ina watu wasio na uchungu na wana uwezo mdogo katika Wizara, napenda niseme tena mbele ya Taifa kuititia Bunge lako Tukufu kwamba wafanyakazi wangu wote wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa wana uchungu na uwezo usio na kifani. Wanachapakazi katika mazingira magumu, wamesoma na wamepikwa. Kazi tuliyonayo ni kuwashukuru tu kwamba wanaweza wakafanya kazi ndani na nje ya nchi katika mazingira magumu ambayo Waheshimiwa Wabunge mnayafahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeulizwa pia swali kwamba Wizara ina wafanyakazi wake wote, hapana kwamba *APRM* yaani *African Peer Review Mechanism* mbona inachelewa sana kuratibiwa au kuwa *evaluated*. Jibu lake ni kwamba ni ufinyu wa Bajeti ya mwaka 2009 ambao tulitegemea *APRM* ifanye hiyo *self evaluation* na kuratibiwa tulikuwa na ufinyu wa Bajeti. Tulikuwa tumepeanga kutumia pesa zilizopungua shilingi bilioni 100. Lakini tulipata shilingi milioni 600. Kwa vyovyyote vile shilingi milioni 600 zingeweza kuifanya kazi hiyo. Hiyo ni sababu kubwa sana iliyofanya tuchelewe kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matumaini yangu ni kwamba mara baada ya uchaguzi Profesa Adebeg Abebayo pamoja na Mama Gracia Machel wako tayari sasa kurudi na kuendelea kazi ya nchi kujikosoa yenyewe na hivyo kujipatia walau nafuu katika nyanja za Kimataifa za kuheshimika yaani *credibility* ya nchi inakuwa pale inapo jikosoa na kujirekebisha. Kwa hiyo, msimamo huo upo na nina hakika tutauendezea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna swali tuliulizwa hapa kwamba vipi Wizara mbona haina sera, haina malengo, haina miongozo na kwamba kwenye Balozi zetu Mabalozi wanafanya kazi kiholela, wanaelea elea tu. Naomba niseme kwamba si kweli, kwanza kabisa tuna *vision* ya 2020 - 2025. Pili, ukisoma kitabu changu cha Bajeti ukurasa wa 39 nimeainisha malengo ya Wizara, tatu malengo, tuna kijitabu kabisa cha malengo ya Wizara cha mwaka 2001. Ningetaka Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed bahati mbaya hayupo hapa, lakini nitamwekea kwenye *desk* lake aweze kuisoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ipo, lakini siyo hilo tu, pia tuna mpango mkakati yaani *the strategic plan* ambayo tunaitoa kila miaka mitatu kwa Mabalizi. Lakini kama hiyo haitoshi tuna *diplomatic hand book*. Hiki ni kitabu cha Kibalozi kinachotolewa kwa kila Balozi anapoapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kijitabu kile kinamweleza anakokwenda, akafanye nini kutokana na maslahi ya Taifa na kutegemeana na eneo analokwenda kuliwakilisha Taifa. Kama kuna *institution* ya Wizara ambayo iko *well organized* katika *documentation* ni Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na ningetaka Kambi ya Upinzani ijue hivyo na nitamgawia nakala zote ili kesho kutwa asiniulize tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar. Swali liliulizwa na Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji kuwa mbona Wazanzibar wapo 15 tu katika Wizara. Ningependa kusema kwanza ndiyo wapo 15, Zanzibar lakini kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, tuna Wanzanzibar 43 sawa na asilimia 20. Si haba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Kabwe Zitto ameuliza suala la Morocco kwamba ina *lobby* sana, ni kweli. Serikali ya Morocco ina-*lobby*, ina-*lobby* kwa mambo mawili kwanza kutaka kurudi katika *African Union* maana iliondoka yenyewe. Lakini pili wana-*lobby* ili nchi za Afrika zikatae, sasa *Western Sahara* na isiitambue *Western Sahara* badala yake iitambue Morocco peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kutoa tamko na msimamo wa Serikali kwamba ingawa kila mwananchi anao uhuru na Waheshimiwa Wabunge wanao uhuru wa kutoa maoni yao kuhusu nchi ya Morocco. Lakini msimamo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania upo pale pale. *Principal* ya kutambua *right* ya *self determination* kwamba kila koloni katika Bara la Afrika linastahili haki ya kujitawala yenyewe *Western Sahara* ilikuwa koloni ya Waspanishi, walikuwa na bendera ya Spanish, ilikuwa na Gavana wa Spain, wakaondoka bila kuaga wakawaacha nyuma wananchi wa *Western Sahara* ambao wananchi hawa wana haki ya kujitawala wenyewe, kama tulivyojitala wenyewe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nilikwenda Morocco nikatoa *Olive Branch* (Tawi la Amani) likitumwa na Mwenyekiti wa AU, tulipokuwa ni Mwenyekiti mwaka 2008, tukimuambia Mfalme kule, kwa sababu kuna *tension* kubwa kati ya Algeria na Morocco kuhusu *Western Sahara* na kwa kuwa hili ilikuwa ni jukumu la Mwenyekiti wa AU, nilikuwa nimekwenda ili tuwe na mazungumzo kati ya Algeria na Morocco na tuwe na uhusiano mzuri tu ili tuweze kulimaliza tatizo lile. Lakini sikuruhusiwa kumuona Mfalme kwa sababu sikuitambua ama sikuipenda *Western Sahara* na nikarudi, lakini ujumbe ulifika.

Mheshimiwa Mwenyekiit, nimekwenda Algeria nikatoa msimamo huo kwamba msimamo wa Tanzania ni ule ule mpaka *mediation* ya *United Nations* itakapomaliza kazi yake na kutushauri ni nini tufanye, Tanzania itaendelea kusimama na msimamo wake wa kuitaka Morocco iwapatie wa *Western Sahara right* yao ya *self determination*, wanastahili na hatupunguzi hilo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Kabwe Zitto, ulikuwa sahihi kabisa uliposema tusiyumbe katika suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Burundi wenzetu wako katika mchakato wa uchaguzi. Uchaguzi wa Madiwani ulikwisha tarehe 24 Mei, uchaguzi wa Rais umemalizika tarehe 28 Juni na wamemchagua Rais Pierre Nkurunziza kwa 91%. Kati ya kura 3,000,000 zilizopigwa, amepata karibu kura 2,000,000 na ushee. Wakati wa kura za Madiwani Chama Tawala cha *CNDD* kinachoongozwa na Mheshimiwa Pierre Nkurunziza kilipata 64% ya kura. Baada ya kupata 64% vyama 12 vikaamua kususia uchaguzi wa Rais eti kwa madai kwamba uchaguzi ule wa madiwani ulikuwa ni *fake*. Wakatoa mifano minne ya mambo ambayo yalitokea. Lakini *European Union, Great Lakes Region, East African Community* na *AU*, baada ya ku-monitor uchaguzi ule walitambua wakasema uchaguzi ulikuwa ni wa haki na ulikuwa huru. Kutokana na kauli zile uchaguzi uliambiwa uendelee, lakini vyama 12 vikasita na vikasusia. Miiongoni mwa watu waliosusia uchaguzi huu ni mpinzani mkubwa, Agathon Rwasa ambaye chama chake kilipata 14%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitumwa na Rais mara mbili, kwanza peke yangu lakini pili kuongoza ujumbe wa Mawaziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Afrika Mashariki. Tumewaambia Warundi na ningependa kupidia Bunge lako Tukufu niwaambie tena wenzetu Warundi kwamba Tanzania imebeba sana mzigo wa wakimbizi wa nchi jirani na hasa Burundi. Tungependa watuelewe hivyo kwamba Tanzania inapenda amani na wayamalize mambo haya ndani ya nchi yao. Kitendo cha wapinzani kwanza kukimbilia tena porini ili walete fujo Burundi na ili Tanzania ibebe mzigo wa wakimbizi *single hended*, hakikubaliki. Viongozi wote wa wakimbizi watakaoingia nchini tutawakamata ili baadaye tuwarudishe kule. Hatupo tayari Tanzania iwe ni kichaka cha viongozi wanaoleta fujo kwa makusudi. Nadhani wamenielewa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *fake companies* kwamba yapo makampuni katika nchi hii yanakuja kuwarubuni Watanzania, lakini wanapotaka kwanza kazi, yanabainika kwamba yalikuwa ni *fake*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli makampuni ya aina hii yapo na ninaomba nitumie nafasi hii kuwaomba tena watanzania; Balozi pamoja na *Consultes* zilizoko nje ya nchi zipo kwa ajili yenu. Unapomuona mtu amekuja kwa jina la kampuni na akakueleza kwamba muingie *partnership* kwa ajili ya kuanzisha kampuni au shughuli yoyote ya uwekezaji nchini, usisite kuja kimya kimya, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, lete jina lake, lete *e-mail* yake, lete *website* yake, *address* yake, tuache tukufanyie kazi tujue kama huyu mtu ni tapeli au ni halali. Wapo baadhi ya watu wamefanya hivyo na tumewapa majibu yanayostahili. Ni wajibu wangu kuwakumbusha Watanzania hasa wafanyabiashara, msiingizwe mkenge, tuleteeni tuwachapie kazi, tupo kule duniani tutawajua na tunapobaini kwamba ni matapeli, tutawashauri muachane nao, kwa sababu rangi si hoja, nadhani mmenielewa. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya majengo katika Balozi zetu, ilikuwa inasikitisha. Lakini naishukuru Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti mahiri Mheshimiwa Wilson Masilingi, sasa Bajeti yetu ya Maendeleo imeongezwa mara mbili, kama mtaiidhinisha, badala ya shilingi bilioni 20, safari hii naomba shilingi bilioni 40, na mkiidhinisha hapa, tumeanza mchakato wa kurekebisha na kukarabati majengo yetu ya Ubalozi. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Raphel Chegeni alisemea kuhusu mishahara ya Ubalozini iende kwa wakati. Nina hakika Hazina wanakusikia kwa sababu Wizara ya Mambo ya Nje ndio tumewaambia hivyo wenzetu kwa maandishi na kwa mdomo kwamba ni vizuri sasa mishahara ya wafanyakazi wetu iende walau ya mwaka mmoja kwa mkupuo au ya miezi mitatu kwa mkupuo ili kuondoa adha na fedheha ninayoibeba mimi pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa watumishi wetu kukaa miezi kadhaa bila kupewa mishahara yao kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kigoma na *Pepenburg, Lower Saxon*; ni kweli kwamba mwezi wa tatu ujumbe ulikuja Tanzania ukaenda Kigoma na baadaye ulikwenda kwenye baadhi ya sehemu za Maziwa Makuu kwa lengo la kufufua meli ya Liemba, lakini pia kwa lengo la kufufua na kuweka *partnership* kati ya mji wa Kigoma na *Lower Saxon*, mji wa *Papenburg*. Sasa tumepiga simu mchana huu, suala hili limeshapelekwa kwenye *sanete* yao ili lipate *approval*. Mara baada ya *approval* kutoka ya kurekebisha na kukarabati *MV Liemba* pamoja na ku-twin mji wa Kigoma na *Lower Saxon*, kwa vyovoyote vile tutakuwa wa kwanza kulishabikia suala hili na sehemu ya miji mingine na Mheshimiwa Kabwe Zitto, nakushukuru kwa kutukumbusha hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *diaspora* na *dual nationality*, naomba nirudie kama nilivyosema asubuhi kuwa Watanzania hatuna haja ya kuogopa, kama tunaweza kuwapa uraia Warundi na Wanyarwanda 169,000 kuwa raia wa Tanzania haitakuwa dhambi hata kidogo kwa nchi hii kuwaruhusu Watanzania wake walio nje ambao kwa sababu zozote zile wanapochukua uraia wa nchi ile tuwaruhusu wafanye hivyo badala ya kuwafutia uraia wao wa kuzaliwa, ni dhambi ambayo haiwezi kukwepeka, tusifanye hivyo. Hatuwezi kuheshimu zaidi wageni na kuwadharau Watanzania wetu eti tu kwa sababu amekaa nje. Mtanzania anapoishi nje, narudia ndugu Waheshimiwa Wabunge, Mtanzania anapokaa nje huyu si msaliti, amekwenda kuhemea juani ili alie kivulini, *he is not a traitor, he is just smart citizen.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani anayesema kwamba kwenda kukaa nje ni usaliti? Ni nani na ni usaliti gani? Tuna mfano gani wa Mtanzania ambaye ameisaliti nchi katika kipindi chetu cha miaka 50? Wasaliti ni sisi wenyewe ndani ya nchi hii, tuiswasingizie sana Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, nawaomba viongozi wenzangu, nazungumza tena, nawaomba viongozi wenzangu, tusikwamishe jitihada za kulikwamua jambo hili, Wizara yangu itapeleka Muswada kwanye *cabinet* kuziagiza kila Wizara inayohusika katika *element* ya *dual nationality* na *diaspora to play its' part* ili tulilete Bungeni, mljadili, mlipitishe, tuwanusuru Watanzania wenzetu wanaoishi nje, ili tuwa-*engage* katika maendeleo ya nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote inayokaa na kuwaacha raia wake nchi za nje na kudhani kwamba inaweza kuendelea, inajidanganya yenyewe. *Diaspora* ni sehemu ya maendeleo ya uchumi wa nchi yetu na ni dhambi tusipokwenda na kufikiria *beyond our borders*. Wale ni Watanzania wana *collective competences*, wana uwezo na utaalamu wa hali ya juu sana. Badala ya sisi kuhaha kila siku kuwatafuta wataalamu kutoka kona zote za dunia, wakati tuna Watanzania wenzetu ambao wanashindwa tu kurudi nchini

kwa sababu wamejilipua, tusiogope, sisi ni lazima ku-*provide leadership* katika Afrika, hapana kuniambia Namibia inafanya nini au Uganda inafanya nini, *we have to provide leadership* na hakuna sababu ya kuogopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemalizia hapo na ningependa niombe radhi kwa yale ambayo sijayajibu, inawezekana kwenye kifungu nitapata nafasi ya kuyajibu, nina muda gani zaidi? Bado dakika 10, ngoja basi niseme moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutayajibu haya kwa kuandika, lakini ningeomba tu niseme kuhusu suala la Mabalozi. Mabalozi watusaidie, asubuhi sikulisema lakini kuna mmoja ameliandika pale kwenye hati yake kwamba ni nini mchango wa Mabalozi katika Uchaguzi wetu Mkuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wa Mabalozi katika Uchaguzi wetu Mkuu, ni kwamba *UNDP* ikishirikiana na *European Union*, wamechanga dola milioni 23, sawa na karibu shilingi bilioni 32 za Tanzania. Pesa hizi zilizochangwa na wafadhili kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu nasema ninawashukuru sana, zinalenga kwanza kabisa kuzisaidia *ZEC* na *NEC* kutekeleza wajibu wake katika kipindi chote cha uchaguzi. Lakini pia tuna *referendum* Zanzibar ambayo itatumia zaidi yan shilingi bilioni 3.9, lakini sio hilo tu, kwa upande wa Tanzania Bara na Visiwani, fedha hizi zina lengo la kuwaelimisha waandishi wa habari na kuwashamasisha wananchi ili waelewe haki zao na mambo kama hayo. Lakini pia kuna timu za ku-*monitor* ambazo zitakuwa zinakwenda hapa na pale. Huo ndio msaada amba Mabalozi wanatakiwa kuutoa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kipindi hiki cha uchaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi tunawategemea, watakuwa wana-*monitor* na kutuhakikishia kama uchaguzi wetu ni wa haki na kama unakwenda kiuhuru yaani ni huru. Hatutegemei kwamba Mabalozi watufundishe namna ya kupiga kura, wala kutufundisha namna ya kuliongoza Taifa hili. Watananza wamesoma sana, wana utaalamu mwangi na ujuzi mkubwa sana, ni matusi kwa Balozi kuja kutufundisha utawala au kutumia mwanya wa fedha tunazozipata za msaada kutuingilia hadi jikoni na kutuambia ni nini cha kufanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabalozi wetu walioko nchi za nje, hawaruhusiwi kamwe kuingilia shughuli za ndani za nchi walizopo, hamtasikia na vivyo hivyo kwa Mabalozi walioko hapa, uje ku-*monitor* uchaguzi, lakini hapana kuingilia mambo ya ndani. Lakini pia nasema tunawaruhusu Mabalozi, wanaweza wakafanya kazi na wapinzani *24 hours, seven days a week*, wafanye kazi na wapinzani tu; lakini hawaii kufanya kazi ya wapinzani nchini, kuna *clear distinctions* kati ya *working with the opposition and working for the opposition*. Hapana kufanya kazi *for the opposition*, tutang'oana, *you can work with the opposition* na dunia nzima iko hivyo na nalisema bila woga na-*read my lips*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia tena kwa kiingereza *you can work with the opposition 24 hours, seven days, don't work for the opposition*, ni dhambi. *Don't work for the ruling party*, ni dhambi. Hapana kufanya kazi kwa ajili ya chama, fanya kazi na

chama. Nikigundua kwamba umekwenda huko mkoani au mmekwenda kwenye vyama, halafu unawafundisha kwamba tufanye nini ili tuking'oe Chama Tawala au Chama Tawala tufanye nini ili tuking'oe CHADEMA, nitakuondoa. Nitaomba ruhusa kwa Mheshimiwa Rais, tukuondoe nchini, hiyo sio kazi ya Mabalozi; *read my lips*. Nadhani wamenielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema tena, nawashukuru sana kwa michango mizuri na mikubwa mliyotupitishia. Ninarudia nilichosema asubuhi, nawatakieni wote uchaguzi mwema, wale msiosema mnataka kuchagua wapi, chagua Jimbo mrudi, *we will miss you*. Ni lazima mrudi ili tulisaidie Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

Kifungu 1001 – *Administration and General* Sh. 5,466,341,288

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko kwenye mshahara wa Waziri. Kuhusu hoja ya uraia mara mbili, Waziri wakati anajibu hoja za wachangiaji, ameonekana akilalamika sana kuhusu uraia wa nchi mbili. Sasa nataka kujua, je, anamlalamikia nani? Na ni jukumu la nani kusimamia sheria hiyo ikaletwa hapa Bungeni?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, kuhusu *dual nationality* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapolalamika ni stahili yangu ya sauti ambayo Mheshimiwa Martha Mlata, anadhani ninalalamika, lakini kwa kuyasema haya ninayoyasema ndio ninapeleka ujumbe kwa watu wote amba walikuwa na mashaka kuhusu suala hili na ni matumaini yangu kwamba ujumbe huu umeingia na Bunge lijalo, nina hakika kabisa kwamba malalamishi haya hutayasikia tena, isipokuwa sasa yatakwenda na vitendo.

MHE. MWADINI ABBAS JECHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilitaka ufanuzi kujua kwamba ile ardhi ambayo Serikali ya Rwanda imeipatia Tanzania kujenga Ofisi zake na za Ofisi za Maafisa wa Ubalozi pale Kigali, ni muda mrefu sasa kwamba eneo lile halijaendelezwa na kuna fununu kwamba Serikali ya Rwanda inataka ku-revoke ile hati ya kumiliki lile eneo la ardhi ambayo

limeipatia Serikali ya Tanzania. Nilitaka kujua ni kwa nini Serikali ya Tanzania inaizembea hii fursa ambayo imeipata na ni hatua gani ambayo Serikali ya Tanzania inachukua ili kulidhibiti eneo hilo?

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani nilikuwa napata *clarification* ya swali. Sasa ni kweli na sio Rwanda peke yake, tunapata maeneo ya viwanja lakini tulikuwa bado hatujajenga. Tatizo ni kwamba katika kipindi cha kabla ya miaka miwili iliyopita, Wizara yangu haikuwa na *Development Budget*, haikuwa na Bajeti ya Maendeleo. Matokeo yake tulikuwa tunategemea tu ridhaa na huruma ya Serikali au *Treasury* kutupatia pesa kwa ajili ya kujengea majengo yale. Sasa kwa vile katika kipindi cha miaka miwili iliyopita tumeanza kupata *Development Budget* ambayo mwaka huu kama kwa idhini yako na Waheshimiwa Wabunge wenzako mtatupatia shilingi bilioni 40, utaanza kuona mabadiliko ya sisi kuanza kuvijenga viwanja vile kwa sababu sasa tunayo Bajeti ya Maendeleo ambayo Waheshimiwa Wabunge, tumewaomba na mtatupatia. (*Makofi*)

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shida na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, nakiri kwamba ni mtu anayechapa kazi usiku na mchana, kwa hiyo, nawatakia kila la heri. Ila nilichangia hoja ndogo kwa maandishi kwamba sisi kule Itigi tuna kampuni inaitwa *General Business & Equipment Supplies Co. Ltd.* Hii kampuni na watu wake walidhulumiwa mali zao na Serikali ya Rwanda, walikuwa na kazi ya kusafirisha *gypsum* kutoka Itigi kupeleka Rwanda. Sasa kule wanajeshi au Serikali ya Rwanda ikawa imetaifisha magari yake pamoja na mali hiyo iliyokuwa imebebwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala analifahamu lakini sasa ni muda mrefu hao watu, miaka karibu 15 wanapigwa danadana pamoja na kwamba Mahakama za Rwanda na Tanzania, zote mbili zimewapa haki hawa watu. Lakini wakati wa kukazia hiyo hukumu, tatizo linakuja kwenye Serikali ya Rwanda kwamba inapiga danadana katika kukaza hiyo. Sasa ningependa kujua ni kwa nini wanafanya hivyo? Na ni hatua gani Mheshimiwa Waziri, atatusaidia? Ahsante sana.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru kwa kutupongeza lakini kuhusu dhuluma zinazofanywa na baadhi ya nchi kwa makampuni yetu, kwa kawaida ni jambo ambalo tunalipeleka kwanza kwenye Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kwa kesi hii kwa kushirikiana na *Tanzania Chamber of Commerce* pamoja na *Tanzania Investment Centre* wale baadaye wanashirikiana na Wizara yangu na sisi Wizara yetu tunapeleka suala hili kwenye Ubalozi. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa John Lwanji suala hili linaeleweka kwa kuwa amenikumbusha naomba tu anipitishie Bajeti yangu leo halafu mimi nilifanyie kazi na wadau wenzangu Serikalini ili kulinusuru jambo hili na mwenzangu upate heshima kule unakotoka Itigi. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts..... Sh.336,790,000*

Kifungu 1003- <i>Foreign Affairs Office Zanzibar</i>	Sh.321,480,684
Kifungu 1004 - <i>Policy and Planning</i>	Sh.377,108,968
Kifungu 1005 - <i>International Cooperation</i>	Sh.1,285,405,997
Kifungu 1006 - <i>Europe and America</i>	Sh.305,943,504
Kifungu 1007 - <i>Asia and Australia</i>	Sh.347,704,240
Kifungu 1008 - <i>Africa</i>	Sh. 2,727,108,842
Kifungu 1009 - <i>Regional Cooperation</i>	Sh.2,594,750,196
Kifungu 1010 - <i>Protocol</i>	Sh.14,094,355,679
Kifungu 1011 - <i>Legal Services</i>	Sh.2,129,791,200
Kifungu 1012 - <i>Information, Education and communication</i>	Sh.113,865,880
Kifungu 1013 - <i>Middle East Division</i>	Sh.209,539,733
Kifungu 1014 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.162,150,464
Kifungu 1015 - <i>Procurement Unit</i>	Sh.284,057,376
Kifungu 2001 - <i>Embassy of Tanzania - Addis Ababa</i>	Sh.1,007,613,179
Kifungu 2002 - <i>Embassy of Tanzania - Berlin</i>	Sh.1,346,836,564
Kifungu 2003 - <i>Embassy of Tanzania - Cairo</i>	Sh.559,315,960
Kifungu 2004 - <i>Embassy of Tanzania - Kinshasa</i>	Sh.765,460,180
Kifungu 2005 - <i>High commission of Tanzania - Abuja</i> ...	Sh.737,040,108
Kifungu 2006 - <i>High Commission of Tanzania - London</i>	Sh.1,400,202,252
Kifungu 2007 - <i>High Commission of Tanzania - Lusaka</i> ...	Sh.809,463,900
Kifungu 2008 - <i>Embassy of Tanzania - Maputo</i>	Sh.769,340,516
Kifungu 2009 - <i>Embassy of Tanzania - Moscow</i>	shs. 1,151,514,488
Kifungu 2010 - <i>High Commission of Tanzania - New Delhi</i>	Sh.1,377,558,904
Kifungu 2011 - <i>Permanent Mission to The UN- New York</i>	Sh. 2, 720,877,824
Kifungu 2012 - <i>High Commission of Tanzania - Ottawa</i>	Sh.1,090,568,888
Kifungu 2013 - <i>Embassy of Tanzania - Paris</i>	Sh.1,870,373,796
Kifungu 2014 - <i>Embassy of Tanzania - Beijing</i>	Sh.1,127,555,952
Kifungu 2015 - <i>Embassy of Tanzania - Rome</i>	Sh.1,789,969,250
Kifungu 2016 - <i>Embassy of Tanzania - Stockholm</i>	Sh.1,263,324,568
Kifungu 2017 - <i>Embassy of Tanzania - Tokyo</i>	Sh.1,608,476,384
Kifungu 2018 - <i>Embassy of Tanzania - Washington</i>	Sh.1,800,875,952
Kifungu 2019 - <i>Embassy of Tanzania - Brussels</i>	Sh.1,358,380,080
Kifungu 2010 - <i>Permanent Mission to the UN - Africa</i>	Sh.1,795,574,928

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 2021 - *Embassy of Tanzania - Kampala*..... Sh.719,970,456

MHE. DR. LUKA J. SIYAME: Mheshimiwa Mwenyekiti, toka huko mwanzo tulivyokuwa tuna *address* nchi za Jumuiya ya Madola tulikuwa tukiona ni *High Commissioner* lakini hapa naona *Embassy of Tanzania* - Kampala, nimeona hata huko mbele hata na Nairobi ni *Embassy* sijui huu utaratibu huu umeanza lini.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni makosa tunatumia neno *High Commissioner* kwenye nchi zote ambazo zilikuwa chini ya utawala wa Muingereza, Uganda ilikuwa chini ya Uingereza, Kenya ilikuwa chini Uingereza kwa hiyo haya ni makosa ambayo tutayarekebisha.

MWENYEKITI: Hii ni *typing error* ambayo nadhani itabidi irekebishwe humo kwenye vitabu lakini nadhani itakuwa imeelewaka, Mheshimiwa Mbunge amekuelewa.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2022 - <i>High Commission of</i>	
<i>Tanzania - Harare</i>	Sh. 814,530,012
Kifungu 2023 - <i>Embassy of Tanzania - Nairobi</i>	Sh.1,522,708,378
Kifungu 2024 - <i>Embassy of Tanzania - Riyadh</i>	Sh.854,671,320
Kifungu 2025 - <i>Embassy of Tanzania - Pretoria</i>	Sh.1,105,317,200
Kifungu 2026 - <i>Embassy of Tanzania - Kigali</i>	Sh.678,875,158
Kifungu 2027 - <i>Embassy of Tanzania - Abu-Dhabi</i>	Sh.1,178,654,052
Kifungu 2028 - <i>Embassy of Tanzania - Bujumbura</i>	Sh.708,712,804
Kifungu 2029 - <i>Embassy of Tanzania - Muscat</i>	Sh.664,801,840
Kifungu 2030 - <i>Embassy of Tanzania - Lilongwe</i>	Sh.642,269,704
Kifungu 2031 - <i>High Commission of</i>	
<i>Tanzania - Brasilia</i>	Sh.933,076,448
Kifungu 2032 - <i>High Commission of</i>	
<i>Tanzania - Kuala Lumpur</i>	Sh.915,586,904

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa

MIPANGO YA MAENDELEO

Kifungu 1004 - *Policy and Planning*..... Sh. 44,500,000,00

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA URISHIRIKIANO WA KIMATAIFA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba Makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono, sasa kazi niliyonayo mimi hapa ni kuhoji wale wote wanakubaliana kwamba Bajeti ya Wizara hii ipitishwe waseme ndiyo. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa mwaka 2010/2011 yalipitishwa na Bunge*)

MWENYEKITI: Hoja imepita kwa asilimia mia moja wote wameikubali, nachukua nafasi hii kukupongezeni sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wenu kwa kazi kubwa sana na nzuri ambayo umeifanya, lakini pamoja nanyi pia niishukuru Wizara ya Afrika Mashariki na wao kuweza kuitisha hoja siku ya leo, hoja mbili kwa wakati mmoja imeweza kufanyiwa kazi na zimepitishwa na zimekubaliwa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha Bunge nikumbushe tu kwamba kuna semina kesho saa nne na nusu ya masuala ya Wizara ya Ardhi kuhusiana na masuala ya nyumba kwa hiyo nawakumbusha Waheshimiwa Wabunge wote ili waweze kuwepo kwa wakati kesho kwa ajili ya semina hiyo saa nne na nusu asubuhi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa kwenye *Order Paper* shughuli zote ambazo zimepangwa kufanyika kwa shughuli za leo zimekamilika sasa nachukua nafasi hii kuliahirisha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 12.55 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 5 Julai, 2010 saa tatu asubuhi*)

